Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 29 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Ninayo taarifa kutoka Ikulu kwamba katika Mkutano huu uanoendelea tulipitisha Muswada mmoja unaoitwa *The Written Laws of Miscellaneous Amendments Bill*, Taarifa kutoka Ikuli ni kwamba Rais ameshatoa kibali chake kwamba Muswada huo uwe sheria na sasa ni Sheria ya Nchi. (*Makofi*)

Tunaendelea na Agenda inayofuata, Katibu endelea na *Order Paper.*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MASILIANO NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006. Pamoja na masahihisho kuwa neno bilioni linaoonekana kwenye fedha zinazoombwa ukurasa wa 10 litolewe.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

Na. 158

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Chunya**

**MHE. NJELU E.M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakazi wa Wilaya ya Chunya wamekuwa wakijenga Hospitali ya Wilaya kwa kubadili Kituo cha Afya cha Chunya Mjini kuwa hospitali ya Wilaya; na kwa kuwa, majengo ya *MCH,* Meno, Upasuaji, Maabara na Wodi ya Wazazi yamekamilika ila bado jengo la *OPD* ma Wodi za Wagonjwa ambazo bado hazijakamilika:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la *OPD* katika Bajeti yake ili kusaidia nguvu za wananchi?

(b) Je, baada ya jengo la upasuaji kukamilika; ni lini Serikali itapeleka vifaa vya upasuaji ili shughuli hizo zianze na jengo lianze kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya inayo Hospitali Teule ya Mwambani inayomilikiwa na Kanisa Katoliki ambayo ipo umbali wa km. 72 kutoka Chunya Mjini. Barabara kutoka Chunya Mjini hadi Hospitali hiyo bado ni mbaya na wakati wa mvua baadhi ya maeneo hayapitiki. Kutokana na hali hiyo wananchi wa Chunya waliamua kupanua Kituo cha Afya cha Chunya Mjini kuwa Hospitali ya Wilaya. Hadi sasa majengo yaliyokamilika na yanatumika ni *MCH Clinic*, jengo la meno, Maabara*, X-Ray,* jengo la wazazi na jengo la kupumzisha wazazi wenye matatizo yaani *maternity waiting house*. Majengo ambayo hayajakamilika ni pamoja na jengo la wagonjwa wa nje *OPD,* wodi ya wananume, wodi ya wananwake, wodi ya watoto, jengo la jiko na chumba cha kuhifadhi maiti, jengo la huduma ya upasuaji na Wodi ya akima Mama.

Kazi zote hizi ziligharimu jumla ya shilingi 193,000,000/= zikiwemo shilingi 101,000,000/= kutoka Serikalini, sh. 73,000,000/= kutoka kwa wahisani, na shilingi 19,000,000/= zikiwa ni mchango wa wananchi. Majengo yaliyosalia yatagharimu jumla ya sh. 233,000,000/= yatakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uwezo mdogo wa bajeti ya Serikali na hali ya uchakavu wa majengo ya kulaza wagonjwa ambayo ni hatari kwa watumiaji, kipaumbele cha mchango wa Serikali kimewekwa katika kukamilisha wodi. Jengo la *OPD* litaendelea kutengewa bajeti katika utaratibu wa kawaida wa Halmashauri na litagharimu shilingi 40 milioni. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Kasaka wa Jimbo la Chunya na wananchi vile vile kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujitolea kujenga hospitali yao ya Wilaya. Serikali ipo tayari kushirikiana na wananchi hawa kuendelea na ujenzi wa Hospitlai yao hadi itakapokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli jengo la upasuaji lilishakamilika. Baadhi ya vifaa vya upasuaji kama vile meza ya kupasulia, taa ya kupasulia na chombo cha kutakatisha vifaa vya upasuaji vilishanunuliwa na kufungwa. Vifaa ambavyo havijanunuliwa na kufngwa ni *Oxygen Cylinder*, *EMO Machine*, mikasi ya kupasulia na meza ya kusukumia wagonjwa. Serikari itakamilisha upatikanaji na ufungaji wa vifaa hivyo mapema iwezekanavyo ili uasuaji uweze kufanyika na kuokoa maisha ya wananchi.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda niongeze swali moja dogo kwamba kwa vile, hospitali teule ziko mbali kama alivyoeleza Waziri iko kilomita 72 kutoka Mjini Chunya na barabara ni mbaya na kuifikia siyo rahisi;

Je, sasa Serikali katika ile gharama ya shilingi milioni 230 haiwezi sasa kutenga fedha hawataweza kutafuta msaada mwingine kutoka kwa wafadhili ili hii hospitali iweze kujengwa na kukamilika katika muda mfupi ili kuondoa matatizo yanayowakabili wananchi wa Chunya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema juhudi zipo zinafanyika kujaribu kuhakikisha kwamba hospitali hii inakamilishwa mapema, lakini muda wote utata imekuwa ni fedha zenyewe tunazopata lakini ninatambua kabisa uzito wa hospitali hii kwa sababu niliwahi kuitembelea labda tutakachofanya tutajaribu tu kushirikiana kwa karibu zaidi tuone kama kuna namna nyingine zozote zinaweza kufanyika ili kusukuma zaidi ujenzi wa hiyo hospitali. (*Makofi*)

Na. 159

**Viwango vya Kodi ya Mapato**

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI (k.n.y MHE. AISHA P. MAGINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 imetoa viwango vya kodi ya mapato kwa kuzingatia kiwango cha mauzo kwa mwaka kama vile mauzo ya kuanzia 0 – 3,000,000 kuwa shilingi 35,000/= na kutoka 3,000,000 – 7,000,000 kuwa shilingi 95,000/=

Je, kuna uhalali gani kwa halmashauri kutoza kodi za mapato kwa kiwango cha asilimia 10 (10%) ya patapo ya mwezi badala ya kufuata viwango hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisha Philipo Magina, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu Na. (6) hadi (9) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani *(The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982)* Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa iliyorekegbishwa na Sheria ya Fedha Na. 15 ya mwaka 2003 yaani *(The Finance Act No. 15 of 2003),* Serikali za Mitaa hazitozi kodi ya Mapato. Jukumu hili hufanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania yaani *(Tanzania Revenue Authorities - TRA)* kwa kushirikiana na HAZINA kwa viwango mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na kanuni husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zinakusanya mapato kupitia ada, ushuru, faini na kodi mbalimbali kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Mamlaka husika kwa mujibu wa Sheria zilizopo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tumejitahidi sana kujaribu kuchunguza kuona kama taarifa hizi zinaweza kuwa zinahusu Halmashauri gani lakini kwa bahati mbaya tumeshindwa kwa sababu hatuna taarifa zozote zinazoonyesha kwamba kuna Halmashauri inayokusanya kodi ya mapato ineyoelezwa kwa mujibu wa sheria inayohusika kwa kiwango cha asilimia 10.

Na. 160

**Mikopo ya Matrekta na Mahitaji ya Mikokoteni
Kwa Wakulima**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (K.n.y. MHE. LEKULE M. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kilimo ni uti wa mgongo na tegemeo la Taifa letu; na kwa kuwa Serikali inatoa mikopo ya matrekta kwa wakulima, lakini wapo baadhi ya wakulima wadogowadogo ambao hawana uwezo wa kukopa matrekta:-

Je, kwa nini Serikali isiwasaidie wakulima hao kupata mikokoteni ili iwasaidie wakati wa mavuno na wakati wa kuchota maji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Michael Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali imekuwa ikitoa mikopo ya kununulia matrekta mapya na kukarabati matrekta mabovu kupitia kwenye Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Serikali inatambua kwamba wapo wakulima wadogo ambao hawawezi kuchukua mikopo ya kununulia matrekta. Aidha, ni kweli kwamba Mfuko huo hauna uwezo wa kuwapatia mikopo wakulima wote ambao wangependa kuchukua mikopo hiyo. Ni matumaini ya Wizara kwamba wakulima ambao hawatapata mikopo watalimiwa na matrekta ya wale watakaopata mikopo au waliopata kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo hautoi mikopo ya kununulia mikokoteni na Serikali haina mpango wa kuwapatia wakulima mikokoteni kwa matumizi yao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kubeba mazao.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuweza kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kihistoria ni kweli kabisa kwamba nchi za Ulaya zilizo na maendeleo makubwa zilianza na wanyamakazi na ndiyo zilianza kupata maendeleo, katika Tanzania hata wakulima wa Tanzania bado hatujfikia kutumia nguvukazi hiyo.

Je, Wizara ya Kilimo haioni kwamba ni vizuri iwe na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba walau Watanzania wote wanatumia nguvukazi ya wanyama ili kuanza kujipatia maendeleo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwananzila kama ifuatavyo:-

Ni kweli wanyamakazi ni nafuu zaidi na wananweza kupatikana kwa urahisi nchini kuliko matrekta ambayo yanatoka nje, lakini kwa bahati mbaya siyo kila eneo la Tanzania ngo’mbe wanapatikna kiurahisi. Lakini kwa eneo la Mheshimiwa huyu na kwa maeneo mengine ambayo hawapatikani kwa urahisi, Wizara imefanya mpango kwanza kuhakikisha kwamba kuna vyuo maalum *Designated* kufundisha wakulima namna ya kuwatumia, maana lazima ujifunze namna ya kumshika yule ng’ombe, namna ya kuendesa lile jembe na kadha wa kadha.

Hiyo inafanyika na katika *report* ya Taifa ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wiki iliyopita tulielezea ni vyuo vipi na watu kiasi gani wamefunzwa, kweli tunafanya na tunaendelea kufanya na ni jibu sahihi zaidi kuliko trekta.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa lengo la Taifa letu la kuondoa umaskini ni ifikapo 2025 umaskini uwe umeshaondoka, lakini kwa kuwa kikwazo kikubwa cha kuondosha umaskini huo kama alivyosema muuliza swali katika swali lake kwamba wakulima wadogowadogo hawana uwezo wa kukopa matrekta na anavyojibu Waziri hata wanyamakazi hawezi kuwapa. Kikwazo kikubwa ni jembe la mkono.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuondosha jembe la mkono ili kutumia wanyamakazi na matrekta madogomadogo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mbona swali la msingi lilisema hivyohivyo, endelea kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Selelii kama ifuatavyo:-

Wizara inashughulikia suala hili la kuondoa jembe la mkono kwa namna mbili, moja ni kwa matrekta na jingine kwa kutumia ng'ombe wanaovuta *plough* yote yanafanyika lakini tatizo tulilonalo ni kwamba matrekta, ni aghali na yanatoka nje na mfuko una fedha kidogo ambayo haitaweza kusaidia kupatia wakulima wote hayo matrekta kwa sasa mkazo unatiliwa zaidi katika matumizi ya *plough* na matumizi ya ng'ombe kwa sababu vyuo vipo na tunafundisha watu namna ya kufanya hivyo.

Ruvuma ambapo ng'ombe siyo wengi kuna chuo kule tumefundisha, kuna huko anakotoka Mheshimiwa Laizer mifugo au ng'ombe wa maksai siyo tatizo kwa hivyo tunafanya na siyo hiyo tu pamoja na umwagiliaji maji mashambani. Tunafikiri kwa kufanya hayo yote mawili itasaidia sana uzalishaji. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Mheshimiwa Kahumbi naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wizara imekiri kabisa kwamba ukopeshaji wa matrekta ni gharama kubwa na hivyo ni wakulima wachache sana wanaonufaika na mikopo hiyo.

Na kwa kuwa , Wizara imeshaanzisha vituo vya wanyamakazi kwa kuwafusha wakulima ili waweze kutumia majembe ya wanyamakazi.

Na kwa kuwa, vituo hivyo havijapata fedha za kuwakopesha wakulima ili kununua zana hizo za kutendea kazi.

Je, Wizara haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kufundisha katika vituo hivyo lakini vilevile kufanya utaratibu wa kuanzisha Mfuko mdogo wa kuwakopesha wakulima ili wafundishwe na waweze kununua zana za kutendea kazi kulingana na mafundisho waliyopewa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mhagama kama ifuatavyo:-

Tunafanya hayo, kwanza kwa kuhimiza uanzishaji wa vyama vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) kununukia vifaa hivyo, hii ni njia mojawapo na hii inaweza kufanyika popote nchini Tanzania na ni njia rahisi zaidi hasa kwa kununua majembe na mifugo.

Nyingine kuna fedha zinatoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya Wanawake, wangeweza bado kutumia hiyo. Halafu kuna Mfuko wa Vijana, bado wangeweza kufanya hivyo.

Pamoja na hayo yote kuna *DAP,* Mfuko ule wa *DAP* kuna bilioni 4 Wizara ya Kilimo, lazima lakini iibuliwe hukohuko Wilayani. Kwa hivi naungana na Mheshimiwa Mhagama tushirikiane kuihamasisha Halmashauri ya Songea iibue miradi hiyo itumike na mfuko huo.(*Kicheko*)

Na. 161

**Mabonde Yafaayo kwa Kilimo cha Umwagiliaji Kongwa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Kongwa yapo mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kama yale ya Chamkoroma, Mseta, Manghweta, Banyibanyi na kaddhalika; na kwa kuwa, mabonde hayo yanaweza kutumika kwa kilimo cha Nyanya, vitunguu na kuongeza kipato cha wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi kuboresha kilimo hicho katika mabonde hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2002, Serikali iliandaa Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Mpango huo umebaini kuwa, Wilaya ya Kongwa ina jumla ya hekta 15,114 zinazofaa kuendelezwa kwa gharama ndogo kwa kutumia maji yanayotoka katika chemchem na vijito na kwa kuvuna maji ya mvua. Mabonde yaliyoainishwa katika mpango huo kabambe ni Mbuga, Hekta 4,728, Mtanana, Hekta

3,692, Mlali – Bondeni, hekta 2,479, Iduo, hekta 2,409, Kiraugisi, hekta 1,026, Kongwa – Bilauli Plain, hekta 500, Chamkoroma, hekta 80, Mseta, hekta 80, Mkutano, Hekta 60 na Banyibanyi, hekta 60.

Aidha, uchunguzi uliofanywa na Wataalam wa umwagiliaji kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula, walipotembelea Wilaya ya Kongwa mwaka wa 2001/2002, unaonyesha kwamba, kuna haja ya kubadili baadhi ya miundombinu ya umwagiliaji iliyopo kwa lengo la kutumia maji vizuri na kupanua ukubwa na maeneo yanayolimwa. Kwa mfano, skimu ya Chamkoroma inahitaji kujengewa *intake* mpya, kukarabati maeneo ya mifereji yaliyuobomoka na kujenga bwawa dongo la kukusanya maji ili liwezeshe kupanuliwa kwa eneo linalolimwa kutoka hekta 80 za sasa hadi hekta 120.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itatuma wataalm kwenda kushirikiana na wataalam waliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kufanya makadirio ya gharama zinazotakiwa kuendeleza skimu za umwagiliaji katika mabonde yaliyotajwa. Makadirio hayo yatatumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kutayarisha miradi ya umwagiliaji itakayojumuishwa katika Mipango ya Maendelo ya Kilimo ya Wilaya kwa ajili ya kuombewa fedha. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Natangulia kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa wananchi wa Chamkoroma, Tubugwe, Manghweta, walikwisha lundika mawe siku nyingi kwa ajili ya kuboresha skimu yao ya Chamkoroma ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani wa Kata yao Shitindi lakini ni karibu miaka 10 sasa hakuna chochote ambacho kimakuwa kikifanyika kutoka upande wa Serikali.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini baada ya kupitisha bajeti ya Wizara juzi kuhusu kuwasaidia watu hao?

La pili, Idara ya Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa imekuwa ikiandika miradi mara kwa mara ya umwagiliaji katika Wilaya ya Kongwa na kupeleka Wizarani, lakini miradi hii imekuwa haitazamwi kabisa kabisa na ushahidi ni juzi kwenye skimu zote za nchi nzima za miradi ya umwagiliaji hapakuwa na mradi hata mmoja wa umwagiliaji kwa Wilaya ya Kongwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya mimi kusema ndiyo kwenye bajeti ile unasemaje kuhusu watu wa Kongwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ndugai kama ifuatavyo:-

Kwanza ni sasa napata taarifa hiyo kuwa mawe yalikusanywa kule Chamkoroma na hakuna kilichofanyika na mimi nimetembelea kule Kongwa sikupata taarifa hizo laiti ningepata tungetekeleza. Nasikitika haikutekelezwa kwa sababu taarifa haikutufikia.

La pili, anasema kuwa miradi haijafanyika, moja ni kwa sababu miradi ni mingi sana kwa nchi nzima na afadhali kidogo ahuweni kwako kuna miradi kadhaa niliyoitaja hapa ambayo mingine inafanya shughuli. Sasa kwa sasa ni vigumu kidogo kwa sababu kila senti imepangwa kwenda katika mpenyo maalum lakini tumetoa ahadi katika mwaka huu wa fedha tunakuja huko wataalam. Wataalam wetu watakuja huko tusaidiane na viongozi wa huko tutengeneze, ibuliwe miradi ipate *fund the next Financial Year. (Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, mabonde yaliyozungumzwa katika swali la msingi yanafanana sana na mabonde ya Takanya na Mlunga, Wangi, Lwamelo na Mwanawota.

Je, katika ahadi ileile aliyoitoa Kongwa yuko tayari kuleta wataalam kushirikiana na wataalam kuibua mabonde hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Proffesor Daimon Mwaga kama ifuatavyo:-

Tumesikia ombi, nitahakikisha nimewaagiza wataalam wafike hata huko lakini hii haikuzuii Mheshimiwa ukaandika barua maalum kukumbushia maana sisi wengine pengine tutatoka kuingia Namtumbo halafu huku nyuma ikachelewa na ukaona kuwa hatukutimiza ahadi. (*Kicheko*)

Kwa ahadi hiyo ukiishaandika tutahakikisha tunatekeleza lakini hata hivyo nitawazungumzia suala hilo na unajua hili tumefanya sasa nimefika kule na nimetembelea miradi mingi sana.

**SPIKA:** Mwisho mabonde ya Mpwapwa, Mheshimiwa Lubeleje.(*Kicheko*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kabisa kwamba nchi hii ina mabonde mengi yakiwemo mabonde ya Wilaya ya Mpwapwa, Matomondo, Godegode na Lumuma.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubalina nami kwamba ili kuondokana na tatizo la njaa katika nchi hii iko haja ya kutenga fedha za kutosha kusaidia wakulima ili mabonde yaweze kulimwa na kuondoa tatizo la njaa katika nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Lubeleje kuwa tunahitaji kutenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba chakula kinakuwepo na tunajitahidi lakini tunachopata ndiyo hicho kwa hivi tunashindwa kufanya.

Wizara ya Kilimo yenyewe inahitaji shilingi bilioni 30 kila mwaka ili kuweza kufanya umwagiliaji uwe kilimo chenye tija kubwa. Sasa tunachoomba ni kuwa huko mbele tukipata nafasi hiyo tutaweza kufikiria pamoja na mabonde mengine mengi lakini tunajitahidi zaidi hasa ni bilioni 30 kila mwaka mpaka mwaka 2017.

Na. 162

***TRA* na Wafanyabiashara wa Mafuta Toka Kenya**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (K.n.y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wako vijana wengi Moshi Mjini ambao wanafanya biashara ya kununua mafuta kutoka Kenya kupitia Chekereni Relini na kuyauza kwenye sehemu mbalimbali za Mji wa Moshi; na kwa kuwa, vijana hao wengi wao wana elimu ndogo, na hutengemea biashara hiyo kama mhilimi mkubwa wa maisha yao lakini wamekuwa wakikamatwa na watu wa *TRA* na kunyang'anywa mafuta hayo pamoja na bidhaa nyingine na haijulikani kwamba baada ya kupora bidhaa hizo zinapelekwa wapi.

(a) Je, mafuta na bidhaa nyingine wanazongyang'anywa *TRA* inazipeleka wapi?

(b) Je, hadi sasa *TRA* wamekamata kiasi gani kutoka kwa vijana wangapi; na endapo bidhaa zilizokamatwa zimeuzwa zimapatikana fedha kiasi gani, zimetumika vipi na wapi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani na vijana hao ambao nguvu ya soko huria inawasaidia kununua bidhaa kutoka sehemu inapouzwa kwa bei nafuu na kuuza mahali penye bei nzuri na hivyo kupata faida kidogo inayowapa nguvu za kuishi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** aslijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla a kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, naoma kuanza na maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mkoa wa Kilimanjaro kuna vituo vitatu vilivyoteuliwa kisheria kutumika kuingiza mali nchini toka nchi jirani na nchi za nje. Vituo hivyo ni Holili na Tarakea katika Wilaya ya Rombo, na uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro katika Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara au mtu yoyote anayetumia njia nyingine zaidi ya zilizoteuliwa kisheria kuingia au kuingiza mali nchini anavunja Kifungu Na. 15 cha Mkataba wa Umoja wa Forodha na Nchi za Afrika Mashariki. Mali yoyote inayokamatwa ikiingizwa nchini kwa kutumia njia zisizoteuliwa rasmi, huzuiwa katika mabohari ya Forodha Holili na Moshi na wahusika kufunguliwa kesi ambayo hushughulikiwa na Kamishna wa Forodha kwa kutumia kifungu Na. 219 cha Sheria ya Umoja wa Forodha wa Nchi za Afrika Mashariki

Mheshimiwa Spika, Chekereni Relini sio kituo rasmi. Kwa hiyo, mali inayoshukiwa kupitia njia hiyo hushughulikia kisheria na hati ya kukamata mali iliyoainishwa kisheria hutolewa kwa mhusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mafuta ya taa na bidhaa nyingine zinazokamatwa wakati wa doria na ikithibitika kwamba zimeingizwa kinyume na taratibu za sheria, huhodhiwa kwa mujibu wa vifungu husika.

Kamishna wa Forodha anaruhusiwa kutumia kifungu Na. 210 cha Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutaifisha mali husika, au kutoza kodi na faini na kurudisha mali kwa mhusika.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2005 hadi Aprili, 2004 vijana 147 walikamatwa na mafuta ya taa yenye ujazo wa lita 32,816 yenye thamani ya shilingi 9,844,800/= ambayo yalitaifishwa na kuuzwa kisheria na kupata kiasi cha shilingi 10,501,120.

Bidhaa nyingine zilizokamatwa kwa kipindi hicho zilikuwa na thamani ya shilingi 94,560,445 ambapo Serikali ilikusanya kodi ya kiasi cha shilingi 42,220,222.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inawashauri vijana wa Moshi Mjini Mkoa wa Kilimanjaro na kote nchini kufanya biashara halali kwa kupitia kwenye mipaka inayoruhusiwa na kulipa kodi ambayo sasa ni ndogo sana kama inavyotakiwa kisheria.

Biashara za magendo huwafanya vijana wafilisike pindi wanapokamatwa na mali kutaifishwa. Mamlaka ya Mapato Tanzania inatoa elimu ya kodi ura kupitia idara yake ya

Huduma na Elimu kwa Walipa Kodi. Vijana wote nawaasa kupata maelekezo zaidi kutoka ofisi za Mamlaka ambazo zipo katika Mikoa na Wilaya zote nchini.

Aidha kwenye vituo vya Holili na Tarakea yapo maelezo kwenye mabango makubwa yanayotoa utaratibu wa kutoa na kuingiza bidhaa za Kenya.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo la vijana hawa wa Moshi pengine na wao niwaite Wamachinga ni tatizo linalofanana na vijana wote wa nchi nzima ambao wanabeba bidhaa kwenye migongo yao wakitafuta namna ya kuishi na kwa kuwa tatizo hili limesababishwa na uzembe wa Serikali wa kutowaundia vijana nafasi za ajira. Je, Wizara sasa ina mpango gani wa kushirikiana na Serikali kwa ujumla ili kuweza kutafuta njia muafaka za kuwakopesha vijana ili waweze kufanya kazi zao halali na walipe kodi halali bila kubughudhiwa? Je, Serikali ina Mkataba gani na Wamachinga na wa miaka mingapi ili waendelee kufanya kazi hizo ambazo hawalipi kodi wala ushuru lakini wanasumbuliwa kila mara ili kuweza kuzuia tatizo hili kuendelea kukua ili vijana wasiwe wengi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Wamachinga ni baadhi tu ambao hawafanyi kazi zao kihalali na pale Mamlaka ya Mapato inapogundua kwamba kuna mali ambayo wana wasiwasi haikulipiwa ushuru, hatua zimechukuliwa na kutafuta *source* ya mali ile imepatikana kutoka wapi na kuhakikisha kwamba inatolewa ushuru. Hata Mheshimiwa Mutungirehi hana uhakika kwamba Wamachinga hao mali walizokuwa nazo hawakulipia ushuru.

Mheshimiwa Spika, pili, mara nyingi katika Mikoa mbalimbali wanashikwa hawa kwa sababu wanafanya biashara katika sehemu ambazo hawaruhusiwi na wametengewa sehemu mbalimbali katika Mikoa mbalimbali ili wafanye shughuli hizo. Kwa hiyo, Wamachinga wafuate zile taratibu za Mikoa zilizowekwa na wasipofuata hawatopuuziwa.

Na. 163

**Utunzaji wa Kumbukumbu – Kitengo cha Mafao ya Uzeeni**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu usiofaa wa utunzaji wa kumbukumbu katika kitengo cha mafao ya wastaafu umechangia kwa kiasi kikubwa wastaafu wengi waliostaafu kwa miaka mingi na wengine wamekufa bila kupata mafao yao ya uzeeni na wengine wategemezi wao bado wanahangaika bila mafanikio:-

(a) Je, ni wastaafu wangapi ambao wamekosa haki zao kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu za utumishi wao?

(b) Je, Wizara ya Fedha imechukua hatua gani kwa kushirikiana na zile Wizara ambako wastaafu hao walikuwa wakifanya kazi ili kupata kumbukumbu sahihi na hatimaye waweze kulipwa stahili zao mara moja?

(c) Je, ni lini Serikali itatangaza majina ya wadai wastaafu kutoka katika orodha yake wastaafu ambao hawajalipwa kama vile Shirika la *NSSF* linavyofanya ili kuokoa hali hiyo mbaya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nilipojibu swali Na. 121 la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, ili kuwezesha mtumishi kulipwa mafao yake mara anapostaafu, mtumishi husika anpaswa kutoa taarifa ya kustaafu kwa mwajiri wake miezi sita kabla ya tarehe kustaafu. Mwajiri naye anawajibika kuwasilisha Hazina majalada ya mtumishi huyo miezi mitatu kabla ya tarehe ya kustaafu. Kumbukumbu zinazotakiwa kuwepo ndani ya majalada hayo ni pamoja na barua za ajira, kuthibitishwa kazini, kuingizwa katika masharti ya kazi ya kudumu na malipo ya uzeeni, kupandishwa cheo cha mwisho kabla ya kustaafu na ya kibali cha kustaafu, mwaka halisi wa kuzaliwa, picha mbili (*passport size)* za mstaafu na fomu ya *retiring award* ambayo inaonyesha mishahara ya miaka mitatu ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mirathi, mwajiri anatakiwa awasilishe pia nyaraka zifuatazo: Cheti halisi cha kifo kilichotolewa na Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo, hati halisi ya msimamizi wa mirathi, cheti cha ndoa endapo mhusika alikuwa ameoa au kuolewa, kiapo cha mjane kinachotolewa Mahakamani, kiapo cha kutunza watoto chenye picha ya anayewatunza watoto kilichogongwa mhuri wa Mahakama; vyeti vya kuzaliwa watoto wa marehemu wenye umri usiozidi miaka 21 wakati wa kufariki marehemu na picha mbili (*passport size*) za msimamizi wa mirathi, watoto wote wa marehemu na mjane zilizogongwa mhuri wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa uwasilishaji wa kumbukumbu kutoka kwa mwajiri na upungufu wa nyaraka husika ndizo sababu kubwa za ucheleweshaji au ukosehwaji wa malipo ya mafao na mirathi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya wastaafu ambao wamekosa haki zao kwa sababu ya kukosekana kumbukumbu za utumishi wao ni 1,043 kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania. Ni jukumu la Wizara na Idara

kuhakikisha kumbukumbu hizo zipo kabla ya mtumishi kustaafu ili asicheleweshewe malipo yake.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la nyaraka pungufu limekuwa likikabiliwa kwa kuchukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Waajiri wanaohusika hupeleka barua za kuwaomba nyaraka hizo na wengi wao hawazitumi Wizara ya Fedha mapema iwezekanavyo.

(ii) Waajiri huandikiwa barua kuhusu ni nyaraka zipi zinazotakiwa ziambatane na majalada ya mstaafu yanapoletwa Hazina. Wengi hawazingatii sharti hilo.

(iii) Maafisa wa Hazina huzifuatilia nyaraka hizo hata kwa kufika maofisini na kutoa elimu kwa waajiri husika juu ya kuandaa na kutuma nyaraka kamilifu Hazina. Bado wengi hawasikii.

Ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge kuwa na orodha ya nyaraka zinazotakiwa ili waweze kuwashauri wastaafu na kupambana na waajiri ipasavyo kabla ya kufika Hazina. Wastaafu wenye kumbukumbu hawapati matatizo ya malipo wanapostaafu.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hatua nzuri aliyochukua kwa mpiga kura wangu Lutasi Muhire ambayo ni ya matumaini kwamba pengine atapata haki zake baada ya mika kumi na nane hivi, lakini nina maswali mawili madogo ya kuuliza. Kwa kuwa majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamekuwa ndio hayo hayo kwa miaka mingi katika nyumba hii na malalamiko haya ni makubwa na watu bado wanapata matatizo kutokana na kumbukumbu mbaya zinazowekwa katika maeneo mawili kwa mwajiri na Wizara ya Fedha. Je, Serikali inasema nini juu ya kupunguza mzigo huu wa miaka mingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni njia zipi ambazo mtumishi mstaafu anapokuwa amefariki wategemezi wake wataweza kupata haki za marehemu baada ya kifo chake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, ni kweli majibu yangu ni hayo hayo kila ninapopanda hapa juu kuhusu wastaafu na malipo yao kwa sababu ndio ukweli wenyewe ulivyo. Siwezi kubadilisha na kusema kauli nyingine, nikawa na kauli mbili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sebabili mwenyewe anaelewa kwa sababu mara nyingi tumekuwa pamoja. Katika Mkoa wake yeye peke yake kuna hoja 65 za wastaafu. Hata yeye Mheshimiwa Mbunge alipokwenda Mkoani au kwa waajiri waliohusika ameshindwa kupata baadhi ya hizo nyaraka.

Mheshimiwa Spika, njia zipi. Narejea jibu langu la msingi njia za kufanya ni zile zile. Lakini vile vile tunaomba msaada wa Waheshimiwa Wabunge waende kama yeye alivyokuwa anakuja. Katika barua yake ya mwisho anayo nakala yangu ya barua katika kuhakikisha tumefanya nini kumsaidia mstaafu ambaye kwa muda wa miaka mitano sasa anahangaika kupata malipo yake. Bado hatuchoki, tupo tayari kusaidiana na Waheshimiwa Wabunge ili kuwasaidia wastaafu waliomo katika Majimbo yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, Serikali imetambua adha ambayo wastaafu wameipata kwa muda mrefu na kwa hiyo kwa wastaafu wanaostaafu sasa hivi kumbukumbu zimeboreshwa na waajiri wameelekezwa kuhakikisha kwamba kumbukumbu za watumishi wote zimewekwa vizuri ili wakati wanapostaafu wasipate adha. Kwa wale ambao wamekwishastaafu ndio ambao kuna matatizo makubwa na hata hivyo wale wote wanaohusika kwa kweli wanajaribu kutafuta njia mbalimbali za kupunguza adha hizo. Naomba nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwakumbusha waajiri wote kwamba wao ndio wana *registry*, ni kazi ya mwajiri kuhakikisha kwamba kumbukumbu na nyaraka zinazohusu watumishi zinawekwa vizuri. Ni pale tu ambapo inatokea bahati mbaya labda *registry* imeungua ndio mtumishi anawajibika sasa kuleta za kwake, lakini jukumu la mwanzo kabisa ni la waajiri. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Utumishi pamoja na Naibu Waziri wa Fedha: Je, ni lini Ofisi ya Waziri wa Fedha itatambua uzembe wa watumishi wake kuhusu watu waliofiwa kupotea mafaili yao kila leo. Usumbufu unaopatikana pamoja na hawa wastaafu pamoja na kwamba anasema sheria hawezi kubadilisha, lakini ni lini atakapotambua uzembe wa watumishi wake na akawachukulia hatua kwa sababu watu wanapata matatizo. Anaweza kuwa mfiwa ana kila kitu cha uthibitisho lakini halipwi na anazungushwa chini ya miaka mitatu au mitano. Mpaka lini atakapotambua na kuchukua hatua katika ofisi yake? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, pale inapobainika kwamba mtumishi amefanya uzembe anachukuliwa hatua ya kinidhamu kwa uzembe alioufanya.

**WABUNGE FULANI:** Aaa, aaa!!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** Ndio ukweli wenyewe. Lakini kama haikuthibitika hivyo basi. Lakini kama kuna Mheshimiwa amehisi kuna mtu anamfahamu kwa jina amefanya uzembe atuletee, atwambie kwamba huyu alifanya uzembe fulani na tutamchukua hatua inayofaa.

Na.164

**Uvuvi Haramu – Ziwa Victoria**

**MHE. JOEL N. BENDERA (K.n.y. MHE. IBRAHIM W. MARWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa uvuvi haramu wa kutumia sumu katika Ziwa Victoria hususan katika Wilaya ya Musoma umekuwa ni kero kubwa kwa wakazi wa Wilaya hiyo na kwa kuwa wananchi baada ya kutopata ushirikiano wa kutosha katika kudhibiti tatizo hilo wameamua kuchukua sheria mkononi na kuwaadhibu watuhumiwa wa makosa hayo, hasa baada ya kukatishwa tamaa na vyombo vya dola; na kwa kuwa, Serikali iliunda Tume ili kuchunguza madai hayo licha ya taarifa zilizokuwa zikitolewa kwa viongozi mbalimbali wa Chama Tawala cha CCM na Serikali ikiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara Mkoani Mara mwaka 2004:-

(a) Je, taarifa ya Tume hiyo ilibaini nini na ni hatua gani zimechukuliwa katika kukabiliana na uhalifu huo?

(b) Je, ni madhara gani yanayoweza kusababishwa na ulaji wa samaki wanaovuliwa kwa sumu kama vile *Thiodan* na dawa ya kusafishia maiti?

(c) Je, tatizo hilo ni janga au ni tatizo la kawaida kama yalivyo matatizo mengine yasiyohitaji uharaka wa kushughulikiwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba kutoa maelezo ya awali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua ukubwa wa tatizo la uvuvi haramu katika maeneo ya uvuvi nchini imeweka mkakati Kitaifa kudhibiti uvuvi haramu nchini ikiwemo Ziwa Victoria. Mwaka 2003, Serikali ilianzisha vituo vya kudhibiti uvuvi haramu kikanda kwa kuanzia na maeneo ya maji makuu. Katika ukanda wa Ziwa Victoria vituo hivyo vipo katika Mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara. Vituo hivyo vimepatiwa vitendea kazi muhimu, watumishi wenye taaluma inayotakiwa pamoja na fedha kwa ajili ya kuendesha doria.Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kuunda Tume ya kuchunguza madai ya matukio ya wananchi wa Wilaya ya Musoma Mjini ambao walituhumiwa kuchukua sheria mkononi na kuwaadhibu watuhumiwa wa uvuvi haramu wa kutumia sumu Wilayani humo. Hata hivyo doria za mara kwa mara zimekuwa zikifanyika kwa kushirikisha jamii inayozunguka rasilimali hiyo kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu pamoja na kero za uvuvi huo kwa jamii.

(b) Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kisayansi unaeleza kuwa mtu aliyekula samaki aliyevuliwa kwa sumu kama vile aina ya *thiodan* anaweza kupata madhara ya kuhara na kutapika na hata kupoteza maisha. Kiwango cha madhara hutegemea kiasi au kiwango cha sumu kilichopo kwenye nyama ya samaki aliyemla. Mlaji pia anaweza kupata madhara ya kuvimba miguu pamoja na kuwashwa midomo. Aidha, iwapo mlaji atakula samaki waliovuliwa kwa kutumia sumu hata kwa kiwango cha chini lakini kwa

muda mrefu anaweza kupata ugonjwa wa saratani au kuwa na afya duni. Inafahamika pia kuwa sumu hii huua kizazi.

(c) Mheshimiwa Spika, tatizo la uvuvi haramu wa kutumia sumu ni tatizo kubwa kwani matumizi ya sumu huathiri *bioanuwai* ya majini wakiwemo samaki. Vile vile sumu hiyo huathiri binadamu wanaokula samaki waliovuliwa kwa njia hiyo kunywa maji na kuathiriwa au kuwekwa sumu. Tatizo hili linahitaji ushirikiano mkubwa na jamii wa kudumu ili kulitokomeza kabisa.

Mheshimiwa Spika, ili kupambana na tatizo hili, Serikali inaendelea kuviimarisha vituo vya doria pamoja na kuelimisha jamii kuhusu uvuvi endelevu. Hata hivyo, Serikali haina uwezo wa kuwa ziwani kufanya doria nyakati zote, hivyo ushirikishwaji wa jamii ndiyo silaha kubwa ya kufanikisha udhibiti wa uvuvi haramu. Nashauri Halmashauri za Wilaya zihakikishe kuwa kila Kijiji kinakuwa na kikundi cha ulinzi wa rasilimali *(BMU)* kwa kuzingatia ukubwa wa eneo husika. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awahamasishe wananchi wa Jimbo lake katika suala zima la kuzingatia sheria na kanuni za uvuvi kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Mwaka 2000, JWTZ waliweka vizuizi katika maeneo ya Ziwa Victoria kwa ajili ya kukagua mazao yanayotokana na bahari, yaani hao samaki na kuwa na utaratibu wa kugundua aidha wavuvi wale wametumia sumu au wametumia mabomu au nguvu ya kawaida na inapobainika huwa wanachukuliwa taratibu za kisheria. Je, utaratibu huo kwa nini Serikali isiuendeleze ili kuzuia kabisa tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, la pili, haya matatizo sugu kama hili ambalo linatokea katika Ziwa Victoria ndio yanayopelekea mara nyingi wananchi kuchukua hatua mikononi mwao. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kukomesha kabisa tabia hii ili kuepuka *mob psychology*, wananchi wasije kufanya mambo ambayo sio ya kawaida kwa binadamu wenzao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2001 Januari, Serikali iliendesha doria maalum dhidi ya uvuvi haramu kwa Ziwa lote kwa siku 42 mfululizo. Lakini vile vile Serikali tarehe 1-28 Februari, 2005, iliendesha kampeni nyingine katika Ziwa hili kwa kushirikisha Wilaya zote katika Ziwa Victoria. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba mara kwa mara doria zinafanyika, lakini kama nilivyoeleza awali umuhimu hasa hasa ni kwa wananchi wenyewe na ndio maana mpaka hivi sasa tunashukuru na kuwapongeza wananchi katika Ziwa Victoria kwamba wameunda vikundi vya ulinzi wa rasilimali 511 na bado wanaendelea kuhamasika. Lile ambalo lilitokea kwa wakati ule kwa kweli ni jambo ambalo Serikali inalipinga kwa sababu Serikali siku zote inapinga watu kuchukua sheria mikononi mwao, lakini tunasema kwamba ni muhimu sana kwa wananchi kuweza kuelewa na kueleweshwa madhara ambayo yanatokea katika Ziwa hili.

Na. 165

## Msitu wa Mbizi- Sumbawanga

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA (K.n.y. MHE. PAUL P. KIMITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa msitu wa Mbizi ulioko kwenye eneo la Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga Mjini ni chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Mjini Sumbawanga:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa msitu huo una wanyama na baadhi ya miti ambayo haipatikani mahali popote duniani?

(b) Je, kwa nini Serikali isiufanye msitu huo kuwa sehemu ya hifadhi ya Taifa kufuatana na umuhimu wake ili pamoja na watalii wanaokwenda kwenye Mbuga za Wanyama za Katavi, wapate nafasi ya kujionea umaarufu wa msitu huo?

(c) Je, kuna utafiti wowote uliokwishafanyika na Serikali ambao ingefaa uongozi wa Mkoa ukajulishwa kuhusu msitu huo na mingine ya Mkoa wa Rukwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Msitu wa hifadhi wa Mbizi wenye eneo la hekta 17,373 ulihifadhiwa kama msitu wa Serikali Kuu (*Territorial Forest Reserve*) mwaka 1950 (*Declaration Order No.* 132 ya 1950) kwa madhumuni ya kuhifadhi vyanzo vya maji, mimea na wanyama wanaopatikana katika eneo la msitu huo.

Wizara yangu kwa kushirikiana na mradi wa *RUDEP* (Rukwa *Development Programme*) ulifanya utafiti katika msitu huo kuanzia mwaka 1986 hadi 1996 ili kupata takwimu za mimea na wanyama waliopo katika msitu huo kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuimarisha ulinzi na kusimamia uendelezaji wake.

Utafiti huo umebaini kuwa katika msitu wa hifadhi wa Mbizi kuna mimea adimu zaidi ya 50 na wanyama ambao wapo hatarini kutoweka kama mbega wekundu *(red colobus monkeys)*. Aidha, Wizara yangu imepata taarifa kutoka Chama cha Maendeleo ya Utalii Mkoani Rukwa (Katavi *Press Club and Rukwa Journal Tourism Development*) kuwa kuna vivutio vingi katika msitu huu ikiwa ni pamoja na vinu vya kale vya kufulia zana za kilimo na uwindaji, mapango ya kuabudia na nyumba za kale za Machifu wa kabila la Wafipa.

Mheshimiwa Spika, ili kubadilisha msitu wa hifadhi kuwa Hifadhi ya Taifa, vigezo vifuatavyo ni lazima vizingatiwe:-

(i) Kuwa na viumbe hai wasiopatikana katika hifadhi nyingine nchini au mahali pengine duniani (*endemic species*)

(ii) Kuwa na viumbe ambavyo vinakaribia kutoweka kutokana na sababu mbalimbali (*endangered, threatened or rare species)*

(iii) Kuwa na idadi kubwa ya viumbe hai mbalimbali (*high biodiversity*)

(iv) Msitu wa hifadhi kuwa karibu na hifadhi ya Taifa na ni muhimu kwa mahitaji ya viumbe hai kutoka hifadhi hiyo kwa kipindi fulani cha mwaka, kwa mfano, maji na malisho mabichi wakati wa kiangazi.

(v) Msitu wa hifadhi kuwa ni chanzo kikuu au muhimu cha maji kwa hifadhi ya Taifa iliyoko jirani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuubadilisha msitu wowote wa hifadhi kuwa hifadhi ya Taifa hutolewa mapendekezo na Wilaya na hatimaye Mkoa ambako eneo hilo lipo. Mapendekezo hayo baadaye hupelekwa Serikalini ambako hufanyiwa uchunguzi kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa hapo huu. Baada ya uchunguzi endapo Serikali itaridhia mapendekezo hayo hupelekwa Bungeni kwa hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa msitu wa hifadhi wa Mbizi ni chanzo kikuu cha maji kwa wananchi waishio Mjini Sumbawanga na Vijiji kama vile Wipanga, Muze, Ng'ongo, na kadhalika. Serikali inatambua kuwapo wanyama na mimea ndani ya msitu huo. Aidha, Serikali haina taarifa ya kuwepo wanyama na mimea ambayo haipatikani mahali popote duniani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaangalia uwezekano wa kuubadili msitu wa hifadhi wa Mbizi kuwa hifadhi ya Taifa baada ya Mkoa wa Rukwa kufuata utaratibu nilizoeleza hapo awali.

(c) Mheshimiwa Spika, utafiti umefanyika kama nilivyoeleza hapo awali chini ya usimamizi wa Mradi wa *RUDEP* ambapo ulifadhiliwa na Serikali ya Finland. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na uongozi wa Mkoa kwa ajili ya kupata taarifa zaidi ya utafiti huo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amekiri kwamba ni kweli kuna mimea na baadhi ya wanyama ambao ni muhimu na hawapatikani mahali pengine na kwa kuwa ametushauri sisi tukutane katika vikao na kuleta mapendekezo: Je, anakubali kwamba tutakapoleta mapendekezo Wizara yake italeta wataalam ili tuweze kushirikiana na kufikia uamuzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba eneo hili lina ukubwa wa hekta 17,000 alizosema, lakini bado sehemu yenye miti ni ndogo na

tungehitaji Serikali kupitia Wizara yake ishirikiane na Mkoa ili kuweza kupanda miti mingine zaidi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa yote mawili nakubaliana naye.

Na. 166

**Tatizo la Maji Mji wa Korogwe**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Mji wa Korogwe na vitongoji vyake umekuwa na tatizo sugu la kukosa maji na maji madogo yaliyopo hutolewa kwa mgao na hayafiki kwenye maeneo ya Habitat, Mlima Fundi, Mtonga juu, Kwasemagube, Kwambo, Bagamoyo, Kilole, Kambi ya Maziwa, Kilole Mzee na kadhalika na kwa kuwa kwa muda mrefu nimekuwa nikiomba Mji huo upatiwe maji ya uhakika toka kwenye chanzo cha maji ya uhakika cha Tabora ambapo maji yake hupita katikati ya Mji wa Korogwe na kwa mantiki hiyo mtu yeyote hawezi kukuelewa ukisema kuwa Mji huo una shida ya maji:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Mji huo kupatiwa maji toka kwenye chanzo cha Tabora hasa ikitiliwa maanani kuwa Wilaya ya Korogwe ni miongoni mwa Wilaya zinazofadhiliwa na Mfuko wa Maji wa Benki ya Dunia na huo ukawa ni Mardi wa kushughulikiwa kwa haraka?

(b) Kwa kuzingatia hali mbaya ya shida ya Maji Korogwe: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuupatia Mji huo maji hasa kwa kuchimba visima katika maeneo ya Habitat Zungnat, *TTC Korogwe,* Kilole Mzee, Bagamoyo, Mtonga Juu, Mlima Fundi na kadhalika?

(c) Kwa kuwa shamba la Katani la Kwamdulu linapata maji toka Mto Ruvu: Je, Serikali haioni kuwa ni busara mradi huo ukapanuliwa ili maji yake yatumike kuwahudumia wananchi wa Mitaa yote ya Kilole hasa kwa kuongea na wawekezaji hao na kujenga tanki na kupeleka maji hayo Kilole yote hadi Bagamoyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali za kuupatia Mji wa Korogwe huduma ya maji kutoka chanzo cha Tabora zilianza siku nyingi. Utafiti wa kutumia chanzo hicho ulikamilika tangu mwaka 1978 na ulionyesha kuwa chanzo cha maji cha Tabora kina uwezo wa kuongeza na kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Korogwe. Upimaji na uchoraji wa ramani ya njia kuu ya bomba toka chujio la Tabora kupitia Vijiji vya Tabora, Kitifu, Mgambo na Ngombezi nao umekamilika. Gharama ya utekelezaji wa mradi huu inakadiriwa kuwa ni sh. 2.3bn/= kwa bei ya mwaka 2004/2005.

Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo. Hata hivyo, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kuupa mradi huu kipaumbele na kuuingiza katika Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao utaanza kutekelezwa Wilayani Korogwe punde fedha zitakapotolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Korogwe. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuchimba visima virefu vitatu katika maeneo ya *Old Korogwe,* Shule ya Wasichana Korogwe na Mtonga. Aidha, Serikali katika mwaka 2001/2002, ilichimba kisima kingine kimoja eneo la Mtonga kwa gharama ya sh. 7m/=.

Vile vile mwaka 2003/04, Serikali ilitoa sh. 100,700,000/= kwa ajili ya kujenga tanki lenye ukubwa wa mita za ujazo 90 kwenye kilima cha Mtonga. Kazi nyingine zilikuwa ni pamoja na kununua mabomba na viungio vyake, kujenga kibanda, kununua na kufunga mtambo na kulaza mabomba kutoka Kisima cha Mtonga hadi kwenye tanki. Kazi hizo zote zimeshakamilika na mtambo wa maji umeshafungwa kwenye kisima hicho na hivi sasa mradi unafanya kazi kwa majaribio. Vile vile mwaka 2004/2005, Wizara ilitenga kiasi cha sh. 30m/= za kununulia mabomba kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na mita za maji ili kudhibiti matumizi ya maji Mjini Korogwe. Hatua hizi zimeongeza upatikanaji wa maji kutoka mita za ujazo 2,400 hadi 2,700 kwa siku, sawa na asilimia 68 ya mahitaji ya maji kwa Mji wa Korogwe.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na asasi ya *DEVIN AID KOROGWE*, imechimba visima vifupi vitatu katika maeneo ya Bagamoyo na Mlima Fundi. Uchunguzi wa kuchimba visima katika maeneo ya Habitat, Zunguat, *TTC Korogwe,* Kilole Mzee, Bagamoyo, Mtonga Juu na Mlima Fundi nao unaendelea.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba shamba la katani la Kwamdulu linapata maji kutoka Mto Ruvu (Pangani) kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiwandani. Maji hayo sio safi wala salama kwa matumizi ya binadamu mpaka yafanyiwe tiba. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, itafanya utafiti wa namna ya kuchepua sehemu ya maji toka Mto Ruvu (Pangani) na kuyaboresha kwa ajili ya matumizi ya binadamu kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, niishukuru Serikali kwa juhudi ambayo kwa kweli inafanya kusaidia Mji wa Korogwe kupata maji. Lakini kwa kuwa

mradi wa maji wa kutoka Tabora kwa maji ya Mto Ruvu umeanza toka mwaka 1978. Je, Serikali haioni kutokana na hali halisi kwamba mto Ruvu unapita au mto Pangani unapita katikati ya Mji wa Korogwe, suala la mradi huu wakaupa kipaumbele hasa tukitilia maanani kwamba sasa hivi Korogwe imeingia kwenye Mradi wa World wa Bank wa kupata maji na tayari nimeishahamasisha wananchi wa Korogwe wachangie?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba utafiti ulianza toka mwaka 1978 na kwa kweli ulichukua muda mrefu kwa sababu kama tunavyofahamu utafiti unakusanya mambo mengi. Lakini naomba nitumie nafasi hii kwamba tokea mwaka 2001/2002 yeye Mheshimiwa Mbunge alipoamua kulisimamia na kulifuatilia suala hili Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kushirikiana na yeye na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe tumeweza kugharamia maendeleo ya maji hayo ukiwemo uwezekano wa kuchepua maji katika mto huo ambao umeishagharamia shilingi milioni 180. Kwa hiyo, ningeomba wananchi wa Korogwe waendelee kumpa ushirikiano Mheshimiwa Mbunge ili hatua hii aliyoifikia iweze kuendelea mpaka pale tutakapoweza kuyachukua maji ya Mto Ruvu na kuweza kutumika katika Mji huo wa Korogwe. *(Makofi)*

Na. 167

**Miradi ya Maji - Morogoro Kusini Mashariki**

**MHE. LEPHY B. GEMBE (K.n.y. MHE. SEMINDU K. PAWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na wafadhili kama vile TASAF, World Vision, KKKT, Waholanzi na World Bank imefanya kazi kubwa sana ya kusimamia na kufanikisha baadhi ya miradi ya Maji Jimboni Morogoro Kusini - Mashariki kwenye maeneo ya Ngerengere, Mkulazi, Chanyumbu, Selegete A, Kidugallo, Kiloka, Kiziwa, Mkuyuni, Kinole, Kibwaya, Koo, Mkambalani, Lukonde na kadhalika:-

(a) Je, hadi sasa kuna mpango gani wa kuchimba malambo kwenye shamba la *DAFCO* la Ngerengere ili mifugo na wananchi wa Mikobora wanaoshitakiwa mara kwa mara na Meneja wapatiwe huduma ya Maji?

(b) Je, kwa mabomba chakavu kama yaliyoko Koo, Magera, Kiwegene, Pangawe, Kizinga, Serikali itasaidiaje kurudisha mabomba mapya?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuipongeza Serikali pamoja na wafadhili mbalimbali kwa jitihada zao za kufanikisha ujenzi wa miradi ya maji katika Jimbo lake na hasa katika maeneo aliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha shamba la kuzalisha mifugo ya Ngerengere lililokuwa chini ya Kampuni ya uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa *(DAFCO)* katika miaka ya nyuma, kwa kujenga miundombinu mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji wa mifugo. Ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo ni mojawapo ya kazi zinazofanywa hapo shambani kuanzia mwaka 2003/2004. Hadi sasa lambo moja limekarabatiwa na ukarabati wa lambo la pili unaendelea. Aidha, ukarabati wa visima virefu viwili kati ya vinne vilivyopo unaendelea. Ni matarajio yangu kwamba tatizo la maji katika shamba la Ngerengere litatatuliwa katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo mvutano kati ya uongozi wa shamba na wananchi wanaoishi katika vijiji jirani juu ya kuwapatia maji. Tatizo hili limesababishwa na upungufu wa maji katika vijiji hivyo na kutokuwepo utaratibu mzuri wa kuwapatia wananchi hao maji. Uongozi wa shamba umechukua hatua madhubuti za kushauriana na wananchi wa vijiji jirani, kikiwemo kijiji cha Makobora kutatua tatizo hili wakati Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini inatafuta fedha za kujenga malambo na kuchimba visima nje ya shamba kwa ajili ya wananchi hao. Upatikanaji wa maji nje ya shamba utaimarisha uhusiano kati ya shamba na vijiji jirani na kuliwezesha shamba kutekeleza shughuli zake bila kuingiliwa na wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mabomba ya maji katika maeneo ya Koo, Kinege, Pangawe na Kizinga yamechakaa. Napenda kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini kuupa mradi huu kipaumbele na hivyo kuuingiza katika Mpango wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini ambao tayari umeanza kutekelezwa na Serikali katika Wilaya ya Morogoro Vijijini. Pia mifuko ya maji itumike katika kugharamia matengenezo madogo madogo ya mradi.

**SPIKA:** Wahesimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Tunaendelea nina matangazo ya vikao vitatu vya leo vya Kamati.

Kamati ya kwanza ni Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mwenyekiti anaomba niwatangazie Wajumbe Kamati hiyo kuwa kutakuwa na kikao leo saa 11.00 jioni katika ukumbi namba 133. Kamati ya pili ni ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, anawatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 29/6/2005 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika chumba namba 231.

Kamati ya mwisho ni ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anaomba niwatangazie Wajumbe kuwa leo tarehe 29/6/2005 kikao cha Kamati kitafanyika saa 4.30 asubuhi katika chumba namba 227. Mwisho wa matangazo ya

Vikao vya Kamati. Tangazo la Ratiba ya leo. Leo Waheshimiwa Wabunge tunaanza kujadili Wizara ambazo zimepangiwa siku moja moja tu. Kwa hiyo, ratiba itakuwa ni kwamba tutachangia mpaka saa 7.00 mchana na tutaendelea kuanzia saa 11.00 jioni mpaka saa 12.00 hivi. Halafu ndiyo watoa hoja wataanza kuhitimisha hoja zao.

Kwa hiyo, *Chief Whip* wa Serikali ameniomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa wale wanaochangia kwa maandishi ni bora wachangie mapema asubuhi hii ili Mawaziri wapate nafasi ya kujibu michango hiyo ya maandishi. Wakipelekewa mapema inawapa nafasi ya kujibu michango kwa maandishi. Mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2005/2006**
**Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu na marafiki za wabunge wenzetu wafuatao waliotutangulia mbele ya haki Marehemu Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Abubakar Towogale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rahaleo, Marehemu Frank Michael Mussati aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki na Marehemu Margareth Bwana aliyekuwa Mbunge Viti Maalum kutoka mkoa wa Rukwa.

Mchango wa marehemu Wabunge hawa ulikuwa ni wa muhimu sana kwani ulisaidia maendeleo ya majimbo yao na katika kuboresha utendaji wa shughuli za Bunge na Serikali kwa ujumla. Aidha, mchango wa marehemu Frank Mussati kwenye Kamati ya Miundombinu ulisaidia sana katika utendaji wa sekta za mawasiliano na uchukuzi. Nawapa pole pia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Mikoa ya Kusini Unguja, Kusini Pemba na Ruvuma kwa kufiwa na Wenyeviti wa Chama cha Mapinduzi wa Mikoa hiyo. Mwenyezi azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa CCM wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi, kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM pamoja na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuchaguliwa na CCM kuwa mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2005. Nampongeza vilevile Mheshimiwa Balozi

Salim Ahmed Salim mwanadiplomasia, na mzalendo halisi kwa kufikia hatua ya mwisho katika uteuzi wa nafasi ya ugombea Urais kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hotuba ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kutoa hoja za Wizara zao hapa Bungeni. Kwa ujumla hotuba zao zimefafanua utekelezaji wa sera mbalimbali, ukuaji wa uchumi, uimarishaji wa huduma za kijamii na matarajio kwa kipindi cha 2005/2006. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hoja za Wizara zilizotangulia. Hoja na maoni yao yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha hotuba ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda (Mb) na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba (Mb) kwa hotuba zao. Hotuba zao zimeeleza kwa kina hali halisi ya kiuchumi na kifedha hapa nchini kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 na mwelekeo kwa mwaka 2005/2006. Hotuba zao zimefafanua kuwa, pamoja na kwamba sehemu nyingi nchini zilikabiliwa na upungufu wa mvua kwa kipindi hicho, kulikuwa na mafanikio katika shughuli za kimaendeleo. Katika kipindi hiki cha 2005/2006, ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa tunaendeleza mafanikio hayo kwa kusimamia utekelezaji wa mipango yetu kwa kuweka mikakati inayotekelezeka ili tuweze kufikia kiwango bora katika maisha ya kijamii. Tunatarajia kuwa miundombinu ya sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa itaendelea kuboreshwa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itaendelea kusimamia vyombo vyake vya udhibiti, wakala na kampuni za kisekta ili kuhakikisha kuwa zinatoa huduma kwa kuzingatia viwango na gharama zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imefafanua vizuri utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za jamii na hivyo kupunguza kero za wananchi zinazosababishwa na umaskini, ujinga na maradhi. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwa ujumla maendeleo na changamoto zililizopo katika sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa. Baada ya maelezo aliyotoa, jukumu langu leo ni kufafanua kwa kina utekelezaji wa mipango ya maendeleo na mwelekeo katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hali ya kiutendaji ilivyokuwa kwenye sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa kwa kipindi cha 2004/2005, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Robert Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini; kwa ushauri, maoni yao na maelekezo ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza mipango ya kiutendaji katika sekta zetu. Katika kipindi hiki, Kamati ilitembelea miradi na maeneo muhimu ili kuona jinsi sekta zetu zinavyotekeleza majukumu yake.

Kamati ilitembea maeneo yafuatayo: Shirika la Reli Tanzania (Tabora), Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia *(TAZARA)* kutoka Dar es Salaam hadi Mbeya, Karakana ya *TAZARA Mbeya* na Kiwanda cha Kutengeneza Mataruma ya Reli na Kokoto-Mbeya

*(Kongoro Concrete Sleeper Quarry).* Kamati pia ilikagua ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe (Mbeya), Kituo cha Mizigo cha Malawi *(Malawi Cargo Centre-Mbeya),* Magati ya Kasanga (Rukwa), Kinesi, Shirati na Mwigobelo (Mara), Viwanja vya ndege vya Arusha, Moshi, Singida, Tabora, Mwanza, Musoma, Shinyanga na Tanga. Kamati pia ilitembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ambapo ilipata fursa ya kuona Redio Tanzania Dar es Salaam *(RTD), Radio One,* Televisheni ya Taifa (TVT) na *Independent Television (ITV).* Maeneo mengine waliyotembelea ni Chuo cha Usafirishaji (NIT), Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Hali ya Hewa (Tabora). Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ambapo iliona mitambo ya kupima mafuta yanayoingizwa nchini *(Flow Meters).* Kamati ilikagua Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA),* kuona ndege mpya ya Rais ambayo ilizinduliwa rasmi mwezi Oktoba, 2004. Kwa upande wa Tanzania Visiwani, Kamati ilipata fursa kutembelea kisiwa cha Pemba na kuona shughuli za sekta ya mawasiliano na uchukuzi. Baadhi ya shughuli zilizotembelewa ni vituo vya kurushia mawasiliano vya Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* (Utaani-Wete, Kwale na Michakaeni), Ofisi za *ZANTEL*, Posta za Wete na Chakechake, Uwanja wa Ndege wa Karume na Bandari ndogo ya Wete. Kamati ilishauri na kutoa maelekezo ya msingi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha huduma pamoja na miundombinu ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Novemba, 1995 hadi June 2005, Serikali imeendelea kufanya mabadiliko makubwa katika sera ili kutoa miongozo ya kuendeleza sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa nchini kwa lengo la kuboresha huduma zitolewazo na sekta hizo. Ili kutekeleza malengo na majukumu Serikali iliandaa na kupitisha sera zifuatazo:-

(i) Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu (1997);
(ii) Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2002);
(iii) Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2003); na
(iv) Sera ya Taifa ya Posta (2003).

Ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa nchini, katika kipindi hiki Serikali ilianzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* 1999, Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA) 2003,* Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* 2004, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA) 2005,* Wakala wa Hali ya Hewa *(TMA) 1999,* na Wakala wa Ndege za Serikali (*TGFA) 2003.* Aidha, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iliridhia mikataba na makubaliano mbali mbali ya kimataifa na ushirikiano ya kikanda. Mikataba na makubaliano haya yanahusu sekta ndogo za usafiri wa majini, usafiri wa anga, usafiri wa nchi kavu, mawasiliano ya posta na simu na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya usafiri wa anga iliendelea kukua katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005. Ukuaji wa huduma hiyo ulitokana na udhibiti mzuri na usimamzi unaofanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA),* uboreshaji wa viwanja vya ndege unaosimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* pamoja na

huduma za usafiri wa anga zinazotolewa na kampuni za ndege za *ATCL, Precision Air* na kampuni nyingi za kukodi *(charter)* na mashirika ya ndege ya nchi za nje.

Mheashimiwa Spika, Ushiriki wa sekta binafsi kwenye utoaji wa huduma za usafiri wa anga umeongezeka. Katika kipindi cha 1995 hadi 2004, safari za ndege ndani na nje ya nchi ziliongezeka kutoka safari 80,637 mwaka 1995 hadi safari 137,298 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 70. Idadi ya abiria wa ndani na nje, iliongezeka kufikia 1,521,191 mwaka 2005 ikilinganishwa na abiria 773,290 waliosafirishwa mwaka 1995 sawa na ongezeko la asilimia 97. Ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya viwanja vya ndege na mitambo mbalimbali vimechangia ongezeko hilo. Katika kipindi hicho pia kumekuwepo na ongezeko la leseni zilizotolewa kwa kampuni za ndani na nje za kutoa huduma za usafiri wa ndege nchini. Jumla ya Kampuni hizo imefikia 30 kwa mwaka 2004 ikilinganishwa na 13 mwaka 1999. Aidha, kununuliwa kwa rada ya kisasa mwaka 2002 inayotoa huduma katika viwanja vya ndege kwa saa 24 kumeongeza ufanisi katika huduma za usafiri wa anga nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usafiri wa anga, vifaa na mitambo ya kisasa ya kuongozea ndege vimefungwa katika viwanja vya Zanzibar, Arusha, Mwanza na Mtwara. Aidha mitambo ya mionzi ya jua kwa ajili ya kuboresha nguvu za umeme ilifungwa katika viwanja vya Kigoma, Mtwara, Songea na Zanzibar. Serikali ilinunua magari 11 ya kisasa ya zimamoto ambayo yamewekwa katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Arusha, Kigoma, Tabora, Shinyanga na Mtwara. Ili kudhibiti usalama katika viwanja vya ndege, Serikali iliimarisha ukaguzi wa ndege na hivyo kupunguza matukio ya ajali za ndege kutoka 28 mwaka 1995 hadi kufikia 10 kwa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kuhudumia Mizigo *(DAHACO)* inatoa huduma za abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya Dar es Salaam na Kilimanjaro. Katika kipindi cha mwaka 2004, idadi ya abiria, ndege na mizigo iliyohudumiwa iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 1999. Jumla ya abiria 554,000 wa ndani na nje walisafirishwa kutoka Dar es Salaam kwa mwaka 1999 ikilinganishwa na abiria 1,426,000 waliosafirishwa mwaka 2004. Wakati huo huo katika kipindi cha mwaka 1999, jumla ya tani 10,705 za mizigo zilihudumiwa ikilinganishwa na tani 17,124 zilizohudumiwa mwaka 2004. Aidha, *DAHACO* ilikamilisha ujenzi na kuzindua majengo ya kutoa huduma za kuhifadhi bidhaa katika ubaridi *(cold storage facilities)* kwa viwanja vya ndege vya Kilimanjaro mwaka 1999 na Dar es Salaam mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 hadi 2005 matengenezo makubwa yalifanyika katika viwanja vya Musoma, Tabora, Bukoba, Zanzibar, Shinyanga, Lindi, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Mtwara, Mwanza na Kigoma. Serikali inaendelea na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe mkoani Mbeya kitakachokuwa na uwezo wa kupokea ndege kubwa aina ya *Boeing 737.* Hatua hiyo itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi nchini hususan katika kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua madhubuti za kuhakikisha kuwa usalama unaimarishwa hasa kwenye viwanja vyote vikubwa nchini. Hatua hizo ni pamoja

na kuvijengea viwanja hivyo uzio na kuweka ulinzi wa saa 24, kuweka vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na rada ili kuimarisha usalama angani, kuongeza mashine za *X-ray* na vifaa maalum vya mionzi kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo na abiria, kamera maalum za kuchunguza mienendo ya watu katika majengo ya abiria na kuweka chombo cha kutambua mabomu.

Ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika viwanja vya ndege nchini, viwanja 25 kati ya 63 vya ndege vimepimwa na kati ya hivyo nane (8) vimepata hati miliki. Viwanja hivyo ni Dar es salaam, Kilimanjaro, Arusha, Moshi, Tanga, Musoma, Kigoma na Bukoba. Upatikanaji wa hati miliki utasaidia kuzuia wananchi kuvamia maeneo ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 mpaka 2005, sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo katika nchi yetu. Miundombinu na huduma ya uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarishwa kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi. Uboreshaji huo umeongeza ushindani mkubwa miongoni mwa watoa huduma na hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za uchukuzi. Kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kutoa huduma, Serikali itaendelea kushirikiana nao pale inapowezekana kwa lengo la kuboresha usafiri mikoani na vijijini.

Aidha, Serikali imeingia mikataba ya makubaliano *(Bilateral Road Transport Agreements)* kati yake na Malawi, Zimbabwe, Zambia mwaka 2000. Rasimu ya mkataba kati ya Tanzania na Msumbiji imekamilika na Mkataba utasainiwa mwezi Julai 2005.*(Makofi)*

Mheshimikwa Spika, huduma za usafiri wa reli nchini na nchi jirani zimeendelea kutolewa na Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA).* Katika kipindi cha 1995 hadi 2005 Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha reli hizo. Kwa upande wa *TRC*, Serikali ilipata msaada kutoka Benki ya Dunia chini ya Programu ya Marekebisho ya Reli. Serikali imeendelea kukarabati na kuimarisha njia, injini za reli na mabehewa ya mizigo na abiria. Njia ya Manyoni hadi Singida imeendelea kuimarishwa ambapo kilometa 92 zimewekwa kokoto na kilometa 40 za reli zimebadilishwa kutoka uzito wa paundi (lbs) 40 kwa yadi kufikia paundi 56. Sehemu ya kugeuzia treni kwenye stesheni ya Singida na tuta la reli lenye urefu wa kilometa 40 limeimarishwa. Serikali imepata msaada wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kukarabati kilometa 197 za reli zilizochakaa na kuwekwa mpya zenye uzito unaokidhi mahitaji kati ya stesheni za Kitinku hadi Makutupora, Itigi hadi Malongwe, Igalula hadi Tabora, na Tabora hadi Mabama. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati wa njia ya reli kati ya Kaliua na Mpanda.

Mheshimikwa Spika, jumla ya madaraja 31 yalifanyiwa ukarabati. Kati ya hayo, 9 yapo kati ya Tabora na Kaliua; na Tabora na Mwanza. Madaraja mengine 13 yapo kati ya Manyoni naTabora na 9 yapo kati ya Bahi na Makutupora. Uimarishaji wa madaraja na njia za reli, umeongeza ufanisi na kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali katika njia ya reli ya kati. Awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa njia za mawasiliano kati ya Dar es

Salaam, na Morogoro, na Morogoro hadi Dodoma kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya *optic fibre* ulikamilika mwaka 2001. Awamu ya tatu ya ujenzi wa njia ya mawasiliano katika reli kati ya Dodoma na Tabora yenye urefu wa kilometa 383, imeanza kutekelezwa. Uwekaji wa alama katika njia za reli kutoka Manyoni hadi Singida umekamilika. Injini 63 za treni zilifanyiwa matengenezo na mabehewa 469 ya mizigo na 48 ya abiria yalikarabatiwa. Hatua hizo zimeongeza uwezo wa uchukuzi wa Shirika katika kukidhi mahitaji ya usafirishaji ambayo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha kuanzia 1995 hadi 2004 jumla ya abiria 6,747,277 walisafirishwa na mizigo tani 11,145,381 ilisafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TAZARA* karakana ya matengenezo ya vichwa vya treni ya Mbeya iliimarishwa. Kiwanda cha kutengeneza mataruma ya reli kilichopo Igurusi Mbeya *(Kongoro Concrete Slipper Quary)* kilijengwa. Aidha, vifaa vya kupakua na kupakia mizigo vimesimikwa katika stesheni za Dar es Salaam na Makambako kwa upande wa Tanzania na Kasama na *New Kapiri Mposhi* kwa upande wa Zambia. Katika kipindi hicho, *TAZARA* imeweza kusafirisha kiasi cha tani milioni 6.8 za mizigo na abiria milioni 13.0. Kituo cha kupakia na kupakua mizigo katika reli za *TAZARA* na *TRC* kilichopo Kidatu, kimeimarishwa na hivyo kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka na kwenda nchi za kusini mwa Afrika na za Maziwa Makuu kupitia reli hizo. Aidha, ili kukabiliana na wizi wa nyaya za kuwezesha mawasiliano, mwaka 2000 TAZARA ilibadilisha mfumo wa mawasiliano kutoka wa kutumia nyaya za shaba na kutumia teknolojia iitwayo *Digital Microwave Radio (DMR)* kwa msaada wa Serikali ya China. Mradi huu ulianzia sehemu ambazo zilikuwa na matukio mengi ya wizi wa nyaya. Sehemu hizo ni kati ya stesheni za Dar es Salaam na Kidunda zenye umbali wa kilomita 120. Inategemewa kwamba mradi huu wa Digital Microwave Radio utakamilika katika kipindi cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Usafirishaji wa majini umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni uchukuzi baharini, huduma za bandari na uchukuzi katika maziwa. Uchukuzi wa baharini umekuwa ukiendeshwa na kampuni za meli kutoka nje ya nchi na kwa kiasi kidogo kampuni za ndani ya nchi. Huduma za bandari zinatolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Uchukuzi katika maziwa unaendeshwa na Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* na kampuni binafsi. Serikali imefanya juhudi za kuimarisha na kuboresha miundombinu ya huduma ya usafiri majini na kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha sekta binafsi kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia 1995 hadi 2005 Serikali ilifanya jitihada za kuboresha huduma za usafiri wa majini katika bandari za Dar es salaam, Tanga, na Mtwara. Kuhusu Bandari ya Dar es salaam, Serikali imeboresha lango la Bandari ya Dar es salaam na kufikia upana wa meta 120 na kina cha meta 10.2 na kunyoosha kingo kuwezesha meli kubwa za uzito wa tani 40,000 kuingia na kutoka bandarini kwa saa 24. Uboreshaji huo umeipandisha hadhi bandari na umechangia ongezeko la ufanisi na tija kwa ujumla na hivyo kuongeza idadi ya meli bandarini kutoka meli 962 kwa mwaka 1995 na kufikia meli 1,256 mwaka 2005. Jitihada nyingine ni kupanuliwa kwa Gati la Mafuta la Kurasini *(KOJ)* na kuwekwa kwa vifaa muhimu vya kupakua mafuta na vifaa vya kupambana na moto ambavyo vimeongeza kasi ya upakuaji wa mafuta na usalama wa bandari na kuwezesha meli kubwa zaidi kutia nanga.

Idadi ya meli imeongezeka baada ya kupanuliwa kwa lango la Bandari ya Dar es Salaam, viwango vya utoaji wa huduma vimeboreshwa. Kubinafsishwa kwa Kitengo cha Kontena cha Bandari ya Dar es salaam mwaka 2000 kumeongeza ufanisi katika kushughulikia mizigo bandarini hapo. Katika kitengo hicho muda wa kuhudumia meli umepungua kutoka wastani wa saa 24.2 mwaka 1995, hadi saa 19.1 mwaka 2004. Aidha, tija imeongezeka kwa asilimia 64 kutoka kuhudumia kontena 14 kwa saa mwaka 1995 hadi kontena 23 kwa saa mwaka 2004. Kitengo hicho kinahudumia kontena 23 kwa saa ikilinganishwa na Bandari ya Durban, Afrika Kusini ambayo inahudumia kontena 16 kwa saa na Bandari ya Mombasa, Kenya ambayo inahudumia kontena 10 kwa saa. Katika kitengo cha mizigo ya kawaida *(General Cargo),* muda wa meli wa kusubiri kuhudumiwa umeshuka kutoka wastani wa saa 28.5 mwaka 1995 hadi saa 7.1 mwaka 2004. Aidha, muda wa kuhudumia meli umepungua kutoka wastani wa saa 124 hadi saa 96 wakati muda wa meli kukaa bandarini umeshuka hadi saa 103.1 mwaka 2004 ikilinganishwa na saa 153.4 mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Mtwara, hatua iliyochukuliwa ni kuiboresha kwa lengo la kuiandaa kuhudumia shehena inayotarajiwa kuongezeka kufuatia mradi kabambe wa kitaifa wa kuendeleza ukanda wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor).* Bandari ya Mtwara imepanua eneo lake kwa kuongeza eneo la kuwekeza kwa shughuli za bandari, viwanda na shughuli za biashara *(EPZ). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine katika usafirishaji majini ni katika uchukuzi wa mizigo na abiria, ulinzi na usalama na utunzaji wa mazingira ya bahari. Kutokana na kuimarishwa, kumekuwepo na ongezeko la mizigo inayohudumiwa katika bandari zetu. Jumla ya tani 5,375,746 zilihudumiwa mwaka 2004 ikilinganishwa na tani 4,663,497 zilizohudumiwa mwaka 1995 sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Kwa upande wa usafirishaji wa abiria, kumekuwepo na ongezeko la abiria wanaotumia meli na boti kati ya Bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar na kati ya Dar es Salaam na bandari za Mtwara na Lindi. Jumla ya idadi ya abiria waliohudumiwa katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ulifikia 733,735 kwa mwaka 2004 ikilinganishwa na abiria 667,771 kwa mwaka 1995. Changamoto tuliyo nayo ni kuweka mazingira mazuri ili kuwavutia wasafirishaji watumie bandari ya Dar es Salaam ili uwezo wa bandari hiyo wa kuhudumia mizigo ya tani milioni 10 kwa mwaka ufikiwe.

Mheshimiwa Spika, idadi ya kampuni za simu iliongezeka kutoka kampuni 2 mwaka 1995 hadi kufikia 7 kwa mwaka 2004. Kati ya kampuni hizo, moja inatoa huduma za simu za msingi, nne zinatoa huduma za simu za mkononi kupitia mtandao uliojengwa ardhini na mbili zinatoa huduma za simu za mkononi kupitia satelaiti. Katika jitahada za Serikali za kuleta mabadiliko katika sekta ya Mawasiliano, idadi ya njia za simu zilizounganishwa imeongezeka kutoka 90,198 mwaka 1995 hadi 2,090,360 Desemba 2004. Idadi ya wateja wa simu za mkononi zilizounganishwa imeongezeka kutoka 2,198 mwaka 1995 hadi kuifikia 2,480,000 Mei 2005 na simu za msingi ziliongezeka kutoka 88,000 mwaka 1995 hadi kufikia 153,265 Mei 2005. Uwezo wa simu za msingi *(exchange capacity)* uliongezeka toka njia 182,379 mwaka 1997 hadi kufikia 234,887 Desemba 2004.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma za mawasiliano kwa njia ya Posta, zimeongezeka kutokana na ongezeko la kampuni zinazotoa huduma hiyo. Idadi ya posta zinazoendeshwa na wakala wa Shirika la Posta, imeongezeka kutoka 46 mwaka 1996 hadi wakala 93 mwaka 2004. Posta kamili zenye kutoa huduma zote za kiposta nchini zimefikia 199. Jamii habari ni mfumo wa maisha ambao jamii ina haki na uwezo wa kuwasiliana, kujifunza, kupashana habari bila vikwazo kupitia mtandao wa teknolojia ya mawasiliano. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano mwaka 2003, yenye lengo la kufanikisha jamii habari.

Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, imeratibu ujenzi wa vituo vinane vya mawasiliano nchini kati ya mwaka 1999 na 2004. Vituo hivyo ni pamoja na T*anzania Global Distance Learning Centre (TGDLC)* mkoani Dar es Salaam; Sengerema Telecenter mkoani Mwanza, Ngara *UNHCR Telecentre* mkoani Kagera, Wino Telecentre kwa ajili ya wakulima wa kahawa mkoani Ruvuma; Multipurpose Telecentre, Kinampanda mkoani Singida; na Mpwapwa mkoani Dodoma. Aidha, Kituo cha Intaneti cha Kasulu mkoani Kigoma nacho kimeanzishwa. Vituo hivyo vinatumiwa na jamii kwa ajili ya biashara, masomo, afya, utawala na uendeshaji wa shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi. Changamoto kwetu ni kuhakikisha kuwa huduma hizi zinaenea kote nchini na zinatumiwa kikamilifu. Vituo vya intaneti vimeongezeka toka chini ya vituo 10 mwaka 1995 kufikia zaidi ya vituo 500 Desemba 2004.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha huduma za hali ya hewa nchini. Hadi kufikia mwaka 2004 Serikali imejenga vituo vinne vikubwa vya hali ya hewa na hivyo kuongeza idadi ya vituo kufikia 26 ikilinganishwa na vituo 22 vilivyokuwepo mwaka 1995. Ongezeko hilo limeisadia Mamlaka ya Hali ya Hewa kupata taarifa kuhusu hali ya hewa kutoka sehemu mbalimbali nchini. Vituo 14 vya kupima hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe vimeanzishwa. Hivi sasa Mamlaka ina uwezo wa kupata taarifa ya hali ya hewa kutoka katika vituo vyake vya Morogoro, Iringa, Songea, Mbeya, Sumbawanga, Kigoma, Tabora, Dodoma, Mwanza, Musoma, *Kilimanjaro International Airport (KIA),* Moshi, Arusha, Pemba, Zanzibar, Mtwara, Bukoba, Same, Shinyanga, Mahenge, *Dar es Salaam International Airport (DIA),* Tanga, Bandarini Dar es Salaam, Handeni, Kilwa Masoko na Singida.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa ziliendelea kuimarisha utoaji huduma kutokana na uboreshaji wa miundombinu. Utendaji wa sekta hizi umeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kupunguza Umaskini, Sera ya Usimamizi wa Mazingira, pamoja na zile za sekta za Mawasiliano na Uchukuzi. Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika kurekebisha mifumo ya uendeshaji ya sekta ili kuongeza ufanisi na kuondoa kero zinazowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliadhimisha kwa mara ya pili Wiki ya Uchukuzi ambapo kila Mkoa uliandaa maonyesho na shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta ya uchukuzi. Kitaifa Wiki ya Uchukuzi iliadhimishwa Dar es Salaam na kufikia kilele chake tarehe 15 Oktoba 2004. Madhumuni makubwa ya wiki hii

ni kuwafahamisha wadau wa sekta na wananchi kwa ujumla kuhusu sera, mikakati, programu, dira na dhamira zinazosimamia utendaji wa sekta hizo na huduma zitolewazo kwa wananchi. Mengine ni kuwafahamisha wananchi kuhusu utendaji wa sekta, mafanikio, mapungufu na changamoto zilizopo katika utoaji wa huduma za sekta. Midahalo, maonyesho na mijadala mbalimbali ilifanyika ili kuwapa fursa wanachi kutoa maoni na ushauri kuhusiana na utendaji wa sekta ya uchukuzi. Aidha, wakati wa maadhimisho ya wiki hiyo mwaka 2004, matukio mbali mbali yanayohusu sekta ya uchukuzi yalifanyika. Matukio hayo ni pamoja na uzinduzi wa ndege mpya ya Serikali, na huduma za kuhifadhi bidhaa katika ubaridi *(cold storage facilities)* katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam. Wizara iliendelea kutoa Jarida la Uchukuzi *(Transport Bulletin)* ambalo ni mojawapo ya njia za kuwafahamisha wadau na wananchi masuala yanayohusu sekta ya uchukuzi nchini. Jarida hili hutolewa kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri mijini ikiwemo Jiji la Dar es Salaam, imeendelea kuboreshwa ili kupunguza kero za usafiri kwa wananchi. Serikali inaendelea na taratibu za kulibinafsisha Shirika la Usafiri Dar es salaam *(UDA)* ili kuliimarisha liweze kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi. Hivi sasa Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* inafanya utaratibu wa kuiuzia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam hisa za Serikali kwenye shirika hilo. Aidha, jitihada za kuongeza idadi ya mabasi zinaendelea ili kuimarisha shughuli za Shirika na hivyo kuweza kuhimili ushindani uliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha huduma za usafiri Jijini Dar es Salaam. Juhudi hizo ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi *(Bus Rapid Transit - BRT).* Mwezi Machi, 2005 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilisaini mkataba na kampuni iitwayo *M/s LOGIT ENGENHARIA CONSULTIVA* ya Brazil. Kampuni hiyo ya ushauri (Consultant) inafanya upembuzi yakinifu (feasibility study) wa mradi huo. Kulingana na taratibu za utekelezaji, mradi una kanda sita (6) nazo ni; ukanda wa barabara ya Morogoro unayoihusisha njia ya Ubungo-Mwenge, ukanda wa barabara ya Mandela na ukanda wa Kilwa. Kanda nyingine ni ukanda wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi, ukanda wa barabara ya Kawawa, na ukanda wa barabara ya Nyerere. Kwa kuanzia, Kampuni ya ushauri inafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina *(detailed design)* kwa ukanda wa barabara ya Morogoro. Inatarajiwa kuwa mradi utakamilika baada ya miaka miwili. Utekelezaji wa mradi huu utatoa mwelekeo wa utekelezaji wa aina ya usafiri wa aina hii kwa miji mengine mikubwa nchini. Mashirika ambayo yameshathibitisha kugharamia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi huo ni Benki ya Dunia, *USAID, GEF, UNDP na ITDP.* Tunazishukuru asasi hizo kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuendeleza na kuboresha huduma za usafiri katika Jiji la Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilikuwa inaendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha chombo cha kusimamia Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA).* Napenda kutoa taarifa kuwa taratibu hizo zimekamilika. Mamlaka hii imeanza kazi rasmi mwezi Januari, 2005. Aidha, Baraza

la Watumiaji *(Consumer Consultative Council)* la *SUMATRA* limeanzishwa chini ya Uenyekiti wa Ndugu Said El Maamry. Jukumu kubwa la Baraza hili ni kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa usafiri wa reli, barabara, na majini. Bodi ya Mamlaka hiyo pia imeteuliwa chini ya uenyekiti wa Ndugu Peter C. Bakilana aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa mashirika yaliyo chini ya Wizara yakiwemo *THA, NTC* na *TRC.* Kwa mujibu wa Sheria hiyo bodi hiyo ina wajumbe sita (6). Mtendaji Mkuu wa *SUMATRA* ameshateuliwa ambaye ni Bwana Israel Zakayo Sekirasa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa lililokuwa Shirika la Kudhibiti Shehena nchini *(TCFB).*

Ni matumaini yangu kuwa chombo hiki kitatekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa wakati huu ambapo kuna ushindani mkubwa katika usafiri wa majini na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya mbalimbali ikiwemo ya Afrika Mashariki *(EAC)* na ile ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Katika kipindi cha 2004/2005 Wizara ilishiriki kwenye mikutano ya *SADC* ukiwepo ule wa Wakuu wa nchi za *SADC* uliofanyika nchini Mauritius. Katika mikutano hiyo, Wizara ilitoa taarifa ya utekelezaji wa masuala ya ushirikiano na majukumu yanayohusu sekta zetu za Mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa. Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na utekelezaji wa programu za kisekta ikiwemo uimarishaji wa miundombinu na utoaji huduma za posta, simu, usafiri wa anga, majini, reli na barabara. Wizara pia ilishiriki katika mkutano wa nchi za maziwa makuu uliofanyika nchini mwaka huu ambapo shughuli za uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu na matumizi ya rasilimali za kwenye maziwa yetu zilisisitizwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)* Wizara pia imeendelea kutekeleza miradi na shughuli mbalimbali zinazohusu utoaji huduma za usafiri wa reli, barabara, majini, anga, huduma za mawasiliano na hali ya hewa. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kuboresha uchukuzi na usalama katika Ziwa Victoria. Miradi mingine ni mapendekezo ya kufanya upembuzi *(study)* wa Ujenzi wa Reli ya Arusha hadi Musoma na mapendekezo ya kufanya upembuzi wa uwezekano wa kituo Kikuu kimoja cha kuongoza ndege katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwa mratibu wa sekta za miundombinu chini ya Mpango Mpya wa Ushirikiano na Maendeleo ya Umoja wa Afrika *(NEPAD)* na imeshakamilisha mapendekezo ya awali ya miradi kwenye maeneo muhimu yaliyobainishwa. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kwamba miradi hiyo imewasilishwa kwenye Sekretariati ya *NEPAD* kwa hatua zinazofuata. Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zinaendelea. Inatarajiwa kuwa miradi hiyo ikikamilika itaimarisha miundombinu hivyo kuboresha huduma za usafiri wa majini, barabara, anga na mawasiliano. Kati ya miradi iliyopendekezwa kitaifa, ujenzi wa daraja la umoja kati ya Tanzania na Msumbiji umeanza baada ya nchi hizi mbili kusaini makubaliano ya utekelezaji wake. Utekelezaji wa miradi mingine utaanza kulingana na ratiba na masharti mengine ikiwemo upatikanaji wa fedha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mawasiliano kati ya Wizara na Benki ya Dunia ya kumpata mtaalamu mwelekezi

*(Consultant)* atakayeishauri Wizara katika kutekeleza Programu ya miaka kumi ya Uwekezaji katika sekta ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Program).* Nafurahi kutoa taarifa kwamba mtaalamu huyo amekamilisha kazi hiyo na hivi sasa Wizara imekamilisha Rasimu ya Programu hiyo ambayo sasa inajadiliwa na wadau mbalimbali kwa nia ya kuiboresha. Ni matumaini yetu kuwa Programu hii itakuwa mhimili wa maendeleo ya sekta ya uchukuzi katika kuimarisha miundombinu ya uchukuzi pamoja na kuboresha hali ya usafiri nchini. Programu hii inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai 2006.Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara kwa kushirikiana na *PSRC* iliendelea na zoezi la kuratibu ubinafsishaji wa Mashirika na asasi zilizoko kwenye sekta. Kwa upande wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kukamilisha taratibu za kumpata atayekodi huduma za *TRC.* Inatarajiwa kwamba taratibu za kumpata atakayekodi zitakamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kuirekebisha *TAZARA,* Serikali za Zambia na Tanzania ziliunda Kamati ya pamoja *(Task Force)* chini ya taasisi zinazohusika na ubinafsishaji kwa kila nchi. Aidha, Kampuni ya *M/s PriceWaterHouseCoopers* iliyoteuliwa kuwa Mtaalam Mwelekezi *(Consultant)* wa kushauri namna ya kufanikisha utekelezaji wa zoezi hilo ilikamilisha kazi na kutoa ripoti kwa Serikali za Tanzania na Zambia mwezi Desemba, 2004. Ripoti hiyo ilijadiliwa na wadau wa pande zote mbili. Baada ya maoni ya wadau kujumuishwa, mshauri mwelekezi amekamilisha ripoti ambayo hivi sasa inafanyiwa kazi na wataalam wa Serikali zetu mbili. Aidha katika hatua za kufanikisha zoezi la kuibinafsisha *TAZARA,* Serikali za Tanzania na Zambia kwa pamoja zitajadiliana na China ili kuona uwezekano wa Wachina kuingia ubia katika uendeshaji wa *TAZARA.* Mwaka 2004 wametoa mkopo nafuu wa Yuan milioni 80 sawa na dola za kimarekani milioni 10 kuisaidia *TAZARA.* Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa misaada yao wanayoendelea kutupatia tangu wakati wa ujenzi wa reli hii hadi kipindi hiki ambapo *TAZARA* iko kwenye hatua za marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la ubinafsishaji wa vitengo vilivyobaki vya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* baada ya kitengo cha Kontena kubinafsishwa. Mkakati wa ukodishaji uliokubalika ni kuwa TPA itamiliki na kuendesha bandari zote nchini zikiwemo zile za maziwa kwa mfumo wa *Landlord Port Model. TPA* ilianzishwa rasmi na Sheria ya Bandari Tanzania *(Tanzania Ports Act, 2004)* ambayo ilifuta Sheria ya Mwaka 1977 iliyoanzisha Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA).* Kulingana na Sheria ya Bandari 2004, TPA ina uwezo wa kumiliki, kuendesha na kuendeleza bandari za mwambao na za maziwa na vitengo vya bandari ambavyo havitakodishwa. Kwa hivi sasa, zoezi la kuvibinafsisha vitengo vilivyobaki, linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli *(Marine Services Company Limited)* mkakati uliokubalika wa kubinafsisha Kampuni hii ni kuwa huduma katika kila ziwa zitabinafsishwa kipekee. Zoezi la kuunda kampuni kwa kila ziwa (Nyasa, Tanganyika na Victoria) kwa ajili ya ubinafsishaji wa Kampuni ya Huduma za Meli linaendelea na linatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha usafiri kwa njia ya reli, Serikali za Tanzania na Rwanda zilitiliana saini makubaliano ya kuendeleza ukanda wa kati wa maendeleo kwa lengo la kutekeleza miradi ya pamoja *(An Agreement on the Central Development Corridor).* Makubaliano haya yalisainiwa mwezi Januari 2005. Kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya Isaka hadi Kigali ambao uko katika ukanda huu, makubaliano ya awali *(MOU)* kati ya Tanzania na Rwanda yalitiwa saini Januari 2004. Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* imekubali kutoa fedha *UA* milioni 1.66 sawa na Dola za Kimarekani milioni 2.5 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study).* Hivi sasa Serikali za Tanzania na Rwanda zinaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha hizo baada ya kusaini itifaki husika. Utayarishaji wa hati za zabuni za kumpata mtaalam mwelekezi tayari zimewasilishwa *ADB* ili kupata maoni yao. Kazi ya upembuzi yakinifu itaanza mwezi Januari 2006.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara imeendelea kupitia Makubaliano ya Usafiri wa Anga *(Bilateral Air Services Agreements)* kati ya Tanzania na nchi mbalimbali. Lengo la makubaliano hayo ni kuyawezesha mashirika ya ndege ya Tanzania na nchi hizo kutoa huduma za usafiri wa anga katika mazingira ya ushindani na hivyo kumnufaisha mtumiaji wa huduma hizo. Katika kipindi hicho Tanzania ilitia saini Makubaliano ya Usafiri wa Anga kati yake na Serikali ya Uingereza na kupitia Makubaliano kati yake na Serikali za Ethiopia, Msumbiji, Rwanda na Zambia. Aidha mnamo mwezi Mei, 2005 Serikali ilifanya mazungumzo ya awali na Serikali ya Kifalme ya Thailand kwa lengo la kuanzisha mkataba mpya kati ya nchi hizo. Wizara inafanya juhudi za kuhakikisha kuwa maelekezo ya Sera ya Uchukuzi yanatekelezwa kwenye mikataba iliyopo, na wakati wa kuanzisha mikataba mipya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuzingatia ipasavyo suala la usalama wa usafiri wa anga hasa kwa kufuatia matukio ya kigaidi yanayozidi kutokea kote duniani. Suala hili linatiliwa maanani wakati wa kufanya mapitio na kuanzisha makubaliano mapya ya usafiri wa anga na nchi nyingine. Aidha, katika kutekeleza matakwa ya sheria za usalama wa usafiri wa anga, mwezi Agosti, 2004, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)* lilifanya ukaguzi wa mipango ya usalama *(Airport Security arrangements)* na programu ya usalama *(Civil Aviation Security Programme)* katika Kiwanja cha Kimataifa cha Dar es salaam.

Lengo la ukaguzi huo lilikuwa ni kutathmini jinsi nchi yetu inavyotekeleza viwango vya kimataifa vya usalama wa anga na viwanja vya ndege (aviation security) kwa lengo la kuzuia, kukabiliana na kuondoa kabisa vitendo vya kigaidi kwenye huduma za usafiri wa anga. Baada ya ukaguzi huo *ICAO* ilitoa ripoti na *TCAA* tayari imeandaa ratiba ya urekebishaji wa mapungufu yaliyobainika. Ukaguzi huo umeisadia Wizara kutambua kasoro zilizopo kwenye kiwanja hicho. Wizara inaendelea na urekebishaji wa mapungufu yaliyojitokeza ili kuimarisha hali ya usalama kwenye sehemu husika. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuwavutia wawekezaji na watalii kuja nchini pamoja na kuwahakikishia wananchi wetu usalama wa usafiri wa anga hivyo kuwajengea imani katika usafiri huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kutekeleza sheria mpya *(Tanzania Civil Aviation Authority Act, 2003)* iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Kulingana na sheria hii, Mamlaka ina uwezo zaidi wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini kulingana na viwango vya kimataifa kama ilivyoainishwa *ICAO*. Uteuzi wa Bodi ya Mamlaka chini ya Uenyekiti wa Ndugu Mwamtumu Malale umekamilika. Uteuzi wa Baraza la Watumiaji *(Consumer Consultative Council)* chini ya Uenyekiti wa Dr Charles Vivian Mpinga Mgana, lenye wajumbe saba, ambalo linawawakilisha watumiaji wa huduma za usafiri wa anga nao umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/05, Mamlaka iliendelea kusimamia Mfuko wa Usalama wa Anga *(Aviation Security Fund).* Mfuko ulianzishwa mwaka 2002/2003 kwa nia ya kuboresha usalama viwanjani ili kukabiliana na matukio ya ugaidi. Mfuko huu umeweza kununua vifaa na kutoa mafunzo kwa maofisa usalama wa viwanja vya ndege na anga. Mafunzo yataendelea kutolewa pamoja na kununua mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo *(X ray machine)* kwa kiwanja cha Mwanza. Serikali inaangalia njia bora za kuendeleza mfuko huu ili kuendelea kuboresha usalama wa viwanja vyetu vya ndege nchini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kupata msaada wa utalaam na mafunzo yanayotolewa na Serikali ya Marekani chini ya mradi wa *Safe Skies for Africa Initiative*. Mradi huu ulianzishwa na aliyekuwa Rais wa Marekeni, Bill Clinton mwaka 1998 kwa lengo la kuimarisha usalama wa anga endelevu na kujenga mazingira ya kukuza ukuaji wa huduma za usafiri wa anga kati ya Afrika na Marekani. Serikali ya Uingereza pia ilitoa msaada kuchunguza mianya inayoweza kutumiwa na magaidi na kutoa mafunzo kwa vyombo vyetu vya usalama katika Mamlaka na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kuhusu kuanzishwa kwa kituo cha pamoja cha nchi za Afrika Mashariki cha kuongozea ndege, utafutaji wa ndege zilizopata ajali *(Search and Rescue co-ordination services),* ramani *(AIS MAP facilities and services)* na mradi wa matumizi ya vyuo vya mafunzo (East Africa Civil Aviation Safety Project). Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huu unatekelezwa kwa msaada wa kiufundi kutoka Serikali ya Marekani. Aidha, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo *(Harmonized Safety Oversight)* uliendelea katika kipindi cha 2004/2005. Katika awamu hii, nchi za Afrika ya Mashariki zimeweza kupitia sheria za usalama wa anga kwa lengo la kuziboresha na kuzifanya ziwe linganifu ili kutekeleza ibara ya 92 ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wa kuongeza ushirikiano katika matumizi ya rasilimali na watalaam.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kituo cha Udhibiti na Kuongoza Ndege Katika Anga la Eneo la Nchi za *SADC (SADC Upper Air Space Control Centre)* unaendelea kutekelezwa. Mkandarasi aliyepewa kazi ya utafiti wa mradi huu anaendelea vizuri na juhudi zinafanywa ili kazi hiyo iweze kukamilika ifikapo Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuboresha uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini, Wizara iko katika hatua za kufanya uchambuzi wa kubaini njia mbalimbali zinazofaa katika kuishirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa viwanja vya ndege. Kwa hivi sasa Wizara imekamilisha uchambuzi wa namna bora na sahihi ya kuishirikisha sekta binafsi kwa kuifanyia mapitio sheria ya muundo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi ziliendelea kutolewa kwa ufanisi na Kampuni ya ndege Tanzania *(ATCL)* na Kampuni binafsi ikiwa ni pamoja na Precision Air. Hivi sasa *ATCL* imepanua huduma zake katika miji ya Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Johannesburg, Entebbe na Hahaya. Katika kipindi cha 2004/2005, *ATCL* ilisafirisha abiria 217,261 mwaka 2003/2004 ikilinganishwa na abiria 84,000 mwaka 2002/03. Precision Air ilisafirisha abiria 314,720 ikilinganishwa na abiria 248,375 mwaka 2002/2003; sawa na ongezeko la asilimia 27.

Aidha, Kampuni ya Precision Air imeongeza huduma zake na sasa inatoa huduma katika miji ya Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kigoma, Mtwara, Tabora, Shinyanga na Zanzibar. Kampuni pia inatoa huduma kwenye miji ya Nairobi, Mombasa na Johannesburg. Kutokana na kukua kwa biashara, Kampuni hiyo imehamisha makao makuu yake kutoka Arusha kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba baada ya kulibinafsisha Shirika la ndege nchini *(ATC)* mwezi Desemba, 2002 Serikali iliunda chombo kijulikanacho kama *'Air Tanzania Holding Company' (ATHCO)* ambacho kinashughulikia madeni, mali na rasilimali za iliyokuwa *ATC* ambazo hazikuchukuliwa na mbia. Tangu Kampuni hiyo ilipoundwa, imeweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kufanikiwa kupata hati safi ya hesabu zilizokaguliwa. Kampuni imeweza kupata kiasi cha shilingi milioni 240.7 kwa kuuza baadhi ya nyumba zilizoko Dar es salaam na Mtwara katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2004. Kampuni pia imejiingizia mapato kutokana na vyanzo mbalimbali na hivyo kuweza kulipa madeni ya waliokuwa wafanyakazi wa *ATC* ya jumla ya shilingi bilioni 31.4.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya mawasilliano Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu imelenga kufikia simu 6 *(teledensity)* kwa kila watu 100 ifikapo mwaka 2015. Lengo hilo litafikiwa kabla ya hapo kwa kujumlisha simu za msingi na simu za mkononi. Hadi kufikia Desemba, 2004 *teledensity* kwenye makao makuu ya Wilaya na Mikoa ilifikiwa simu 5 kwa watu 100.

Pamoja na mafanikio hayo katika malengo ya sekta, bado uwiano wa huduma za mawasiliano sio mzuri. Sehemu kubwa ya huduma za mawasiliano bado zimebakia katika miji mikubwa wakati maeneo mengi vijijini hayana huduma hizo. Ili kutatua tatizo hilo, Serikali inafanya juhudi za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano ambao utasaidia kurekebisha uwiano wa mgawanyiko wa simu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT),* Wizara imeweza kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuainisha miradi ya *ICT* vijijini, hususan kwa wanawake, kama sera hiyo inavyoelekeza. Katika kipindi cha 2004/2005 Wizara ilipata msaada toka Shirika la

Kimataifa la Simu Duniani *(ITU)* wa kuanzisha vituo vya mawasiliano*(Tele-Centres)* vinavyosimamiwa na wanawake katika miji ya Singida, Mtwara, Morogoro na Mpwapwa. Lengo la miradi hiyo ni kuwawezesha wanawake kuongeza vipato na hivyo kuboresha maisha yao na ya jamii kwa ujumla. Vituo hivyo vimeweza kuwapatia wananchi huduma bora, ya karibu na kurahisisha mawasiliano na upatikanaji wa habari katika sehemu hizo. Katika kipindi hicho Wizara imekuwa ikivitembelea vituo hivyo ili kutathmini maendeleo ya miradi hiyo. Miradi hiyo imesaidia katika kuboresha huduma za mawasiliano katika maeneo hayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inaendelea na matayarisho ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT).* Napenda nichukue fursa hii kutoa taarifa kuwa Rasimu ya kwanza ya Mkakati huu imekamilika na imekwishajadiliwa na wadau wa sekta. Aidha, kwa kuwa ICT ni suala mtambuka na linalohusisha matumizi ya teknolojia mpya na linalogusa kila sekta hapa nchini, mwezi Machi 2005 Wizara iliandaa semina ya kujadili rasimu hiyo. Semina hiyo iliwashirikisha Makatibu Wakuu wote. Semina kama hiyo ilifanywa pia kwa Wadau wa Taasisi za Umma na Sekta binafsi mwezi Mei, 2005 kwa lengo la kupata maoni na mapendekezo yao. Hivi sasa taratibu zinakamilishwa ili Serikali iidhinishe Mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa juhudi zinaendelea za kujenga uwezo wa wananchi kwa kutoa mafunzo kwa kutumia *ICT.* Ujenzi huo wa uwezo nchini unazingatia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *ICT* ambayo inasisitiza kuwekeza katika uanzishaji, uimarishaji na uendelezaji wa matumizi ya huduma za *ICT* shuleni, vyuoni na katika taasisi mbali mbali. Kwa kutambua umuhimu wa teknolojia hii katika jamii, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inashirikiana na Wizara za Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kuhakikisha kuwa aina hii ya mafunzo inatolewa katika vyuo vyote hapa nchini. Hatua iliyofikiwa kwa hivi sasa ni kwamba somo la *ICT* limeingizwa katika mitaala ya Elimu nchini na limeanza kufundishwa katika baadhi ya shule za awali, msingi na sekondari hususan shule za binafsi. Aidha vyuo vingi vikiwemo vyuo vikuu vyote nchini na baadhi ya vyuo vya kati pia vinafundisha ICT.Vyuo hivi ni pamoja na Chuo Kikuu Dar es Salaam *(UDSM)* na vyuo vyake vishiriki, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA),* Chuo Kikuu cha Mzumbe *(MU),* Taasisi ya Teknolojia cha Dar es Salaam *(DIT),* Chuo Kikuu cha Tumaini na vyuo vyake vishiriki, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino *(SAUT),* Chuo cha Uhasibu Tanzania *(TIA)* na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MIST).*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kutoa taarifa kwamba kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *ICT*, mradi wa kuweka programu za komputa katika lugha ya kiswahili, unaofadhiliwa na *SIDA* (Sweden), kwa ushirikiano na Idara ya Kompyuta ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea kutekelezwa. Mradi huu umefanikiwa kuandaa Programu za Kiswahili zinazotumika kufanya kazi kwenye kompyuta. Aidha, matumizi ya kompyuta yatarahisishwa kiasi kwamba mtu yeyote aliyemaliza elimu ya msingi akipewa mafunzo ataweza kutumia kompyuta.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Wizara iliingia mkataba na kampuni ya Cisco yenye makao makuu California, Marekani kwa nia ya kutumia teknolojia yake ya vifaa vya mawasiliano na mitaala ya ufundi. Vifaa vya kampuni hii na mitaala yake vinatumika kote duniani. Mafunzo hayo yanatolewa katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam, *SAUTI* (Iringa), Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya na Kampuni nyingine za teknolojia ya habari *(IT)*. Kwa kushirikiana na *Cisco* juhudi zinafanywa za kuwafundisha wakufunzi wa vyuo vya ualimu nchini ili hatimaye waweze kufundisha vijana wetu taaluma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na hatua za kulirekebisha Shirika la Posta ili liweze kufanya kazi kibiashara. Serikali kupitia *PSRC* iliteua taasisi ya ushauri ya *British Postal Consultancy (BPCs)* kufanya upembuzi *(study)* na kushauri njia bora ya kulirekebisha Shirika. Taasisi hiyo imetoa ripoti yake. Hivi sasa Serikali inakamilisha utaratibu wa kutekeleza mkakati wa kulirekebisha Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, maandalizi ya Sera ya Hali ya Hewa nchini yaliendelea. Sera hii inatoa mwongozo wa utoaji wa huduma za hali ya hewa, uratibu na namna ya kuboresha shughuli za hali ya hewa. Ukamilishaji wa Sera hii utakuwa ni hatua kubwa katika huduma za hali ya hewa hapa nchini. Baada ya kukamilika kwa Sera hii, Tanzania inakuwa nchi ya pili duniani baada ya Marekani kuwa na Sera ya Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhakiki na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini kwa kiwango cha kuridhisha. Taarifa za hali ya hewa zimeendelea kutoa mchango mkubwa kwa sekta za ulinzi, kilimo na hifadhi ya chakula, nishati, maji na usafiri wa anga, ujenzi wa miundombinu na katika tafiti mbali mbali. Mamlaka inahitaji kuwa na uwezo wa kupambana na majanga kama vile vimbunga, *Tsunami,* mafuriko, mvua na upepo mkali. Kupitia vyombo vya habari, redio, televisheni na magazeti wananchi wameendelea kujulishwa na kutahadharishwa dhidi ya majanga mbali mbali.

Aidha, vyombo vya habari vimepata nafasi ya kufanya mahojiano na Mamlaka kila kunapokuwa na hali ya hewa isiyo ya kawaida na hivyo kuwatahadharisha wananchi kwa haraka zaidi. Pamoja na uhaba wa vifaa vya kisasa, Mamlaka imeendelea kutoa huduma bora ndani na nje ya nchi, na hivyo kuwa mfano wa kuigwa katika Afrika na nje ya Afrika. Mamlaka inapokea wageni mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi kuja kujionea uendeshaji wa shughuli za hali ya hewa katika nchi yetu. Tanzania imeendelea kupewa heshima ya kutoa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO)* Kanda ya Afrika, na ujumbe katika Kamati ya Utendaji ya baraza hilo huko Geneva kwa vipindi viwili vya miaka minne mfululizo kuanzia 1998 hadi 2006. Aidha, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa mashirika ya hali ya hewa duniani, na hivyo kuendeleza mahusiano ya Tanzania kimataifa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mwishoni mwa 2004 dunia ilikumbwa na tukio lisilo la kawaida la mafuriko ya bahari yaliyosababishwa na tetemeko la chini ya bahari. Janga hili lililotokea katika bahari ya Hindi na kuleta maafa makubwa katika nchi

za Asia na pwani ya nchi yetu. Napenda nikumbushe kuwa majanga kama haya hayahusiani na hali ya hewa wala utabiri unaotolewa kila siku kwani suala la matetemeko ya ardhi halishughulikiwi na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini. Ni nchi chache duniani ambazo zimeunganisha shughuli za matetemeko na zile za hali ya hewa. Ni wakati muafaka kwa nchi yetu kufikiria kuwa na chombo cha kushughulikia na kuratibu shughuli za matetemeko hapa nchini. Hivi sasa Mamlaka imekuwa ikiripoti matukio ya matetemeko pale yanapotokea kwa kushirikiana na Idara ya Jiolojia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kufuatia janga hilo, Wizara inafanya juhudi za kuhakikisha kuwa kunakuwa na chombo cha kufuatilia na kuratibu majanga kama hayo ili kupunguza athari zake katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara ilianza taratibu za kuirekebisha Sheria Na.6 ya Mwaka 1978 iliyounda Idara Kuu ya Hali ya Hewa baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 1977. Marekebisho haya yanatokana na sheria ya Wakala wa Serikali, Na 30. ya 1997 na Sheria Na.3 ya 2001 inayohusu kanuni za fedha na ununuzi. Marekebisho hayo yanazingatia Sera ya Serikali ya kujiondoa kwenye biashara na mabadiliko ya uchumi yanayotokea nchini na duniani kote. Ni matarajio yetu kuwa marekebisho hayo yatasaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria Namba 12 ya 2003 kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* napenda kutoa taarifa kwamba, Mamlaka hiyo inaendelea kufanya kazi kwa ufanisi. *TCRA* imeweza kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na vyombo vilivyoundwa kwa mujibu wa sheria. Vyombo hivyo ni pamoja na Bodi ya Mamlaka ambayo ina jukumu la kusimamia utendaji kazi wa Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara; Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano ambalo jukumu lake kubwa ni kuwakilisha na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano. Napenda kuvipongeza vyombo hivi kwa kazi nzuri waliyofanya katika kipindi hiki tangu vilipoundwa rasmi Mwezi Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano duniani, taratibu za utoaji huduma za Mamlaka ya Mawasiliano zilifanyiwa marekebisho ili kuweza kulingana na mazingira yaliyopo. Marekebisho hayo ni pamoja na taratibu za utoaji wa leseni ili kuweka mazingira sawa ya kutoa huduma na udhibiti kwa vyombo vya mawasiliano na utangazaji hapa nchini. Utaratibu wa zamani ulikuwa wa leseni moja kwa ajili ya aina moja ya huduma. Kwa mfano simu peke yake na intaneti peke yake. Utaratibu wa sasa, ni leseni moja kwa huduma mseto.

Kwa mfano simu pamoja na intaneti. Katika kufanya hivyo Mamlaka iliwashirikisha wadau wote wa mawasiliano ili waweze kutoa maoni yao. Maoni ya wadau yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa kama ilivyokubalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kuwa, kipindi cha ukiritimba kwa *TTCL* katika kutoa huduma za simu za msingi *(Landline)* hapa nchini kilikwisha tarehe 22 Februari, 2005. Hivi sasa kampuni nyingine za simu zinaweza kutoa huduma hizo kulingana na sheria na taratibu zilizopo. Majukumu ya sasa ya *TTCL* ni pamoja na ujenzi, uimarishaji, uendelezaji wa miundombinu ya msingi ya mtandao wa simu nchini

*(National Communication backbone). TTCL* itakuwa mhimili wa kutoa huduma kwa watoa huduma wengine *(carrier of carriers)* na itasimamia matumizi ya mkongo *(optic fibre)* wa njia za kupitisha mawasiliano. Wamiliki wa njia hizo ni pamoja na kampuni za *TANESCO, TRC, TAZARA* na *SONGAs* na *TTCL* yenyewe. *TCRA* imepewa jukumu la kuratibu mazungumzo ya matumizi na usimamizi huo. Katika kutekeleza hayo, *TTCL* imebuni mradi mkubwa wa kujenga na kukarabati miundombinu *(Tanzania Communications Infrastructure Improvement Program-TCIIP).* Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano na kampuni zinazomiliki mtandao wa mawasiliano. Hivi sasa utafiti wa awali umefanywa kwa ushirikiano na Serikali ya China na taarifa ya awali imewasilishwa Wizarani kwa hatua zaidi. Aidha, mradi huu unatarajiwa kufadhiliwa na wadau mbali mbali wakiwemo Benki ya Dunia, *SIDA, EAC* na *ADB.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 kampuni ya SIMU 2000 Limited imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia mali zisizokuwa za msingi *(non-core assets)* zilizokuwa za *TTCL* kabla ya *TTCL* kubinafsishwa. Jukumu lingine la SIMU 2000 ni kulipa deni la pensheni kwa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, Kampuni imeuza nyumba 17 na viwanja 13 na kufanikiwa kulipa kiasi cha Shilingi bilioni 3.97 kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambazo ni pensheni na kamisheni.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Kampuni imekamilisha ulipaji wa deni la pensheni la wafanyakazi wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki waliorithiwa na Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL).* Ulipaji huu umefanyika kwa awamu nne ambapo jumla yake ilikuwa shilingi bilioni 10.96. Baada ya kumaliza deni hilo Kampuni inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa inakamilisha majukumu yake mengine hasa lile la uuzaji wa nyumba na viwanja katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyotoa yanaonyesha hali ya utendaji wa jumla wa sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005. Napenda kuchukua nafasi hii kufafanua kwa kina malengo, mikakati na mwelekeo wa utendaji wa sekta hizo kwa kipindi hicho na matarajio ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera ya Taifa ya Uchukuzi, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha usafiri wa barabara katika kipindi cha 2004/2005. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa upande wake imeendelea na jukumu lake la kusimamia Sera na utoaji huduma za usafiri wa barabara. Jukumu la kuendeleza miundombinu ya barabara limeendelea kutekelezwa na Wizara ya Ujenzi. Maelezo kamili ya uendelezaji wa miundombinu yametolewa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alipokuwa anawasilisha hoja ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za usafiri wa barabara mikoani na vijijini pamoja na uendelezaji wa miundombinu umeendelea kusimamiwa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Halmashauri za Miji na Wilaya pamoja na sekta binafsi. Katika kipindi cha 2004/2005, huduma za usafiri katika sehemu nyingi za miji mikubwa zimekuwa za kuridhisha.

Idadi ya watoa huduma imekuwa ikiongezeka baada ya mindombinu kuboreshwa. Hata hivyo, huduma za usafiri wa barabara vijijini imeendelea kuwa ya wastani kwa kuwa miundombinu bado haijawa ya kuridhisha. Hali hii inakwamisha maendeleo katika maeneo hayo na hivyo kusababisha kero na kikwazo katika upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii. Wizara itahakikisha kuwa Sera ya Taifa ya Uchukuzi pamoja na mikakati yake inatekelezwa ipasavyo ili kuboresha miundombinu hiyo.

Aidha, kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi, katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wanapata huduma bora ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi imeendelea kutoa huduma ya usafiri katika miji yetu. Huduma hii imetolewa kwa ushindani mkubwa hali ambayo imesaidia kuinua kiwango cha huduma, na kurahisisha upatikanaji wake. Kwa wakati huu, utoaji wa huduma unakabiliwa na tatizo la kupanda kwa bei ya mafuta na vipuri kunakotokana na kupanda kwa bei ya mafuta ghafi duniani na kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola ya Kimarekani. Kwa ujumla suala hili ni changamoto kwetu katika utoaji huduma za usafiri nchini kote.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya kupanda kwa gharama za uendeshaji, mwezi Machi, 2005 watoa huduma za usafiri kwenye mikoa yote nchini walipandisha nauli za mabasi ya daladala kwa kiasi cha shilingi kati ya mia hamsini mpaka mia mbili hamsini. Zoezi hilo lilitekelezwa kwa kuwasiliana na Mamlaka za Usafirishaji za Mikoa ili kuhakikisha kuwa maslahi ya wananchi yanalindwa. Ni matarajio yetu kuwa hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwafanya watoa huduma hizo waweze kuboresha huduma hiyo, hivyo kuwapunguzia wananchi kero ya usafiri mijini. Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaendelea na jitihada za kuboresha huduma za usafiri mijini kwa kuandaa utaratibu wa kuhakikisha kuwa wamiliki wa mabasi wanawaajiri madereva na wasaidizi wenye sifa ili kuboresha huduma hii. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu uhusiano wa kupanda kwa nauli na bei ya mafuta ili kuhakikisha kuwa wananchi wanalipa nauli inayostahili, na watoa huduma wanapata wanachostahili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa idadi ya mabasi ya abiria imeongezeka bado hayajakidhi mahitaji ya miji yetu ambayo inapanuka siku hadi siku. Mabasi mengi ya abiria ni madogo, hayana nafasi ya kutosha kwa wasafiri kuweza kukaa bila usumbufu. Aidha, kwa kuwa mabasi hayatoshi yanachukua abiria wengi kuliko uwezo wao hivyo wakati mwingine husababisha ajali. Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba hali hii inarekebishwa hasa baada ya Serikali kuanzisha Mamlaka ya udhibiti wa Usafiri Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)*. *SUMATRA* ina majukumu ya kusimamia, pamoja na mambo mengine, utoaji huduma za usafiri na usalama wake. Wizara itaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi (Kikosi cha Usalama Barabarani) ili kuhakikisha kuwa sheria za barabarani zinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 utendaji wa Shirika la Usafiri Dar es salaam (UDA) ulikuwa wa wastani. Hii ilitokana na idadi ndogo ya mabasi, na ushindani. Aidha, kiasi cha nauli bado kilikuwa chini hivyo kutokidhi gharama za uendeshaji ambazo zimekuwa zikiongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na vipuri vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Shirika liliweza kusafirisha abiria milioni 2.9 ikilinganishwa na abiria milioni 1.9 waliosafirishwa 2003/2004. Mapato ya Shirika yaliyotokana na shughuli za usafirishaji kwa mwaka 2004/2005 yalikuwa shilingi milioni 795.4 ikilinganishwa na shilingi milioni 792.6 zilizopatikana mwaka 2003/2004. Katika kipindi hichohicho Shirika lilikuwa na jumla ya mabasi 43 ukilinganisha na mabasi 37 ya mwaka 2003/2004. Ongezeko hili lilitokana na kufufua mabasi 6 yaliyokuwa yamesimama. Katika mwaka 2005/2006, Shirika lina mpango wa kuongeza idadi ya mabasi kufikia 46.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza rasmi *SUMATRA,* jukumu la usimamizi na udhibiti wa uchukuzi kwa njia ya barabara lilikuwa likifanywa na Wizara kupitia iliyokuwa Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji *(CTLA)* na Mamlaka za Leseni za Mikoa *(RTLAs).* Majukumu hayo hivi sasa yanatekelezwa na *SUMATRA.* Aidha, Wizara ya Ujenzi imeendelea kushughulikia udhibiti wa uzito wa magari. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inasimamia utekelezaji wa sheria za usalama barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi, 2005 jumla ya leseni 16,039 zilizotolewa kwa magari ya abiria na mizigo ikilinganishwa na leseni 7474 zilitolewa katika kipindi cha Julai 2003 hadi Machi, 2004. Kiasi cha fedha zilizokusanywa kama maduhuli kutokana na ada za leseni hizo ni shilingi bilioni 1.20 ikilinganishwa na shilingi billioni 1.13 zilizokusanywa katika kipindi cha Julai, 2003 hadi Machi,2004.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yametokana na juhudi za Mamlaka za kusogeza huduma za utoaji leseni karibu zaidi na wateja hasa wa mikoani. Mamlaka pia imetumia nafasi nzuri ya kujitangaza kwenye vyombo vya habari kama televisheni, radio na magazeti ili kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuwa na leseni za magari kwa wakati unaohitajika. Mamlaka imeendelea kuimarisha ofisi zake za kanda ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Mamlaka iliendelea kushirikiana na watoa huduma za usafirishaji wa barabara kwa lengo la kuboresha zaidi huduma hiyo. Mamlaka imeweza kuwahamasisha wamiliki wa magari ya mizigo na abiria na wananchi kwa ujumla umuhimu wa kuwa na leseni za usafirishaji kwa magari yao na kuzingatia masharti ya leseni hizo. Hatua hii imepunguza kwa kiasi kikubwa udanganyifu uliokuwa unafanywa na wenye magari kuhusu ukataji wa leseni sahihi kulingana na ukubwa na uzito wa magari yao.

Katika kipindi cha 2005/2006 Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara itafanya mapitio ya sheria zinazosimamia utoaji wa huduma barabarani ili kuboresha utoaji wa huduma na kukidhi matakwa ya kisera. Aidha, Mamlaka itaendelea na mpango wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa leseni barabani ili kubaini wasio na leseni na

wenye leseni bandia ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Jitihada pia zitaendelea kufanywa za kuwahusisha wadau wengine kwa lengo la kuboresha huduma za usafirishaji na uchukuzi mijini na vijijini kwa makundi maalum ya wanafunzi, wazee, wasiojiweza na watu wenye ulemavu. Aidha, Mamlaka itajenga uwezo wake wa kupata takwimu sahihi za usafirishaji ili kuimarisha utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2004/2005 hali ya utendaji wa sekta ndogo ya uchukuzi wa reli ilikuwa ya wastani. Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* ziliendelea kukabiliwa na tatizo la uchakavu wa vitendea kazi na miundombinu. Kwa upande wa *TRC,* baadhi ya mifumo ya mawasiliano ni ya zamani na imepitwa na wakati na sehemu kubwa ya miundombinu ya njia ya reli imechakaa. Hali hii inahitaji kurekebishwa ili shirika liweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa upande wa *TAZARA,* Mamlaka imeendelea kukabiliwa na tatizo la uhaba wa injini za treni na mabehewa ya mizigo na ya abiria licha ya kuwa mfumo wake wa njia ya reli iko kwenye hali ya kuridhisha. Aidha, tatizo la wizi wa nguzo za simu na waya ilisababisha mawasiliano kuwa hafifu na kuathiri utendaji kwa *TRC* na *TAZARA.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zinazoikabili sekta ya reli, *TRC* katika kipindi cha 2004/2005 iliweza kusafirisha jumla ya tani milioni 1.333, ikilinganishwa na tani milioni 1.442 zilizosafirishwa mwaka 2003/2004. Lengo la Shirika lilikuwa ni kusafirisha tani 1.45. Utendaji huo ni pungufu kwa asilimia 7.6 ukilinganisha na ule wa mwaka 2003 wa asilimia 8.1 chini ya lengo. Mwaka 2004 Shirika lilisafirisha jumla ya abiria 627,969 ikilinganishwa na abiria 683,481 waliosafirishwa katika kipindi cha mwaka 2003. Lengo la Shirika lilikuwa kusafirisha abiria 720,000. Utendaji huu ni asilimia 13.5 chini ya ule wa mwaka uliopita na asilimia 13 ya lengo la mwaka 2004. Kutofikiwa kwa malengo kulisababishwa na kuendelea kupunguka kwa nyenzo za kutendea kazi pamoja na uchakavu wa miundombinu.

Hali hii pia iliongeza kasi ya ukwamaji wa treni njiani kutokana na ubovu na ajali. Baadhi ya ajali zilitokana na hujuma, kama vile wizi wa mataruma na reli. Dosari hii ilichangia pia uharibifu na ufungaji wa njia na ongezeko la udhibiti wa mwendo ambayo kwa ujumla yote haya yalisababisha mzunguko hafifu wa mabehewa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004 Shirika liliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 56.3, ikilinganishwa na shillingi bilioni 60.7 zilizokusanywa katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Lengo lilikuwa kukusanya shillingi bilioni 68.4. Kwa misingi hii mapato yalikuwa chini ya pato la mwaka 2003 kwa asilimia 7.7 na chini ya lengo la mwaka 2004 kwa asilimia 18; hii ni sawa na upungufu wa shillingi bilioni 12.1.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kutatua changamoto hizo, mwaka 2005/2006, *TRC* inakusudia kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa unaojumuisha; ununuzi wa mabehewa 66 ya abiria, ununuzi wa mataruma ya reli, ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na ukarabati wa vichwa 20 vya treni. Miradi mingine inayotarajiwa kutekelezwa ni:-

(i) Kubadilisha mataruma na reli katika maeneo yafuatayo:- Itigi - Tabora (km. 73), Kaliua- Mpanda (km. 20), Kilosa - Kidatu (km. 30) Manyoni-Singida (km. 20).

(ii) Ujenzi wa vituo vya makontena Mwanza na Shinyanga.

(iii) Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli inayotarajiwa kujengwa kati ya Isaka na Kigali.

(iv) Ubadilishaji wa mataruma na reli katika baadhi ya maeneo katika sehemu mbalimbali yenye jumla ya km 60 kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

(iv) Ujenzi wa magenge mawili ya 'pigilia' katika reli za Kaliua hadi Mpanda na Manyoni hadi Singida.

(v) Ujenzi wa matanki 10 chini ya ardhi ya kuhifadhi maji kwa magenge 10 (Matanki 3 Dar es Salaam, 3 Tabora, 2 Tanga na 2 Dodoma).

(vi) Ukarabati wa madaraja na makalavati yapatayo 14.

(vii) Utandazaji wa nyaya za mawasiliano ya simu *Optic fibre* kupita chini ya ardhi kati ya Dodoma na Tabora, na uboreshaji wa mawasiliano katika yadi ya stesheni ya Pongwe na Tanga.

(viii) Ukarabati wa ghala la pamba Shinyanga.

(ix) Ununuzi wa mashine na mitambo kwa ajili ya kituo cha makontena cha Ilala.

(x) Utafiti wa namna ya kuepuka athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira kwenye njia za reli pamoja na uchafu kutoka kwenye karakana za reli na namna ya kuuepuka na itafanyika tathmini ili kutambua gharama za kuwahamisha wavamizi katika njia za reli.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa *TAZARA* kwa mwaka 2004/2005 ulikuwa wa kuridhisha. Mamlaka iliweka lengo la kusafirisha tani 650,000 za mizigo na abiria milioni 1.0 ambapo ingepata jumla ya shilingi bilioni 41. Kati ya Julai 2004 hadi Machi 2005, Mamlaka ilisafirisha tani 325,656 za mizigo ikilinganishwa na tani 364,000 zilizopangwa. Hii ni pungufu ya asilimia 11. Aidha, katika kipindi hiki, Mamlaka ilitarajia kusafirisha abiria 549,996 na iliweza kusafirisha abiria 565,629 hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 3. Katika kipindi hicho cha Julai hadi Desemba 2004, Mamlaka ilipata jumla ya shilingi bilioni 19.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 20.5 zilizokadiriwa. Hilo ni sawa na asilimia 95 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, lengo la Mamlaka ni kusafirisha mizigo ya tani 700,000 na abiria milioni 1.2 na inatarajia kupata jumla ya shilingi bilioni 44. Ongezeko hilo la mapato litatokana na Mamlaka kuzidi kuimarisha mikakati madhubuti na ya makusudi iliyojiwekea kusafirisha shehena zinazokwenda masafa marefu na uboreshaji wa matumizi ya vifaa. Pia, jitihada zinazoendelea za kukarabati vichwa vya treni na mabehewa zinatarajiwa kuchangia sana katika uboreshaji wa huduma za Mamlaka kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki mamlaka iliendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha. Hali hiyo imeathiri sana uendeshaji na pia imesababisha kuahirishwa kwa matengenezo makubwa ya vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na ya abiria na hivyo kuathiri upatikanaji utoaji huduma. Aidha, uhaba huo wa fedha umeathiri kwa kiasi kikubwa ukarabati wa miundombinu, hususan upande wa Tanzania ambako hali ya njia ya reli hairidhishi, hivyo kusababisha kupunguza mwendo *(Speed-Restrictions)* katika sehemu hizo. Mimomonyoko ya ardhi upande wa Tanzania (Mlimba - Makambako) hususan kilometa 555 imeendelea kuathiri ubora wa njia ya reli hivyo kusababisha kupungua kwa mwendo kasi wa treni na kusababisha ajali za mara kwa mara.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na matatizo hayo, *TAZARA* imeendelea kujiwekea mikakati kabambe ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na kukarabati reli, kukarabati vichwa vya treni na mabehewa, kununua injini 4 (nne) zilizokarabatiwa *(reconditioned)* na vipuri vya matengenezo ya kati *(medium repairs).* Aidha, matengenezo na uboreshaji wa mawasiliano kwa njia ya *micro-wave* na *HF Radio* yamekuwa yakiendelea katika kipindi husika. Serikali kwa mara ya kwanza, katika mwaka wa 2005/2006, itachangia kwa kiasi matengenezo ya njia ya reli kati ya Kitete na Mpanga kutokana na fedha za hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya vikwazo vilivyoathiri utendaji wa mashirika ya reli ya *TRC* na *TAZARA* ni pamoja na ajali zilizotokea katika njia za reli. Katika kipindi cha nusu ya mwaka 2004/2005, ajali za treni katika Mamlaka hizi zilipunguka kiasi kidogo.

Katika kipindi hicho jumla ya ajali za treni 122 zilitokea ikilinganishwa na ajali 129 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2003/2004 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 5.4. Kupungua kwa ajali kunatokana na juhudi za kuimarisha usalama sehemu mbalimbali kwenye njia za reli na ukarabati wa injini na mabehewa. Serikali katika mwaka 2005/2006 itaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa ajali zinapungua. *SUMATRA,* ambayo inadhibiti usafiri na usalama wa reli, itabuni na kuweka taratibu thabiti zaidi ya namna ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, huduma za bandari, na usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji katika kipindi cha 2004/2005, zimeendelea kutolewa kwa ufanisi na iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA),* Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL),* Kampuni ya Meli ya China na Tanzania *(SINOTASHIP)* pamoja na kampuni binafsi. Miundombinu inayotumika katika utoaji wa huduma ya usafiri kwa njia ya maji iliendelea kuimarishwa

na kuboreshwa ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Juhudi za kuimarisha huduma hii zinaendelea kwa kuhamasisha sekta binafsi ili itoe huduma katika bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA)* [ambayo sasa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)]* iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza, kutunza, kuanzisha, kusimamia na kuziendesha kibiashara bandari zote nchini. Aidha, Mamlaka imewajibika kuhifadhi mazingira katika bandari zote na fukwe ili kupunguza athari za shughuli za kibandari kwenye sehemu hizo. Mamlaka imeendelea kutoa huduma za bandari kwa nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo,* Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo yake ya kipindi cha 2004/2005. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilitarajia kuhudumia jumla ya tani za mizigo 4,822,500 katika bandari zake. Katika kipindi cha Julai-Desemba 2004 shehena iliyohudumiwa na Mamlaka ilikuwa tani 2,425,383 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho la tani 2,393,270.

Hili ni ongezeko la tani 32,113 au asilimia 1.3. Kitengo cha kontena kinachoendeshwa na kampuni binafsi ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)* tangu mwaka 2000, kilitarajia kuhudumia makontena *(TEUs)* 204,243 katika kipindi cha 2004/2005. Katika kipindi cha Julai-Desemba 2004 *TICTS* walihudumia makontena 106,814 ambayo ni zaidi ya lengo kwa makontena 6,754 sawa na asilimia 6.7. Utendaji huo unaonyesha jinsi Mamlaka inavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ililenga kupata jumla ya shilingi bilioni 86.4 na matumizi ya shilingi bilioni 72.6 na hivyo kupata ziada ya shilingi bilioni 13.8 katika kipindi cha 2004/2005. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2004, mapato yalifikia shilingi bilioni 43.2 wakati lengo lilikuwa kupata jumla ya shilingi bilioni 48.2 hivyo kuna pungufu ya mapato kwa shilingi bilioni 5.0. Matumizi halisi yalikuwa shilingi bilioni 32.1 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 36.4. *(Makofi)*

Matumizi yalipungua kwa shilingi bilioni 4.3 sawa na asilimia 11.6 ya lengo. Hivyo ziada halisi kabla ya kodi imekuwa shilingi bilioni 16.0 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 6.8 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 9.2 au asilimia 134.3. Katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2003/2004, ziada kabla ya kodi ilikuwa shilingi bilioni 10.4. Aidha, katika kipindi cha 2005/2006, Mamlaka imejiwekea lengo la kuhudumia jumla ya tani 5,045,100 kupitia katika bandari zake zote nchini. Lengo hilo ni zaidi kwa tani 22,600 au asilimia 4.6 ikilinganishwa na lengo la mwaka jana. Kitengo cha Kontena kina lengo la kuhudumia makontena 212,400 ambalo ni zaidi kwa makontena 8,157 au asilimia 4 ikilinganishwa na lengo la mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza na kuimarisha huduma za miundombinu ya usafiri, katika kipindi cha 2004/2005 Mamlaka ilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo na ununuzi wa vifaa vyenye kugharimu shilingi bilioni 21.2. Kati ya hizo, shilingi bilioni 14.9 au asilimia 70 ni fedha za kigeni. Hatua za utekelezaji katika kipindi cha Julai-

Desemba 2004 ni uteuzi wa mtaalamu mwelekezi wa kushauri jinsi ya kutekeleza miradi hiyo na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Aidha, miradi mingine mikubwa iliyopangwa kutekelezwa ni:-

(i) Uboreshaji wa bomba la mafuta *(KOJ Improvement; Upgrading of Fire Equipment and Installation of Flow Meters).*

(ii) Ujenzi wa gati katika bandari ndogo ya Mafia.

(iii) Ujenzi wa kituo cha kuongozea Meli *(New Signal Station).*

(iv) Ujenzi wa eneo la kuhudumia Makontena*(Heavy Duty Paving at Mtwara Port.).*

(v) Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia mizigo kwa bandari zote.

(vi) Ukarabati na ujenzi wa maeneo ya kazi katika bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

(vii) Uendelezaji wa gati za maziwa makuu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Mamlaka iliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zilizoathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na hali mbaya ya uchumi na kisiasa katika nchi zitumiazo bandari za Mamlaka na uwezo mdogo wa reli zetu kuondosha mizigo katika bandari. Aidha, kumekuwa na ongezeko la ushindani wa kibiashara baina ya bandari za ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika kama vile Mombasa na Beira, kutokuwepo kwa maeneo huru ya biashara *(EPZ),* na uhaba wa karakana za kuhudumia meli katika bandari zetu kumeathiri utendaji wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka katika mwaka 2005/2006 itaendelea kushirikiana na wadau wengine kama vile *TRC, TICTS, TAZARA,* Shirika ka Reli la Uganda *(URC),* Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na kampuni za wakala wa meli *(Clearing & Forwarding Companies)* ili kuhakikisha kuwa huduma inatolewa katika ubora unaokubalika. Ili kuweza kukabiliana na ushindani wa bandari nyingine, Mamlaka itaendelea kushirikiana na wadau hao kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo ni za gharama nafuu, zinatolewa kwa ubora zaidi na kwa wakati muafaka, ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa mzunguko wa meli na muda wa shehena kukaa bandarini. Aidha, Mamlaka ina mpango wa kushiriki katika kuanzisha maeneo huru *(EPZ)* ili kuchochea maendeleo ya shughuli zenye maslahi *(Value Adding Activities)* sambamba na uanzishaji wa bandari za nchi kavu ili kuzidi kuwavutia watumiaji wakubwa pamoja na kupanua na kushikilia masoko.

Mamlaka itaendelea kushiriki kwenye mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Mpango mpya wa Maendeleo Afrika *(NEPAD)* katika kuweka mikakati na programu za kuboresha usafiri wa majini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa bandari ya Mtwara inafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na uhaba wa shughuli za kiuchumi katika maeneo yanayoizunguka. Ili kuongeza ufanisi wa bandari hii upo mpango kabambe ujulikanao kama *Mtwara Port Master Plan* kwa ajili ya kupanua eneo la bandari ili kuongeza idadi ya magati kutoka mawili ya sasa hadi kufikia matano. Eneo lilioachwa kwa ajili ya upanuzi huu ni ekari 200. Aidha, pamoja na eneo hilo kuna eneo la ekari 60 ambalo limetegwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo za kibandari. Eneo hili pia linafaa kwa kuanzisha *EPZ* na shughuli za usambazaji. Juhudi za kuendeleza maeneo kama hayo kwenye kiwanja cha ndege cha Mtwara zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Mamlaka inatarajia kuingiza pato la jumla la shilingi bilioni 98.6. Pato la shilingi bilioni 67.3 litatokana na shughuli zinazoendelea kuwa chini ya Mamlaka *(TPA),* na pato la shilingi bilioni 31.2 litatokana na Kitengo cha Kontena. Matumizi yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 80.7 na hivyo kutakuwa na ziada ya shilingi bilioni 17.8. Mpango wa Maendeleo wa Mamlaka kwa kipindi cha 2005/2006 umezingatia kuboresha maeneo ya kazi ili kulinda ufanisi na ubora wa rasilimali iliyopo, kuinua uwezo wa bandari kwa kukarabati na kubadilisha vifaa na maeneo ya kuhudumia meli na mizigo, na pia kuendeleza utekelezaji wa miradi iliyoanza na ile ambayo ilichelewa kuanza katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Mpango huu unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 16.8. Kati ya hizo shilingi bilioni 11.1 au asilimia 66.1 ni fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *SINOTASHIP* inamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China. Hivi sasa Kampuni ina meli tatu zinazosafiri masafa marefu baharini ambazo zina uwezo wa kubeba jumla ya tani 46,645 kwa wakati mmoja. Mwaka 2004/2005 meli za kampuni zilifanya safari 24, kama ilivyokuwa imepangwa. Katika safari hizo jumla ya tani 262,337 za shehena zilisafirishwa, ambalo ni ongezeko la asilimia 3.6 ikilinganishwa na tani 253,241 zilizosafirishwa mwaka 2003/2004. Aidha, usafirishaji huo ulikuwa ni ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa na lengo la tani 250,000 zilizokuwa zimekadiriwa kusafirishwa katika mwaka wa 2004/2005. Mapato ya kampuni yaliongezeka kwa asilimia 47.82 kutoka dola za Marekani milioni 6.5 zilizopatikana mwaka 2003 hadi dola 9.6. Hili lilikuwa ni ongezeko la asilimia 46.7 ikilinganishwa na dola milioni 6.5 zilizokuwa zimekadiriwa kupatikana. Baada ya kutoa matumizi, faida ilikuwa ni dola milioni 1.8 ambayo ni ongezeko la asilimia 496 ikilinganishwa na faida ya dola 309,617.01 iliyopatikana mwaka 2003. Aidha, ikilinganishwa na lengo lililokuwa limewekwa la dola 450,000 faida iliongezeka kwa asilimia 310.

Mheshimiwa Spika, katika uendeshaji wa shughuli zake, kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, Kampuni ilikabiliana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na mfumuko mkubwa wa bei za vipuri na vifaa vya meli. Gharama za vifaa vya meli na vipuri zilipanda kwa asilimia 149 kutoka dola za kimarekani 226,324.90 mwaka 2003 hadi dola 563,843.87 mwaka 2004. Aidha, gharama za matengenezo ya meli zilipanda kwa asilimia 396 kutoka dola 143,725.97 mwaka 2003 hadi dola 713,299.34 mwaka 2004 wakati gharama za kununulia mafuta zilipanda kwa asilimia 20.6.

Pamoja na soko la shehena kuimarika mwaka 2004 ikilinganishwa na 2003, bado kulikuwepo na uhaba wa mizigo kwenye baadhi ya maeneo, hususan Mashariki mwa Afrika kwa sababu ya hali ya uchumi ya nchi za eneo hilo kuendelea kubaki duni. Hata hivyo, kutokana na kuongeza jitihada katika kutafuta mizigo, Kampuni ilifanikiwa kusafirisha shehena za magogo kutoka Msumbiji kwenda Mashariki ya Mbali. Shehena hizo siyo tu ziliingizia kampuni mapato, bali pia ziliiepushia gharama za meli kusafiri zikiwa tupu toka pwani ya Afrika kwenda kupakia mizigo kwenye maeneo mengine ya Mashariki ya Kati au Asia Kusini.

Mhemishiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Kampuni ilikamilisha kanuni na taratibu za mkataba wa kimataifa wa usalama wa meli na bandari ujulikanao kama *International Ship & Port Facility Security (ISPS) Code* ambao ulianza kutumika Julai,2004. Inatarajiwa kuwa taratibu hizi zitaendelea kuimarisha biashara ya usafirishaji wa shehena hivyo kuongeza ufanisi katika Kampuni.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto zinazoikabili kampuni, juhudi za makusudi zilifanywa kubana matumizi na kuepuka gharama zisizo za lazima. Baadhi ya jitihada hizo ni kupunguza gharama za meli kucheleweshwa bandarini kwa kupeleka mameneja wa Kampuni kwenye bandari zenye tija duni ili kusimamia na kuhimiza kazi za upakiaji na upakuaji wa mizigo. Katika kipindi cha 2005/2006, Kampuni imejiwekea lengo la kusafirisha tani 250,000 kwa kukamilisha safari 24 ikitumia meli zake tatu, na hivyo kupata faida ya dola milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha hali ya usafiri katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Baada ya kukamilika kwa Daraja la Mto Rufiji, wakazi wa mikoa hiyo wameweza kuwa na uchaguzi wa aina ya usafiri wanaotaka kutumia kati ya meli, barabara au ndege. Kwa ujumla hali hii inaongeza ushindani uliosababisha hali na nauli kubakia kuwa za wastani. Hata hivyo mikoa hiyo bado haina shehena na abiria wa kutosha hivyo watoa huduma za usafiri katika mikoa hiyo hushindwa kuendelea kwa kuwa gharama za usafiri zinakuwa kubwa wakati faida ni kidogo. Aidha, Serikali inaendelea kuwahamasisha na kuwashirikisha sekta binafsi ili waweze kutoa huduma ya usafiri katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2004/2005 huduma za usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ziliendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli *(Marine Services Company Limited (MSCL)* ikishirikiana na sekta binafsi. Aidha, sekta binafsi imeendelea kukua katika kutoa huduma hizi za usafiri majini kwa kuwa mpaka sasa kuna meli zaidi ya 20 ukilinganisha na mwaka jana ambapo kulikuwa na meli 15 tu. Kati ya meli 20 zilizopo hivi sasa, 13 ni za MSCL. Kati ya meli zinazomilikiwa na *MSCL,* 8 zipo Ziwa Victoria, 3 Ziwa Tanganyika na 2 Ziwa Nyasa. Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ili kuhakikisha kuwa wawekezaji wanakuwa na mazingira mazuri ya kutoa huduma za usafiri katika maziwa hayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya usafiri kwenye maziwa makuu, Serikali imeweza kukamilisha ukarabati wa magati ya Shirati, Kinesi na Nansio. Ujenzi wa gati la Bukondo katika Ziwa Victoria unaendelea na umefikia asilimia 90.

Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 250 kwa kipindi cha 2005/2006 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa magati. Ukarabati utajumuisha gati la Kasanga, Mbamba Bay na Manda na kuanza ujenzi wa magati ya Kiamkwikwi, Maisome, Nkome, Mwigobelo, Nansio na Bukima katika Ziwa Victoria na Karema katika Ziwa Tanganyika. Uendelezaji wa ukarabati na ujenzi wa gati hayo sasa ni jukumu la *TPA.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, *MSCL* ilisafirisha jumla ya tani 167,177 za mizigo. Kiasi hiki ni kikubwa ikilinganishwa na tani za mizigo 152,601 ziliosafirishwa mwaka 2003/2004. Kampuni iliweza kusafirisha jumla ya abiria 483,619 mwaka 2004 ikilinganishwa na abiria 389,991 ambao walisafirishwa mwaka 2003. Kiwango hicho cha utekelezaji kilikuwa juu kwa asilimia 16 kwa upande wa mizigo na asilimia 31 kwa upande wa abiria. Aidha, kampuni iliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5.64 ukilinganisha na shilingi bilioni 4.48 zilizokusanywa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa meli, hali mbaya ya kisiasa katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo (DRC)* na Jamhuri ya Burundi ambazo ndio watumaji wakubwa wa huduma za Kampuni hiyo. Hali hii imesababisha upungufu wa mizigo na abiria kupitia bandari zetu za maziwa hasa katika ziwa Tanganyika. Hata hivyo Kampuni inafanya juhudi za kuendelea kuzifanyia matengenezo meli mara kwa mara ili kuongeza ufanisi. Kampuni imepanga kununua injini mpya kwa ajili ya meli ya MT Nyangumi inayosafirisha mafuta na nyingine kwa ajili ya MT Wimbi inayosafirisha mizigo katika ziwa Victoria. Aidha, Kampuni inaendelea kuwaelimisha wafanyakazi wanaoendesha meli juu ya kuzingatia usalama na umuhimu wa kuwa waangalifu ili kuepukana na ajali. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Kampuni imelenga kusafirisha jumla ya tani 154,121 za mizigo na abiria 475,094. Kampuni inategemea kupata jumla ya shilingi bilioni 5.6 kwa kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha usalama wa abiria na mizigo, Wizara imeendelea kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini. Wizara kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikifanya jitihada za kuweka tahadhari dhidi ya uharibifu wa mazingira katika utoaji wa huduma hii na kusisitiza kuzingatia sheria na matumizi sahihi ya vyombo vya usafiri majini. Kwa kipindi cha 2004/2005 Wizara imeweza kufanya semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kuwaelimisha watumiaji na watoa huduma za usafiri wa majini sheria za usalama majini. Ili kupunguza mlundikano wa meli zinazokuja kwenye bandari zetu, mwezi Desemba, 2004 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini *(IMO)* iliendesha semina kuhusu Mkataba wa Kimataifa *(Facilitation Convention)* unahusu namna ya kuzishughulikia meli za kimataifa zinazotumia bandari zetu ili kupunguza muda wa meli kukaa bandarini. Matokeo ya semina hiyo ni kwamba imeundwa Kamati itakayosimamia utekelezaji wa matakwa ya mkataba huo pamoja na kuandaa kanuni zitakazotumika.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2005, Wizara kwa kushirikiana na Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa semina huko Mwanza kuhusu jinsi ya kuboresha usalama wa usafirishaji katika Ziwa Victoria. Semina iliwashirikisha wadau wote muhimu wakiwemo wabunge wa Kanda ya Ziwa hilo. Madhumuni ya semina hiyo

yalikuwa ni kupitia rasimu ya Sheria ya Usafiri wa Majini ya Ziwa Victoria ambayo inatoa mwongozo wa kulinda usalama wa usafiri wa majini kwenye Ziwa hilo. Majumuisho ya semina hiyo yalihusu kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa Ziwa linakuwa na vifaa vya kuongoza meli, upimaji wa kina cha maji, kuwa na nyenzo imara za kujiokolea na mawasiliano na ramani za kutumia wakati wa kuendesha meli. Mwezi Machi,2005 Wizara kwa kushirikiana na *IMO* iliandaa warsha kuhusu usalama wa usafiri katika Ziwa Nyasa na Tanganyika. Warsha hiyo ilizishirikisha nchi za jirani zinazotumia maziwa hayo ambazo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo,* Burundi, Zambia, Msumbiji na Malawi. Semina hiyo ilipendekeza njia mbalimbali za kushirikiana ili kulinda usalama wa Ziwa ya Tanganyika na Ziwa Nyasa. Aidha, semina za kuhamasisha watumiaji wa vyombo vya usafiri majini zimefanyika katika Mikoa ya Mwanza, Rukwa pamoja na Kigoma. Katika semina hizo Serikali imeweza kuweka mikakati ya makusudi ya kuwawezesha watumiaji wa usafiri wa maziwa kuwa na nyenzo imara za kujiokolea, mawasiliano na kuwaelimisha jinsi ya kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuyashukuru Mashirika hayo ya kimataifa na wadau wengine kwa ushirikiano na misaada yao inayotuwezesha kuendesha mafunzo ambayo ni muhimu katika kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri na hivyo kuweza kupunguza ajali. Ni matarajio yetu kuwa usimamizi wa usafiri na usalama wa vyombo vya majini, utaimarika zaidi baada ya Serikali kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA).*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha lieleza Bunge lako Tukufu, *SUMATRA* ilianzishwa rasmi kwa tarehe 20 Agosti 2004, kwa Tangazo la Serikali Na. 297/2004. Utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ulianza mwezi Januari 2005 baada ya kukamilisha uundwaji wa Bodi na uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Mamlaka husimamia na kudhibiti usafiri katika sekta za reli, barabara na usafiri wa majini.

Mheshiwiwa Spika, madhumuni ya *SUMATRA* ni:-

(i) Kuhimiza/Kukuza ushindani na ufanisi katika soko la usafirishaji wa nchi kavu na majini.

(ii) Kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma

(iii) Kulinda na kujenga mazingira ya kuvutia kwa watoa huduma.

(iv) Kuendeleza na kuhakikisha kuwa huduma za usafirishaji zinakidhi mahitaji ya watumiaji.

(v) Kuwaelimisha watumiaji huduma na wananchi kwa ujumla kuhusu sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na:-

(a) Haki na wajibu wa walaji na watoa huduma na bidhaa.
(b) Jinsi ya kuwakilisha malalamiko/ migongano na utatuzi wake.
(c) Kazi na majukumu ya Mamlaka.

(vi) Kuboresha na kusimamia viwango vya usalama katika sekta zinazosimamiwa na kudhibitiwa na Mamlaka.

(vii) Kuhakikisha kwamba watoa huduma na watumiaji wanalinda na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Mamlaka ni :-

(i) Kusimamia na kudhibiti usalama wa usafirishaji wa majini, reli na barabara.

(ii) Kutekeleza majukumu yaliyo chini yake kwa mujibu wa sheria za kisekta.

(iii) Kutoa leseni na kuweka viwango na masharti mengine kwa watoa huduma za usafiri wa majini, reli na barabara.

(iv) Kusimamia utendaji kazi wa sekta zilizo chini ya Mamlaka.

(v) Kuratibu na kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migongano katika soko la usafirishaji katika sekta za majini, barabara na reli.

(vi) Kutoa taarifa mbalimbali kuhusu sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka na kukuza ushirikiano na Wakala zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki kifupi tangu Mamlaka imeanzishwa imeweza kutengeneza muundo na ikama ya Mamlaka ili kuruhusu kujaza nafasi za kazi katika vitengo mbali mbali.Mamlaka pia imeweza kujitangaza kwa wadau na wananchi ili wafahamu vizuri zaidi majukumu ya Mamlaka. Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na *TCFB* na Mamlaka za Leseni na Usafirishaji wa Barabara na taasisi nyinginezo zilizokuwa zinatekeleza majukumu yaliyo chini ya Mamlaka hii. Ili kufanikisha shughuli hizo Mamlaka imeendelea kutumia wafanyakazi na taratibu zile ambazo zilikuwepo ili kuhakikisha kuwa watoaji na watumiaji huduma wanaendelea na shughuli zao bila kukwama.

Katika kipindi cha kuanzia Agosti, 2004 hadi Machi, 2005 Mamlaka imeweza kutoa leseni 28 za uwakala wa meli. Kabla ya Mamlaka kuanza kazi, utoaji wa leseni ulikuwa ukifanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Septemba - Desemba 2004, Mamlaka iliweza kutatua tatizo la mlundikano wa mizigo na makasha katika Bandari ya Dar es Salaam. Mamlaka ilibaini kwamba mlundikano huo ulitokana na ongezeko la kijumla la mizigo na hasa mizigo inayosafirishwa kwa makasha *(containerized cargo).* Ili kutatua tatizo hilo Mamlaka ilipendekeza hatua za muda mfupi za kurejesha matumizi ya kituo cha Makasha ya Ubungo *(Ubungo Inland Container Depot),* na mizani ya kupimia

mizigo iwekwe bandarini ili kuharakisha upimaji wa magari ya mizigo. Aidha, Mamlaka iliweza kupendekeza hatua za muda mrefu za kuanzisha vituo vya kuhudumia makasha nje ya bandari ili bandari pawe ni mahali pa kupakia na kupakua makasha tu. Kuhusu usimamizi wa huduma za usafiri wa barabara, Mamlaka inaendela kutekeleza kikamilifu majukumu yote ya iliyokuwa *CTLA* ikiwa pamoja na shughuli za Mamlaka za Leseni za mikoa ambazo zinasimamiwa na Wakuu wa Mikoa. Hivi sasa uongozi wa *SUMATRA* kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa wanaandaa taratibu rahisi wa kuendeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na sheria ya *SUMATRA,* Mamlaka pia itatekeleza majukumu ya ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini, kwa kuzingatia Sheria ya *Merchant Shipping Act, 2003.* Aidha, Mamlaka inasimamia na kudhibiti masuala hayo, ikiwa ni pamoja na kusimamia viwango vya huduma na sheria za kimataifa zinazosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini *(IMO).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yake ya msingi katika mwaka 2005/2006, Mamlaka inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kujitangaza kwa wadau kwa kuandaa semina, kutumia redio, televisheni, magazeti na kushiriki katika mikutano, semina/ kongamano.

(ii) Ili Mamlaka iweze kusimamia vizuri sekta ya usafiri na usalama wa vyombo, zoezi la kutathmini shughuli/majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na vyombo na mamlaka mbali mbali kabla ya kuanza Mamlaka, litafanyika. Zoezi litalenga katika kufahamu hali, upatikanaji na ubora wa huduma. Vile vile zoezi litalenga kufahamu udhibiti na usalama wa vyombo vya usafiri.

(iii) Mamlaka kwa kushirikiana na wadau itaandaa kanuni *(code of conduct)* kwa watoa na watumiaji wa huduma kwa ajili ya kulinda ubora wa huduma, kuhimiza ushindani na kuzuia uharibifu wa mazingira.

(iv) Ili kuinua kiwango cha utendaji kazi na kutimiza malengo yake, Mamlaka itatilia mkazo wa kutoa mafunzo ya udhibiti na usimamizi kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, huduma ya usafiri wa anga katika kipindi cha 2004/2005 ziliendelea kutolewa katika kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi hicho idadi ya kampuni za ndani zilizopewa leseni ni 27 ikilinganishwa na kampuni 29 mwaka 2003/2004. Aidha safari za ndege za kimataifa na za ndani ziliongezeka kutoka safari 158,297 mwaka 2003/2004 hadi kufikia safari 174,847 mwaka 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Ongezeko hili limetokana na sekta binafsi kujiimarisha katika utoaji wa huduma. Idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 1,876,553 mwaka 2003/2004 hadi kufikia abiria 1,950,383 mwaka 2004/2005 ambalo ni ongezeko la asilimia 3.9. Idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi kupitia kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam iliongezeka kutoka abiria 898,864 mwaka 2003/2004 hadi kufikia abiria 953,844 mwaka 2004/2005; ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.1. Idadi ya abiria waliosafiri humu nchini katika kipindi cha

mwaka 2004/2005 iliongezeka kwa asilimia 10.4, kutoka abiria 973,262 mwaka 2003/2004 hadi kufikia abiria 1,074,035. Safari za ndege za kimataifa kupitia viwanja vyetu ziliongezeka kwa asilimia 23.8, kutoka ndege 20,060 mwaka 2003/2004 hadi kufikia ndege 24,835 mwaka 2004/2005.

Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kutoa huduma za uongozaji ndege katika viwanja 13 hapa nchini. Mamlaka ilitoa huduma kwa saa 24 kwa siku katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar; kwa saa 17 katika kiwanja cha Mwanza, na kwa viwanja vya Dodoma, Arusha, Kigoma, Tabora na Pemba kwa saa 12. Viwanja vya Mtwara, Mbeya, Iringa, Tanga na Songea vilihudumiwa kwa saa 8 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Mamlaka inatarajia kutekeleza miradi ya ufungaji wa meza za kisasa za waongoza ndege pamoja na radio za kuongoza ndege katika kiwanja cha Songwe. Miradi mingine ni ya ufungaji wa vifaa vya radio za kuchunguza hali ya utendaji wa mitambo ya kuongozea ndege viwanja vya Arusha, Kigoma na Tabora. Shughuli nyingine ni kubadilisha mitambo michakavu ya kuongozea ndege kiwanja cha Tabora, ununuzi na ufungaji wa vifaa vya radio za dharura kwa viwanja vya Songwe, Dodoma na Kigoma na kufunga mtambo wa usambazaji wa mawimbi ya radio Mkoa wa Ruvuma. Aidha, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufunga mitambo ya nguvu ya mionzi ya jua kwa ajili ya umeme wa akiba kwa viwanja vya Songwe na Tabora na kuanza kutoa huduma za uongozaji ndege kiwanja kipya cha Songwe. Mamlaka pia itahakikisha kuwa miundombinu iliyowekwa kwa ajili ya usalama wa anga inakuwa salama na endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha utendaji mwaka 2004/2005 wahitimu 15 kutoka Chuo Kikuu walifuzu mafunzo na kuajiriwa na Mamlaka. Aidha, Mamlaka ilihuisha mpango wa mafunzo ya marubani ili kukabiliana na upungufu wa marubani nchini. Marubani 5 akiwemo mwanamke mmoja waliopelekwa Afrika ya Kusini kwa mafunzo ya mwaka mmoja wa urubani walihitimu. Tayari marubani hao wameajiriwa na kampuni mbalimbali za ndege nchini. Wahandisi wawili (2) akiwemo mwanamke mmoja ambao wako Ethiopia kwa mafunzo ya miaka miwili katika fani ya matengenezo ya ndege *(Aircraft Maintenance Engineering)* wanaendelea na masomo yao. Mamlaka itaendelea kutoa na kusimamia mafunzo ya marubani na wahandisi ili nchi iwe na wataalam wazalendo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia sera ya kuwezesha viwanja vya ndege kujiendesha kibiashara, kujitosheleza na kujitegemea. Mamlaka iliendelea na matengenezo ya kawaida ya viwanja ili kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama. Aidha, Mamlaka imekamilisha matengenezo makubwa ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo. Matengenezo mengine yaliyokamilika kwenye kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam ni pamoja na ufungaji wa vivuko *(airbridge)* vinne kati ya vitano vya abiria kutoka kwenye ndege. Aidha, mradi wa ukarabati wa mfumo wa umeme katika Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam ulikamilika.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea kuimarisha usalama wa viwanja vingine. Kwa kuanzia Mamlaka itaimarisha ulinzi katika viwanja vya Arusha, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Tabora, Kigoma, *Lake Manyara,* Lindi na Dodoma. Katika jitihada hizo Mamlaka inaendelea kujenga uzio katika viwanja vya Mwanza, Mtwara, Kigoma, Moshi, Bukoba, Lake Manyara, Musoma na Dodoma.

Hatua nyingine za uimarishaji usalama ni pamoja na ununuzi wa mitambo ya kutambua mabomu, ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa mizigo, ununuzi wa milango maalumu ya ukaguzi wa abiria na mashine maalum za mkono za kutambua vyuma. Aidha, mtambo maalum wa kuona kwa njia ya televisheni *(CCTV)* utawekwa katika Kiwanja cha Kimataifa cha Dar es Salaam. Pia vifaa maalum vya doria ikiwa ni pamoja na magari, pikipiki na darubini maalum vitanunuliwa kwa ajili ya viwanja vitano vya *DIA*, Arusha, Mwanza, Mtwara na Dodoma. Huduma za zimamoto pia zitaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, *TAA* imekamilisha mradi mkubwa wa ukarabati wa umeme *(power supply system)* katika kiwanja cha Dar-es-Salaam. Taratibu zinafanyika za ununuzi na usimikaji wa mitambo *(common user terminal equipment-CUTE)* kwa ajili ya kuhudumia na uhakiki wa mizigo na abiria, ili kwenda sambamba na mifumo ya kisasa iliyopo kwenye viwanja vingine vya kimataifa duniani. Mamlaka inaendelea na ukarabati mkubwa wa barabara ya kurukia na kutua ndege, maegesho ya ndege pamoja na viungio vyake. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi.

Mheshimiwa Spika, matengenezo yaliyofanywa na Mamlaka kwenye kiwanja cha ndege cha Mwanza ni pamoja na ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilometa 10, kwa awamu ya kwanza, kuzunguka kiwanja, kwa ajili ya kuimarisha usalama. Ujenzi wa awamu ya pili yenye urefu wa kilometa 4.8 pia inaendelea. Matengenezo ya maeneo ya maegesho ya ndege za mizigo na abiria pamoja na viungio vyake yameendelea kufanyika hivyo kuwezesha ndege kusimama kwa usalama. Katika kiwanja cha ndege cha Arusha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha awamu ya kwanza ya ukarabati wa mita 500 wa njia ya kurukia na kutua ndege. Ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilometa 4.5 kuzunguka kiwanja kwa ajili ya kuimarisha usalama unaendelea. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka imefanikiwa kupata eneo la ekari 200 kwa ajili ya uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha. Aidha, kazi mbalimbali zilifanywa kukiendeleza kiwanja cha ndege cha Mtwara ikiwa ni pamoja na kufanya matengenezo ya njia ya kurukia na kutua ndege pamoja na ukarabati wa jengo la abiria.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa kiwanja kipya cha Ndege cha Songwe, Mbeya unaendelea. Ujenzi wa kituo cha nguvu za umeme umekamilika. Ujenzi wa jengo la kufikia abiria *(arrival terminal),* ujenzi wa kituo cha Zimamoto, kituo cha kuongozea ndege, na ujenzi wa barabara ya kurukia na kutua ndege unaendela. Kazi nyingine ni ujenzi wa maeneo ya maegesho ya ndege, viungio vyake na miundombinu mingine ya kuwezesha ndege aina ya *B737* kutumia kiwanja hicho. Serikali imepata mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 7.0 toka Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa awamu ya pili ya kiwanja cha ndege cha Songwe.

Serikali pia inatarajia kupata mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 4.6 kutoka mfuko wa *OPEC (OPEC Fund).* Kazi za Ujenzi wa kiwanja hicho inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha viwanja vingine matengenezo yalifanyika kwenye viwanja vya Musoma, Tabora, Bukoba, *Lake Manyara,* Shinyanga, Lindi, Kigoma na Dodoma hasa kwenye barabara za kurukia na kutua ndege. Aidha, katika kuimarisha usalama wa viwanja vyetu na hasa kufuatia matukio ya kigaidi duniani, Mamlaka inaendelea na juhudi za kuinua viwango vya usalama hasa katika viwanja vya *DIA,* Arusha, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Tabora, Kigoma, Lake Manyara, Lindi na Dodoma kwa kuanzia. Mamlaka inaendelea na ujenzi wa uzio katika viwanja vya Mwanza, Mtwara, Kigoma, Moshi, Bukoba, Lake Manyara, Musoma na Dodoma ikiwa ni hatua za kuimarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kutoa huduma na kuvifanyia matengenezo viwanja vya ndege nchini. Huduma za matengenezo zitaelekezwa kwenye viwanja vinavyohudumia ndege za abiria zenye ratiba *(scheduled and regular flights)* kama vile Tabora, Kigoma, Bukoba, Lake Manyara, Mafia, Shinyanga,Tanga na Lindi. Vile vile Serikali imeweka mipango endelevu itakayowezesha kuboresha miundombinu ya viwanja vya *DIA,* Mwanza, Arusha, Bukoba, Singida, Mafia na Songwe. Barabara za kurukia na kutua, maegesho pamoja na viungio vyake, kwa pamoja vitafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makazi yanayozunguka Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam *(DIA),* Serikali imeamua kuwa eneo la Kipawa liwe eneo mahususi la *DIA.* Makazi ya Kigilagila na Kipunguni yatarasimishwa ndani ya umiliki wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa masharti yatakayozingatia pamoja na mambo mengine, usalama wa kiwanja na Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* ilianzishwa rasmi baada ya kubinafsishwa kwa lililokuwa Shirika la Ndege Tanzania *(ATC),* Desemba 2002. Utendaji wa Kampuni hii imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwisho wa kipindi cha mwaka 2003/2004 Kampuni imeweza kuhudumia vituo tisa (9) ambavyo ni Dar es salaam, Zanzibar, Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Johannesburg, Entebbe na Hahaya. Aidha, imeweza kubeba abiria 217,261 na imeweza kubeba tani za mizigo 1,200, katika kipindi hicho.

Kwa kipindi cha 2003/2004, Kampuni iliingiza mapato kiasi cha shilingi bilioni 39.6. Kati ya mapato hayo shilingi bilioni 35.9 zilitokana na biashara ya kusafirisha abiria na mizigo wakati shilingi bilioni 3.7 zilitokana na mapato mengine. Aidha, Kampuni iliweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi baada ya kuwa na Muundo mpya wa ajira ya wafanyakazi unaokubalika na hivyo kuongeza mshikamano katika Kampuni. Mafanikio mengine ya Kampuni ni ongezeko la idadi ya ndege zake kutoka 1 iliyorithi (kutoka *ATC*) hadi nne (3 aina ya *Boeing 737* na 1 aina ya *Fokker 28).* Hali hii iliwezesha ongezeko la mapato *(turnover)* kwa zaidi ya mara mbili kutoka shilingi bilioni 15 kwa

mwaka wakati Shirika la Ndege la Tanzania *(ATC)* lilipobinafisishwa hadi shilingi bilioni 39 kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimwa Spika, Kampuni pia ilipata ongezeko la abiria kutoka wastani wa abiria 84,000 hadi 217,000 kwa mwaka. Katika kipindi hicho pia kumekuwepo na ongezeko la mtandao *(route network)* kutoka safari 10 za ndani kwa juma kwenye vituo vya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Zanzibar na Mtwara. Mafanikio mengine ya Kampuni ni ongezeko la kiwango cha ndege kuondoka kwa wakati (on time performance) kutoka asilimia 54 hadi asilimia 90. Aidha Kampuni imeweza kusimamia vizuri matumizi ya fedha, matunzo ya ndege na masuala ya kiufundi kwa kutumia teknolojia ya kompyuta *(IT).* Ili kuongeza ufanisi katika utendaji, marubani wote 19 wa kampuni wamepata mafunzo. Wahudumu wa ndege na kada nyingine kama mafundi, wahasibu na wafanyakazi katika kitengo cha biashara nao wameendelezwa. Mafunzo hayo yamefanyika nchini Afrika ya Kusini kwa kiwango kikubwa na mengine yamefanyika Dar es salaam kwa kutumia wakufunzi wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kampuni ilikabiliwa na changamoto ya ushindani wa usafiri wa anga ndani na nje ya Tanzania kutoka kwa mashirika mengine yanayoendesha biashara ya usafiri wa anga.

Katika kutatua changamoto hii, Kampuni imeendelea kuboresha mipango yake kila mara na pia kubuni mikakati ya biashara kama vile aina za ndege zinazofaa zitumike kwenye njia zipi, na namna ya kupunguza matumizi bila kuathiri ubora wa huduma. Mipango mingine ni kuongeza ufanisi na uadilifu wa wafanyakazi, kuongeza ushirikiano wa kibiashara kwa mfano *code-share,* kati yake na mashirika mengine ya ndege ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kampuni inakabiliwa pia na changamoto ya namna ya kuongeza mtandao wake hasa wa masafa marefu ili kupata wateja kutoka nchi za nje na kuongeza abiria katika mtandao uliopo tayari. Hata hivyo Kampuni inategemea kutatua tatizo hili kwa kuhudumia njia nyingi zaidi ikianzia na Dubai, Mumbai, Harare na Lusaka. Upanuzi huu utapelekea kuongeza vifaa vya utendaji na mafunzo ya wafanyakazi katika kada mbalimbali. Upanuzi huu pia unalenga kukiwezesha kituo cha Dar es Salaam kuwa kitovu kimojawapo cha usafiri wa anga kwa kanda ya Afrika ya Mashariki *(Regional Hub).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wakala wa Ndege za Serikali uliendelea kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa katika kutoa huduma zake kwa viongozi. Katika kipindi hicho uwezo wa kuwabeba viongozi uliongezeka baada ya kuwasili kutoka Marekani kwa ndege yenye uwezo wa kuruka masafa marefu inayohudumia viongozi wakuu wa Serikali. Ndege ya F.28 inaendelea kutoa huduma kwa viongozi wa Serikali na vilevile kukodishwa kwa watu binafsi.

Ndege aina ya F.50 imendelea kutoa huduma kwa Serikali na wananchi, Ndege aina ya *Piper Navajo* inaendelea kukarabatiwa ili iweze kutoa huduma ya uhakika kwa Serikali na wananchi. Wakala umefanikiwa kukusanya madeni yake ya huduma za

ukodishaji ndege kwa asilimia 75. Madeni mengine sugu yamekabidhiwa kwa watalamu wa kukusanya madeni *(Debt collectors).* Wakala umelipa madeni yote ya vipuri na kuwa na uwezo wa kukopeshwa na watoaji huduma. Hatua hii imeongeza muda wa urukaji wa ndege.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma zake,wakala umekamilisha jengo la *Flight Operations* lililoko *DIA* na ofisi yake kuhamishiwa huko ili kuweza kutoa huduma zake kwa urahisi na ufanisi zaidi. Wakala uliendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kuwa na *incentive package and scheme of service* wa kuwapatia mishahara mipya na kuwapandisha vyeo. Aidha, Wakala umeendelea kuajiri watumishi wapya wenye sifa katika hatua ya kuboresha kazi, kwa kuzingatia muundo mpya wa Wakala wa kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na ushindani, mikakati mbalimbali ya kuboresha biashara iliendelea kutekelezwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kubadilisha mfumo wa ukodishaji ndege kwa wateja wasio wa Serikali kwa kufanya malipo kabla ya huduma, wanahewa na watumishi wengine kupewa mafunzo ili kukidhi mahitaji ya Wakala, kuendelea kununua vifaa mbalimbali vya ofisi kama kompyuta pamoja, na ukarabati wa majengo ya ofisi na matengenezo ya ndege na magari.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza biashara na mapato, mwaka wa 2005/2006 Wakala utaendelea kutoa huduma kwa viongozi wakuu wa Serikali kwa kutumia ndege mpya ya *Gulfstream G550* kwa safari za masafa marefu na kukodisha ndege nyingine kwa watu binafsi ili kuweza kuiongezea Wakala mapato.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza mikakati ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi kwa kuendelea kuboresha huduma na miundo ya usafiri nchini. Lengo hilo linatekelezwa kwa kuendeleza mpango wa kanda za maendeleo *(Development Corridors).* Kanda hizo ni Ukanda wa Maendeleo wa *Mtwara (Mtwara Development Corridor)* kutoka bandari ya Mtwara hadi Mbamba Bay na kuhusisha mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, Iringa na Mbeya. Ukanda huu unaunganisha nchi za Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia. Ukanda wa Dar es Salaam unaunganisha bandari ya Dar es Salaam na Tunduma-Mbeya. Ukanda wa Kati ni kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi Kigoma/Mwanza. Ukanda huu unaiunganisha Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo (DRC),* Rwanda, Burundi na Uganda. Ukanda wa Tanga unaanzia bandari ya Tanga na unaishia Ziwa Victoria na kuunganisha Tanzania na nchi za *DRC,* Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine iliendelea na jitihada za kuimarisha kanda hizo. Kwa upande wa ukanda wa Mtwara, mpango wa utekelezaji *(Action Plan)* uliandaliwa na kukamilika. Hatua ya kufanya upembuzi yakinifu wa awali *(pre-feasibility study)* kabla ya kuendelea na hatua ya upembuzi yakinifu ya miradi mbalimbali iliyo chini ya ukanda huo inaendelea. Mipango hiyo itakapokamilika Serikali itaendelea kuwahamasisha wawekezaji ili waweze kuwekeza katika kanda hizo. Aidha kupitia mpango huu inatarajiwa kuanzishwa kwa Maeneo ya Biashara Huru *(EPZ)* kwenye bandari na kiwanja cha ndege cha Mtwara.

Wakuu wa nchi za Malawi, Msumbiji, Zambia na Tanzania walisaini makubaliano ya pamoja ya kuendeleza ukanda wa Mtwara mwezi Desemba 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuboresha huduma za usafiri wa meli katika ziwa Nyasa, Serikali za Tanzania na Malawi zilisaini makubaliano ya awali *(MOU)* kwa ajili ya kuweka kivuko chenye uzito wa juu *(Heavy Capacity Ferry).* Kivuko hiki kinatarajiwa kufanya kazi kati ya bandari za *Mbamba Bay* na *Nkhata Bay.* Kutokana na makubaliano hayo yaliyosainiwa mwezi Oktoba, 2003 Serikali hizo kwa pamoja zimeandaa mchanganuo wa mradi *(Project Proposal)* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study).* Hatua iliyofikiwa ni ya kupeleka maombi kwa wafadhili walengwa *(Potential donors)* kwa ajili ya kufadhili mradi huo. Aidha, mradi huo wa kivuko cha kuunganisha *Nkhata Bay* na *Mbamba Bay* umepewa kipaumbele katika idadi ya miradi ya Tanzania iliyowasilishwa *NEPAD*. Inatarajiwa kuwa mradi huu utakapotekelezwa utasaidia kuimarisha shughuli za maendeleo katika maeneo yanayozunguka bandari hizo.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Dar es Salaam unalenga kuboresha utumiaji wa reli ya *TAZARA,* barabara ya *TANZAM* na bomba la Mafuta la *TAZAMA* katika kusafirisha shehena za nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi na Zambia. Kamati ya pamoja ya kuratibu utekelezaji wa shughuli za ukanda huo imeundwa.

Ili kuwa na msimamo wa pamoja katika kuendeleza ukanda wa Kati, Mwezi Machi, 2005 ulifanyika mkutano wa pamoja uliozijumuisha nchi za Tanzania, Burundi, *DRC,* Rwanda na Uganda, kwa lengo la kuwa na makubaliano ya pamoja ya jinsi ya kuratibu shughuli za kuendeleza ukanda huo. Katika makubaliano hayo ilipendekezwa kuwepo mkataba utakaoanzisha ofisi ya pamoja ya kuratibu shughuli za kanda ijulikanayo kama Wakala ya Usafirishaji wa Kanda ya Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency)* ambayo makao yake makuu yatakuwa Dar es salaam. Benki ya dunia wameombwa kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi hiyo kwa muda wa miaka mitatu ya kuanzia. Fedha hizi zitakuwa msaada *(grant).* Hatua nyingine ambayo imetekelezwa kwa ajili ya uendelezaji wa Ukanda huo ni kuwa meneja wa Mradi *(Project Manager)* ameajiriwa na ameanza kazi rasmi mwezi Aprili, 2005 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini *(DBSA).*

Meneja huyo ambaye ni Mtanzania ameajiriwa kwa mkataba wa muda wa miaka mitatu. Ni matarajio yetu kuwa juhudi hizi zitaleta maendeleo yanayohitajika katika kanda hizi na nchi yetu kwa ujumla. Aidha uwekezaji katika kanda hizi utasaidia nchi yetu kutumia nafasi yake ya kijiografia na hivyo kuimarisha uchumi wake kwa kuzihudumia nchi zisizo na bandari.

Mheshimiwa Spika, huduma za sekta ya mawasiliano zinaendelea kukua kwa haraka sana hapa nchini kufuatia mabadiliko ya teknolojia yanayotokea kote duniani. Mabadiliko hayo yameongeza kwa kiasi kikubwa uwekezaji kwenye sekta katika miaka ya hivi karibuni. Kwa ujumla sekta hii inajumuisha huduma za simu za msingi na zile za mkononi, huduma za mawasiliano kwa njia ya posta, na mawasiliano kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeundwa kutokana na kukua na kuunganika kwa teknolojia za mawasiliano na habari. Katika kipindi cha 2004/2005 Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Mamlaka imeendelea kuboresha, kupanga na kusimamia matumizi ya masafa ya mawasiliano nchini. Baada ya kukamilika ujenzi wa jengo la mtambo wa kudhibiti masafa *(fixed frequency monitoring station)* eneo la Mikocheni, Mamlaka sasa ina uwezo wa kudhibiti masafa. Aidha, Mamlaka imekamilisha taratibu za ununuzi wa software ambayo itasaidia kurahisisha kazi ya kupanga matumizi ya masafa *(frequency planning).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka pia imeendelea na jukumu la kutoa leseni kwa kampuni za kusafirisha vipeto *(courier companies).* Idadi ya kampuni zilizopewa leseni ya kutoa huduma hizo mpaka sasa inafikia 16, likiwemo Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yake mengine, Mamlaka inaiwakilisha Tanzania katika mashirika ya kimataifa yafuatayo:-

(i) Shirika la Kimataifa la Simu Duniani *(International Telecommu nication Union - ITU)* lenye makao makuu mjini Geneva, Uswisi;

(ii) Shirika la Mawasiliano ya Simu Jumuiya ya Madola *(Common wealth Telecommunications Organization - CTO),* lenye makao makuu London, Uingereza;

(iii) Umoja wa Posta Duniani *(Universal Postal Union - UPU)* lenye makao makuu Berne, Uswisi;

(iv) Shirika la Mawasiliano ya Simu Afrika *(African Telecommunica tion Union - ATU)* lenye makao makuu mjini Nairobi, Kenya;

(v) Umoja wa Posta Barani Afrika *(Pan African Postal Union - PAPU)* lenye makao makuu Arusha;

(vi) Chama cha Wadhibiti wa Mawasiliano Kusini mwa Afrika *(Tele communications Regulators Association of Southern Africa - TRASA)* chenye makao makuu Gaborone, Botswana; na

(vii) Umoja wa Wadhibiti wa Mawasiliano na Watoa Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Posta Afrika Mashariki *(East Africa Regulatory, Postal and Telecommunications Organization (EARPTO).*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko kuhusu gharama za matumizi ya simu. *TCRA* ilitoa zabuni kwa Kampuni ya Analysys ya Uingereza kuchunguza gharama halisi za mawasiliano nchini ili kuweka msingi wa kufanya makadirio ya gharama za maingiliono ya simu *(interconnection).* Baada ya kampuni hiyo kukamilisha kazi yake, *TCRA* imeweza kupanga gharama zinazokubalika za maingiliano ya mawasiliano ya simu

katika kipindi cha miaka minne ijayo kuanzia mwaka 2005. Hatua hii inatarajia kumaliza migogoro kati ya kampuni za mawasiliano na hatimaye kuyawezesha kupunguza bei kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 sekta ndogo ya posta imefanya vizuri kulinganisha na mwaka uliotangulia hasa katika maeneo ya ushindani, wingi na ubora wa huduma. Mamlaka ya Mawasiliano imekuwa na mikakati ya kusimamia na kuendeleza sekta ya posta ikiwa ni katika kutekeleza sera ya Posta nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha huduma za msingi za Posta, kuanzisha na kuendeleza mfumo wa anwani nchini na kushirikisha sekta binafsi katika utoaji huduma za posta nchini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekuwa ikitoa leseni kwa kampuni binafsi kwa kuzingatia masharti na kanuni zilizowekwa. Katika kipindi cha 2004/2005 kampuni zifuatazo zimekuwa zikitoa huduma za posta nchini:-

Huduma za kimataifa *(International couriers); DHL Worldwide Express,TNT Express Worldwide, Skynet Worldwide Express, East Africa Courier na Sangare Enterprises.* Huduma za ndani ya nchi *(Domestic couriers)* ni:- *Scandinavia Bus Express,Travel Services, Ndeng'aro Agencies and Consultants, Akamba Bus Service Ltd, M/S John Terry Establishment Ltd, M/S Shift Cargo Ltd, Malai Freight Forwarders Ltd, M/S Swift Express (T) Limited, Sumry Bus Express, Millenium Trackers Ltd, Clayton Marketing, Konsad Investment, NIKI Electrical Company,Babeja Company Ltd, Alpha Quality Service, Mhasibu Consultants, Delmonte (T) Ltd, N & K Investment Ltd* na *One World Courier (T) Ltd.*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Mamlaka ya Mawasiliano iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano Mkuu wa 23 wa Umoja wa Posta Duniani uliofanyika Bucharest, Romania. Tanzania ilipata nafasi ya kuhutubia mkutano huo ambapo ilisisitiza azma yake ya kuendeleza ushirikiano na nchi wanachama wa Umoja huo na kutoa wito kwa nchi tajiri kusaidia nchi maskini kuboresha huduma za posta. Mkutano huo pia ulipitisha azimio la kufanya Mkutano Mkuu wa 24 Nairobi, Kenya mwaka 2008. Hii ni changamoto kwetu kuhakikisha kuwa inatumia fursa hiyo kuvutia wajumbe wa Mkutano huu kutembelea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Mamlaka ya Mawasiliano ina mpango wa kununua mtambo maalum ambao utakuwa unapima ubora wa huduma za posta nchini. Katika kipindi hicho Mamlaka itanufaika kwa kupata taarifa za kuaminika na za haraka katika kupima utendaji wa Shirika la Posta. Aidha katika kipindi hicho, kamati maalum itaundwa ikishirikisha Mamlaka ya Mawasiliano, Makumbusho ya Taifa, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuanzisha makumbusho ya mawasiliano Tanzania. Mapendekezo yaliyopo ni kuwa na makumbusho maalum ya mawasiliano ambayo yatahifadhi kumbukumbu za mawasiliano ya posta, simu na redio kabla ya uhuru hadi nyakati za sasa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inatarajia kufanya utafiti kuhusu utoaji wa huduma za msingi za posta *(Mapping the demand for postal service in Tanzania).* Aidha, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Posta, imeonekana kuna haja ya kurekebisha Sheria ya Posta nchini ili iendane na mazingira mapya ya uchumi wa soko.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ilitekeleza majukumu yake katika kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi hicho Kampuni ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kupanua mtandao na kuboresha huduma za mawasiliano ya simu nchini. Katika mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2004/2005, *TTCL* ilidhamiria kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mradi wa uimarishaji wa njia *(lines)* za simu kwa wateja kwa kutumia teknolojia ya *Asynchronous Digital Subscriber Lines (ADSL)* ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za kisasa (broad band) kama Intaneti, *Data,* n.k.) kwa kutumia rasilimali iliyopo ya nyaya *(copper wire).* Mradi huu kwa sasa uko katika majaribio na endapo utafanikiwa, utaanza kufanya kazi rasmi Agosti 2005. Vile vile, Kampuni iliendelea kuweka mitambo ya kuzuia wizi na hujuma *(Revenue Assurance Management System - RAMS)* kwa lengo la kudhibiti wizi na hujuma ili kuzuia upotevu wa mapato ya Kampuni. Mradi huu unategemewa kuanza kazi rasmi mnamo mwezi Septemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na uwekaji wa mitambo mipya ya *microwave* katika njia kuu *(backbone)* za Dar es Salaam/Lugoba/Mnyusi;Dar es Salaam/Lindi/Mtwara; na Mwanza/ Nyamanyama. Njia ya Dar es Salaam/Lugoba inakuwa njia mbadala *(alternative route)* ya ile inayopitia Zanzibar kuelekea Tanga/Moshi/ Arusha. Njia ya Dar es Salaam /Lindi/Mtwara itawezesha kuboresha huduma kwenda mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kuondolewa mtambo wa zamani wa *VSAT* ulioko Mtwara pamoja na kuwezesha kuondolewa mitambo ya simu za kukoroga *(magneto)* huko Kibiti, Utete, Muhoro, Kilwa Masoko na Mafia. Njia kuu ya Mwanza/Nyamanyama itawezesha kupeleka laini za kutosha za simu za *digital* kuelekea Bukoba na Kigoma pamoja na nchi jirani za Uganda, Rwanda na Burundi. Katika mwaka 2005/2006 *TTCL* imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 13.6 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iliyofanyika katika kipindi cha mwaka 2004/2005 ni uondoaji wa mitambo *(switch)* inayotumia teknolojia ya *analogue /magneto* na kuweka mitambo ya kisasa inayotumia teknolojia ya *digital*. Mitambo ya kukoroga *(manual boards)* imeondolewa huko Kondoa, Tunduma, Kiomboi na Namanyere, wakati mitambo ya *analogue* imeondolewa huko Mtwara, Tabora na Mwanza. Kazi ya kuondoa mitambo ya kukoroga iliyobaki inaendelea awamu kwa awamu kulingana na bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, *TTCL* imepanga kutekeleza mikakati na kufikia malengo yatakayokidhi mahitaji ya uchumi wa soko. Katika kipindi hiki, *TTCL* itatekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na

uwekaji wa njia kuu ya *backbone digital microwave link* ya Dodoma hadi Mbeya kupitia Iringa na Nyololo. Mtambo uliopo Dodoma ni wa zamani utapanuliwa kutoka njia 1,900 kwenda njia 3,800. Aidha, njia ndogo *microwave - 480 channels* iliyopo kati ya Dodoma na Kondoa/Babati itaendelezwa hadi kufika Arusha na hivyo kuwezesha kupatikana kwa njia nyingine mbadala kwenda/kutoka Arusha.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuondoa simu za kukoroga na kuweka simu za *digital* itaendelea katika kipindi hiki. Miji itakayofaidika na mradi huu ni Nachingwea, Liwale, Ruangwa, Itigi, Malya, Ngudu na Misungwi ambayo itapata huduma za kisasa. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Kampuni pia inatarajia kuboresha huduma kwa kuweka *switches* mpya katika baadhi ya miji ya mikoa mbalimbali. Lengo ni kubadilisha mitambo *(switch)* ya zamani na kuweka mipya ili kukidhi mahitaji halisi ya simu kwa sasa. Mitambo itakayoondolewa na kubadilishwa na mingine ni pamoja na *GX 5000* ya Arusha, *Neax 61E* za Moshi, Tanga na Mkoani, na *HDX 10* ya Morogoro, *Fetex 150* za Singida, Bukoba na Kigoma. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2005. Ili kukidhi mahitaji ya huduma za mawasiliano katika nyanja za biashara na uchumi kuelekea nchi za jirani, Kampuni imepanga kuweka *Cross Border Links* katika njia ya Mbeya-Kasumulo-Songwe (Malawi); Nyamanyama-Bukoba-Uganda; na Nyamanyama-Kigoma. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2005. Miradi yote hiyo itakapokamilika mtandao utakuwa umepanuka. Njia za mawasiliano kati ya miji mikuu zitakuwa zimeboreshwa na huduma za mawasiliano kwa ujumla zitakuwa za uhakika. Mafanikio haya yanategemea kuongeza mapato ya Kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitafakari majukumu ya kimsingi ya *TTCL* baada ya kuzingatia pamoja na mengine, kukua kwa haraka kwa sekta ya mawasiliano, mabadiliko makubwa na ya haraka ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kwisha kwa muda wake wa ukiritimba, mabadiliko ya soko na huduma za mawasiliano na mfumo mpya wa utoaji leseni, na kuwepo kwa kampuni nyingi za mawasiliano.

Serikali imeamua kwamba *TTCL* iwe muhimili mkuu wa mawasiliano nchini (national backbone) na kuwa mtoa huduma kwa watoa huduma *(carrier of carriers).* Nafurahi kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba kwa makubaliano na mbia wetu katika *TTCL,* usimamizi wa *TTCL,* kwa maana ya Bodi na Menejimenti *(Board and Management Control)* sasa unarudishwa kwa mwenye hisa nyingi katika *TTCL*, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, huduma za simu za mkononi zimeendelea kupanuka katika sehemu mbalimbali nchini. Huduma hizi zimeendelea kutolewa na Kampuni za *Vodacom, Celtel, Mobitel* na *Zantel.* Kampuni ya Vodacom imepanua mtandao wao kufikia sehemu zifuatavyo:- Dar es Salaam: Jiji la Dar es Salaam; Pwani: Kisarawe, Bagamoyo, Mkuranga, Kibaha, Chalinze, Mafia, Mlandizi na Kinyerezi; Tanga: Tanga Mjini, Muheza, Lushoto, Segera na Korogwe; Morogoro: Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Kilosa, Mvomero, Mtibwa Sugar,Turiani na Gairo; Dodoma: Dodoma Mjini,

Kongwa, Dodoma Vijijini; Singida: Singida Mjini, Singida Vijijini, Manyoni, Iramba; Arusha : Arusha Mjini, Arumeru, Monduli, Makuyuni, Ngorongoro, Karatu, Namanga; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Hai, Rombo, Marangu, Moshi Vijijini, Mwanga, Same na *Kilimanjaro Airport;* Manyara: Mererani, Ngorongoro, Babati, Hanang, Mbulu na Simanjiro; Mara: Musoma Mjini, Musoma Vijijini, Bunda, Sirari, Serengeti na Tarime; Mwanza: Mwanza Mjini, Nyamagana, Magu, Misungwi, Ilemela, Sengerema na Geita; Kagera: Bukoba Mjini, Karagwe, Bukoba Vijijini, Muleba, Ngara, Biharamulo; Shinyanga: Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini, Mwadui, Maswa, Bariadi, Isaka na Kahama, Meatu, Kishapu, Bukombe na Tinde; Tabora: Tabora Mjini, Igunga, na Nzega; Kigoma: Kigoma Mjini, Kigoma Vijijini, Rukwa: Sumbawanga; Lindi: Lindi Mjini, Nachingwea, Mtwara: Mtwara Mjini, Masasi, Newala; Ruvuma: Songea Mjini, Tunduru, Songea Vijijini, Mbinga; Mbeya: Mbeya Mjini, Rujewa, Mbalizi, Chimala, Vwawa, Mlima Nyoka, Songwe, Kyela,Tunduma, Bulyaga,Uyole, Kiwira, Igurusi, Mabarali, Mbozi na Tukuyu; Iringa: Iringa Mjini, Tanangozi, Ifunda, Mafinga, Ludewa, Makambako, Njombe; Zanzibar: Unguja Kaskazini A, Unguja Kaskazini B, Magharibi, Kusini, Wete, Micheweni, Chakechake, Mkoani.

Aidha, mtandao wa Vodacom uko katika barabara kuu zifuatazo:- Arusha-Makuyuni-Monduli-Ngorongoro; Moshi-Arusha-Namanga; Dar es Salaam-Kibaha-Chalinze-Morogoro-Ifakara; Chalinze-Segera-Tanga; Segera-Same-Moshi-Mwika-Marangu; Iringa-Makambako-Njombe; Makambako-Mbeya-Tunduma; Mbeya-Tukuyu-Kyela; Nzega-Shinyanga-Mwadui; Shinyanga-Isaka-Kahama-Sengerema; Mwanza-Sengerema-Geita-Muleba-Bukoba. Kampuni ya Vodacom imepanua mtandao wake katika mikoa yote ya Tanzania. Hadi kufikia Desemba, 2004 Vodacom ilikuwa na wateja wapatao 1,050,000. Kufikia Mei, Kampuni ilikuwa na wateja 1,283,370.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel* imeeneza huduma zake katika sehemu zifuatazo:- Arusha:Arusha Mjini, Arumeru, Ngaramtoni, Mererani, Tengeru, *KIA,* Makuyuni,Namanga,Ngorongoro, *Usa-river,* Monduli na Longido, Geikurum, Kisongo, Lengijabe, Losiminguri na Buti; Dar es Salaam: Temeke, Kinondoni na Ilala; Dodoma: Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini, Kwambe, Kongwa, Mpwapwa, Kibaigwa, Kondoa na Chimwaga, Chamwino na Kigea; Iringa: Iringa Mjini, Tanangozi, Changalawe, Mafinga, Rungemba, Kibena, Mtwango, Ilembula, Makambako, Njombe, Nyololo, *Brooke Bond*, Ifunda, Wanging'ombe, Sawala na Kadete; Kagera: Kyaka, Kagera Sugar, Bukoba Mjini, *Kemondo Bay,* Karagwe, Rubya, Bugera, Ngara, Muleba, Rusumo, Biharamulo, Kabanga, Rulenge, Nyarugusu, Ushirombo,Chato, Kamachumu, Katoro na Kiziru; Kigoma: Kigoma Mjini na Kigoma Vijijini (Ujiji), Kibondo na Kasulu; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Moshi Vijini, Hai, Machame, Arusha-*Moshi Road, TPC,* Marangu, Moshi-Tanga Road, Himo, Mwika, Rombo, Mwanga, Same, Holili, Usangi, Hedaru,Gonja, Ndungu, Tarakea, Mlima Kilimanjaro, Kibosho, Hakwe na Karanga; Lindi: Lindi Mjini, Lindi Airport, Nachingwea, Ruangwa na Liwale; Mbeya: Mbeya Mjini, Chunya, Mbarali, Mbeya Vijijini (Songwe na Mbalizi), Mlowo, Vwawa, Tunduma, Mbozi, Mahonje, Igawa, Matema, Kasumulo Mpakani, Chimala, Igulusi, Tukuyu, Kigoe, Kiwira, Makongorosi, Makete, Rungwe, Mlima Nyoka, Mkwajuni, Ipinda, Ileje, Itungi na Kyela; Tanga: Tanga Mjini, Pongwe, Muheza, Pangani, Mombo, Lushoto, Handeni, Kilindi,

Korogwe, Tanga-*Segera Road na Segera-Chalinze road;* Pwani: Kibaha, Utete, Somanga,Rufiji, Kibiti, Wami, Lugoba, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze, Mlandizi, Bagamoyo, barabara ya Dar es Salaam- Chalinze-Segera na ya Dar es Salaam-Morogoro; Morogoro: Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Kilosa, Mvomero, Turiani, Mzumbe, Mikumi, Dar es Salaam-Mikumi Road *(Mikumi National Park),* Kilombero, Ifakara, Dakawa, Gairo,Mtibwa Sugar, Mahenge Mlimba, Ubenazomezi, Mang'ula; Manyara: *Lake Manyara* na Magugu; Mbeya: Mbeya Mjini, Chunya, Mbarali, Mbeya Vijijini (Songwe na Mbalizi), Mlowo, Vwawa, Tunduma, Mbozi, Mahonje, Igawa, Matema, Kasumulo Mpakani, Chimala, Igulusi, Tukuyu na Kyela; Ruvuma: Songea Mjini, Peramiho, Tunduru, Songea Vijijini na Mbinga; Rukwa: Sumbawanga Mjini, Sumbawanga Vijijini na Mpanda; Tabora:

Tabora Mjini, Ulyankulu, Ndala, Nzega, Usoko, Sikonge, Igunga, Kakanda, Kaliua na Urambo: Singida: Singida Mjini, Singida Vijijini, Itigi, Kondoa, Kiomboi, Shelui, Igugumo, Iramba, Manyoni na Kalesh; Shinyanga: Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini, Bariadi, Isaka, Meatu, Maswa, Kahama Mjini na Kahama Mining, Bukombe, Maganzo na Mwadui; Mwanza: Igogo Industry na Kawekamo.Kwa upande wa Tanzania Visiwani Kampuni ya *CELTEL* imepanua huduma zake katika maeneo yafuatayo: Mkoa wa Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini B, Kusini Kati, Kusini kusini. Maeneo mengine ni Wete, Micheweni, Chakechake na Mkoani. Hadi Desemba 2004 Kampuni ya *Celtel* ilikuwa na wateja wapatao 504,000. Kufikia Mei 2005, Kampuni ilikuwa na wateja 720,000.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Kampuni ya Mobitel imepanua mtandao na ilipofika Desemba 2004 ilikuwa na wateja 303,000. Sehemu ambazo mtandao huu umefika ni pamoja na Dar es Salaam: Kinondoni, Temeke na Ilala; Pwani: Kibaha, Kisarawe, Bagamoyo, Chalinze na Mlandizi. Morogoro: Morogoro Mjini, Mikumi, Kihonda; Tanga: Gomba, Buiko, Kabuku, Maramba, Mbwewe, Mikanjuni, Mombo, Tanga Cementi, Tanga Mjini, Muheza, Korogwe na Segera; Dodoma: Dodoma Mjini, Msalato; Arusha: Arusha Mjini, Ngorongoro, Tengeru, Mererani, *AICC*, Njiro, Makuyuni, Oldeani, *TANAPA,* Tengeru, *Unga Ltd,* Losiminguri na Maji ya Chai; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Rombo, Hai,Sanya Juu, Marangu, Kavambunju, *KCMC,* Kibosho, Kwa Sadala, Machame, Mwanga, *TPC*, Same na Hedaru. Iringa: Iringa Mjini, Makambako, Mafinga na Njombe; Mbeya: Mbeya Mjini, Meta; Mwanza: Sengerema, Geita, Ukerewe, Nyegezi, Bugando, Kahangara, Kawekamo, Nyanguge, Kisesa, Nasa(Bulima) Lamadi, Makongoro, Misungwi na Nyamagana; Shinyanga: Bulyankulu, Gula Hill, Malya, Maswa, Meatu, Ngudu, Isaka, Shinyanga Mjini, Kahama na Mwadui; Mara: Muganza, Bunda, Musoma, Tarime,Butiama, Mkasesero, Mbuyuni, Nyamongo, Nyamwaga, na Sirari; Kigoma: Kigoma Mjini, Garaganza, Kibondo, na Kasulu; Ruvuma: Songea Mjini, Kigonsera, Liuli, Mbamba Bay na Stone town; Mtwara: Mtwara Mjini,Tandahimba, Newala, na Lilungu; Rukwa: Sumbawanga na Mpanda; Tabora: Tabora Mjini; Zanzibar: Kaskazini A; Kaskazini B: Kaskazini B; Mjini Madharibi: Mjini Magharibi; Magharibi: Magharibi; Kusini: Kusini. Ilipofika Mei, 2005, Kampuni ilikuwa na wateja 360,000.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya simu ya Zanzibar *(ZANTEL)* imeendela kutoa huduma za simu za mkononi katika Mikoa yote ya Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Mei

2005 Kampuni ilikuwa na wateja 120,000. Imepanua huduma zake katika sehemu zifuatazo:- Nungwi, Mtoni, Makunduchi, Tumekuja, Madema, Matemwe, Mkwajuni, Mahonda, Tunguu, Kizimkazi, Hamamni, Lumumba, Michamvi, Kitongani, Kiwengwa, Chwaka, Amani, Kisiwandui, Bububu, Masingini, Fumba, Mazizini, Jambiani, Chake chake, Mkoani, Wete, Konde, Kichunjuu, Micheweni, Bhanasa, Bumbwini, Chukwani, Fuoni, Mtoni, Chaanjamjawiri na Mabenjani. Asilimia 60 ya wateja wa Zantel wako Unguja na asilimia 40 wako Pemba. Hadi Desemba, 2004 Zantel ilikuwa na wateja wapatao 85,000. Tarehe 23 Februari, 2005 Kampuni ya Zantel ilipata mwendelezo wa leseni kutoa huduma Tanzania bara. Zantel imepanga kuanza rasmi huduma hizo tarehe 7 Julai 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004 Shirika la Posta liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha wastani. Kwa kipindi hicho barua zilizotumwa na kusambazwa kupitia mtandao wa Posta ndani ya nchi zilikuwa milioni 19.0 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4 ikilinganishwa na milioni 18.2 zilizotumwa mwaka 2003. Barua zilizotumwa nje ya nchi zilikuwa milioni 7.1 ambazo ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na barua milioni 6.7 zilizotumwa mwaka 2003. Vifurushi vilivyotumwa katika soko la ndani vimeongezeka kwa asilimia 43 kutoka vifurushi 29,832 vya mwaka 2003 hadi kufikia vifurushi 42,710 vya mwaka 2004. Vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi navyo vimeongezeka kwa asilimia 13 kutoka vifurushi 6,664 vya mwaka 2003 hadi kufikia vifurushi 7,531 vya mwaka 2004. Barua zilizosajiliwa Posta (rejista) zilizotumwa katika soko la ndani katika kipindi cha mwaka 2004 zilikuwa 542,327 ikiwa ni ongezeko la asilimia 33 zikilinganishwa na rejista 405,100 za mwaka 2003. Pia rejista zilizotumwa katika soko la nje zilikuwa 69,699 ikiwa ni ongezeko la asilimia 64 zikilinganishwa na rejista 42,386 za mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 hawala za Posta (Express Money Orders) zilizotumwa zilipungua kwa asilimia 9 kutoka 269,209 mwaka 2003 hadi 246,317 mwaka 2004. Thamani halisi ya hawala za Posta kwa mwaka 2003 ilikuwa shilingi bilioni 9.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.8 za mwaka 2004. Hata hivyo kwa upande wa utumaji fedha katika nchi za Afrika Mashariki (Interstate Money Order-IMO) idadi ilipungua kwa asilimia 25 kutoka 2136 mwaka 2003 mpaka 1592 mwaka 2004. Thamani halisi za *IMO* kwa mwaka 2003 ilikuwa shilingi milioni 163.0 ikilinganishwa na shilingi milioni 207.2 kwa mwaka 2004. Aidha, idadi ya hundi za Posta (Postal Orders) ilipungua kwa asilimia 30 kutoka 15,815 mwaka 2003 hadi 10,933 mwaka 2004. Thamani halisi za hundi za Posta kwa mwaka 2003 ilikuwa shilingi milioni 180.0 ikilinganishwa na shilingi milioni 124.4 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Shirika la posta limeendelea kutoa huduma ya EMS inayohusisha ukusanyaji na usambazaji wa nyaraka na vipeto. Idadi ya nyaraka na vipeto vya haraka vilivyosambazwa ndani ya nchi viliongezeka kwa asilimia 8 kutoka 268,708 mwaka 2003 hadi kufikia 290,254 mwaka 2004. Vile vya kimataifa viliongezeka kwa asilimia 48 kutoka 19,671 mwaka 2003 hadi kufikia 29,210 mwaka 2004. Kadhalika utumaji fedha kwa njia ya haraka *(Money Fax)* uliongezeka kwa asilimia 36 kutoka 203,821 mwaka 2003 hadi kufikia 277,531 mwaka 2004.

Aidha, utumaji wa taarifa za haraka *(EMS fax Messages)* uliongezeka kwa asilimia 11 kutoka 18,826 mwaka 2003 hadi kufikia 20,964 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Shirika limeendelea kuboresha na kuendeleza huduma mpya za uwakala wa kukusanya na kufanya malipo (Post Giro), usambazaji wa mizigo (Post Cargo) na usambazaji wa matangazo (Advertising Mail) na kuendesha vituo vya huduma ya barua pepe (Internet Café). Aidha, Shirika limeendelea kuimarisha huduma zake kwa kuunganisha Posta kuu zote za mikoa kupashana habari toka ofisi moja hadi nyingine kwa kutumia teknolojia mpya ya programu ya kaunta. Mtandao wa mawasiliano wa Posta umeendelea kuimarishwa ambapo wadau wa Shirika wanatarajia kunufaika na huduma kama vile uuzaji wa stempu kupitia tovuti ya Shirika www.posta.co.tz na kutuma barua *(Hybrid Mail)* kupitia mtandao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004, Shirika liliongeza kasi ya usafirishaji na usambazaji wa barua kati ya Dar es Salaam na mikoa ya Kaskazini, Kati, Nyanda za Juu Kusini na Zanzibar kufikia siku moja (1) na kufanikiwa kwa kiwango cha asilimia 93.4. Kwa mikoa ya Magharibi, Ziwa na Kusini ilikuwa siku tatu (3) na mafanikio ni kiwango cha asilimia 94.3. Kasi ya usafirishaji na usambazaji kupitia EMS kati ya Dar es Salaam na mikoa ya Kaskazini, Kati na Nyanda za Juu Kusini pamoja na Zanzibar ilikuwa siku mbili (2) na mafanikio ni kiwango cha asilimia 98. Kwa upande wa usafirishaji nyaraka na vipeto kati ya Dar es salaam na mikoa ya Magharibi, Ziwa na Kusini kasi ilikuwa siku tatu (3) na kufanikiwa kwa kiwango cha asilimia 99.2. Kasi ya usambazaji wa hati za fedha kati ya Dar es Salaam na Mikoa ya Kaskazini, Kati na Nyanda za Juu Kusini pamoja na Zanzibar ilikuwa siku mbili (2) na kufanikiwa kwa kiwango cha asilimia 97.9. Kwa mikoa ya Magharibi, Ziwa na Kusini kati ilikuwa siku tatu (3) na kufanikiwa kwa kiwango cha asilimia 99.5.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004 Shirika lilikabiliwa na changamoto ambazo ziliathiri utendaji. Changamoto hizo ni pamoja na kupungua kwa ufanisi wa kusambaza barua kwa wateja katika maeneo ya vijijini ambako kumeathiriwa na ubovu wa miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji kwa baadhi ya njia. Changamoto nyingine ni udogo wa mtaji wa shirika. Shirika lilishindwa kununua vitendea kazi. Ilishindikana pia kuwekeza vilivyo kwenye miradi ya maendeleo na uboreshaji huduma. Hali ya ukwasi *(liquidity)* ya Shirika kutokana na madeni inasababisha Shirika kutumia kiasi cha mapato yake kulipia madeni na kushindwa kutoa huduma kwa ufanisi unaotakiwa. Aidha, ongezeko la ushindani katika sekta ya Posta kutoka kampuni binafsi zinazoendesha biashara za Posta ni mojawapo ya changamoto ambazo zinalikabili Shirika.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hizo, Shirika limeendelea kuimarisha na kuendeleza bidhaa na huduma na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Katika kuukabili ushindani Shirika lilianzisha huduma za intaneti (Internet Café), Giro ya Posta na kutumia mtandao wa Posta katika kupashana habari toka Posta moja hadi nyingine.

Mafunzo yameendelea kutolewa kwa wafanyakazi ili kuongeza uwezo na ujuzi na kuweza kuboresha utoaji wa huduma/bidhaa. Shirika pia liliendelea na jitihada za kutafuta mikopo na misaada ya kiufundi kutoka taasisi na mashirika yanayojihusisha na maendeleo ya sekta ya Posta ili kuboresha hali ya ukwasi. Shirika lilipata mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki *(EADB)* na misaada toka Umoja wa Posta Duniani.

Mheshimiwa Spika, kuongeza kasi ya kusafirisha barua, nyaraka na vifurushi toka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini, Kati na Nyanda za Juu Kusini, mpango wa *"Overnight Mail Services"* uliimarishwa. Mpango wa mpito wa miaka mitatu wa mkakati wa biashara (2005-2007) umeandaliwa ili kuliwezesha Shirika kuwa la kibiashara zaidi. Katika kuimarisha dhana ya masoko na mauzo, Shirika limeendeleza na kuanzisha uhusiano wa kibiashara na kampuni zingine kwa lengo la kupanua wigo wa soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006 Shirika linakusudia kutekeleza miradi mbalimbali ambayo ni kutumia teknolojia ya kompyuta katika mawasiliano. Shirika litaboresha majengo ya Posta na vitendea kazi na litaongeza idadi ya magari ya kusambazia mifuko ya barua.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)* ni jinsi jamii inavyoweza kukusanya, kuandaa, kutawanya na kutumia habari kwa teknolojia ya kisasa. Huduma za zinajumuisha matumizi ya simu, kompyuta, fax, barua pepe, intaneti, tovuti, televisheni, radio, magazeti na nyinginezo. Katika mazingira ya uchumi wa soko, jamii inaweza kutumia huduma za *ICT* kuweza kupata masoko, biashara, elimu, huduma za afya, bei za mazao na pembejeo, hali ya hewa, taarifa za utalii na usafiri. Ni kwa misingi hii ambapo unaweza kuona kuwa ICT ni suala mtambuka linalotoa fursa katika kunufaisha sekta zote. *ICT* imejikita kwenye mihimili mitatu ambayo inategemeana. Mhimili wa kwanza ni wa mtandao wenyewe kwa maana ya uunganishaji wa njia na namna ya mawasiliano. Mhimili wa pili ni uwezo wa miundombinu pamoja na uwezo wa watumiaji. Mhimili wa tatu ni kinachopitishwa kwenye mtandao na kuwafikia watumiaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mabadiliko ya mifumo yanayoendelea katika sekta ya mawasiliano kuanzia mwaka 1993/1994, tumeweza kuwa na mafanikio mbalimbali hususan katika matumizi ya *ICT*. Mafanikio hayo ni pamoja na kuwa na Kituo cha Kupitishia Mawasiliano ya Intaneti *(Tanzania Internet Exchange Point (TIX))* chenye lengo la kuhakikisha watumiaji wa intaneti wanabadilishana mawasiliano bila ya kupitia nchi mbadala na hivyo kupunguza gharama. Kituo hiki kilipoanzishwa mwaka 2003 mtoa huduma za Intaneti (ISP) alikuwa mmoja, hadi kufikia mwaka 2005 kituo kimewaunganisha *ISP 11*. Mgawanyiko wa ISP nchini ni kama ifuatavyo; Dar es Salaam 11; Arusha 1; Kilimanjaro 1; Mbeya 1; Mara 1; na Zanzibar 1. Katika mwaka 2005/2006 kituo hiki kinatarajiwa kuwaunganisha watumiaji wa nchi za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuunganisha huduma za intaneti kwa kila mkoa, ililazimu kuwa na vituo vya kuunganishia *(distribution point/point of presence)*. Vituo hivi vimefikia 23 kati ya hivyo 21 ndivyo vinafanya kazi. Mgawanyo wa vituo hivyo ni

kimoja kimoja kwa mikoa ya Dar es Salaam; Arusha, Kilimanjaro; Mara; Mbeya; Dodoma; Mwanza; Pwani; Iringa; Singida; Morogoro; Kigoma; Kagera; Tanga; Mtwara; Lindi; Ruvuma; Manyara; Shinyanga; Tabora na Zanzibar. Pemba na mkoa wa Rukwa tunatarajia kuwa na vituo kama hivyo ifikapo Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio hayo, kumekuwa na ongezeko pia la vituo vya huduma za tovuti *(internet Café)*. Ongezeko la ISP ndilo limefanikisha kuwepo kwa vituo vya intaneti. Kwa mfano *TTCL* ina vituo 309 vilivyogawanyika kama ifuatavyo; Dar es Salaam 230; Arusha 10; Kilimanjaro 5; Mara 2; Mbeya 5; Zanzibar 5; Dodoma 5; Mwanza 10; Pwani 5; Iringa 5; Singida 2; Ruvuma 3; Manyara 3; Shinyanga 3; Tabora 2; Morogoro 6; Kigoma 2; Kagera 3; Tanga 3 na Mtwara 2;. Shirika la Posta lina vituo 9 vimegawanyika kimoja kimoja kwa mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mtwara, Iringa, Moshi Mwanza, Bukoba na Zanzibar. Aidha, yapo pia makampuni binafsi yenye huduma kama hizo. Makampuni hayo ni pamoja na Afsat, AfriCa online na SimbaNet.

Katika kipindi hicho, kumekuwepo na kasi ya uwekezaji pia katika miundombinu na huduma za *ICT*. Uwekezaji huu umewezesha Bunge, Serikali, taasisi za elimu, taasisi za fedha, taasisi za mawasiliano na uchukuzi kutumia huduma za *ICT*. Kwa mfano Wizara nyingi zina tovuti zao ambazo zinaweza kusomwa na mtu ye yote mahali po pote.

Kama msimamizi wa Wizara inayoratibu huduma za *ICT,* napenda kulitambua Bunge lako tukufu kwa kuwa na tovuti yake. Kitaifa tunayo tovuti ya Taifa www.tanzania.go.tz, Wizara ya Fedha inatumia mtandao kwa taratibu zao za usimamizi wa fedha kwenye Wizara mbali mbali. Orodha ya tovuti za Idara mbalimbali za Serikali ni ndefu napenda kuwatambua wote kwa juhudi zao.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya *ICT* katika huduma za Benki yamepiga hatua. Karibu benki zote zina huduma za *Automatic Teller Machine (ATM)* ambazo zimerahisisha sana huduma za benki kwa mteja. Huduma za mabenki zimerahisishwa pia kwa kuunganisha mabenki mbalimbali na matawi yao, na mawasiliano ya benki moja kwenda benki nyingine. Mabenki yenye huduma kama hizo ni pamoja na *National Bank of Commence (NBC), Cooperative and Rural Development Bank (CRDB);, National Microfinance Bank(NMB)* na *Standard Charted Bank.* Mitandao pia inatumika katika kufanikisha malipo kati ya Benki Kuu ya Tanzania na mabenki mengine ndani na nje ya nchi. Aidha, taasisi nyingi za elimu zinatumia mtandao kwa ajili ya huduma mbali mbali za kielimu zikiwemo kujiandikisha, kusambaza masomo, kufanya mitihani na kupata matokeo ya mitihani. Napenda kukitambua Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine kwa jitihada zao za kuelimisha kupitia mtandao.

Mheshimiwa Spika, huduma za utangazaji nazo ni huduma za *ICT*. Mwaka 1994 vituo vya redio vilikuwa 3 na vituo vya televisheni vilikuwa 3. Katika mwaka 2005 vituo vya redio vimefikia 33 na vituo vya televisheni vimefikia 15.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ni meelezea awali, baada ya kipindi cha ukiritimba wa *TTCL* kuisha, kumekuwa na mabadiliko ya mfumo wa udhibiti. Hivi sasa *TCRA* wanatarajia kuongeza ushindani katika soko kwa kuhakikisha kuwa huduma zinakuwa bora na kwa bei nafuu. Chini ya utaratibu huo, udhibiti utafanyika kuzingatia

huduma inayotolewa bila ya kuangalia aina ya teknolojia. Aidha, huduma za simu kwa sasa zinaweza kupitia kwenye mtando wa intaneti kitaalam unaitwa *Voice over Internet Protocol.* Mteja atatumia mtandao wa intaneti kwa kupitisha sauti kama njia mbadala ya matumizi ya simu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja kati ya nchi 191 za wanachama wa Umoja wa Mataifa iliyoazimia kufikia Malengo ya Milenia ya Umoja huo *(UN Millennium Goals).* Kwa mazingira ya uchumi wa soko na mabadiliko ya teknolojia, malengo hayo yanaweza kufikiwa kwa urahisi iwapo mwelekeo huu wa jamii katika matumizi ya *ICT* utaendelezwa. Aidha, katika kufanikisha matumizi ya *ICT* kama nchi bado tunakabiliwa na chanagamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na hali ya uchumi unaotegemea kilimo cha kubahatisha, uwezo mdogo katika uwekezaji wa miundombinu na ukosefu wa uwelewa na viwango vya elimu kuwa chini. Katika jitihada za kupambana na changamoto hizo, Serikali imeanza hatua za kuwa na mkongo wa kitaifa *(national backbone)* ambao pamoja na njia nyingine utatumia *fibre optic cable* na *satellite link* kwa ajili ya kupitishia mawasiliano kwa uwezo mkubwa kama njia mojawapo ya kuboresha miundombinu ya *ICT.*

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha Tanzania inahusika vilivyo katika mradi wa *NEPAD* wa kuunganisha Afrika ya Mashariki na mkongowa *fibre optic* utakaopita chini ya bahari ya Hindi toka Mtunzini (Afrika Kusini) kupitia Maputo, Beira, Dar es Salaam, Zanzibar, Mombasa, mpaka Djibouti. Mradi huo ukikamilika mwambao wa Afrika yote utakuwa umeunganishwa na "fibre optic" na kuwezesha mawasiliano ya haraka na gharama nafuu na sehemu nyingine duniani. *TTCL* na *Zantel* wanatuwakilisha katika mradi huo uitwao *East Afica Sub Marine Cable (EASSy).*

Mheshimiwa Spika mchakato wa ujenzi wa Jamii Habari nchini ulianza tangu mwaka 2002. Juhudi za ujenzi wa Jamii Habari ni moja kati ya mfululizo wa juhudi za Kimataifa zilizobuniwa kwa lengo la kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kupambana na umaskini duniani. Kimataifa, majadiliano yamefanyika katika ngazi ya wataalam na ngazi ya wakuu wa nchi. Maazimio mbalimbali yamepitishwa yenye lengo la kujenga Jamii Habari kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)* kama nyenzo ya kuharakisha hatua hiyo. Pamoja na maazimio ya mikutano hiyo, mpango wa programu ya kazi *(WSIS Plan of Action)* ulipitishwa. Iliamuliwa kuwa kila nchi iendelee kwa kushirikisha wadau na wananchi wote.

Katika ngazi ya Taifa, kuna mikakati mbalimbali inayotumika katika programu za utekelezaji wa ujenzi wa Jamii Habari. Katika mikakati hiyo, Serikali imeazimia kuanza na uaandaaji na uendeshaji wa Programu ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi katika ngazi zote kuhusu umuhimu wa matumizi ya *ICT* katika kufanikisha ujenzi wa Jamii Habari; kuhimiza uwekezaji na uendelezaji wa miundombinu yote muhimu ikiwemo ile ya *ICT* kwa kushirikiana na wadau wote wa nje na wa ndani ya nchi; kuandaa na kutekeleza mkakati wa kujenga uwezo wa wataalam wa fani ya *ICT* wa ngazi zote *(Human Capacity Building)* ili nchi iweze kujitegemea ipasavyo na; kufanya mapitio ya sheria, taratibu na kanuni zote nchini ili kuanisha mapungufu na kufanya marekebisho kwa lengo la kuwezesha matumizi ya *ICT* katika mchakato wa ujenzi wa Jamii Habari.

Mchakato huu utashughulikia masuala yote yakiwemo yale ya *Commerce,* Hati na Haki miliki, matumizi na usimamizi wa intaneti. Wizara kama mratibu imekamilisha mikakati ya Sera ya *ICT* ambayo itatumika katika kufanikisha programu ya Jamii Habari. Aidha, inakamilisha tathmini ya mkongo ambao utatumika kama nyenzo muhimu ya kuzambaza mawasiliano nchini. Katika juhudi hizo, Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi ya *ICT* kwa shughuli za uchumi, utawala, afya, kilimo na biashara na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhakiki na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini, pamoja na kutoa tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa kwa kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Mamlaka imefunga vifaa vya kisasa katika maeneo mbalimbali nchini. Vifaa na mitambo hii ni pamoja na vituo kumi na nne (14) vinavyopima hali ya hewa vyenyewe bila kuwepo mtu wa kuviendesha.

Mitambo mingine ni pamoja na *Meteorological Data Distribution (MDD),* mtambo ambao unaleta taarifa za hali ya hewa kwa ajili ya usafiri wa anga *(Aviation Data)* kutoka kwenye satelaiti *(Satelite Distribution System - SADIS)* ambayo inatoa takwimu kwa ajili ya usafiri wa anga na mabadiliko ya hali ya hewa, na mfumo *HORACE* ambao unaleta takwimu za hali ya hewa na hasa michoro kuonyesha mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, mitambo mingine iliyofungwa ni pamoja na *Automatic Meteorological Distribution System (AMEDIS)* ambao ni mtambo maalum unaopokea na kutuma takwimu kutoka katika vituo vya hali ya hewa hapa nchini na ule wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) uitwao *Global Transmission System (GTS)* kupitia *Regional Telecomunication Hub (RTH) Nairobi.* Mtambo huu unapokea na kutuma takwimu za hali ya hewa bila kuendeshwa na mtu. Mtambo mwingine ni *Meteosat Second Generation (MSG)* ambao unafanya kazi kama *MDD* isipokuwa katika ubora wa hali ya juu zaidi. Mitambo hii imeboresha kwa kiasi kikubwa huduma za hali ya hewa katika nchi yetu na kuongeza kwa kiasi kikubwa ubora wa takwimu na tabiri zinazotolewa. Aidha, Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006 inakusudia kuboresha huduma za hali ya hewa kwa kuiongezea Mamlaka uwezo wa kutabiri majanga na matukio yasiyo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, idadi ya vituo vya kupima hali ya hewa katika nchi yetu bado ni vichache. Kitakwimu, kila kilometa za mraba 250 kunapaswa kuwa na kituo cha hali ya hewa. Kwa ukubwa wa nchi yetu, inatakiwa kuwe na vituo angalu 100 lakini kwa sasa vipo vituo 26 tu. Katika mwaka 2004/2005 Mamlaka imefanikiwa kujenga kituo kimoja cha hali ya hewa huko Kilwa Masoko na tayari kimeanza kufanya kazi. Katika bajeti ya mwaka 2005/2006 Mamlaka imedhamiria kujenga vituo viwili vya kawaida (not automatic) huko Mpanda na Tukuyu, na kuanza matayarisho ya ujenzi wa vituo vingine huko Babati na Kibondo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)* kimeendelea kutimiza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Chuo

kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wakiwemo wanaochukua masomo ya stashahada ya juu ya uongozi katika usafirishaji pamoja na stashahada ya ufundi wa magari, stashahada ya wakala wa uchukuaji na usafirishaji mizigo pamoja na cheti cha uongozi. Ongezeko hili ni kutoka wanafunzi 351 mwaka 2003/04 hadi kufikia wanafunzi 365 mwaka 2004/2005, ikiwa ni ongezeko la asilimia nne (4%). Wanafunzi wa kike wameongezeka kutoka 48 mwaka 2003/04 hadi kufikia 65 mwaka 2004/2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 35. Ongezeko hili limetokana na jitihada za makusudi zilizofanywa za kuhakikisha kuwa idadi ya wanafunzi wa kike inaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usafirishaji kimeendelea na utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa maendeleo kwa kuzingatia dira na dhamira kama ilivyoainishwa katika Mpango huo. Hivi sasa hatua za kupitia upya sheria iliyokianzisha Chuo zimekamilika. Aidha, urekebishaji wa muundo wa utawala wa Chuo na miundo ya utumishi imekamilika kwa asilimia 90. Chuo kiliweza kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kazi za utafiti na uelekezi.

(ii) Kuanzisha Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

(iii) Kutayarishaji na kuhifadhi takwimu katika nyanja za usafirishaji na uchukuzi.

(iv) Kuongeza programu zinatakazotolewa kuanzia mwaka 2005/2006 na kuziwasilisha Taasisi ya Ufundi na teknolojia *(National Coun cil for Technical Education)* ili kupata ithibati *(Accreditation).*

(v) Kukitangaza Chuo nje na ndani ya nchi. Chuo kimeendelea kuwa na ushirikiano na vyuo vya nje na ndani ya nchi. Chuo kimeimarisha ushirikiano kwa kubadilishana wataalamu na Chuo Kikuu cha *Leeds Metropolitan* cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha ufundi *(DIT)*, Chuo cha Mabaharia na *ESAMI* cha Arusha.

(vi) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya *Ph.D.,* Shahada ya Uzamili, Shahada na Stashahada katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Wafanyakazi 20 wapo mafunzoni hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake chuo kilipata changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Chuo kinafanya juhudi za kuandaa mkutano wa wafadhili ili kupata fedha kutekeleza mpango mkakati ambao unahitaji zaidi ya dola za kimarekani milioni 11.4. Aidha, baada ya tathmini mpya ya mitaala ya chuo, Chuo kimetayarisha mitaala mipya 12 ambayo imepangwa kuanza kutumika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kina jukumu la kurasimisha taaluma *(Professionalism)* katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Utekelezaji wa jukumu hilo umeendelea vizuri hasa baada ya kuanzishwa kwa taasisi ya wataalamu wa sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini, *The Tanzania Institute of Logistics and Transport (TILT).* Kuanzishwa kwa taasisi hiyo kutakuwa chachu ya maendeleo ya

taaluma katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Inatarajiwa kuwa taasisi hiyo itakiwezesha Chuo kuendelea na kuitumia kikamilifu nafasi yake ya kuwa chuo cha pekee mashariki na kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Chuo kinatarajia kuongeza usajili kwa kiwango cha asilimia 30 ikilinganishwa na usajili wa 2004/2005. Hali kadhalika mafunzo ya kozi fupi kwa wamiliki wa magari ya abiria na mizigo, Wizara na idara mbalimbali za Serikali pamoja na asasi za umma na za watu binafsi nchini yameendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam *(DMI)* kimeendelea na kuimarisha mitaala na utoaji wa mafunzo mbali mbali ya sekta ndogo ya usafiri wa majini. Chuo kimeweza kuboresha simuleta *(Simulator)* zake za *radar* na *ARPA (Automatic Radar Plotting Aid)* ili kutoa mafunzo bora. Aidha, juhudi zinazoendelea ni za kupata ithibati *(full acreditation)* toka Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)*. Katika mwaka wa 2005/2006 chuo hicho kimetengewa fedha kwa ajili ya kununua Ship Maneuvering Simulator na hivyo kupata uwezo wa kuendesha mafunzo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usalama wa Usafiri wa Anga *(CATC )* kipo chini ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(Tanzania Civil Aviation Authority)* na kilianzishwa mwaka 1985. Chuo hiki kinatoa mafunzo maalum yanayokidhi viwango vya Kimataifa *(International Civil Aviation Organization - ICAO)* katika sekta ya usalama wa anga kwa Watanzania, nchi za Jumuiya ya nchi za kusini mwa Afrika *(SADC)*, Uganda na Rwanda. Mafunzo yanayotolewa ni ya fani za uongozaji ndege, mawasiliano, usambazaji wa taarifa za safari za ndege, usalama wa viwanja vya ndege *(Aviation Security)* na utafiti na ushauri kuhusu usalama wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Chuo kimefanikiwa kutoa wahitimu 155 katika kozi 20 tofauti. Kati ya hao, wanafunzi wasichana walikuwa 39. Kati ya hao wahitimu 119 ni Watanzania na waliobaki 36 ni wanafunzi wa kigeni ambao wametoka Uganda, Namibia na Botswana. Pamoja na mafanikio hayo, Chuo kinakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na taaluma ndogo ya walimu, kutokufahamika kwa Chuo ndani na nje ya nchi, uchakavu wa vitendea kazi na kutokuwa na majengo kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika kukabili changamoto hizi, mwaka wa 2005/2006 Chuo kina mpango wa kuongeza idadi ya wanafunzi wa nje na ndani ya nchi. Chuo kitajitangaza zaidi na hivyo kupanua masoko kufikia nchi nyingine ambazo zinahitaji huduma za Chuo. Kitafanya juhudi ili kupate ithibati ya *National Council for Technical Education (NACTE)* na pia *ICAO Trainair* ili kuingia katika mtandao wa kimataifa wa ufundishaji. Kitashirikiana kwa karibu zaidi na taasisii nyingine ndani na nje ya nchi katika kuendesha mafunzo maalum. Jengo jipya la Chuo litajengwa. Chuo kina mpango wa kupata vifaa vipya vya mafunzo na kuhamasisha wahitimu wa vyuo na shule za sekondari kujiunga na Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kipo chini ya Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA).* Chuo hiki kilianzishwa mwaka 1978 kwa ajili ya kuwaandaa wafanyakazi wa daraja la nne na la tatu *(Meteorologists Class IV-III).* Chuo hutoa mafunzo maalum kwa watumishi (Adhoc courses) ili kuwawezesha watumishi kumudu mabadiliko yanayojitokeza katika utendaji wa kila siku. Chuo pia hupokea wanafunzi wa awali *(pre-service)* ambao huchaguliwa kwa utaratibu wa usaili kwa kuzingatia sifa. Katika kipindi cha 2004/2005 wanafunzi wa awali *(pre-service)* wanaume walikuwa 18 na wanawake walikuwa 5. Kutoka kazini *(in service),* wanaume walikuwa 36 na wanawake walikuwa 18. Katika mwaka unaoanzia Januari 2005, Chuo kimepokea wanafunzi wa awali wanaume 34 na wanawake 6 na wa kutoka kazini, wanaume 13 na wanawake 6.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Chuo kilifanikiwa kuwapatia wafanyakazi wa Mamlaka mafunzo na hivyo kupunguza fedha za kigeni ambazo zingetumika kupata mafunzo kama hayo nje ya nchi. Pamoja na mafanikio hayo Chuo kinakabiliwa na uhaba wa majengo ya kufundishia; uhaba wa vifaa vya kufundishia; ukosefu wa maktaba ya kisasa; na upungufu wa waalimu wenye sifa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Chuo kinatarajia kuimarisha utendaji wake kwa kuanzisha mafunzo ya *WMO Class II* kwa ajili ya wafanyakazi wa Mamlaka na nchi jirani zikiwemo Angola, Burundi, Rwanda, Zimbabwe Malawi na Zambia. Chuo pia kinatarajia kuanza kutoa Mafunzo ya *IT (Information Technology).*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara ilianza kutumia mfumo wa kuboresha utendaji kazi serikalini *(Performance Management System).* Aidha, Wizara imekamilisha mkataba wa huduma kwa wateja *(Client Services Charter)* na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza rasmi mwaka 2005/2006.

Kuhusu mapambano dhidi ya janga la UKIMWI, Wizara kwa kushirikiana na Taasisii ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS)* iliendelea na jukumu la kuendesha mafunzo mbalimbali kwa nia ya kuwaelimisha watumishi. Wizara inatarajia kuendelea na mafunzo kama hayo kwa mwaka 2005/2006 ikiwa ni juhudi za kuhakikisha kuwa watumishi wake wanaelewa na kubadirisha mwenendo wao. Aidha, Wizara pia itaendelea kutoa semina za maadili ya utumishi, utawala bora ikiwemo rushwa kwa watumishi wake ili kuongeza ufanisi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na juhudi za kuwapatia mafunzo watumishi wake ili kuwaongezea ujuzi na uzoefu wa kazi. Mafunzo hayo yalihusu utunzaji wa kumbukumbu *(records keeping),* uhasibu, ukarani *(secretarial)* na masomo ya biashara. Katika kipindi cha 2004/2005, watumishi 10 walihudhuria mafunzo ya utunzaji kumbukumbu na kati yao wanne (4) walihitimu ngazi ya cheti na wengine sita (6) walihitimu ngazi ya stashahada. Katika kipindi hiki Wizara iliwasomesha watumishi kumi na mbili (12) kozi ya shahada ya kwanza na ya uzamili (ya pili). Kati ya hao wanne wanachukua shahada ya kwanza katika vyuo mbalimbali nchini na watumishi nane wanachukua shahada ya uzamili *(MBA* na *MPA)* hapa nchini ambapo mmoja anachukua

shahada ya uzamili huko Sweden. Maafisa ishirini na mbili (22) walihudhuria kozi mbalimbali nchini na nje ya nchi. Ili kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapata mafunzo kulingana na kazi anayofanya na kwa wakati muafaka, Wizara imeandaa programu ya mafunzo ambayo itakuwa ni mpango endelevu wa utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wataalam wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imeeleza, kwa muhtasari tu, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, na masuala muhimu ya kisera na kiutendaji ya sekta za Mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005. Aidha, hotuba imetoa mwelekeo na matarajio ya mwaka 2005/2006. Nina matumaini kwamba maelezo hayo yanatosha kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla jinsi sekta hizo zinavyochangia maendeleo ya uchumi wetu. Wizara inakabiliwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Juhudi zinafanywa kwa kushirikiana na wadau wake ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Serikali inawajibika kuimarisha sekta hizi muhimu katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini na hivyo kuweza kuwaletea wananchi maendeleo yanayotarajiwa. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa tayari kutukosoa pale tulipokosea, kutuweka sawa pale tulipoteleza na bila shaka kuwapongeza wafanyakazi wa sekta hii pale walipofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara Mawasiliano na Uchukuzi napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi kipindi cha mwaka 2004/2005 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu ziwaendee pia wahisani mbalimbali wanaotusaidia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa. Wahisani hao wanajumuisha mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Nchi na Mashirika hayo ni pamoja na; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Majini *(IMO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia Usalama wa Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia masuala ya Simu *(ITU),* Jumuiya ya Kimataifa inayosimamia masuala ya huduma za Posta *(IPU),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Benki ya Dunia (WB), Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA), OPEC Fund,* Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini *(DBSA),* Umoja wa nchi za Ulaya, Nchi za Uholanzi, Sweden, Kuwait, Finland, Denmark, Ujerumani, Uingereza, Japan, China,Ubelgiji, Ufaransa, Italia, Urusi na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara ya Sekta nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari (Mb.), Katibu Mkuu Ndugu Salim Himidi Msoma, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Wakala, Mamlaka na Asasi zote zilizo chini ya pamoja na watumishi wengine wote wa Wizara na wa asasi zilizo chini yake. Wamenipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu niliyopewa ya kusimamia uendelezaji wa sekta za Mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa. Ni kweli kwamba, michango yao ya mawazo na utendaji yameweza kuifanya kazi yetu kuwa rahisi na yenye mafanikio. Nawashukuru.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mlionipa katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya tatu. Maoni na maelekezo yenu ndio yamefanikisha mageuzi na mabadiliko makubwa ambayo yamefanyika katika sekta za mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa. Binafsi nawashukuru, Waheshimiwa Wabunge, kwa dhati kabisa na kwa moyo kwa wengi wenu kunitia moyo wakati wa mchakato wa uchaguzi wa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Nilifanikiwa kufika hatua ya mwisho katika uteuzi huo na kupata medali ya shaba. Shaba si haba. Mapokezi mliyonipa mwanzoni mwa kikao hiki yameniongezea unyenyekevu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka 2005/2006, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe jumla ya shilingi 80,065,770,880. Kati ya fedha hizo, shilingi 35,915,847,900 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 5,002,812,200 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 39,147,110,700 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi 14,600,000,000 ni za hapa nchini, na shilingi 24,547,110,700 ni fedha za kigeni kutoka kwa Wahisani mbalimbali.Pamoja na hotuba hii nimeambatisha majedwali yanayotoa kwa ufupi takwimu zitakazowawezesha Waheshimwa Wabunge kufahamu na kuelewa vizuri zaidi utendaji wa sekta za Sekta kwa kipindi cha 2004/2005. Naomba takwimu hizo zichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inaweza kupatikana vile vile katika tovuti ya Wizara, tovuti ya Serikali na tovuti nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004 Kanuni Na. 81(1) napenda nitumie fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Miundombinu inayohusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya sijatoa maoni ya Kamati yangu ningependa kutumia nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati yangu na wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini kutoa pole na rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kilombero kwa msiba wa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga aliyefariki dunia tarehe 2 Juni, 2005. Aidha tunatoa pole kwa familia na

wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Margaret J. Bwana aliyefariki dunia tarehe 23 Juni, 2005. “Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. (Amin)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa mchango wao mkubwa katika kupitia na kuchambua Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa ufasaha. Mawazo yao na ushauri wao ndivyo vilivyowezesha kukamilika kwa Taarifa hii. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 103 B(1) Toleo la 2004 napenda niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao ni:-

1. Mhe. Prof. Henry R. Mgombelo, Mb.- Mwenyekiti;
2. Mhe. Henry D. Shekiffu, Mb. - M/Mwenyekiti;
3. Mhe. Lydia T. Boma, Mb. - Mjumbe;
4. Mhe. Zamda S. Bozzen, Mb. - Mjumbe;
5. Mhe. Dr. Batilda S. Burian, Mb. - Mjumbe;
6. Mhe. Robert J. Buzuka, Mb. - Mjumbe;
7. Mhe. Bakar S. Faki, Mb. - Mjumbe;
8. Mhe. Abdallah Kh. Feruzi, Mb. - Mjumbe;
9. Mhe. Dr. Amani W. Kabourou, Mb.- Mjumbe;
10. Mhe. Ally A. Karavina, Mb. - Mjumbe;
11. Mhe. Mohammed J. Khatib, Mb.-Mjumbe;
12. Mhe. Dr. Thadeus M. Luoga, Mb.- Mjumbe;
13. Mhe. Zubeir A. Maulid, Mb. - Mjumbe;
14. Mhe. Ibrahimu W. Marwa, Mb. - Mjumbe;
15. Mhe. Mohammed H. Missanga, Mb.- Mjumbe;
16. Mhe. Dr. James A. Msekela, Mb. - Mjumbe;
17. Mhe. James P. Musalika, Mb. - Mjumbe;
18. Mhe. Prof. Daimon M. Mwaga, Mb. - Mjumbe;
19. Mhe. Ludovick J. Mwananzila, Mb. - Mjumbe;
20. Mhe. Karim S. Othman, Mb. - Mjumbe;
21. Mhe. Sijamini M. Shaame, Mb. - Mjumbe; na
22. Mhe. Maria D. Watondoha, Mb. - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2005/2006. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Prof. Mark J. Mwandosya, (Mb) Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Naibu wake Mhe. Dr. Maua A. Daftari, (Mb) pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Salim H. Msoma kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata maelezo mbalimbali kuhusu dira (vision) na dhamira, majukumu, na malengo ya Wizara pamoja na taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Miundombinu kwa mwaka 2004/2005. Kamati ilipata maelezo pia kuhusu mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa kipindi kilichopita. Aidha, Kamati ilipata taarifa ya kina kuhusu kazi zilizopangwa

kufanyika katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2005/2006 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza maelekezo yote waliyopewa na Kamati yangu kwa mwaka 2004/2005 kwa kadiri walivyoweza. Mojawapo ya utekelezaji huo ni:-

* Wizara imeboresha huduma za Mawasiliano na Uchukuzi ndani na nje ya nchi kwa kupanua mtandao ili kuchochea kasi ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii ifikapo mwaka 2025;

* Kuendeleza makubaliano na makabidhaino ya Chuo cha *TTCL* kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili Chuo Kikuu kiendelee kutoa taaluma kwa Chuo cha *TTCL* kwa manufaa ya Watanzania;

* Kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano nchini *(Communications Universal Access Fund).*

* Kuanzisha *SUMATRA, TCRA* na *TCAA;*

* Kushughulikia usanifu na utayarishaji zabuni za Ujenzi wa gati la Mafia;

* Kuanzisha huduma za *TTCL Pre paid Card;* pamoja na

* Kutayarisha mapendekezo ya muundo wa utumishi na marupurupu kwa Wafanyakazi wa Wakala wa Ndege Tanzania ili kupunguza kasi ya kuhamia katika Mashirika mengine.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake kwa Kamati, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi aliainisha mafanikio na matatizo kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 mafanikio yaliyopatikana ni:-

* Kukamilisha sera za Huduma za Posta, kukamilisha rasimu ya awali ya Sera ya Taifa ya Huduma ya Hali ya Hewa na rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia za Mawasiliano na Upashanaji Habari.

* Kukamilisha muundo na kuanza kazi kwa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA).*

* Kuanzishwa kwa mfumo wa Performance Management System wenye lengo la kuboresha utendaji ndani ya Serikali.

* Wizara katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya sekta, imejenga vituo viwili *(gang camps)* kwa ajili ya watumishi wanaohudumia vituo vya njia ya reli Kaliua - Mpanda na Manyoni - Singida.

* Pia imekamilisha ujenzi wa maghati katika Ziwa Victoria na Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa 2004/2005 matatizo mbalimbali yalijitokeza na kusababisha baadhi ya majukumu yasikamilike kwa ufanisi uliokuwa umetarajiwa; matatizo hayo ni kama ifuatavyo:-

* Upungufu wa Wakaguzi wa Serikali wa vyombo vya majini;

* Upungufu wa watumishi katika Mamlaka ya Leseni za Usafirishaji *(CTLA)* katika Ofisi za mikoa;

* Upungufu wa fedha zinazotolewa na Hazina kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Matumizi ya Kawaida *(OC)* na hata kwa *(CTLA)* ambayo huhitaji fedha kwa wakati ili kufuatilia ukusanyaji wa mapato; na

* Utaratibu wa Hazina kutoa fedha kwa mwezi *(Cash Budget)* badala ya robo mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2005/2006 Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imezingatia katika kuendeleza jitihada za Serikali katika kuboresha utoaji wa huduma za Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi; kupanga majukumu ya Wizara kwa kuzingatia umuhimu (Kipaumbele) na kiwango cha fedha kilichowekwa kwa matumizi ya kawaida ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Wizara inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi milion 3.5 kiasi ambacho ni kidogo kuliko shilingi bilioni 1.94 kilichopangwa kukusanywa mwaka wa fedha uliopita. Upungufu huu katika makadirio ya makusanyo ya mapato unatokana na kuhamishia Mamlaka ya Nchi Kavu na Majin*i (SUMATRA)* vilivyokuwa vyanzo vikuu vya mapato Wizarani. Vitengo hivyo ni Mamlaka ya Leseni za Usafirishaji, Leseni za Mabaharia na Leseni za Vyombo vya Majini. Baada ya kutoa tathmini ya mawasilisho ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wa Mwaka 2005/2006, naomba sasa nitoe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na kwa Serikali kwa ujumla kama ifuatavyo:-

1. Kamati inashauri kuwa Wizara iandae programu ya utekelezaji *(Action Plan)* kwa kila sera ili Mipango itakayotekelezwa ijulikane. Aidha Sera na mikakati ya Wizara iainishwe ili kuwezesha tathmini ya utekelezaji.
2. Matatizo ya Shirika la Posta Tanzania *(TPC)* ya kutokuwa na mtaji wa kujiendesha na kurithi madeni makubwa ni kikwazo kwa Shirika hilo kuingia katika soko la ushindani na kutoa huduma zilizo bora na kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kupata ufumbuzi wa matatizo hayo haraka iwezekanavyo.

3. Kamati inaishauri Serikali kuwa zoezi la kubinafsisha Mashirika ya Posta Tanzania *(TPC),* Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Kampuni ya Huduma za Meli *(MSC LTD)* lifanyike haraka, kwa ufasaha na maslahi ya Taifa yapewe kipaumbele.

4. Kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha *ATHCO* ukomo wa Kampuni hiyo unaisha Desemba, 2005, Kamati inashauri Serikali kuwa *ATHCO* waongezewe muda ili kukamilisha kazi waliyopewa. Aidha Kamati haiafiki wazo la kuifuta *ATHCO* na majukumu yake kuhamishiwa chini ya idara Serikalini, kwani uzoefu umeonyesha kuwa kwa kufanya hivyo zoezi litakosa uwazi na kuongeza urasimu usio wa lazima na kupelekea mali kupotea.

5. Kamati imesikitishwa na utaratibu mbovu wa Serikali kuchukua nyumba na vifaa bila kulipiwa. Kwa mfano vipuli vya ndege vyenye thamani ya Tsh. 240,647,208/= ambavyo Shirika lilitarajia kuviuza, vilihamishiwa kwa *ATCL,* ambayo ni Kampuni binafsi bila utaratibu mzuri. Aidha nyumba 7 zilizopo nje ya nchi zimehamishiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa bila kutathminiwa ili kufuta madeni. Kamati inashauri taratibu na sheria za kuhamisha mali za Serikali zizingatiwe.

6. Kamati inaagiza Wizara kufuatilia suala la hati za nyumba ambazo bado zinahodhiwa na waliokuwa wafanyakazi wa *ATC,* ambao wanajulikana ili zirejeshwe. Aidha Kamati inaipongeza *ATHCO* kwa ukusanyaji wa madeni; juhudi hizo ziendelee ikiwa ni pamoja na kuongeza ufuatiliaji wa kesi zilizoko mahakamani.

7. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa na kutayarisha mafao ya wafanyakazi wa *TPA,* kwani mkataba wa hiari tayari umeshaandaliwa na uko katika hatua za mwisho; kasi hii ionyeshwe kwa vitendo.

8. Kamati inaishauri Serikali kuwa Kitengo cha Nafaka *(Grain Terminal)* isikodishwe, ibaki chini ya Mamlaka ya Bandari *TPA* kwa ajili ya masuala ya usalama.

9. Serikali awali ilipitisha uamuzi wa kukiacha Kitengo cha Mafuta cha Keko *(Keko Jet Oil -KJO)* chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), uamuzi ambao ulikuwa muafaka; Kamati inashauri kuwa kitengo hicho kisibinafsishwe.

10. Kamati inaupongeza uongozi mpya wa *TAZARA* kwa juhudi zake za kurekebisha utendaji wa Shirika hasa kuimarisha mapato yao; juhudi hizo ziendelezwe na pia *TAZARA* itafute watu wa kukaa katika vituo na nyumba zilizoachwa wazi pamoja na kuweka ulinzi katika madaraja makubwa.

11. Kutokana na *Kongoro Concrete Sleeper Quarry* kuwa na deni kubwa la **TRA (Sh. Mil 607)** kwa *TRA* na kushindwa kulilipa, *TAZARA* iliamua kuvunja Kampuni na kuwa Idara iliyo chini ya *TAZARA*. Kamati inaitaka *TAZARA* isitishe mpango wa kuvunja Kampuni hiyo na badala yake Kongoro wajitangaze ili waweze kupata soko la bidhaa zao sehemu zingine kama *TANESCO* na kwingineko. Kamati inapendekeza TRC waanze kutumia *concrete sleepers* kutoka *Kongoro Concrete Sleeper quarry* badala ya kuagiza mataluma ya chuma kutoka nchi za nje.*(Makofi)*

12. Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Mkandarasi katika ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Songwe, Kamati inasisitiza kuwa kazi hiyo imalizike mapema kwani uwanja huo ni kichocheo kikubwa katika sekta ya uchumi na uwekezaji katika kanda ya Nyanda za juu Kusini.

13. Kutokana na umuhimu wa viwanja vya ndege vya Arusha na Moshi katika kukuza huduma za kijamii, kiuchumi na uwekezaji Kamati inashauri kuwa taratibu za uhamiaji zianze kufanyika katika viwanja hivyo ili kuondoa tatizo la wasafiri kufuata huduma hiyo *KIA*.

14. Kuhusu deni la Sh. 850,000,000/= ambazo Mamlaka ya viwanja vya ndege *(TAA)* wanaidai Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikiwa ni fidia baada ya kutumia kiwanja cha Tanga kama eneo la mazoezi ya kijeshi na kukiharibu vibaya kiwanja hicho, Kamati inashauri kuwa kwa vile majadiliano kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi yamekamilishwa, Serikali basi ilipe fidia hiyo ili kuiwezesha *TAA* kuendelea na mipango yake ya ukarabati wa kiwanja hicho ili kuepuka uharibifu zaidi.

15. Kamati inaishauri Serikali kusimamia utekelezaji wa miradi yake ili kukidhi ubora na viwango vinavyotakiwa. Aidha Makandarasi wenye historia ya kushindwa kutimiza kazi zao kulingana na mikataba iliyowekwa wasipewe zabuni.

16. Serikali ifuatilie kwa karibu suala la *ATCL* na kuangalia upya mikataba na ubia iliyoingia na *SAA*. Aidha Serikali imalize matatizo yaliyojitokeza na mwekezaji huyo hasa utaratibu wa fedha kupelekwa Afrika ya Kusini na kuwa na ubia usio shirikishi ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadaye.

17. Kuhusu suala la *TTCL* na *Celtel,* Serikali iangalie muundo huu kwa manufaa ya Taifa na kuondoa utata uliojitokeza wakati wa zoezi la ubinafsishaji.

18. Kamati inaishauri Serikali kuuwezesha Mfuko wa Maendeleo ya Mawasiliano Vijijini *(Rural Telecommunication Fund)* kuanza kazi mapema iwezekanavyo ili huduma ya simu ifike vijijini.

19. Kamati inaishauri Serikali kuinunulia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* vifaa vya kisasa ili ilingane na nchi za Afrika Mashariki kama rada kwa kuboresha huduma zinazotolewa ili ziende na wakati.

20. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kubuni Sera ya matumizi ya Optical Fibre. Suala hili liharakishwe ili nchi inufaike na utaratibu huo mapema iwezekanavyo.

21. Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali wa kukabidhi Chuo cha Posta kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kamati inashauri kuwa zoezi hilo lifanywe mapema na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kipewe bure chuo hicho cha Posata kama vile Chuo cha

Kiislam kilichopewa majengo ya *TANESCO* ili mipango ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ianzwe kutekelezwa.

22. Suala la usalama katika Ziwa Tanganyika ni la muhimu sana katika kuinua uchumi wa taifa, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika upatanishi wa nchi za *DRC,* Rwanda na Burundi. Juhudi hizi ziendelee.

23. Suala la *fuel levy* linahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi. Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria wa Ushuru wa Mafuta *(fuel levy),* lakini kodi hii imeelekezwa kwenye matengenezo na ujenzi wa Barabara na Madaraja tu. Kamati inashauri kuwa Serikali ifikirie utaratibu ambao Meli, Reli na Viwanja vya Ndege vitafaidika na kodi hii kama Sekta muhimu katika maendeleo ya miundombinu hasa katika kuinusuru *TRC na TAZARA.*

24. Kuhusu wizi wa mafuta ya Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* jambo ambalo limekuwa ni tatizo sugu katika reli ya Kati hasa Dar es Salaam, Morogoro, Tabora na Mwanza, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani wafanye juhudi ili kukomesha wizi huu.

25. Kamati inashauri hatua zichukuliwe dhidi ya Mkandarasi wa Ghati la Mbamba Bay kwa kushindwa kukamilisha kazi kama ilivyotarajiwa.

26. Kwa vile maji katika Ziwa Victoria yanapungua na kusababisha Ghati zilizojengwa Kinasi na Shirati kutotumika ipasavyo kutokana na kina kifupi, Kamati inashauri kwamba mazingira yatunzwe na yalindwe. Aidha barabara zinazokwenda katika Maghati hayo ni mbaya mno, hivyo Serikali itengeneze barabara hizo.

27. Kamati inapongeza Makampuni ya Simu za mikononi *(Vodacom, Mobitel, Celtel na Zantel)* kwa kazi nzuri za kusambaza huduma zao. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa gharama hizo zipungue zaidi ili kuwawezesha wananchi wengi kumudu huduma hiyo.

28. Kamati inaishauri Wizara kuwathibitisha wafanyakazi wanaokaimu ofisi kwa muda mrefu, (kwa mfano Kaimu Meneja Uwanja wa Ndege wa bado anakaimu. Ni vema ukawekwa muda maalum wa kukaimu.

29. Kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri Serikali kuangalia tatizo la kukwama kwa usafirishaji wa Boti ziendazo kasi Mwanza *(Lake Fast Ferries)* na kulimaliza kwa manufaa ya wananchi wa ukanda wa Ziwa Viktoria lakini vile vile bila kuathiri miundombinu iliyopo. *(Makofi)*

30. Kamati inashauri Serikali kuandaa Semina kwa Wabunge kuhusu dhana ya Uchumi wa Kijiografia ili kuchochea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasilisho ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006; na kwa kuwa kwa niaba ya Bunge lako Tukufu Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa

kina taarifa hizo,  ninaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na likubali kupitisha kiasi kilichoombwa cha shilingi 80,065,770,800/= Kati ya hizo shilingi 40,918,660,100/= ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 39,147,110,700/= ni fedha za miradi ya maendeleo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu mpango wa Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2005/2006.  Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Mb, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri, Mhe. Dr. Maua A. Daftari, Mb, Katibu Mkuu Ndugu Salim H. Msoma pamoja na Wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya matayarisho ya Bajeti pamoja na Ushirikiano wao kwa Kamati ya Miundombinu. Aidha Kamati inaishukuru Wizara kwa maandalizi ya ziara za Kamati zilizofanyika Tanzania Bara na Visiwani kabla ya kuanza vikao hivi vya Bajeti.  Ziara hizo ziliwapa fursa Wanakamati kujielimisha na kuzifahamu vema shughuli za Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara na hata kufanya uchambuzi wa Bajeti kuwa rahisi. Maandalizi na mawasilisho ya kina yaliyofanywa na Wizara kwa Kamati yangu yamewezesha kukamilisha kazi za Kamati kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe binafsi na Ofisi yako kwa ujumla.  Namshukuru pia Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Henry D. Shekiffu (Mb) kwa ushirikiano katika kuiongoza Kamati hii, Waheshimiwa Wabunge hususan Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Lakini nawashukuru pia Wabunge wote, Katibu wa Bunge, Ndugu Damiani S. L. Foka, bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii ambao ni Ndugu Justina M. Shauri na ndugu Bisile M. Dickson kwa juhudi waliyoonyesha katika kuwezesha na kukamilika kwa uchambuzi wa mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2005/2006 kwa ufanisi na kwa kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha imeshawekwa kwenye ubao lakini watakaopata nafasi nafikiri ni wale ambao hawajachangia kabisa walikuwa wanasubiri Wizara hii na wale ambao wamechangia mara moja tu.  Ambao hawajachangia kabisa ni vizuri wajiandae ni Mheshimiwa Feter Said Mgeni, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Omar Chubi na Mheshimiwa Philip Magani.

Ambao wamechangi mara moja ni Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Abdukarim Shah, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Beatus Magayane. Nafikiri hao ndio watapata nafasi kwa muda tulionao.  Sasa namwita Msemaji wa kambi ya Upinzani kwa sekta hii ya mawasiliano na Uchukuzi atoe maoni ya Kambi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2005/2006 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wenzangu na Watanzania wengine katika kuomboleza vifo cha marehemu Magreth Bwana aliyekuwa Mbunge viti maalum wa Mkoa wa Rukwa kilichotokea wiki iliyopita, na marehemu Abu Towegale Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero. Nachukua pia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Profesa Ibrahim H. Lipumba na Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa wagombea wa nafasi ya Urais wa Tanzania na Zanzibar kupitia *CUF.* Nawapongeza pia Waheshimiwa wengine wote wanaogombea urais wa Jamhuri wa Muungano na Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Dk. Sengodo Mvungi *(NCCR-Mageuzi),* Mheshimiwa John Momose Cheyo *(UDP),* Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema*(TLP),* pamoja na wengi wengineo ambao wamepitishwa na vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, bado wananchi wanaendelea kuhoji ununuzi mzima wa ndege hiyo ambayo inatumiwa na Rais wetu. Ndege hiyo ya bei ya kutisha ikifananishwa na umaskini uliokithiri wa Watanzania,inaendelea kuonekana kama kioja cha aina Fulani.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya ndege hiyo bado ni madogo ikilinganishwa na uwezo wake. Ndege hiyo HAITUMIKI KIUCHUMI au kwa kuzingatia faida na muda mwingi huwa imeegeshwa tu. Ndege hiyo inakwenda viwanja vichache nchini na hivyo kulazimu kuwakodishia ndege nyingine viongozi wetu. Yamekuwepo madai ya ndege hiyo kuwa na matatizo kadhaa ya kiufundi. Uzima wa ndege hiyo umeanza kutiliwa mashaka. Hata hivyo, bado ufumbuzi upo kwani upinzani utakapokamata dola baadaye mwaka huu utahakikisha kuwa ndege hiyo inauzwa kwa sababu ni kufuru kubwa kuwa nayo kwa nchi yenye umaskini wa kupindukia kama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiondoa hali ilivyo sasa kati ya Dar Es Salaam na Zanzibar ambako wawekezaji kadhaa wanaendesha safari za maboti yaendayo kasi, hali katika maeneo mengine yanayohitaji usafiri wa majini siyo ya kuridhisha. Usafiri wa baharini kati ya Dar Es Salaam na mikoa ya kusini, na kati ya Dar Es Salaam na kisiwa maarufu cha Mafia umedidimia kabisa. Usafiri katika Maziwa Makuu unategemea meli chakavu za kizamani ambazo mbali ya kuhatarisha usalama wa abiria kutokana na uchakavu, meli hizi zinashindwa kuwa na ratiba za uhakika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendekeza rushwa Serikali imekuwa ikikwamisha juhudi za watu mbalimbali kuwekeza katika usafiri wa majini katika maeneo ambayo hivi sasa yana tatizo kubwa la usafiri huo. Mgogoro uliodumu kwa muda sasa kati ya Kampuni ya Lake Fast Ferries ni kielelezo halisi cha Serikali hii.

Serikali imekuwa ikizuia usafirishaji wa maboti mawili yaendayo kasi yaliyoingizwa nchini na kampuni hiyo kwa ajili ya kutoa huduma katika Ziwa Viktoria

kwa madai kwamba yangeharibu barabara wakati wa kuyasafirisha. Hata hivyo imethibitika kwamba sababu zinazotolewa za uzuiaji huu hazina msingi ila zipo sababu nyingine ambazo hazibainishwi hadharani. Mawaziri wawili waliomo kwenye baraza moja la Mheshimiwa Mkapa wanaendelea kutoa kauli zinazojikang'anya. Kwa kuwa hili ni Bunge la "Lala Salama", tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tupatapo ridhaa ya wananchi hapo tarehe 30 Oktoba, 2005 inatarajia kufanya juhudi kubwa kupata wawekezaji watakaowekeza katika maeneo yote ambayo hivi sasa yanahitaji usafiri wa majini, na kufanya kila linalowezekana bila kuathiri maslahi ya Taifa kuwasaidia wawekezaji hao kufanikisha utoaji wa huduma hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa vyombo vya majini bado ni wa kuchechemea na jambo hili linaonekana kupalilia majanga mengine yenye ukubwa zaidi ya ule wa *M.V. Bukoba.* Serikali haionekani kujifunza kutokana na makosa, na hilo ni tatizo sugu la Serikali zote mbili za CCM.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ziko ajali nyingi zinazoendelea kutokea na kuua watu wengi ambazo nyingi hazitolewe taarifa na kwa kiasi kikubwa husababishwa na kutokuwepo uthibiti na ukaguzi wa vyombo hivi na hasa vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga siyo maarufu sana kwa Watanzania walio wengi. Kwanza wananchi wengi hawamudu gharama kubwa ya usafiri huo. Pili, kuna mikoa michache tu ambayo ina viwanja vya ndege vinavyoweza kuhudumia ndege kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali siku zote imekuwa ikiitazama aina hii ya usafiri kama anasa kwa wananchi wa kawaida na kwa hivyo haijafanya juhudi zozote kuhakikisha kuwa gharama za aina hii ya usafiri zinakuwa chini ili watu wengi zaidi waweze kumudu. Ukosefu wa viwanja vya ndege katika maeneo mengi ya nchi vyenye uwezo wa kuhudumia ndege muda wote kumesababisha wawekezaji wengi wasivutiwe kuwekeza katika aina hii ya usafiri. Hata viwanja ambavyo vimeshathibitika kuwa na idadi kubwa ya watumiaji kama Bukoba, havishughulikiwi ipasavyo na viko katika hali ya kusababisha ajali wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ikipewa ridhaa na wananchi hapo Octoba Mwaka huu.Haitolichukulia suala la usafiri wa anga kama anasa. Kwa sababu hiyo tumekusudia kuchukua hatua zifuatazo ili kukuza aina hii ya usafiri miongoni mwa Watanzania.

(a) Tutakaribisha wawekezaji kuwekeza zaidi katika eneo hili, na hasa yale makampuni ya nje ambayo yana uzoefu mkubwa katika kutoa huduma za haraka kati ya mji na mji *(Shuttle service).* Kwa kawaida makampuni haya yanatoa huduma ya usafiri wa anga kwa gharama nafuu sana kiasi kwamba huduma zao zinavuta watu wa aina zote wakiwemo na wananchi wa kawaida.

(b) Tutahakikisha kuwa walau kila mkoa nchini una kiwanja kimoja cha ndege kinachoweza kuhudumia ndege muda wote bila kujali majira ya mwaka.

(c) Tutachambua kwa makini gharama mbalimbali za usafirishaji wa anga, na hasa bei za mafuta ya ndege kwa nia ya kuangalia jinsi ya kuzifanyia marekebisho yenye lengo la kushusha nauli.

Mheshimiwa Spika, kuwapo kwa njia za uhakika za usafiri ndani ya nchi kunarahisisha sana usafirishaji wa watu na bidhaa toka upande moja wa nchi hadi mwingine. Njia nzuri za usafiri na mawasiliano zinachangia katika kushusha gharama za kibiashara na hatimaye bei za bidhaa. Tanzania ina tatizo kubwa la mawasiliano ya ardhini kwa maana ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tuhuma za uongozi mbaya unaosimamia Mamlaka za Reli zilizoko nchini, mtandao wa reli uliopo mbali ya kwamba ni chakavu, pia hauko kistratejia. Tanzania ina njia kuu za reli tatu. Kuna reli ya kati inayoanzia Dar-es-Salaam hadi Kigoma na ambayo ina tawi linaloanzia Tabora hadi Mwanza. Kuna reli ya Tanga inayoanzia Tanga hadi Moshi na Arusha na pia kuwa na matawi, moja linaloanzia Korogwe hadi Dar-es-Salaam, na jingine linaloanzia Kahe mkoani Kilimanjaro hadi Taveta mpakani mwa Kenya na Tanzania. Reli ya tatu ni ile ya *TAZARA* inayoanzia Dar-es Salaam hadi Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Spika, Ili kuurejesha umaarufu wa Reli ya Tanga inabidi juhudi zifanyike kuongeza wingi wa mizigo inayohitaji kufikishwa bandarini Tanga. Kuhuishwa kwa shughuli za kilimo cha kibiashara katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, na Tanga yenyewe kutatoa mchango mkubwa katika kufanikisha hili. Lakini huenda mchango mkubwa zaidi ukatokana na kufanikisha juhudi za kuhakikisha kuwa bidhaa za Uganda na Rwanda zinasafirishwa kupitia reli hii kwenda na kutokea bandarini Tanga. Ili suala hili lifanikiwe hata hivyo itabidi kwanza lijengwe tawi la reli au barabara itakayoiunganisha miji ya Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa reli ya kati hadi leo umekuwa ni wa kipekee kabisa ikizingatiwa kuwa kuanzia Dodoma hadi Kigoma na Mwanza(tofauti na maeneo yanayounganishwa na reli za Tanga na *TAZARA* ambayo vile vile yana barabara kuu za uhakika), huu ndio usafiri pekee wa uhakika unaotegemewa na sehemu kubwa ya wananchi wa maeneo hayo ya kanda ya ziwa kwa hivi sasa. Maeneo haya hayana barabara ya uhakika na ni wananchi wachache tu wenye uwezo wa kumudu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ndiyo kwa pamoja yanayokaliwa na idadi kubwa ya Watanzania. Hata hivyo kutegemewa kwa reli hii katika usafirishaji zaidi wa abiria umekuwa ni mzigo mkubwa kimapato kwa Shirika la Reli la Tanzania, na pia kumeathiri kwa kiasi fulani shughuli za kiuchumi za maeneo yanayohusika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kulazimika kusafirisha abiria kwa wingi kumepunguza uwezo wa shirika hilo kusafirisha mizigo kwa wingi na kwa kasi inayotakiwa; hivyo kuathiri shughuli za kibiashara kati ya maeneo mbalimbali yanayoungwa na reli hiyo. Kuna umuhimu mkubwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na usafiri wa uhakika wa

barabara kati ya maeneo mbalimbali yanayounganishwa na reli ya kati ili kuipunguzia reli hiyo msongamano wa abiria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa shirika lilisafirisha mizigo tani 1,450,000 mwaka 2003 na mwaka 2004 ni tani 1,333,249 tu, ikiwa ni pungufu wa asilimia 8.1, hii inaonyesha hata wafanyabiashara wanaanza kukosa imani na shirika la Reli.Tunadhani Serikali inaliendesha shirika hili kisiasa mno badala ya kibiashara,kwani hatuamini kama kweli likipewa uhuru wa kufanya biashara kwa kutumia *"ethics"* za biashara pamoja na *backbone* yake ya *fiber optic* lingekuwa ni shirika la mfano katika Afrika.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Migogoro ya mara kwa mara ya kiuendeshaji inayolikumba shirika la *TAZARA* ni kioo cha hali hii. Zinahitajika juhudi za makusudi kuiokoa reli hii kabla haijafikwa na kile kilichovifika viwanda vyetu. Ni wazi ujenzi wa matawi kati ya Tunduma na Rukwa, Mbeya na mpaka wa Malawi kuunganisha na Songea, Tunduru hadi bandarini Mtwara kutatoa uhai mkubwa sana siyo kwa *TAZARA* tu, bali pia kwa bandari ya Mtwara na shughuli za kiuchumi kwa ujumla kwa eneo lote la kusini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tuingiapo madarakani baada ya kupata ridhaa ya wananchi Octoba Mwaka tunategemea kufanya yafuatayo;-

(a) Serikali itahakikisha mawasiliano ya barabara na reli ni moja ya masuala ambayo yanapewa kipaumbele maalum. Haya ni maeneo ambayo serikali itaruhusu misamaha ya kodi kwa ukamilifu.

(b) Tutahakikisha tunaondoa ukiritimba wa watendaji wa shirika na kuwa na mtazamo wa kibiashara zaidi kuliko kisiasa ambao unasababisha kukata tamaa na vile vile kuimarisha kitengo cha biashara na masoko ili kiendane na hali halisi katika soko huria kwani.

Aidha, Serikali itatafuta wawekezaji kuwekeza kibiashara kwenye ujenzi wa matawi ya reli muhimu ili kuunganisha mikoa na wilaya zenye matatizo makubwa ya usafiri wakati wa kipindi cha mvua au wilaya zisizo na mtandao wa barabara za kuaminika.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa ubora wa simu za mikononi, kuna mfumuko mkubwa wa simu za mikononi zenye ubora usioridhisha au hali ya chini mno. Simu feki zimezagaa na zinauzwa katika maduka karibu yote ya simu za mikononi na wananchi wanatapeliwa kama vile Serikali iko likizo. Simu zisizo na ubora unaokubalika kimataifa ni wizi wa waziwazi wa fedha za watanzania maskini. Tunaitaka Serikali kupitia mamlaka husika ishughulikie kero hiyo kipindi hiki kilichobakia kabla Serikali ya Upinzani haijaingia madarakani kwani hili sio suala la kisera bali suala la utekelezaji tu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, simu za mikononi ni hatua muhimu katika maendeleo ya kimawasiliano katika dunia ya sasa. Hata hivyo Kambi ya Upinzani inaona yapo matatizo makubwa yanayostahili kupatiwa ufumbuzi na Serikali ambayo ni pamoja na:-

(a) Gharama kubwa sana za ununuzi wa muda wa maongezi Gharama kubwa za muda wa maongezi zinaonekana kuchochea umaskini wa watanzania badala ya kurahisisha mawasiliano kati yao, na kwa hali hiyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. (b)Simu za mkononi zinapatikana kwa bei kubwa sana hasa kwa mtu wa kipato cha chini, na kodi kubwa ya Serikali inachangia sana ukali wa bei ya simu hizo. Kama Serikali ilivyojitahidi kurahisisha upatikanaji wa Kompyuta na vifaa vyake kwa wananchi, inaweza pia ikatoa unafuu katika kodi ili kuwafanya watanzania wengi zaidi wamiliki na watumie simu za mkononi, simu hizo si anasa, ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya taifa.

(c) Pamoja na kuwepo kwa teknolojia ya simu za mikononi, Serikali isisahau kwamba bado wapo wananchi wengi, ambao hawatafikiwa na teknolojia hiyo haraka. Simu za kawaida ikiwa ni pamoja na zile za siwaya pamoja na kuimarisha mawasiliano ya barua kupitia Shirika la Posta bado ni mambo yanayostahili kupewa angalizo maalum.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa kisasa unatumia kompyuta na mtandao wa *internet*, na kuwa ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa aina hii ni lazima kuwe na juhudi za makusudi kuwafikishia huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, upinzani tukipata ridhaa za wananchi kuunda Serikali, Mwishoni mwa mwaka tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kuwa huduma za simu, *fax*, na mtandao wa *internet* zinasambaa haraka nchini. Pamoja na mambo mengine serikali itachukua hatua zifuatazo:

1. Itahakikisha kuwa gharama za mawasiliano zinashuka ili kuwiana na gharama hizo katika maeneo mengine ya ulimwengu.

2 Serikali itakaribisha makampuni zaidi ya ndani na nje kuwekeza kwenye sekta hii na yale yatakayowekeza vijijini yatapewa motisha maalum.

3. Kwa muda wa miaka kumi ijayo, kodi yote ya mauzo inayotozwa na serikali kwa watumiaji wa simu, *fax*, na *internet* itarejeshwa tena kuwekezwa kwenye upanuzi wa huduma za mawasiliano vijijini.

4. Pamoja na jitihada nyingine, serikali pia itachukua hatua za kujifunza naiga kutokana na uzoefu walioupata wenzetu wa nchi mbali mbali, hususan Bangladesh na

kampuni yao ya *Grameen Phone*, juu ya sambazaji wa huduma ya simu kwa malengo ya kupiga vita umasikini vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia tutafanya mazungumzo na makampuni yanayosambaza huduma za *internet* nchini kuangalia uwezekano wa makampuni hayo kusambaza huduma hizo hadi kwenye mashule ya sekondari na vyuo kwa gharama nafuu. Gharama hizi zitakuwa zinafidiwa na serikali kama punguzo la kodi katika kodi yake ambayo ilikuwa ilipwe na kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta, ni muhimu Serikali itafute mbia au wabia watakaoshawishika kuwekeza katika Shirika letu la Posta. Hali ya shirika hili ni mbaya sana na kinachoonekana kufanyika kibiashara na labda kwa faida kidogo ni huduma ya *EMS* peke yake. Shirika hili linahitajika lifanyiwe mageuzi makubwa ya kimuundo na shughuli zake zote kwa ujumla. Ili kuimarisha mtaji wa shirika na kuingiza teknolojia mpya ni jambo la busara kumtafuta mwekezaji wa kuaminika. Huduma ya "*postcargo*" inabidi iboreshwe zaidi kwa kuongeza magari na kupanua zaidi eneo la huduma.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege la Tanzania *ATCL* lipo katika wakati mgumu kiufanisi tangu lilipobinafsishwa. Hakuna ongezeko lolote la ndege za kisasa wala ubora wa huduma. Kilichoongezeka ni malalamiko ya wafanyakazi wake pamoja na wateja. Ubinafsishaji wa iliyokuwa *ATC* na kuleta *ATCL* bado umegubikwa na manung'uniko mengi ya watanzania kwa sababu maslahi yao yanaonekana kumezwa na Afrika ya Kusini.

Si busara kukaa kimya mahali ambapo uchumi wa taifa unaangamizwa kwa kuwadekeza wawekezaji wanaotia mashaka. Inasikitisha kuwa bado Serikali inaendelea kuwabeba wawekezaji wa Afrika ya Kusini, ambao hakuna wanachokiboresha katika *ATCL* kwa manufaa ya watanzania, bali wanaendeleza sera zao za kuinufaisha *South African Airways* na uchumi wa taifa lao na kuudhoofisha uchumi wa nchi yetu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Kambi ya Upinzani ilivyokuwa imeshatahadharisha siku za nyuma, kwamba pamoja na usemi wa Mheshimiwa Rais Mkapa kuwa Paka ni Paka ili mradi akamate panya, lakini ni budi tutambue kuwa vile vile yako mapaka majizi yanayoiba kila kitu zaidi ya kukamata panya. (*Makofi*)

Katika suala hili la *ATCL* Kambi ya Upinzani inaingiwa mashaka namna mambo yanavyokwenda na huenda siku si nyingi tutashuhudia mazishi rasmi ya *ATCL*. Kwa mfano katika upembuzi wetu umebainisha mkataba wenye mapungufu mengi na unaotia mashaka baina ya *ATCL* na Kampuni ya Sunfresh Limited ambayo imesajiliwa hapa Tanzania lakini mwenye nayo ni raia wa Afrika ya Kusini.

Kwanza Kampuni hiyo iliteuliwa kinyemela, katika mkataba pamoja na kutakiwa alete *Bank guarantee* hakuleta, badala yake akaweka *Insurance Bond* tena ya Kampuni ya *Kenya Sunflesh* inayoendelea kulimbikiza madeni zaidi ya millioni 400.

Ndani ya *ATCL* kwenyewe pamoja na matatizo ya kiuendeshaji tunajua kwamba viongozi wa vyeo vya juu wanaendelea kukalia masurufu ya kimkopo ya kiasi kikubwa cha fedha; yenye kufikia au kuzidi millioni 100 huku Serikali ikiendelea ku-*inject* pesa lukuki za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika kupitia vyombo vya habari tumesikia kuna mvutano baina ya wanahisa wawili, *South African Airways* na Serikali ya Tanzania na inasemekana tayari imetolewa *notice* ya kusimamisha mkataba; Kambi ya Upinzani inamuomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi halisi kuhusu sakata hilo.

Waziri alieleze Bunge nini kinaendelea ndani ya *ATCL* na nini msimamo wa Serikali ili yasije yakajitokeza yale yale ya *City Water* na *TTCL*. Waziri atueleze, Serikali imejizatiti vipi kuzuia hayo mafedha yasipotee yanayodaiwa kwa *Top Management ya ATCL* na kwa Kampuni kama *Sunfresh Limeted*.

Mheshimiwa Spika, miradi inayotia shaka kimataifa na kiufanisi, uendelezaji wa Uwanja wa ndege wa Singida ni kati ya miradi iliyogubikwa na wingu la mashaka. Pamoja na kutengwa na kutumika shilingi millioni 100 mwaka 2004/2005, matumizi ya shilingi 97 millioni hayaeleweki. *TCAA* inaonekana kufanya kazi bila ya kuwahusisha wadau husika na ndiyo maana viongozi wa Mkoa wa Singida hakuna wanachojua kuhusu matumizi ya fedha hizo.

Ipo miradi mingi katika Wizara hii ambayo inasuasua na hii ni kutokana na matumizi ya fedha yanayotawaliwa na ukosefu wa uwazi na ushirikishwaji wa wadau. Eneo la mradi limejaa vichuguu wakati inadaiwa usawazishwaji ardhi ulikwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuondolewa kwa ukiritimba wa *TTCL* kuhusiana na simu za kimataifa Pamoja na faida zilizokusudiwa za kuondoa ukiritimba wa *TTCL* katika eneo la udhibiti wa simu za kimataifa, bado upo umuhimu wa kuwa makini dhidi ya uholela unaoweza kujitokeza. Mawasiliano ya kimataifa ni suala nyeti kwa uchumi na usalama wa nchi.

Mamlaka ya Udhibiti na Uratibu wa Mawasiliano yaani *TCRA* inatakiwa kuwa imara na makini, na pia kufanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu sana katika mazingira mapya ya soko huria katika sekta ya mawasiliano.

*TCRA* inatakiwa kuoanisha vizuri majukumu yake ya kusaidia kukua na kuimarika kwa mawasiliano ya kisasa na jukumu la kudhibiti uchezaji rafu katika sekta hiyo, Uimarishaji wa *TCRA* kwa njia mbalimbali ni jambo la muhimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ni watu sahihi tu na wanaostahili kwa sifa zisizo na utata kitaaluma, kimaadili, na hata kiuzoefu ndiyo wamo ndani ya tcra. hiki ni chombo cha kitaalamu na kidhibiti na ni vizuri watumishi wake waongozwe na vigezo vya utaalamu na uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ole kwa kuniunga mkono na kushirikiana nami vizuri kwa muda wote ambao nimekuwa Mbunge wao. Ninaamini itawapendeza kunipa tena ridhaa yao niendelee kusaidiana nao kuchochea maendeleo jimboni kama Mbunge. Nakishukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kukitumikia.

Namshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na wasaidizi wake kwa nafasi waliyonipa kuitumikia Kambi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii.

Pia namshukuru Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Maua A. Daftari, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kunipa mashirikiano ambayo yamenisaidia katika kufanikisha shughuli zangu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawaomba watanzania wajiandae vizuri na kujiweka tayari kuupigia kura Upinzani katika Uchaguzi ujao kwa maendeleo yao halisi na siyo maendeleo ya vitabuni tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba nami kuungana na Waheshimiwa wenzangu kutoa pole kwa wenzetu wa Kilombero kwa kumpoteza Mheshimiwa Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga. Vilevile, ningependa kutoa pole nyingi kwa wenzetu wa Sumbawanga - Rukwa, lakini pia kwa wanawake wa Tanzania kwa kumpoteza Mbunge wao Mheshimiwa Margareth Bwana na kwa jumla yao Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda kuwapongeza wanachama wenzangu wa CCM waliojitokeza kugombea nafasi ya kushika bendera ya CCM katika Uchaguzi Mkuu ujao kwa nafasi ya Urais. Ningependa kuwapongeza wote 11, lakini nawapongeza zaidi Mheshimiwa Kikwete na Mheshimiwa Karume kwa nafasi walizozipata pamoja na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Shein kwa kuwa mgombea mwenza upande wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri anayetoa hoja yake leo, kwani yeye amefikia ngazi ya mwisho kabisa. Kwa tabia ya wana-CCM huwa hatukati tamaa, miaka kumi siyo mingi na hasa ukichukua mfano wa Mheshimiwa Kikwete ambaye amesubiri miaka 10 na leo tumempa nafasi yake aweze kutuongoza. Kwa hiyo, nakuomba uwe mstahimilivu, huenda Mungu akikujalia baada ya miaka 10 utaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ningependa kuchukua nafasi kuipongeza Wizara kuanzia Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na

wenzake wote ambao wameitayarisha hotuba hii safi kwa ushirikiano wao wa kutuandalia mambo kama haya mazuri na kuyaleta mbele yetu bila ya kusita.

Mheshimiwa Spika, naanza kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii naomba wapewe kile wanachokihitaji ili waweze kuendelea kufanya kazi hiyo ambayo wameifanya vizuri kwa miaka mitano na nina hakika wakipewa fedha hizo kwa mwaka huu unaokuja 2006 basi pia wataendeleza yale ambayo wameyaombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, kupitia kwako na kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, ningependa kuwashukuru sana wenzetu wa simu za mkononi. Kwa kweli wametusaidia sana katika kupata mawasiliano na hasa nikiongelea Kisiwa cha Mafia na Wilaya ya Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mkazi wa Mkoa wa Pwani, najua mara nyingi mambo mengi mazuri na ya kunona huwa mara nyingi yanaishia Kibaha, Bagamoyo au Kisarawe, lakini kwa Wilaya za Rufiji na Mafia tunakuwa wa mwisho kwa kila jambo! Hawa wenzetu hasa wa *Celtel* ni lazima niwashukuru sana kwani leo mpaka Rufiji unaweza ukaongea na watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tu Mafia yalitokea matatizo baharini. Kwa kweli hizi simu za mkononi ndiyo zimeweza kutusaidia kuweza kupata mawasiliano na wenzetu na wakaweza kuwahi kwenda kuwaokoa watu. Sasa nasema, nawashukuru sana watu wa *Vodacom* na *Celtel. Celtel* ninashukuru kwamba hawakukata tamaa kwa kutuwekea simu hizo Mafia. Pamoja na kwamba walikuwa wa kwanza, baadaye wakapata matatizo, lakini sasa wameweza kufanikisha lengo lao nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la ajabu, kwa taarifa za haraka haraka nilizonazo ni kwamba, watu wa Mafia wana *line* mbili za *Vodacom* na *Celtel* na mimi mwenyewe nikiwa mmojawapo. Nina hakika kwamba katika hayo inaonekana wazi jinsi gani watu wana nia ya kuweza kujiendeleza katika mawasiliano ya simu za mkononi. Kwa hiyo, ninategemea na *Zentel* pamoja na *Mobitel* nao wataiga mfano wa wenzao waweze kusambaza huduma yao katika Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani kwa suala zima la gati. Huko nyuma kila wakati tukisimama watu wa Mafia tulikuwa tunaongelea gati, gati! Lakini leo nimesikia taarifa ambayo kidogo imenifurahisha, pamoja na kwamba bado tunasema tumefunga vidole tunasoma *Kulhu-allahu* ili haya yaliyotamkwa leo, yaani zabuni zilizotangazwa, basi Mungu ajalie zitangazwe na atapikane mzabuni na aweze kutujengea gati katika Wilaya yetu ya Mafia. Tunasikia wenzetu wa Ziwa Victoria na Tanganyika magati yao yamekamilika, lakini sisi wa Bahari Kuu ya Hindi tumeomba gati kwa muda mrefu. Wengine tangu tuzaliwe tumesikia gati likiongelewa mpaka leo tunazeeka. Basi, huenda Mungu safari hii akatujalia na tunaomba Mungu ajalie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Kwa kweli nimefarijika kuona watu hawa wawili wote wameshafanya ziara Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Mwandosya na Mheshimiwa Dr. Daftari, wamekuja Mafia na wameiona Mafia na nina hakika hilo limesaidia. Unajua mtu unapoona na unaposikia ni vitu viwili tofauti. Inawezekana kabisa kwa kuona kwao Mheshimiwa Mwandosya na Mheshimiwa Daftari wamejua matatizo ya Mafia yalivyo na kuweza kuona umuhimu wa kufanya vitu hivi viende kwa haraka. Ningeomba sana Waheshimiwa Mawaziri hasa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na wao waje Mafia. Tunawashukuru mno kwa kutupa greda, lakini tungeomba na wao waje Mafia waone barabara hiyo itakayopitishwa greda iko katika hali gani kama greda litatosha au kuna vingine ambavyo vinatakiwa viongezwe ili na sisi tuweze kupata angalau barabara iliyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia Waheshimiwa hawa ningeomba watuangalie sana kwenye Kiwanja cha Ndege. Pamoja na kusema kwamba gati litajengwa, lakini nina hakika halitamalizika leo wala kesho. Sisi wananchi wa Mafia sasa hivi usafiri wetu tunaoutegemea wa uhakika ni ndege. Lakini jambo la kusikitisha, ndege tulizonazo ni ndege za wafanyabiashara ambao wanazitumia kwa ajili yao wenyewe. Ndege ya *Coastal* mwenye ndege hiyo ndiyo mwenye hoteli Mafia.

Kwa hiyo, utakuta hana njia, lazima alete wageni wake hotelini. Lakini pia anaongeza bei ambazo sisi wananchi wa Mafia hatuzimudu, hata mimi Mheshimiwa Mbunge hapa ninaposema, kama sikulipiwa nauli na Mheshimiwa Katibu wa Bunge, basi safari zangu za kichama huwa nafanya ushauri mkubwa kabla sijaweza kutoa Sh.130,000/= kwenda na kurudi Mafia. Yaani unatumia Sh.130,000/= kwa muda wa saa moja! Je, unaipata kwa muda gani?

Mheshimiwa Spika, mimi Mbunge nikisema hivyo, sijui mwananchi wa Mafia wa Kijijini Baleni, Bweni atasema nini! Pamoja na jitihada nzuri mliyoifanya, naomba sana mkiangalie kiwanja cha ndege, kwani matatizo ya kutokufika ndege siyo kwamba hakuna Makampuni yanayotaka kuleta ndege Mafia, isipokuwa kwa ubovu wa kiwanja ndege zao zinashindwa kutua katika kiwanja kile.

Mheshimiwa Spika, najua mwaka jana mlitutengea Shilingi milioni 50. Nikienda pale kwa kweli hata sioni zimefanya nini! Siyo kama hazikufanya kitu, lakini katika hali ya kiwanja inaonekana kama vile umechukua gunia la sukari ukaenda kutia baharini, bado chumvi itajitokeza pale pale, huwezi kuona kama umetia sukari.

Mheshimiwa Spika, sasa ningewaomba ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri hawa waone pamoja na hiki kidogo walichokitenga tena mwaka huu. Hizo Shilingi milioni 50, nimeziona, kwa kweli tutakuwa hatufanyi kazi inayoonekana. Itakuwa kila siku bado sisi tunapata matatizo ya usafiri Mafia, kwani bado nina hakika wengine wenye Kampuni za Ndege hawataweza kuleta ndege zao Mafia na bado wananchi wa Mafia wataendelea kupata matatizo ya usafiri na kutia hasara hata *Council* yetu ambayo pato

lake ni dogo sana kwa ajili ya Wafanyakazi na Watendaji Wakuu ambao ni lazima waje Mkoani mara kwa mara na sisi Viongozi wa Chama tunaoishi Mafia ni lazima pia tuhudhurie Vikao vya Chama ili kuifanya Serikali ya Chama cha Mapinduzi itawale. Kushindwa kupanda ndege matokeo yake tunapanda viboti ambavyo havina usalama, wala hatuna uhakika wa maisha yetu tukisafiri kutoka Mafia kwenda Kisiju. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kuuliza tu, kwani huko nyuma nilipata taarifa kwamba wenzetu wa *TAA* waliwahi kutenga fedha kwa ajili ya kiwanja hiki cha Mafia; hizi fedha ziko wapi? Imekuwaje mpaka tukawa hatujui ziko wapi? Kwa hiyo, naomba wakati Waziri anatoa majibu ya mahojiano, basi atueleze kidogo hawa wenzetu wa *TAA* waliona kitu gani mpaka leo hatukuziona zile pesa zikifanya kazi katika kiwanja cha Mafia? Lakini pia waone kwamba wanapotoa hela kidogo kama barabara, sio rahisi mkandarasi kutoka Bara kwenda Mafia kufanya kazi ya Shilingi milioni 50 au kwenda kufanya kazi ya Shilingi milioni 200 kwani vitendea kazi vinakuwa ni ghali kuvisafirisha kuliko Mkataba wenyewe wa kutengeneza hicho wanachokitengeneza kwa fedha waliyotengewa.

Kwa hiyo, naomba kama inawezekana, basi wanyang'anye kokote waweze kutenga fedha kiasi cha kutosha ili makandarasi hawa waweze kwenda kututengenezea kiwanja. La sivyo, tutaendelea kuweka viraka tu ambavyo havisaidii chochote na hata machoni mwa watu havionekani, hata rohoni mwa wana-Mafia inaonekana kama tumetupwa, hatuna baba, hatuna mama na wakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina tabia hiyo.

Mheshimiwa Spika, nina hakika baada ya haya niliyoyasema, wenzetu wa viwanja kupitia Mheshimiwa Waziri na wataalam, watafanya jitihada maalum na kuiangalia Mafia kwa jicho la huruma kwa kuona hali halisi tuliyonayo ili basi wakati tunasubiri gati, angalau kiwanja cha ndege kiwe katika hadhi yake, nasi tupate usafiri wa bei nafuu kwani ndege nyingi zikianza kutua, basi kwa vyovyote *Coastal Travel* watapunguza bei zao na hata wale walalahoi wanaweza angalau wakachangishana wakaweza kupata usafiri, pamoja na kwamba tutaendelea kusafirisha mazao yetu kwa mashua bila *insurance*, bila lolote wakati tukisubiri gati liwekwe, hatimaye meli zenye uhakika ziweze kufika Mafia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa narudia kusema kwamba nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Lakini pia kabla sijakaa, ningependa kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwashukuru kwa ushirikiano walionipa wakati nikitumikia Viti Maalum, Wanawake Bungeni. Pia, napenda kuwashukuru wenzangu wote wa Mkoa wa Pwani ambao wamenipa ushirikiano wa kuniwezesha kufanya kazi yangu kwa roho moja.

Lakini mwisho, tutakiane kheri wote na hasa wapenzi wangu Wabunge wa CCM turudi Bungeni ili tuendeleze jitihada zetu ambazo tumezianza kuhakikisha kwamba nchi yetu kupitia Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanikisha Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi na hatimaye kuwasaidia wananchi wetu wa Tanzania kuishi maisha mema ya sasa hivi na ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, naunga mkono hoja na ninawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kuendelea kututengenezea hotuba nzuri ili ziweze kutekelezeka na hatimaye Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipate heshima ambayo imejengwa kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini, napenda nitoe salam za pole kwa familia ya Marehemu Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo; Marehemu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, Rukwa. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niipongeze pia Wizara kwa hotuba nzuri na malengo mazuri ambayo yanatoa kabisa mwanga kwamba tunakoelekea ni kuzuri na hata kuhusu mabadiliko ambayo yamefanywa na Wizara katika masuala ya miundombinu, wale wenzetu ambao wameshakaa nje miaka miwili au mitatu bila kurudi hapa nyumbani, kwa kweli wakirudi wanaweza kuona kila kitu kimeshabadilika, hata umuhimu wa kukaa huko nje unaweza kuwa umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa sababu kwanza imekuwa kama ni ndoto kutoka Dar es Salaam sasa hivi kwenda Kilwa, unakuwa ndani ya mtandao, unawasiliana na jamaa, jambo ambalo lilikuwa haliwezekani kwa miaka yote. Umefungwa mnara Ikwiriri, Muholo, Kitoke pale Somanga na pale Singino. Hiyo ni minara ya *Celtel*. *Mobitel* nao wamefunga mnara pale Singino. Ninafurahi kusikia kwamba katika muda wa wiki mbili/tatu zijazo nao watakuwa wamefunga. Kwa kifupi asilimia kama 75 hivi ya Kilwa itakuwa ndani ya mtandao. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa kazi hiyo ambayo Wizara imetufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba kutoka Kilwa kwa Magharibi mpakani mwa Liwale ni takriban Kilomita 145. Sasa tungeomba basi kama *Celtel* wako tayari, watufungie mtambo mmoja pale Njinjo kwa ajili ya Kambi ya *Selous* pale Miguruwe ambao pamoja na kwamba wana *radio call,* lakini wameshaniomba mara nyingi niwasilishe taarifa *Celtel* kwamba kama wangefungiwa mnara huo ingesaidia sana. Lakini sasa wakifunga pale Miguruwe sijui kama wale watu wa mpakani kule Zinga watafaidika. Kwa sababu mimi siyo mtaalam, kama imeshindikana Miguruwe, basi waende wakafunge pale, kuna mlima mmoja ambao ulikuwa unatumika zamani na Wazungu pale Zinga Kibaoni. Ni mlima mrefu sana kwa kanda ile kabla ya mpakani, Nandanga. Katika mambo ya kutafuta eneo, endapo hao watu watakuja tunaweza kuwapa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kipatimo, kutoka Kilwa mpaka Kipatimo ni takriban kama Kilometa 150. Kwa hiyo, mtu kama una shida inabidi lazima uje Kilwa na kama ni masika hali inakuwa mbaya. Tungeomba pia kama *Celtel, Mobitel* au *Vodacom*, jamaa wowote ambao wako tayari watusaidie kupata hayo mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kule Kipatimo kuna sehemu mbili ambapo wenyeji wa pale wanajua kulingana na hali ya milima ilivyo. Hilo nafikiri ni jambo ambalo hao Kipatimo walishatuma majina ya watu 500 ya watu ambao walikuwa wanataka huduma hizi za simu za mikononi. Maombi yalikwenda *Celtel*, lakini kila tunapokumbusha, kwa sababu pesa ni nyingi, hawajaweza kutusaidia. Sasa hilo namwomba Mheshimiwa Waziri katika utaratibu unaokuja, atusaidie angalau tuweze kufanikiwa tuwe kwenye mtandao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni usafiri. Tulikuwa na usafiri wa ndege Dar es Salaam - Kilwa kupitia Mafia kwa Kampuni ambayo ilidumu kwa miezi mitatu tu ya *Eagle Air,* lakini bahati mbaya mambo yakaenda mrama. Huyo bwana alishindwa kufanya kazi halafu inasemekana akaiuza ile Kampuni, sijui akafanyaje, hiyo hatujui! Lakini imeleta matatizo hasa kwa wafanyabiashara wa Kilwa kusafirisha wale *kambakoche* ambao wanakuja kuunganishwa na *flight* ambazo zinakwenda nchi za nje.

Kwa hiyo, pamoja na matatizo ya uwanja kama alivyozungumza Mheshimiwa Kimbau, lakini uwezo wa ndege kutua kama mwenye ndege yupo, basi nafikiri Kilwa uwanja upo, inaweza ikatua, hata kama marekebisho yatahitajika. Nafikiri kuna haja sasa hivi ya kufanya bidii mtutafutie angalau Shirika linaloweza kutoa huduma kwa sababu uwanja wa Lindi umekarabatiwa katika kiwango kikubwa kabisa, yaani hakuna hata ubishi kusema labda kuna *substandard* au labda choo kichafu. *VIP* imekarabatiwa na kila kitu kiko shwari. Lakini sasa hivi inabidi lazima twende Mtwara, tena tupande mabasi au magari ili twende Lindi. Sasa hiyo kidogo imekuwa adha. Ningeomba hilo nalo Mheshimiwa Waziri atufanyie maarifa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kwamba, nashukuru mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri aliniteua kushiriki kwenye Mikutano ya Usalama wa Anga *Montreal Canada High level – Ministerial Council on Aviation Security*. Lakini kwa wale walioshiriki, naona kuna baadhi yao wanavunja Mikataba kwa sababu viwanja kama hapa *Heath* - *London* au *Hearthow Gateweek* viwanja vya *Shipol* - Amsterdam, huko Hong Kong, *Narita* kule Japan au Nagoya, hakuna mambo unaweza ukafanyiwa ya hatari kama unavyofanyiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa ule wa Dubai. Pale ukiingia unaambiwa uvue viatu, ukishamaliza kuvua viatu uvue mkanda, sasa inakuwa adha! Yaani inakuwa mtu kama ni gaidi, eeh! Kama ni masuala ya usalama, mbona hivyo viwanja vingine vinakuwa *protected* na hatukaraishwi namna hiyo! Kwa sababu kama kuvua mkanda ghafla tu, hata suruali inaweza ikateremka kwa sababu unashtushwa, inakuwa kama gaidi, “vua mkanda.” Wale wako *very unfriendly. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama Mheshimiwa Waziri au Mjumbe yeyote anakwenda kwenye Mikutano ya *Aviation,* kweli kabisa hili jambo ni kudhalilishwa. Sijui wanakopita wakubwa, lakini mimi nimeshuhudia karibu mara nne, hii safari ya juzi ya nne. Kwa kweli ni kashfa kubwa sana. Nilifuatana na mwenzangu mmoja kanizidi uzito, alihangaika sana kwa sababu kuvua viatu kuinama hawezi, maana inabidi ukae

kwanza kwenye kochi ndiyo uvue, lakini anaambiwa: "Vua viatu haraka sana!" Sasa kwa kweli hiyo ni dalili ya unyanyasaji. Sijui sisi waafrika kutoka upande huu wa Kusini mwa Jangwa la Sahara wanatuhesabu vipi! Hilo nalo ninafikiria kwamba kuna haja ya kuweza kulizungumza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba nchi nyingine za kiafrika huwa wanazungumza wazi wazi na mimi kama ningepata bahati hiyo ningekwenda kupayuka kama walivyopayuka wakati ule wale watu wa Cameroon kule kwenye Mkutano wa Usalama wa Anga walikuwa wanasheherekea sana jinsi Muamerika alivyopigwa. Sasa na vitendo hivi vya kuvuliwa vuliwa mikanda na viatu kwa kweli havileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, naomba hilo suala la simu nililosisitiza kule Zinga Kibaoni na pale Miguruwe kwa ajili ya Makao Makuu ya Kanda ya Selous halafu na simu kule Kipatimo, nafikiri hayo ni muhimu. Hata kwangu kule, mimi niko Kilometa 135, nikitaka kuwasiliana na *DC* inabidi nipande mlima mmoja mrefu sana, nikishamaliza mlima halafu nipande kwenye mti, nikishapanda kwenye mti ndiyo nijaribu kama mawimbi yakiwa sawa naweza kupata ile *code* ya kuwasiliana. Lakini kama nikianguka, inakuwa ni bahati mbaya. Kwa hiyo, kwa kutuondolea mambo kama haya na kwa sababu biashara ni hiyo, basi Mheshimiwa Waziri naomba atusaidie hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasema kwamba nawashukuruni sana kwa kuiweka Kilwa kwenye mtandao na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini kabla sijaendelea, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Ruangwa na mimi mwenyewe kutoa pole na salam za rambirambi kwa jamaa na Wapigakura wote wa Jimbo la Kilombero kwa kupotelewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga.

Aidha, nichukue nafasi hii kuwapa pole jamaa na ndugu wa Mheshimiwa Margreth Bwana ambaye amefariki majuzi na kuwapa pole Waheshimiwa na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kupotelewa na Mbunge huyo ambaye alikuwa ni jasiri sana. Naomba Mwenyezi Mungu aweke roho za Marehemu hawa wawili mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nijielekeze kwenye hoja. Awali ya yote nachukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mwandosya, Naibu Waziri wake; Mheshimiwa Maua Daftari pamoja na Wataalam wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu - Ndugu Salum Msoma, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya hata kuletwa kwa majadiliano mbele yetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyozungumzwa na Kamati ya Miundombinu kazi yao ni nzuri kwa kipindi kilichopita na inavyoelekea itaendelea kuwa nzuri kwa kipindi kinachokuja hasa ukitazama mipango ambayo wamejiwekea katika hotuba ambayo imeletwa mbele yetu. Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Profesa Mgombelo na

Kamati yake ya Miundombinu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kufuatilia majukumu mbalimbali ya Wizara hii na kuleta ripoti zao mbele ya Kikao chako. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kwa ufupi tu huduma za simu. Katika hotuba ambayo ametoa Mheshimiwa Profesa Mwandosya, amezungumzia juu ya uboreshaji wa huduma za simu, zile wanaita *landline* ambayo azma ya Wizara na Serikali ni kuondoa moja kwa moja, teknolojia hiyo ambayo imepitwa na wakati ya simu za kukoroga.

Napenda kusema kwamba, katika ratiba waliyoweka ya kutoa teknolojia hiyo Wilaya ya Ruangwa haikutajwa, sijui kama wameisahau! Lakini Wilaya ya Ruangwa mpaka leo bado ina simu za kukoroga ambayo siyo rahisi kupatikana. Kwa hiyo, naomba kama Mheshimiwa Waziri alisahau, basi aiongeze katika orodha yake kwamba Wilaya ya Ruangwa nayo wanahitaji kupata huduma hiyo ya kisasa kwa kuondoa hizo simu za kukoroga.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Wizara hii kwa ushirikiano walionao na Wawekezaji wale ambao ndiyo wanatuwekea huduma ya simu za mikononi. Kwa kweli kama walivyosema waliotangulia, huduma hii imesaidia sana kwenye mawasiliano na kupeana taarifa hapa nchini.

Profesa Mwandosya alipokuwa anatembelea Wilaya ya Ruangwa aliahidi kwamba atawaagiza watu wa *Celtel* wawapatie wananchi wa Ruangwa huduma ya simu za mikononi na kweli watu wa *Celtel* wameweka mnara pale, lakini kwa bahati mbaya mnara ule sasa unakuwa ni kiota cha mbayuwayu kwa sababu mitambo haijawekwa ingawa kwenye ukurasa wa 108 katika *speech* yake amesema kuwa huduma hiyo imetolewa tayari.

Huduma hiyo pale Ruangwa bado haijaanza kutolewa, isipokuwa tunapata hizo *signals* au mawimbi katika sehemu fulani fulani. Kwa hiyo, ukitaka kupiga simu ni lazima uziwinde sehemu hizo, lakini kwa habati mbaya baadhi ya sehemu hizi zinakaliwa na wanyama wakali kama simba na chui, inakuwa siyo rahisi kufikia huko. Naomba sana kama Profesa akiwahimiza wawekezaji hao waweze kutufungulia huduma hii ya simu ya mkono ya *Celtel* pale Ruangwa ili wananchi wa Ruangwa nao wajisikie.

Mheshimiwa Spika, napenda kugusia tu juu ya migogoro ambayo tunasoma kwenye magazeti kati ya Wawekezaji na Serikali hususan *Celtel* na Serikali juu ya nani mwenye *TTCL* na nani mwenye *Celtel*. Inavyoelekea ni kwamba *Celtel* siyo mali ya Serikali, ni mali ya mwekezaji binafsi.

Lakini kwa upande mwingine tunaambiwa kwamba *Celtel* ni mali ya Serikali na ugomvi huu nadhani ndio umesababisha ucheleweshaji wa kusambaza huduma hiyo kwa haraka katika sehemu zile ambazo zimetajwa na tunaomba kama alivyoahidi Profesa katika hotuba yake, suala hili limalizwe haraka ili utata ambao upo sasa hivi wa nani Mwenyekiti *Celtel* uishe na kazi ya kutoa huduma hii kwa wananchi iendelee vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye huduma za usafiri wa anga. Katika eneo hili napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuboresha Viwanja vya Ndege hapa nchini. Siku hizi hali ya usafi katika viwanja hivyo ni nzuri. Kama alivyosema Mheshimiwa Omar Chubi, ukienda unapata mahali pazuri pa kupumzika wakati unasubiri ndege siyo kama ilivyokuwa zamani. Tunaomba kazi hii iendelee ili sehemu zile ambazo bado hawana viwanja, viwanja vijengwe na vipewe huduma kama ile inayotolewa katika sehemu zile ambazo zina viwanja tayari.

Nampongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na timu yake kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege kipya kule Songwe. Kiwanja hiki kilianza kuongelewa tangu miaka ya 1960 wakati nikiwa Bwana Shamba wa Mkoa mwaka 1965 mpaka mwaka 1969. Lakini nashukuru kwamba baada ya miaka mingi, angalau leo tunaona ujenzi unaendelea. Hongera sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi niende kwenye huduma za Bandari. Kwa kweli huduma za bandari zimeboreka sana. Wale ambao wanakwenda Bandarini kupeleka mizigo yao au kupokea mizigo wataona huduma inaboreka hususan katika Kitengo cha *Container*. Hapa nafurahi na kuipongeza Wizara kwa kutoa ahadi kwamba shughuli zinafanywa katika Bandari ya Mtwara kuboresha na kupanua ile *Container Terminal* ili wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na pengine Ruvuma ambapo mizigo inapitishwa pale iweze kupitika kwa urahisi. Aidha, hiyo itaongeza ajira kwa wananchi wa Mtwara na Lindi. Nashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani sitafanya haki kama sitachukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa kazi nzuri inayofanywa na kitengo cha huduma za hali ya hewa. Kwa kweli kitengo hiki kazi zake ni nzuri sana na wale ambao wana luninga wakati wote wanapotaka kujua hali ya hewa Mbeya leo ikoje Ruangwa au Tanga, wanajua. Kama ni mkulima anajua wakati ambao tayari kutayarisha mashamba yake ili aweze kupanda wakati muafaka. Kitengo hiki kinafanya kazi nzuri sana. Napenda kumpongeza Mkurugenzi wa Kitengo hiki Ndugu Muhita kwa kazi nzuri anazofanya na kumtakia kila la heri katika shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia, nichukue nafasi hii kuzungumzia kwa ufupi tu juu ya udhibiti wa *speed* za magari hususan mabasi, haya magari ya abiria. Siku za karibuni tumeshuhudia uongezekaji kwa kasi wa ajali za barabarani na vifo vingi vimetokea hapa na pale. Sababu kuu ya hizo ni *speed* ambayo magari hayo yanaitumia. Ukiwa unaendesha gari dogo kama *Land Cruiser* VX ambayo mimi naendesha kwa *speed* na kukanyaga *speed* 160 lakini napitwa na mabasi kama mshale. *Bus* hili linakwenda kwa *speed* gani siyo 200? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara itazame upya ile sheria ya kudhibiti *speed* na kuwataka hawa wenye mabasi kuweka *speed governors*. Sijui *attempt* ya mwanzo ya kuweka *speed governors* iliishia wapi. Kama teknolojia ilikuwa haifai,

nadhani fursa bado ipo ya kutafuta teknolojia nyingine ambayo inafaa na itakuwa muafaka kwa hao wenye mabasi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ishughulikie suala hili kwa sababu tunapoteza maisha ya wananchi wengi na Wafanyakazi wengi ambao kwa kweli tunawahitaji katika kuendesha uchumi kwa kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nachukua nafasi hii tena kuipongeza Wizara pamoja na Wafanyakazi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na kuwatakia kila la heri katika shughuli zao ngumu katika kuendesha hali ya uchumi na maendeleo ya jamii hapa nchini kwa kutumia teknolojia mbalimbali zile ambazo zimetajwa wakati ninazungumzia katika kumuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na kuomba Wabunge wenzangu wapitishe hoja hii ili Profesa Mwandosya aweze kupata fedha zote hizi ambazo ameziomba na aendelee kufanya kazi vizuri kama ambavyo alikuwa anaifanya huko nyuma. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo katika hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuchangia machache tu kwa sababu nimeguswa sana na jinsi ambavyo Wizara hii Waziri mwenyewe na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu wake walivyo wasikivu sana kwa Wabunge na wanavyojali sana shida na matatizo mbalimbali ya Wabunge. Napenda kuwapongeza sana kwa tabia hiyo njema kwa Watanzania na kufanya kazi nao pamoja. Nawatakieni kila jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kule kwangu Jimbo la Mlalo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo lile, tunashukuru tumepata simu. Kwanza tulianza kupata simu za ndani. Simu zile ziliweza kufungwa kwa maeneo kadhaa hasa katika Tarafa zangu mbili Tarafa ya Mlalo na Tarafa ya Mtae. Lakini jinsi tulivyokwenda tukazungumza na Viongozi hawa, Waziri mwenyewe na Naibu wake na nashukuru kusema kwamba Naibu wake aliwahi kufika mpaka kule kwenye Jimbo langu na kujionea mwenyewe hali ya Jimbo na namna ambavyo watu wanavyotaka mawasiliano hayo ya simu. *(Makofi)*

Baada ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri na kumwandikia barua, basi aliwasiliana na Kampuni ya *Celtel* na muda si mrefu tayari minara ikaanza kujengwa kule kwenye Jimbo langu. Tatizo lililotokea ni kwamba minara ile ilikwishajengwa umeme ukafungwa na majenereta yote yakafungwa karibu vifaa vyote vikafungwa, basi ikatokea ucheleweshaji ambao ulikuwa si wa kawaida.

Sasa ninawashukuru kwa sababu ucheleweshaji ule umefumbuliwa. Wakati Mheshimiwa Waziri mwenyewe akiwa kwenye mchakato wa kutafuta nafasi ya kwenda mbele kama mwenyewe anavyosema nimpongeze kwamba amefikia mahali akapata medali ya shaba, nampongeza sana, basi wakati ule nikawasiliana na Mheshimiwa Dr.

Maua Daftari Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri akajitahidi sana ule mnara wa pale Lukozi ambapo ninaishi mimi ukaweza kufungulia na simu za mkononi zikaanza kusikika.

Baada ya muda kidogo mnara wetu wa pale Malindi na pale Mlalo ikiwa bado haijafanya kazi, wakati huo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amerudi nimewasiliana na Profesa Mwandosya, akaniambia nimwandikie barua na nimpe siku tano. Kabla ya hapo wataalam wake wanaoshughulika na mitambo hiyo kule waliniambia simu hizo zingeweza kupatikana si chini ya miezi miwili au mitatu ijayo. Lakini baada ya kumwandikia Profesa na baada ya kunipa siku tano ili aweze kulishughulikia jambo hilo nilishangaa siku ya tano nilipata simu kutoka Mlalo, simu zile za mkononi. Nakushukuru sana Profesa na nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba shughuli zinapofanyika, basi zisiingiliwe na tabia nyingine kwa sababu haiwezekani wataalam waseme simu zitapatikana miezi mitatu baada ya Waziri kuingilia kati zipatikane katika muda wa siku tano. Kwa kweli kasoro hiyo naomba iondoke. Nawashukuru sana kwa sababu sasa hivi ninavyozungumza Jimbo langu la Mlalo karibu robo tatu nzima sasa vijana wanapita na simu za mkononi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Simu za mkononi kule kwetu ni maendeleo makubwa na sisi tunazihitaji sana kama tunavyohitaji mawasiliano ya barabara, kwa sababu Jimbo la Mlalo ni kama yale maeneo machache sana ya Tanzania ambayo yamejaa sana watu kiasi kwamba uzalishaji wa namna nyingine tena hauwezekani isipokuwa jitihada za kibiashara. Kwa hiyo, vijana katika Jimbo lile wanahangaika na biashara katika Miji mbalimbali kama Dar es Salaam, Tanga, Mombasa, Nairobi na Kampala. Sasa utaona katika hali ya namna hiyo simu hizi za mkononi ni muhimu sana kwa watu wa Mlalo na ni maendeleo na ustaarabu mkubwa sana kwao. Napenda nitoe shukrani hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote nimfahamishe tu Profesa na wenzake kwamba katika jitihada kubwa tuliyoifanya ya kujenga Shule ya Sekondari, leo hii Shule tulizonazo karibu zote zinapata sasa nafasi ya kuwasiliana. Ziko chache ambazo itabidi waende mita chache kidogo mbele ili wapate mawasiliano na nyingine nyingi pale pale walipo wanapata mawasiliano. Hii imeleta matumaini makubwa sana na imeleta msaada mkubwa sana na kuwaondolea wasiwasi Walimu wetu wageni wa maeneo yale ya Vijijini na kupenda kufanya kazi yao kwa sababu sasa mawasiliano yapo. Kwa hiyo, tunakushukuru sana na Wizara yake tunaishukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Jimbo la Mlalo, tunalo tatizo lingine moja ni la usafirishaji. Sasa ni bahati mbaya kwamba sehemu hii ya usafirishaji hasa wa barabara ambayo mimi kule kwangu tunautumia sana, iko katika Wizara tatu, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya TAMISEMI na Wizara hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, yeye anashughulika na uchukuzi, lakini wenzake wanashughulika na marekebisho ya barabara za Mkoa na hizo za Vijijini. Nimesoma katika taarifa yako kwamba mnashirikiana na wenzako kuona

kwamba shughuli hiyo inakamilika vizuri kwa maana ya barabara na kwa maana ya uchukuzi.

Juzi ndani ya Bunge lako niliuliza swali langu Na. 22 lile swali lilieleza jinsi ambavyo barabara za Jimbo lile zinavyopata shida kwa usafiri wa magari mengi na mazito. Sasa barabara kwa mfano ile ya Lushoto kwenda Mlalo inabeba wastani wa magari 195 kila siku na magari haya ni ya mizigo mikubwa, Fuso na mabasi ya abiria na Malori mengine yanayobeba mbao na magogo.

Kwa hali hii, barabara hii inachoka haraka sana. Kwa hiyo, tatizo la uchukuzi kwa eneo lile kama hamkushirikiana vizuri Mheshimiwa Waziri, mimi Jimbo langu litapata shida. Kwa hiyo, ninaomba sana pamoja na kwamba nimezungumza na Wizara zinazohusika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri atengeneze utaratibu wa ushirikiano na Waziri wa Ujenzi na wa TAMISEMI ili barabara zile ziweze kurudishiwa kokoto kwa sababu zinabeba uzito mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana, hapa kwenye kitabu chake, Mheshimiwa Waziri ameeleza namna ambavyo anaimarisha mamlaka ya hali ya hewa. Kwa kweli Mamlaka hii ni muhimu sana. Siku hizi katika dunia ya leo, bila kujua kesho kutakuwaje na keshokutwa kuna nini kinachotokea, kwa kweli binadamu wa leo anaishi kwa mashaka makubwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba ameanza kulichukua jambo hili kwa uzito unaostahili na kwamba amejenga Vituo sasa katika maeneo mbalimbali ya Mikoa yetu ili watu waweze kufahamu hali ya nchi ikoje. Je, tunapokwenda mbele kuna hatari? Kuna matatizo? Kuna mvua? Au kuna ukame? Kwa hiyo, nashukuru sana kwa kazi hii nzuri ambayo Wizara inafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisema nilisimama hapa rasmi kwa ajili ya kuishukuru Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo imefanya katika nchi yetu yote na pia katika Jimbo langu. Sasa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wapigakura wote wa Jimbo la Uchaguzi la Mlalo. Wapigakura wa Jimbo la Uchaguzi la Mlalo wamesaidia sana kushirikiana na mimi katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilikukuta Bungeni, mimi nina vipindi vitatu, kipindi cha kwanza tulipata matatizo makubwa sana ya ugonjwa wa tauni, tumeandamwa na ugonjwa wa tauni na watu wengi sana walipoteza maisha yao. Lakini kwa ushirikiano na wananchi wa Jimbo lile leo tauni inakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya muda kidogo tulibanwa na mafuriko na maporomoko makubwa ambayo pale Mlalo yaliua watu karibu 37 na kwa Jimbo langu zima ni karibu watu 50. Tulipambana na hali ile, leo Jimbo la Mlalo ni tofauti kabisa. Maendeleo yanaonekana wazi! Nilipoingia kwenye Jimbo lile la Mlalo, lilikuwa halina hata *Secondary School* moja. Leo lina *Secondary Schools* 13, Sekondari 10 ni za nguvu za wananchi tumejenga wenyewe, 10 kwa mikono yetu, Sekondari moja ni ya mtu binafsi na mbili za Taasisi za dini. Hivi sasa Jimbo langu tunajenga Shule za Sekondari katika Kata tatu zilizobaki ili tukamilishe kabisa kwamba kila Kata moja inayo Shule ya *Secondary School*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nimeingia kwenye Jimbo lile tulikuwa hatuna umeme, leo kuna umeme umetokea Kilometa zaidi ya 100 huku Mombo mpaka Mlalo na ni ule umeme mzito wa KV 33. Wananchi wale nawashukuru sana kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wamenipa tukafikia hatua hii. Jimbo la Mlalo lilikuwa halina simu, ni historia tumepata simu za mezani, tumepata simu za mkononi, sasa hivi robo tatu ya Jimbo lina simu, vijana wanazungumza na simu, wanafanya biashara zao na simu tunawashukuru sana Serikali kupitia Wizara hii. Lakini nawashukuru wananchi wa Mlalo kwa kuniunga mkono muda wote na kufikia hatua hiyo kubwa ya maendeleo ambayo tumeifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba wananchi na Wapigakura wa Jimbo la Mlalo, siasa ni kuvurugana, siasa ni kudanganyana, naomba wanirudishe ili tuweze kusambaza umeme Mtae, Mnazi na Mng'aro. Naomba wanirudishe ili kule ambako usikivu wa simu siyo mzuri, tuhangaike na Wizara itakayohusika ili tuweze kukamilisha hiyo kazi. Naomba wanirudishe ili tumalizie *Secondary School* zile tatu zilizobaki katika Kata na kuimarisha Shule nyingine zilizobaki.

Naomba wanirudishe tuimarishe barabara za Jimbo lile na kujenga Hospitali na Zahanati zaidi ili watoto wetu wasife kwa magonjwa ya kila siku. Nawatakia kila jema. Nawashukuru sana kwa kunisaidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. Naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**SPIKA:** Haijapata kutokea. *(Kicheko)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Wizara hii muhimu. Nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Ningelifanya kosa, kama alipokuja Pemba tukamdhamini watu 25 na zaidi kwamba hapa leo tusingeliweza kumuunga mkono katika majukumu haya makubwa ya kitaifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nimesimama hapa kumpongeza yeye, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa mafanikio makubwa na hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli imethibitisha maendeleo makubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia nataka kusema kwamba naunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia kwa mia. Kwa kweli hakuna sababu kwamba hotuba hii tusiunge mkono kwa sababu hali nzuri ya mawasiliano ya simu yanayopatikana katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, yameonyesha mchango mkubwa wa maendeleo ya Taifa letu hili. Kwa hiyo, tukiangalia maeneo ya simu, masuala ya anga, usafiri wa ndege na baharini, kwa kweli hakuna sababu ya kusema labda Bajeti hii tuitilie shaka. Namuunga mkono sana Mheshimiwa Waziri. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuifanyie kazi tumpe majukumu amalizie muda wake kama ambavyo alivyojitahidi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na maombi kama matatu kama yatawezekana. Kwa bahati Mheshimiwa Waziri aliwahi kufanya ziara Pemba binafsi, kabla ya kuja hata kuomba kura za kugombea Urais. Alitembelea maeneo ya Kiwanja cha Ndege cha Pemba, Bandari ya Mkoani na ile *gate* yetu ya Wesha. Lakini naona katika hotuba yake hakuna hata eneo moja katika haya. Anatuambia nini au atasaidia vipi? Kwa sababu ili nchi au eneo liendelee, kuna mambo ambayo yanahitajika katika eneo lile yawepo, moja ikiwa ni mawasiliano ya simu, barabara, viwanja vya ndege, Bandari pamoja na umeme wa uhakika na viwanda.

Sasa sisi Pemba tunajikuta muda wote tuko katika migogoro ya kisiasa ambayo haina msingi. Kwa hiyo, ni vizuri kama kuna uwezekano, sijui Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi imezungumzia vipi kuhusu Uwanja wa Ndege wa Pemba. Lakini ingekuwa vizuri tungeliona hapa kwamba pia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasaidia kiasi gani kuimarisha uwanja ule wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu sasa hivi watu wanakwenda kwenye karne kubwa yenye uchumi mkubwa wenye maendeleo makubwa. Nalisema hili kwa dhati kabisa kwa sababu nikinukuu Taarifa ya Habari ya tarehe 24/6/2005 ya Tanzania saa 7.00 na saa 10.00 kwa kweli nilifarijika sana. Tukasema kwamba imefikia mahali sasa hivi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kuangalia hali halisi ya Pemba kuipeleka katika maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Habari hiyo ilisema kwamba Kamati Maalum iliyoundwa kushughulikia kero za Muungano imewasilisha ripoti yake. Ikaendelea kusema kwamba miongoni mwa kero ni suala la uchimbaji wa mafuta huko Pemba na uvuvi wa bahari kuu. Sasa nasema, kama suala hili ni kweli, ni vizuri Serikali ikaliweka wazi ili watu waelewe ili kuondoa ile migogoro na dhana ambayo itakuwa kwa wananchi hata katika Baraza la Wawakilishi nasikia lilitokea hili.

Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ya Muungano ikaliweka wazi. Kama kweli taarifa hii ipo sasa hivi imefika wakati Pemba kuangaliwa kwa mapana na marefu kuhusu masuala ya maendeleo. Kwa sababu kinachoshangaza hapa ni kwamba kuna wakubwa wa dunia wanajua mgogoro, siasa Pemba siyo kwamba watu hawakusoma, ni suala la mafuta. Kuna watu wanapeleka dhana mbaya na bahati mbaya wengine ni Maprofesa, walikuja kuelezea suala la uandikishaji wa Daftari la Kupiga Kura, lakini walipofika Pemba, walisema kwamba Pemba kama tutaibiwa kura zetu itageuka Kosovo, itageuka Darfur. Hivi ni maendeleo hayo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana nikamwomba Mheshimiwa Waziri, tunashukuru kwamba ndege nyingi zinafanya safari Pemba, hatuna tatizo la usafiri wa anga, tuna ndege za kila siku Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na kurudi tena Dar es Salaam. Lakini tutapata faida kubwa kama Uwanja wetu wa Ndege wa Pemba utaimarishwa kama *gate* yetu ile ya Mkoani itaangaliwa vizuri. Yeye mwenyewe alifika nafikiri akakuta ile *gate* imedidimia chini, alipewa historia ya ile *Gate* ya Wesha, ni historia ndefu sana.  Ni eneo kubwa sana la biashara ile ya Wesha.

Kwa hiyo, sasa imefika wakati Serikali ya Muungano wa Tanzania iimarishe miundombinu ya Wesha Pemba. Kwa taarifa nilizosikia za juu juu ni kwamba Mheshimiwa Rais aliwahi kumpeleka Mheshimiwa Ngasongwa kwenda kuzungumzia suala la Bandari na kulikuwa na mpango wa kuitanua Bandari ya Mkoani iwe *gate* ya kisasa.

Kwa hiyo, ningeliomba, kama lipo hilo, tuweze kuliangalia kwa mapana na marefu. Nalizungumza hili kwa kujivunia kabisa kwa kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 26/4/2004 aliyoitua pale Uwanja wa Amani Zanzibar. Mheshimiwa Rais alisema: "Mimi ni Rais atekelezaye Sera ya Chama changu. Sera ya Muungano wenye Serikali mbili, niliapa kulinda Katiba ya nchi. Katiba inasema wazi kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Taifa moja huru lenye muundo wa Serikali mbili. Ninawajibika kwa dhati kuutetea na kuulinda Muungano huo. Zaidi ya yote mimi mwenyewe ninaamini kwa dhati kuwa Muungano wetu na mfumo wake ndiyo sahihi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu maneno kama haya makubwa ya Rais na mimi nataka nikiri kwamba Mheshimiwa Rais ameonyesha umahiri mkubwa katika kuimarisha Muungano wetu wa Tanzania kwa dhati kabisa. Hazungumzi tu ovyo ovyo, anazungumza kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna watu wanajidai wanaomboleza yale mauaji ya mwaka 2001, lakini kwa kweli Serikali ya Muungano ilitusaidia, lile janga lingekuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, sisi wengine tunamuunga mkono Rais, anapotekeleza na kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa na wale ambao wanasababisha migogoro ndani ya Pemba ni vizuri wakawa wakweli wasisababishe migogoro. Rais yuko katika kutekeleza wajibu wake, kulinda Katiba ya nchi na sheria za nchi zilizopo ambazo tumempa sisi wenyewe. Wabunge tumo humu kupitisha sheria hizo na Katiba hiyo. Wakasema kwamba tumekosea, Wapinzani wamo Wabunge wao humu na bahati nzuri Bunge la sasa ni Bunge la Vyama Vingi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaenda zaidi kwenye maendeleo ya maslahi ya nchi na maslahi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumze, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Wizara yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiruhusu Kampuni ya Simu ya *Zantel* kufanya shughuli zake katika sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Suala hili kwenye miaka ya nyuma lilitaka kuchukuliwa kisiasa. Lakini naamini hakuna jambo ambalo halina taratibu zake wala sheria zake. Kitu kilichokuwa kikitafutwa ni kufuata zile taratibu na sheria zilikuwa ni sahihi? Kwa hiyo, nina imani wale waliokuwa wakiamini kwamba labda Serikali ya Muungano ilikuwa na lake la binafsi dhidi ya Kampuni ile, sasa hivi dhana ile itaondoka na wananchi wataelewa kwamba Serikali ilikuwa haina nia mbaya, lakini ilikuwa na misingi na taratibu ambazo ni sahihi ambazo zitakuwa zinafuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo mimi nataka nilizungumze, tulipitisha sheria hapa juu ya udhibiti wa uingiaji wa watu na mizigo katika vyombo vyetu vya usafiri hasa vya baharini. Tunaomba wafanyakazi wa Bandarini wafanye kazi. Kweli vyombo

vinapakia watu wengi sana kupita kiasi. Bado hili linafanyika na vile vile uvutaji sigara katika maboti ni tatizo. Ni vizuri mkawaelekeza wamiliki wa vyombo vile wakaweza kutoa huduma nzuri kwa abiria wao kwa kudhibiti watu wachache wasiwakere watu wengine. Waweke maeneo maalum ya kuvuta sigara. Lakini inafika wakati wanapakia watu idadi kubwa na inakuwa wale wengine wanajivutia sigara ovyo na kwa kweli inasumbua, inaweza kusababisha mgogoro na watu wanataka kuuana kwa sababu kuna wengine hawataweza kuvumilia, wataweza kukataa kwamba usinivutie sigara mbele yangu na yule inategemea atalipokea vipi lile ombi. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri nataka ulipokee vile vile.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wake wa kuja kuchukua fomu kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli baada ya matokeo yale tumemwona ukimya wake na utulivu wake. Hii imethibitisha kwamba Tanzania ni moja na Watanzania ni wamoja. Lengo letu ilikuwa ni kutafuta mtu ambaye atakiwakilisha Chama cha Mapinduzi. Hakuna Waandishi wa Habari waliomtumia yeye kuleta mgogoro ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Profesa tunakupongeza sana Mungu akubariki na tuko pamoja na wewe kwa lolote. Tufuate Katiba na Sheria za nchi na miongozo inayotolewa na viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Naomba kwanza kabisa kama kawaida baada ya kutoa pole ya maombolezo ya wenzetu waliotangulia mbele ya haki, basi naomba tena nimpongeza kwa dhati ndani ya moyo wangu kwa niaba ya wananchi wa Mafia kwanza Serikali kwa ujumla, lakini pili Mheshimiwa Waziri wetu wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mama Maua Daftari; Katibu Mkuu, Bwana Salim Hemedi Msoma, Mkurugenzi Bwana Lufunjo na Wakurugenzi wote wa Idara zote zinazoshughulika, zilizokuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano kwa jinsi walivyoweza kutusaidia sisi au kuona hali jinsi ilivyokuwa ngumu katika Wilaya ya Mafia na baadaye wakaweza kutimiza au kupunguza kama si kuondoa kabisa kero ambazo zinatukabili sisi watu wa kisiwa/Wilaya ya Mafia.

Naomba niwashukuru sana na niwatakie kila la kheri, afya njema duniani na Mungu awajalie hata huko tuendako ahera, basi mambo yatakuwa mazuri tu. Si leo wala kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna aya ndani ya *Quran*, inasema: *"Audhubillahi minashaitwani rajim. Wa-amma bi-nehemat-rabbika-fahaddith,"* Ama neema ya Mola wako uliyoipata basi izungumze na kuiweka bayana. Halafu Mtume wetu Muhammad *(SAW)* amesema: *"Mallam-yashkurunnasu-laa-Yashukurullah."*

Asiyeshukuru watu kwa jambo lolote lile ambalo amepata neema hiyo kupitia kwa watu hao, kwa sababu neema inatoka kwa Mwenyezi Mungu, basi hata Mola hawezi kumshukuru. Hakika nimesimama hapa kukushukuruni wale wote waliofanikisha kuleta maendeleo kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa niaba ya wananchi wa Kisiwa cha Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mama Kimbau, lakini mimi nitakuwa napita kuchombeza tu kwa yale ambayo ameyasema. Tunashukuru *Voda Com* inafanya kazi kama alivyosema, *Celtel* inafanya kazi na pia tunashukuru Kampuni ya *TTCL* kwa kuweka mtambo wa *Digital* katika Wilaya ya Mafia na sasa unafanya kazi. Hiyo ni shukrani kubwa kabisa ambayo pia upande wa *TTCL* lazima tushukuru. *(Makofi)*

Lakini juu ya yote, kawaida binadamu unapoomba nyanda moja, basi roho inasema, basi baada ya kupata upate dhiraa. Sasa mawasiliano ambayo sasa hivi yanapatikana pale Mafia ni asilimia 50 mpaka 60 ya Kisiwa cha Mafia, sasa bado tuna tatizo la eneo la Kaskazini ya Kisiwa cha Mafia, tunahitaji mtandao huu uliokuwepo wa Kampuni ya *Celtel* na *Voda Com*, ikiwezekana, basi ujengwe mnara katika eneo la Kijiji cha Jimbo, kuna sehemu inaitwa Kijichwamchili. Hapo kila siku najaribu kupaeleza pako juu kidogo, pana mlima; mnara ukiwekwa hapo naamini masafa ya Kilometa 25 kwenda Kaskazini na kurudi nyuma Kilometa 20 ili kuungana na pale mawasiliano yanayotoka katika eneo la Kilindoni kuna Kijiji kinaitwa Ndagoni Kilometa 20 hivi inakuwa yanakatika mawasiliano.

Ukijengwa ule mnara kule, basi mawasiliano yataunganika na hatimaye Kisiwa cha Mafia kitakuwa na mawasiliano kwa asilimia mia. Kwa hiyo, tunaomba kupitia kwako kwamba Wizara iangalie uwezekano kwa kupitia Makampuni haya ama *Celtel* au *Vodacom* au *TTCL* na sasa hivi Kampuni ya *Zantel* kama ikijaliwa, kuja basi tunawakaribisha Mafia waje kuungana na wenzao wajenge mnara kwa kushirikiana ili tuweze kupata eneo hili na Kisiwa chote kiweze kupata mtandao.

Kwa sababu katika eneo hilo kuna Kampuni sasa hivi, mwezi wa nane itaanza kazi zake inaitwa *Alfa Krast* inategemea kuajiri watu zaidi ya 600 hapo Kijijini. Ninaamini kwa jinsi watu wa Mafia walivyokuwa na pesa na hamasa ya kuwa na simu sidhani kama watu wa Kampuni ile si chini ya 500 watakuwa wanaweza kutumia mitandao ya simu, ukiacha wananchi wa kawaida 20,000 walio kuwa bado sasa hivi hawatumii mawasiliano hayo. Kwa hiyo, ninaamini biashara itakuwepo na wasiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, la pili nikushukuru tena juu ya ujenzi wa gati, hakika kazi inakwenda vizuri, tuko katika hatua ya usanifu. Mwenyewe nafuatilia kila siku na pia juu ya kushukuru Mamlaka ya Bandari, lakini pia itakuwa si vibaya kuwashukuru ndugu zetu wa *Cowl Consult* jinsi wanavyofanya kazi na jitihada kubwa ya kufuatilia mambo ya kila siku ya kule na hakika na mimi wananishirikisha kila wanapofanya. Kwa hiyo, taarifa ya ujenzi wa gati, gati lipo na linakwenda vizuri. Naomba tu kuiambia jamii kwamba mambo yatakuwa mazuri wakati wowote na kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika

hotuba yake, tunasubiri utangazaji wa tenda ya ujenzi, ule upande wa *Soil Survey* karibu watamaliza na mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la uwanja wa ndege. Hakika nasema ninaona haya hata kusema sana. Lakini inabidi tu wajibu kama binadamu tuzungumze kwa sababu ndiyo Kiongozi au Mwakilishi wa wananchi wa Kisiwa cha Mafia. Mheshimiwa Waziri, mama alizungumza kwamba kulikuwa na pesa ambazo ziliwekwa, lakini naamini kutokana na mipango ambayo Serikali imeona, kwa sababu si wewe au uongozi tu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ukaamua utoe hizo pesa kupeleka sehemu nyingine, lakini umeangalia ni hali ya uzito wa sehemu na kuweza kufanikisha ujenzi huo na baadaye Mafia tutaangaliwa.

Lakini naomba wakati tunazungumza mpango wa gati, bahati nzuri Waziri wa Fedha aliweza kuliingilia hili na akaanza kufanya Kikao cha pamoja, Waziri wa Fedha, mimi na yeye pamoja na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari au Idara ile ya *Maritime* akaweza yeye mwenyewe kutamka kutoa bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa gati. Sasa naomba Wizara ya Fedha iangalie suala hili la uwanja wa ndege. Abiria wapo na Mafia ni Kisiwa kizuri chenye kivutio kikubwa kabisa kwa upande wa utalii.

Kuna hifadhi mzuri ya Bahari ambayo katika Afrika Mashariki na ya Kati hakuna. Kuna aina mbalimbali za samaki na matumbawe. Kwa hiyo, watalii, watafiti, wanakuja Mafia kwa ajili ya kuja kuangalia mambo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaomba tuboreshewe uwanja wetu. Sina haja ya kuzungumza mengi, nikaja kuikoroga tena.

Mheshimiwa Waziri naomba sana kiwanja hiki kitengenezwe. Tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuangalia uwezekano basi, tupate zile Shilingi milioni 350 ukijumlisha na hizi Shilingi milioni 50 ambazo tunazo na yule bwana mkubwa wa *Coastal Travel* amekubali yeye kuendelea kutoa ile Shilingi milioni 100, basi tuiombe Serikali itoe hiyo milioni 200 iongezee (i-*top up)* ili kiwanja kile kiweze kupata angalau katika ile sehemu inaitwa *touch down* upande wa Kusini na Kaskazini ili kuweze kuimarishwa na pale katikati tutakuwa tunaendelea kutia chokaa na udongo na kuzidi kutumia wataalam wetu kuweza kupaimarisha.

Mimi naamini tutafanikisha na Mashirika mengi pia ya ndege yatakuja. Kwa sababu kama alivyosema Mama yangu pale sasa hivi nauli ni Sh.65,000/=. Hali ni ngumu kidogo kwa wananchi wa Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, sina zaidi ya kuwashukuru kwa sababu leo ni sehemu yangu ya pili kuchangia, ni Wizara yangu ya pili na bado nitakuomba niendelee, tena ninataka kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii bado kidogo. Naomba hiyo isinikose pia.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kurejea kushukuru. Mimi leo kazi yangu ni kushukuru tu wale wote ambao wanahusika na maendeleo katika Wizara hii nimewataja Viongozi. Lakini nisije nikamsahau Mkurugenzi wa Bandari, Bwana Samson Luhigo, Meneja wa Bandari Rugaihuruza, Bwana Maro, Mr. Safari, watu wa

*Cowl Consult* kama vile Deogratius, upande wa Viwanja vya Ndege, naomba nimshukuru Mkurugenzi Bwana Tesha, Msaidizi wake Mr. Suleiman, Mkuu wangu wa Mkoa wa Pwani, bila kumsahau kwa sababu tulihangaika pamoja katika kufanikisha mambo haya. Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Mkurugenzi, Mwenyekiti wangu wa Chama cha Mapinduzi - Bwana Shomari Faki. Naomba nimshukuru sana kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Wazee wa Wilaya ya Mafia kwa sababu yeye kwa niaba ya Wazee wa Wilaya ya Mafia aliufanya Mkutano si chini ya watu 370 pale Wilayani. Wakaniita, wakaniombea dua na wakaniambia endelea na sisi tuko mbele yako katika kuhakikisha kwamba unakuwa Mbunge kwa *term* ya pili. *(Makofi)*

Naomba nimshukuru sana huyo Mwenyekiti wa Wazee, Mzee Bakari Amiri Pango na Mzee Abdallah Bin Sheikh na Wazee wote waliohusika na walioshughulika na suala hili. *Wallah* sina mengi ya kusema, ni kusema narejea tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia na kuwaombea kila la kheri viongozi wote wa nchi na sisi tuliokuwemo turejee tena kwa sababu kazi zilizofanywa na awamu hii haijapata kutokea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa njia ya pekee kwa kunipa nafasi asubuhi hii niweze kuchangia mada iliyoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Mawaziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Baada ya hapo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Ndugu Salum Msoma, kwa kazi nzuri na juhudi wanazozifanya katika maendeleo ya mawasiliano na uchukuzi katika nchi yetu. Napenda niwapongeze kwa sababu mawasiliano na uchukuzi ni msingi mkubwa wa uchumi wowote katika nchi yoyote. Nchi ikikosa mawasiliano mazuri na uchukuzi na uchumi wake umekufa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wao wanashika roho ya nchi hii kwa ajili ya kuboresha uchukuzi na mawasiliano ya nchi yetu. Nichukue nafasi nyingine kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Profesa Mwandosya kwa kukubali kufanya ziara kule Wilayani kwangu Same mwaka jana 2004, yapata majira kama haya. Nilimwomba kwa muda mrefu na hatimaye mwaka jana akakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Mwandosya ni mtu mnyenyekevu, mwenye akili nyingi na mwenye uwezo mkubwa. Yeye mwenyewe akaniambia nafasi hii twende kule Same nikaone matatizo ya mawasiliano na uchukuzi. Hata yeye kupata hiyo nishani ya shaba nafikiria anastahili na atakuwa ameweka msingi mkubwa sana wa kuweza kuifikia ile ya dhahabu kipindi kijacho. *(Makofi)*

Lakini Profesa Mwandosya alipofika kule, tulifanya kazi naye siku moja mpaka saa 5.00 usiku, hiyo ziada ya siku moja tulifanya naye kazi mpaka saa tano usiku. Sababu kubwa ni mawasiliano. Kule ambapo ziara ilipangwa hatukuwa na mawasiliano. Kwa hiyo, kila mara tukisema tuwajulishe wananchi tunakuja, hatuwezi. Lakini nilifurahi kuona kwamba ni Waziri mkakamavu sana na ni mtu ambaye anapenda kazi. *(Makofi)*

Lakini alithibitisha kwamba kule katika Wilaya ya Same mawasiliano yako katika *highway* ndipo ambako ningependa kuanzia mchango wangu. Mawasiliano yako katika *highway,* kuna minara mingi imewekwa. Mimi nafikiri si kwa sababu ya wananchi wa Same, wao wamebahatika kwa sababu ya ile *highway* lakini asilimia 90 ya wananchi wa Same hawana mawasiliano ya simu na wanaishi milimani ambapo barabara ni mbaya. Yeye mwenyewe alipita barabara hizo na akajionea jinsi barabara zilivyo mbaya.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara ya Ujenzi kwamba jana imeweza kupitisha kwa bahati pesa ile ya *STABEX* Shilingi milioni 199 kwa ajili ya barabara ya Mwembe-Msindo. Naishukuru sana Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Lakini hiyo ni barabara moja peke yake nyingine zote hazipikiti. Usafiri ni mgumu, mawasiliano ya simu hayapatikani. Tulikwenda na Mheshimiwa Profesa Mwandosya pale Kisiwani, wananchi walikusanyika wengi sana, wakiwa na matumaini ya kupata simu siku hiyo, naye akawa ahadi na matumaini. Lakini sasa yapata mwaka mmoja umekwisha wananchi wale hawajapata mawasiliano ya simu. Mheshimiwa Profesa tatizo linakuja hivi, ukitoka Mji wa Same, Mji unaofuata ni Kisiwani.

Hakuna mawasiliano ya simu, unafuata Gonja. Gonja tumepata, nakushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Same. Nimefurahi kusoma katika hotuba yako kwamba na Ndungu watapata. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri. Lakini hawa wananchi wa Kisiwani wanaona wao wako katika Kisiwa. Wanafikiri Serikali ina nia mbaya nao na kwa sababu hiyo, wanaamua kunifikisha kwenye hukumu hasa katika kipindi hiki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Profesa, mimi nikipewa hukumu mbaya, mimi nitasema na wewe umechangia kidogo. Kwa hiyo, ningekuomba sana wale wananchi wa Kisiwani wananisikia nikiongea, leo uwape majibu kwamba zile simu za *Celtel* ambazo umeahidi patajengwa mnara kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Kisiwani Kata ya Mbaga Msindo na Kata Mbaga Mshewa watapata mawasiliano ya simu za *Celtel* lini?

Nimeandika barua chungu mzima, nimemshirikisha Mheshimiwa Dada yangu Maua Daftari. Lakini bado majibu hayajapatikana na watu wa Shirika hili wapo. Sasa wale wananchi wa Kisiwani hata Mkuu wakamwuliza alipofika pale. Hivi Mheshimiwa Profesa alikuja hapa na vyombo vyote vya mawasiliano na uchukuzi, magari zaidi ya 15 yenye Viongozi wa Mawasiliano na Uchukuzi lakini bado wale watu hawana mawasiliano. Kumetokea nini? Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri ukaliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, sehemu kubwa ya milima ya Same hakuna mawasiliano ya simu. Ukienda kule Kata ya Vudee, Muheza, Mwembe, Mamba Vunta, Mamba Miamba, Mamba Bwambo, Ruvu, Kizungo, hakuna mawasiliano ya simu. Mawasiliano yetu ni ya mguu kushoto, kulia, kushoto, kulia, sasa tunaposema mawasiliano yametapakaa nchi mzima, mbona kule hamna?

Ningeomba Mheshimiwa Spika, wakati mnajibu swali langu la mawasiliano ya simu kule Upareni, Naibu Waziri alisema kuna matatizo ya kijiografia kwa sababu ya

milima. Mbona simu ziko katika milima ya Usangi, ya Lushoto kwa Mheshimiwa aliyeongea sasa hivi na kule kuna milima vile vile? *(Makofi)*

Milima ya Same ina tatizo gani la kiufundi ambalo hatuwezi tukaambiwa? Tunaambiwa matatizo ya kijiografia, *black spot.* Hayo matatizo ambayo wataalam hawawezi kuyazuia yana shida gani? Kule Ulaya kuna milima, lakini watu wana mawasiliano. Sasa hapa kwetu kumekuwa na shida gani? Ningeomba safari hii wananchi wa maeneo hayo wapate majibu na ikiwezekana wajue mpango wa Serikali wa kuwapelekea mawasiliano ya simu.

Baada ya kulisema hilo, Mheshimiwa Waziri napenda kuchangia kuhusu usafiri na uchukuzi kwa njia ya reli. Kwanza nianze na reli ya Tanga, niongelee na reli ya Kati. Reli ya *TAZARA*, nafahamu kuwa nia ya Serikali ni kubinafsisha huduma ama kukodisha huduma za reli. Lakini nafikiri hata hawa wakodishaji watakuja kufanya biashara ya kuchuuza tu ili waweze kupata faida. Nchi nyingi ambazo zimejenga miundombinu ya reli wameshirikiana wakawa na *joint venture.* Hata Tanzania sisi tulipoanza kuwa na reli ya uhuru, Mwalimu Nyerere pamoja na Dr. Kaunda walikaa wakakubaliana kuwa na *joint venture* ya reli ya uhuru hii ya *TAZARA* sasa hivi. Hatukuweza kuijenga sisi wenyewe.

Napenda niishauri Serikali kuwa na *joint venture* na nchi zinazotuzunguka. Lakini tuwe na reli ya kisasa. Labda ya njia tatu kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma ya treni ya abiria ambayo ni *fast train* kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam, labda kwa muda wa masaa matatu. *(Makofi)*

Njia nyingine mbili ziwe za mizigo. Tukishirikiana na nchi za jirani, mimi nina imani tunaweza. Pia, napenda niishauri Serikali kuhusu reli ya Tanga mpaka Arusha, kushirikiana na nchi za jirani kuiendeleza mpaka Musoma kwa njia tatu. *(Makofi)*

Kama Serikali inaweza kwenda kutafuta fedha za kufanyia mabadiliko makubwa ya barabara, kwa nini ishindwe kwa reli? Itafute wachuuzi! Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili ukalifikishe katika Baraza la Mawaziri. Kama tutakuwa na usafiri wa reli wa uhakika nina imani tutaweza kuibua uchumi wa nchi kule Kigoma na kule Musoma na nchi za jirani. Wenzetu hawa wa nchi za jirani wanatuangalia tunavyokalia uchumi wetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli kabisa.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Tunatafuta wachuuzi, hawa wanaokuja wanasema wanataka kufanya biashara na reli zetu, wanakuja kutuchuuza na kupata faida na hatimaye wanaondoka, hawatafanya maendeleo yoyote. *(Makofi)*

Ningeiomba Serikali kabisa kwa nguvu zake ihakikishe kwamba inaamua kuwekeza katika kujenga reli hizi. Hakuna mfanyabiashara anayeweza kujenga reli. Akitaka kupata faida irudi, labda baada ya miaka 100 kwenye vitukuu. Kwa hiyo, Serikali inataka kufanya mabadiliko, ni Serikali yenyewe ikubali kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu usalama wa usafiri kwa njia ya reli, anga na majini. Tumejifunza kwa ajali nyingi zilizotokea za reli, kule Msagati, *MV Bukoba* katika Ziwa *Victoria*. Kwa anga hatujapata, lakini naiomba Serikali ikae sasa ifikiri kwamba hiki kinachoitwa kifuta machozi ni kitu gani? *(Makofi/Kicheko)*

Ni kitu gani kinachoitwa kifuta machozi? Kama tumeanzisha Shirika likawa ni Shirika limekamilika, liwe limekamilika vile vile na kuweza kuwafidia watu wake wanapopatwa na ajali. Watu wanakufa, wanaambiwa unapewa kifuta machozi, hivi kuna kitu kinachoitwa kifuta machozi? Kwenye sheria kuna kitu cha namna hiyo? Ningeomba Mheshimiwa Waziri aangalie, ile ni huruma ama ndiyo Sheria inavyosema?

Vile vile, kuna watu wanapata ajali katika ma-*bus* wanazunguka miaka nenda rudi wakitafuta haki ya kufidiwa kwa Bima, inashindikana, ni kwa sababu gani? Ningeiomba Wizara iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niongelee kuhusu huduma za Posta. Kama ambavyo nimeongea hapo awali, mawasiliano kule kwetu ni shida hata huduma za Posta ni shida. Watu wote wanategemea Posta moja pale Wilayani ile ya Same, kwa ajili ya huduma za *Money Fax* pamoja na *Western Money Union,* kipindi cha bajeti iliyopita niliomba kwamba wananchi wanakuja pale wakisubiri hela kwa muda mrefu, siku mbili siku tatu, wanalala pale, wanatumia hela yao kwa chakula na malazi wakisubiri walipwe, ni kwa sababu gani?

Mpaka leo, pungufu hilo halijaweza kusahihishwa. Ningeomba hayo mapungufu yapunguzwe na ikiwezekana yaondolewe kabisa. Kuhusu Benki ya Posta, Benki ya Posta imekuwa ikitoa huduma katika Vijiji vyetu kule Wilayani Same na kwa usalama wa fedha za wananchi. Lakini sasa hivi wakati wa wimbi la ujambazi wananchi wengi wanaporwa pesa zao kwa silaha. Zamani walikuwa wanaweka fedha zao katika Benki za Posta kwa usalama.

Tunazo Benki Kata kweli. Lakini watu walizoea kuweka pesa katika Benki ya Posta kwa sababu zina mtandao mkubwa zaidi. Akisafiri akienda Dar es Salaam anaweza kupata fedha, akienda Moshi anaweza kupata fedha. Ningeomba Mheshimiwa Waziri ukahakikishe kwamba hizi huduma za Posta zinaboreshwa kule katika Wilaya ya Same kwa sababu wananchi wanapata adha ya kufuata huduma hizi pale Wilayani, kama ametumiwa Shilingi laki moja, inabidi atumie zaidi ya Sh.30,000/= kwa ajili ya safari, malazi na chakula. Kwa hiyo, ile thamani ya ile fedha inashuka. Tungeomba sana Mheshimiwa Waziri hilo ukalipatie majibu wananchi wafahamu hatima yao na huduma ya Shirika hilo la Posta.

La mwisho kabisa, ni usafiri wa anga. Hivi Dodoma kuna shida gani ya kuwa na usafiri wa anga? Kiwanja cha ndege chenyewe cha masaa machache tu na usalama hakuna! Tunasema huu ndio Mji Mkuu wa Serikali na Chama, siku zote tunakimbizana na magari, hapa kuna nini? *(Makofi)*

Kama Serikali imeona hapa ni Kijijini ikatupe majibu leo. Kwa nini, hiki kiwanja hakiboreshwi. Serikali ina mpango gani nao? Ikitokea dharura hapa inabidi watu

kukimbizana na magari kwa sababu ndege hakuna ama ndege ya Serikali iombwe ije, iondoke. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri leo atueleze Dodoma kuna shida gani ya kukosa huduma za ndege kuna shida gani? Ukitaka kusafiri kwa ndege kwenda Arusha, Dar es Salaam, kwenda Tanga haiwezekani, kwa sababu gani? Bunge liko hapa, Serikali iko hapa, Chama kiko hapa tena Chama kilichoshikilia mpini na Spika yuko hapa. Kuna shida gani? Tunataka ndege iwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ana safari ya kwenda Longido, lakini inabidi afanye mikakati ya kwenda huko. Lakini kama mambo yangekuwa mazuri, haya yasingetokea. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri hilo uaaliangalie sana kwa sababu hatimaye linaweza likatuletea hasara hata ya kupoteza maisha ya Kiongozi hapa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda niunge mkono hoja, lakini naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke hoja yangu ya kufikishwa katika hukumu wale wananchi wa Kisiwani na zile Kata za Mbaga waweze kupata huduma za simu za *Celtel* mapema inavyowezekana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Watakaochangia mchana ni Waheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Willfred Lwakatare na Mheshimiwa Beatus Magayane.

Kama nilivyoeleza asubuhi, ni kwamba ni vizuri wanaopenda kuchangia kwa maandishi wafanye hivyo mapema ili Waziri mhusika ajiandae kujibu hoja zao. Nashukuru kwamba imefanyika hivyo, wamepata michango mingi ya maandishi. Kwa hiyo, wanahitaji muda mrefu wa kujibu hoja zote.

Kwa hiyo, hawa watatu watakapomalizika nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri halafu Mtoa Hoja mwenyewe. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa jioni ya leo ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, lakini nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho cha 20 na mimi lilikuwa ni Bunge langu la kwanza. Katika vikao hivi 20 nimejifunza vitu vingi sana, kwanza kutoka kwako wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo nimejifunza ni suala la kuzingatia muda. Kwa kweli kwa Vikao vyote ambavyo nimekuwa hapa saa 3.00 Kikao kinaanza, saa

11.00 juu ya alama Kikao kinarudia.  Sijawahi kuona mahali pengine katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, umenifunza hilo na mimi nitajitahidi katika maisha yangu kujaribu kidogo. Umeona leo nimewahi dakika 15 kabla, nilitaka kuvunja *record*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili umetufundisha namna ya kupanga mipango kisayansi. Mipango inapangwa, kwa tuliokuwa wageni tulikuwa tunasema hii ratiba kweli itaisha? Lakini inakwenda inaishia pale pale ulipopanga, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Lakini kwa maoni yangu, la tatu ambalo nimejifunza ni *system* ya malipo iliyo katika Bunge letu.  Ni *system* ambayo ni *very efficient*. Ni mahali pachache sana katika nchi utakuta mahali pana utaratibu usiokuwa na mikwaruzo wala mkwamo wa aina yoyote kama *system* iliyoko hapa. Kwa ujumla mimi nafikiri hata wanaojifunza wanakwenda nchi za nje huko kujifunza namna ya kuendesha mambo yao, wangekuja hapa Bungeni wangepata mawili matatu namna ya kuboresha jinsi ya kutoa huduma katika sehemu zao za kazi. Ananikumbusha Mheshimiwa hapa kwamba bado moja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijafika mbali, nitoe rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kongwa, kwa kifo kilichotokea cha Mheshimiwa Marehemu Margareth Bwana, Mwenyezi aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nimesema namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo asubuhi hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri ni msomi wetu na ni moja ya wasomi ambao sisi tunajivunia katika nchi hii. Niliwahi kupitia *CV* yake moja wakati fulani sikuamini nilichokuwa nakisoma, kwamba huyu Mtanzania Mzungu huyu!! *(Kicheko)*

Kwa kweli katika Watanzania ambao tunajivunia kabisa kuwa nao tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa *achievement* zote ambazo umefanya katika maisha yako. Ni msomi tunayejivunia kabisa wa ngazi ya *professor*. Pia, nakupongeza kwa kupata medali ya shaba kule Chimwaga, si haba ndugu yangu. Ulijitahidi sana na kama walivyosema wenzangu, asubuhi safari ijayo, basi tumwombe Mungu, uendelee kutuombea na sisi tuwepo tunaokumbuka kumbuka kilichotokea ni nini. Lakini kwa kweli umefanya *achievement* kubwa sana, tunajivunia sana kwamba mwanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi una sifa hizo na umefikia kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza wote walioshinda ambao kama nilivyosema kwenye hotuba yangu iliyopita kwamba kule Kongwa sisi tunasubiri maboksi ya kupiga kura, hatuhitaji debe.  La nini? Kazi iliyofanyika imeonekana, ni kazi nzuri kabisa, wananchi hawana wasiwasi hata kidogo. Pia, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kupata fursa ya kutembelea Kongwa mwezi Aprili mwaka huu 2005, akajionea mwenyewe hali halisi ya mawasiliano ya Wilaya ile na tunakushukuru sana kwa changamoto ulizotuachia.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu sana ambayo inashughulikia sekta muhimu sana ya mawasiliano. Tumekuwa tukizungumza hapa umuhimu wa kuimarisha barabara na kwa kweli tumeona juhudi za uimarishaji wa barabara katika nchi yetu. Lakini iko sekta ambayo ni lazima iende sambamba na uimarishaji wa barabara na sekta hiyo ni Sekta ya Mawasiliano.

Katika mkakati wetu wa MKUKUTA Sekta hii ni lazima iimarishe sana uchukuzi barabarani, usafiri wa reli, usafiri wa anga, usafiri wa majini baharini na maji baridi kwenye maziwa yetu, huduma za Posta, huduma za simu, teknolojia ya habari kwa ujumla iwe ni magazeti, *television*, *redio* na kadhalika na masuala ya hali ya hewa. Haya ni mambo muhimu sana katika mkakati wetu huu wa kupambana na umaskini.

Nilipata bahati ya kusoma nchi moja huko Ulaya wakawa wanasema kwamba *indicator* moja ya mtu maskini ni kukosa simu. Yaani, kukosa mawasiliano ya simu ni *indicator* ya *poverty*. Lakini tumeona sisi wenyewe katika kipindi kifupi kilichopita cha miaka mitatu minne ambacho *Professor* amekuwa Waziri pametokea mabadiliko makubwa sana katika Sekta ya Mawasiliano ya simu na hasa simu za mkononi. *(Makofi)*

Hata kule Kongwa tumepata huduma hiyo, tunakushukuru sana. Siku hizi usiku wa manane ukisikiliza ile *Radio Free Africa* hakuna kulala, utasikia watu wa Kongwa, nao Panda mbili, Kongwa hapa hakuna kulala, Vijijini ndani kabisa huwezi kuamini kabisa. Tunakushukuru sana na hii imesaidia sana huduma za kibiashara. Wananchi wa Kongwa ni wakulima wa karanga na mahindi. Zamani zile lazima asafiri aende Tanga akaangalie soko la karanga likoje ndio arudi atafute roli apakie magunia yake apeleke. Sasa hivi anapiga simu dakika mbili soko bei gani? Arusha soko bei gani? Dar es Salaam vipi? Anajua sasa nipeleke Arusha.

Kwa hiyo, ni hatua kubwa sana ambayo imewasaidia sana watu wetu katika kusonga mbele kimaendeleo. Lakini mbele zaidi nitaongelea baadhi ya maeneo ambayo tunaomba Mheshimiwa Waziri ayatazame kwa maana ya kuimarisha huduma hizo za mawasiliano ya simu. Hivi karibuni mtandao wa *Celtel* umekuwa ukisumbua, wateja wengi wanahangaika lakini hayatoki maelezo mazuri ya nini kinaendelea. *(Makofi)*

Kwa sababu Kampuni hii tunazo Hisa zetu humo Watanzania ,basi nafikiri tunastahili kujua kama kutakuwa na sentensi moja, mbili Mheshimiwa *Professor* akipata nafasi tujue tu ni nini kinachoendelea kwenye *Celtel.* Sasa hivi kuna usumbufu fulani katika mawasiliano ya mtandano huo. Nikirudi kule Jimboni tunayo Hospitali yetu ya Wilaya pale Kongwa ambayo kwa muda mrefu sana haina mawasiliano ya simu ya *TTCL*. Hospitali hii ni ya Rufaa kwa maana ya Wilaya yetu inapokuwa haina mawasiliano ya simu ni jambo la hatari sana.

Nimejaribu sana kuwaona Viongozi wa Shirika letu la *TTCL* hapa Dodoma, lakini imekuwa kidogo vigumu kuweza kutatua tatizo hili. Imekuwa ni mwaka mzima sasa Hospitali hii haina mawasiliano ya simu. Kupitia kwako na kupitia kwa Katibu Mkuu na wataalam walioko huko, naomba mlitazame kipekee tatizo hili la huduma za simu kwa

Hospitali yetu ya Wilaya ya Kongwa kwa sababu iko pale pale Mjini, hakuna sababu kwa nini pasiwe na mawasilino ya simu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo nyuma, Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kutembelea Kongwa nikampeleka katika eneo moja ambalo ndilo eneo kubwa sana la uzalishaji wa mahindi yanayouzwa katika Soko la Kibaigwa. Tarafa ile inazalisha zaidi ya asilimia arobaini ya mahindi yanayouzwa katika Soko lile. Wananchi wale ni wakulima wazuri kwa *standard* zetu za Kitanzania, ni wakulima wakubwa, kwa maana ya wananchi wa kawaida wakiongozwa na Prof. Daimon Mwaga ,Mbunge wa Kibakwe, mkulima mzuri sana katika maeneo hayo hayo. Lakini eneo lote lile halina mawasiliano ya simu. *(Makofi)*

Wananchi wanaomba sana na wamenituma nimkumbushe *Professor* na kwa kweli nimekukumbusha sana na ninachukua fursa hii kukumbusha tena. Sasa bahati mbaya wamefikia mahali wanasema sasa, mzee simu isipokuja lile jengo jipya la Spika hutaliona. Basi na mimi nimesema niende nikajisalimishe kwa Mheshimiwa Waziri kwamba akitoa neno moja tu roho yangu itapona. *(Kicheko/Makofi)*

Tunakuomba sana, sisi pale ni nguzo moja tu basi, itakuwa tumekwishapona kabisa ili wananchi wale waweze kupata huduma hii ambayo wanaililia mara kwa mara katika eneo lao.

Mheshimiwa Spika, jana palikuwa na swali kuhusu reli iliyong'olewa Mtwara - Masasi na Nachingwe zamani zile. Maelelezo yakatolewa hapa kwamba reli ile iko mipango maalum kabisa katika Mtwara *Corridor* ya kuirudisha na kuindeleza mbele ya pale iweze kwenda mpaka Mbambabay. Jambo zuri naipongeza Serikali kwa sababu ya umuhimu tuliofundishwa hapa Bungeni wa uchumi wa jiografia.

Mheshimiwa Spika, lakini nikumbushe kwamba reli ile ilipong'olewa ile ya Mtwara, pia ing'olewa. Reli ya kutoka Kongwa hadi Msagati wakati ule ule na reli hizi nafikiri uamuzi ule wa kuzing'oa haukuangalia mbali sana. Kwa hiyo, nami nilikuwa naweka ombi langu hapa katika kurudisha reli hizi zirudi zote isirudi moja moja. *(Makofi)*

Ile ya Msagati – Kongwa *actual* ilikuwa na lengo la wakati huo ifike Hogoro iweze kwenda Simanjiro, iweze kutokea Arusha ndio ilikuwa *plan* ya wakati ule ya kikoloni. Eneo hilo la katikati hapa Simanjiro, Kiteto, Kongwa mpaka Arusha ni eneo la uzalishaji mkubwa sana; iko mifugo mingi sana na mazao ya kilimo mengi sana. Kwa hiyo, tunakumbushia tu katika jiografia ya kurudishia mtandao wa huduma za reli zilizokuwepo mwanzoni, basi muikumbuke na hiyo reli iliyong'olewa ya kutoka Msagati kwenda Kongwa na kuelekea Hogoro na ikiwezekana ikaunganisha na Arusha.

Mheshimiwa Spika, habari ya reli ya kutoka Arusha kwenda Musoma imekuwa ikiongelewa mara nyingi sana hapa. Yako mambo mawili mimi huwa yananisumbua kwa sababu huwa sipati majibu halisi kutoka Serikalini, ningeomba siku zijazo hata kama si leo yakatolewa majibu ya ufafanuzi wa uhakika. Moja ya reli ya kutoka Arusha kwenda Musoma, mimi taaluma yangu ni Muhifadhi wa Wanyamapori, kwa hiyo, Ngorongoro,

Serengeti ndio maeneo yetu hasa. Kupitisha reli kutoka Arusha kwenda Musoma kwenye hifadhi zile na ukitazama usumbufu unaotokea kwa barabara tu ya Mikumi peke yake hapa utakuta ni tatizo kubwa sana na Serengeti ni hifadhi ambayo ina umuhimu wake na nafasi yake kidunia, Ngorongoro ndio kabisa *World Heritage Site*. Hivi kweli jambo hili linawezekana au huwa tunasema tu! Ifike mahali Serikali iseme kama jambo hili linawezekana au haliwezekani. Ninachojua mimi, *World Bank* wala nani hawawezi kutoa pesa ya jambo hilo, kwa sababu watakaofanya *environmental impact assessment*, *definitely* watasema hiki kitu siyo *feasible*.

Mheshimiwa Spika, liko la pili niliseme hapa hapa, nalo ni la mradi wa *Stigler's Gorge* wa umeme. Waheshimiwa Wabunge wengi sana huzungumzia habari ya *Stigler's Gorge*. *Stigler's Gorge* iko ndani ya *Selous Game Reserve* na hii nayo ni *World Heritage Site,* ni eneo muhimu kabisa la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira. Si rahisi sana kuanzisha bwawa kubwa sana ndani ya hifadhi ya aina hiyo na si rahisi kupata mkopo wa Mashirika makubwa hayo. Kwa sababu wao kitu cha kwanza watauliza mazingira yanasemaje? Labda ndio maana huko nyuma ilishindikana. Lakini huwa nasikia Waheshimiwa wengi wakizungumzia mambo haya mawili. Mimi nafikiri huko mbele ya safari tuelezwe mambo haya yanawezekana au hayawezekani? Ili tuache kuyaongelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho iko habari kwamba wako baadhi ya watumishi wa Mashirika ya Umma waliuziwa nyumba za Mashirika. Lakini pia watumishi hao hao wakauziwa nyumba za Serikali, kwa hiyo wanakuwa wamewapunja wenzao kwa kupata *double allocation*. Nilikuwa nashauri tu Serikali ingejaribu kuangalia chati nzima ya waliokopa nyumba hizi za Serikali au zile za Mashirika ili basi na wale wengine ambao hawakuweza kupata nafasi hiyo wakaweza kuipata nafasi na siyo wengine wanachukua nyumba mbili mbili, tatu tatu. Sina hakika na jambo hili, lakini nimelalamikiwa mara kadhaa kama Mbunge kwamba wako watu ambao wana nyumba kutoka kwenye *source* mbili tatu kwa mlango ule ule wa Utumishi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kukushukuru sana kwa fursa hii na nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba ombi langu ni moja tu, lile lile la nguzo moja tu pale kwenye mlima wa Hogoro, tukipata hiyo nguzo sisi watu wa Kongwa hatuna maneno kabisa. Naomba kushukuru na kusema kwamba naunga mkono hoja iliyo mbele yetu asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kuniruhusu kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasialiano na Uchukuzi kama alivyoitoa leo hii asubuhi. Pia, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri na Naibu wake pamoja na Watendaji wake wote kwa jitihada zao nzuri wanazoendelea nazo ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kabisa bila unafiki wa ndani kwa Mawaziri hawa kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa kweli wote wawili wamejitahidi na wamefika mpaka Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufika kwao kulikuwa ni faraja kwa wanachi wa Jimbo la Bukoba Mjini. Lakini vile vile kazi yao imeweza kuonekana kwa kiasi kikubwa, kwa sababu hivi sasa unapozungumzia Bukoba, mtandao wa mawasiliano upo, *Celtel* wapo, *Vodacom* wapo, *Mobitel* wapo, *TTCL* wanafanya kazi nzuri, kuna *internet café* pale Bukoba Mjini. Kwa hiyo, hata hao waliofikiria kutupandisha hadhi ya kuwa Manispaa, naamini hawakukosea kabisa, kwani Bukoba panapendeza, Bukoba ni *British Kingdom* ambapo panafaa kuishi mtu yeyote yule ambaye anajihisi amekosa amani, amekosa mazingira mazuri ya kuishi. Bukoba panapendeza kwa kweli kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Ukiachilia mbali suala hili na simu, *of course* suala la simu watu kuwa na simu ni jambo lingine, namna zinavyowasaidia kwa hivi sasa ni jambo lingine pia. Labda matatizo mengine ni kutokana na mchakato mzima wa kiuchumi ambao unakwenda sambamba na mambo mengine mengi. Lakini *at least* mtu kuwa na mtandao wa mawasiliano naamini ni hatua moja kubwa sana katika kujaribu kujikomboa kiuchumi. Hata ukikaa na simu ukawa *una-beep,* basi hata na yule unayempigia *aka-beep* pia hiyo ni matatizo mengine. Lakini naamini hayo mambo mengine tutayarekebisha mbele na hasa tukichukua Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuchangia suala moja ambalo kwa kweli limekuwa tatizo kubwa na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanalifahamu pale Bukoba Mjini. Ni suala la Uwanja wa Ndege wa pale Bukoba Mjini kwa kushirikiana na Viongozi mbalimbali na Wadau mbalimbali. Bila shaka, Waziri analifahamu hili, tumetembelea kwenye Ofisi yake mara nyingi, tumekaa naye katika Vikao kuzungumzia suala la Uwanja wa Ndege wa Bukoba. *(Makofi)*

Tunashukuru katika majibu ya Mawaziri, Waziri wa Maliasili na pia katika majibu ya Naibu Waziri jana alilizungumzia suala la Uwanja wa Ndege. Mheshimiwa wa Maliasili alizungumzia jinsi gani Mji wa Bukoba unavyokua kwa kasi kuhusiana na Sekta ya Utalii. Lakini inaangushwa sana na kutokuwa na uwanja unaoaminika, uwanja ambao unaweza ukamudu hali zote za hewa. Uwanja wa Bukoba bado ni wa tope hadi hivi leo tunavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri katika kujibu swali hapa Bungeni alizungumzia uwanja mpya ambao unategemea kujengwa na ambao ulishafanyiwa upembuzi yakinifu wa Mkajunguti. Lakini katika majibu hayo hakuonyesha matumaini kwamba kazi hiyo inaweza ikafanyika kesho au keshokutwa. Mmesema bado suala hili linaombewa pesa, pesa ambazo naamini hakuna ambaye amekwishajitokeza kuweza kufadhili uwanja ule.

Sasa mimi ombi langu ni moja tu, pamoja na kupongeza hizo jitihada zinazoendelea kufanyika za kutengeneza huo uwanja wa Mkajunguti, uwanja mpya, suala nililokuwa naomba ni kujaribu kutafuta uwezekano kama ambavyo tumekuwa tunakuja kwenye Ofisi kuomba uwanja wa Bukoba uwekewe lami. Ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa *ana-sum up* hapa ajaribu kuzungumzia jitihada hizi zimefikia wapi. Kwa sababu ni matatizo, hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri anaelewa,

nilishamletea hata picha za kuonyesha hali halisi ya uwanja ule unavyokuwa pindi mvua inaponyesha, ndege zinashindwa kutua na kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati ndege ilishawahi kukwama hata kwenye tope ikabidi isukumwe kama gari. Sasa katika hali hii naamini tunaweka rehani roho za watu wanaotumia ndege kwa kutumia uwanja ule. Wakati wowote itatokea ajali ukiachilia mbali ajali ambazo zimeshatokea za ndege nyingine japokuwa labda siyo tatizo la tope. Lakini uwanja kwa kweli uko katika hali mbaya sana na hivi ninavyozungumza nafikiri kuanzia kesho au kesho kutwa kwa muda wa siku tatu hakutakuwa na ndege pale Bukoba Mjini. Sasa hii inaleta matizo.

Mheshimiwa Waziri tunaomba kwa kweli hili suala uliangalie na ninaomba uwape matumaini, uwape majibu wananchi wa Bukoba waweze kuelewa ni nini ambacho kinaweza kufanyika kwa mwaka huu wa fedha 2005/2006 dhidi ya uwanja ule. Ninamini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Bukoba Mjini, Serikali tunaweza tukafanya mpango maalum wa kuona namna gani tunavyoweza kushirikiana kuhakikisha uwanja ule unawekewa lami.

Pia, labda kuna mtizamo mmoja ambao wengine wanaweza wakawa nao kwamba labda kwa sababu kuna mipango ya uwanja wa Mkajunguti kwamba labda unataka kujengwa. Tukijenga huu *tuki-invest* kwenye uwanja huu wa Bukoba Mjini tutakuwa tunafanya *double costing*. Mimi nafikiri haina matatizo kutokana na kukua kwa hali ile ya uchumi wa Bukoba, mimi nafikiri hata takwimu zinaonyesha hivyo. Uwanja wa Bukoba abiria wanaotumia ule uwanja ni abiria wengi mno kuliko hata viwanja vingi vya hapa nchini, lakini pia nafikiri hata kuwepo uwanja wa kimataifa Kilimanjaro haukuizuia Serikali kuweza kuufanyia matengenezo makubwa uwanja wa pale Arusha licha ya kwamba viwanja hivi viko karibu karibu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia kuhusiana na suala ambalo nilijaribu kulizungumza jana na ndugu zangu wengine wakasema Sheria Sheria. Suala la boti, licha ya kaka yangu kusema naharibu, mimi natoa kavukavu hapa hapa. Unapozungumza suala la boti kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa unagusa roho za watu, tuache wale ambao hawajui hata meli inafananaje. Lakini kwa mwananchi wa Kanda ya Ziwa unapozungumza suala la meli, suala la boti ni sawa na mtu ambaye amewahi kuumwa nyoka uje ukanyage jani utafikiri nyoka.

Watu wa Bukoba, Mwanza, watu wa Mikoa ambayo inazunguka Ziwa Victoria wanafahamu umuhimu wa kuwa na usafiri unaoaminika wa vyombo hivi vya majini kwa sababu tumewahi kuumwa na nyoka. Watu wamewahi kufa ndani ya *MV Bukoba* kwa sababu ya kujazana sana abiria ndani ya meli hiyo. Kwa hiyo, tunaposikia mtu anafanya mzaha na suala hili, sisi tunasema huyu hatutakii mema, anataka tuendelee kufa.

Meshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili la boti ambazo zilitaka kupelekwa na *Lake Fast Ferries* lisiwe suala la kumalizia malizia kwa maneno ya ajabu ajabu, maneno ambayo hayatoi majibu sahihi, maneno ambayo sisi wengine narudia tena tunashindwa kuelewa *Cabinet* inafanyaje kazi.

Kwa kweli ninapojaribu kukuna kichwa kwa kiasi kikubwa, najiuliza kwamba yule niliyemwona pale Bandarini ni *Proffesor* Mark Mwandosya, msomi kama alivyozungumza, ndugu yangu Joseph Mungai hapa, msomi wa kimataifa, aende pale melini atoke ndani ya *cabinet* hajui sheria hiyo Na.30, aende kuwatangazia Watanzania wa Kanda ya Ziwa kwamba sasa meli zinaondoka.

Halafu kuna mtu mwingine kutoka kwenye Kikao hicho hicho cha *cabinet* anasema *stop*, haziendi! Inaleta walakini, watu hawaelewi hizi. Wengine wanaanza kufikiri kwamba hapa ni mapambano ya mafahari wawili tu, lakini zinazoumia ni nyasi. Watu wa Bukoba wanaumia, watu wa Mwanza wanaumia wanaotaka vifaa hivi kuvitumia.

Mheshimiwa Spika, pia, tunawaweka katika hali ya wasiwasi hata wawekezaji wengine ambao wangetaka kuja kuwekeza pale, wanafikiri labda na wenyewe watazungushwa katika utaratibu huu huu. Sasa mimi nafikiri tukiacha haya mambo ya majibizano, mambo ya kurefusha maneno, ingefaa kwa kuwaacha Mawaziri hawa wawili, Maskari wa Miamvuli ambao kwa bahati mbaya wanagongana huko hewani labda wanakwama ndani ya miti. Serikali itoe kauli rasmi *what is going on?* Tusiache linaeleaelea, tunaacha redio vifuu ndiyo zinafanya kazi Mitaani. Mara wamenyimana mshiko, mara sijui nani kafanyaje, mara bwana anamtilia mkwara anagombea Urais.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi hatuelewi! Tunataka kujua! Sisi tunachotaka ni usafiri wa chombo hiki kwa manufa ya wananchi wa Kanda ya Ziwa ambao tunatumia vyombo hivi vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nitaomba kwa kweli wakati *una-sum up* utueleze kwa upande wako maana yake na wewe hujatueleza. Hivi wataalam wa pande mbili wa Wizara hizi na huyu mwenye boti wameshindwa kukutana kuzungumzia hili suala na kuweka mambo vizuri? Nini kinachoshindikana? Au ni ubabe ubabe tu hapa unaotumika!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wananchi wa Bukoba kupitia Bunge hili tutaomba tufahamu nini msimamo wa Wizara hii. Kwa sababu hili suala limeachwa linayumba kwenye Wizara mbili kwa sababu Serikali haitoi kauli kuhusiana na suala hili. Tueleze sasa upande wa Mawasiliano na Uchukuzi mnasemaje kuhusu suala hili? Au mmeliacha tu lieleeelee, basi wananchi wa Bukoba waendelee kuumia!

Mheshimiwa Spika, mimi nisingekuwa na mengi ya kuzungumza zaidi ya hapo. Lakini nitaomba Mheshimiwa Waziri, suala hili la Uwanja wa Bukoba kuwekewa lami, suala hili la boti ambazo naamini hivi sasa hata mwekezaji hawezi kuzileta tena, kwa sababu hata kama akizileta, kuja kurejesha gharama zake sijui atafanya nauli iwe Shilingi ngapi kwa pale Bukoba Mjini.

Naomba na yenyewe Mheshimiwa Waziri aitolee majibu na mimi nazidi kuwatakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu awasaidie ndani ya Wizara hii wazidi kufanya mambo ambayo Watanzania wengi tunayategemea wayafanye na hasa kuja kutumikia Serikali ijayo ya Chama cha Upinzani ambayo itachukua Serikali na sisi naamini kwa sababu tunataka kutengeneza Serikali ya Kitaifa, hatutasita kuwatazama kwa jicho la huruma, kuangalia Mawaziri wanaofanya kazi zao vizuri kuwapa nafasi katika Serikali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kuendelea, naomba niungane na wenzangu kutoa rambirambi kwa ndugu na jamaa wa Marehemu Margareth Bwana. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kwenda katika mashindano ndani ya *Olympic* ya Chama cha Mapinduzi na kufanikiwa kupata medali ya shaba. Nina hakika katika mashindano yajayo atakuwa ameongeza kiwango cha mbio na anaweza kuambulia medali ya dhahabu. Tunamtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kuhusu mambo mawili, matatu. La kwanza, ni suala la viwanja vya ndege. Viwanja vya ndege ni muhimu sana katika uchumi wa nchi. Ili kiwanja cha ndege kitambuliwe, *ICAO* huwa wanafanya mapitio kuangalia mambo mengi sana ili kiweze kuendelea kutoa huduma. Lakini lililo kubwa huwa ni kuangalia usalama wa kiwanja chenyewe, usalama wa abiria na usalama wa ndege wakati wa kuruka.

Mara ya mwisho nakumbuka Dar es Salaam *International Airport* nadhani ilipofanyiwa *assessment* hiyo, walipata asilimia 64 kwa 100 na hii haikuwa mbaya kwa nchi inayoendelea, lakini haikuwa nzuri pia. Najua mambo mengi yamefanyika baada ya tukio la Septemba, 11 nina hakika mengi yameboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata ukiwa na *engineers* wengi na wazuri kiasi gani, hata ukiwa na wafanyakazi wa kada nyingine nzuri namna gani, kama hutakuwa na *Airport Security Officer* ambao ni wazuri wanaojituma na wamemotishika, bado hali ya *assessment* hiyo inaweza kushuka kwa sababu usalama kwa ujumla wake utakuwa haukufikia kile kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilizungumzia juu ya mishahara ya wafanyakazi wa kada ya *Airport Security Personnel* kwa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, hasa wale ambao walikuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na baada ya muda mrefu sana nadhani ni mwaka huu 2005 au mwaka jana 2004 wakawa wameingia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, wao wamebaki na mishahara ambayo kwa bahati mbaya hawakupandishwa wakati walipokuwa katika himaya ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Mamlaka imewachukua wakiwa na mishahara hiyo hiyo ambayo bado ni ya chini.

Nadhani wanapata Sh.70,000/= mpaka Sh.80,000/= kwa mwezi. Sasa hao walioajiriwa na Mamlaka wana mishahara mikubwa zaidi kuliko hao ambao ndiyo wamewafundisha kazi. Sasa si vizuri kwa kweli nadhani Wizara ingeangalia kama watawapa *accelerated promotion* au watafikisha hapo wengine walipo.

Ningeshauri wangewaangalia kabisa kwa namna ya pekee ili waweze na wao kupata kiwango kinachotakiwa, kwa sababu wakiwa wana motisha ya kutosha, ndivyo watakavyoleta ufanisi wa kiusalama katika viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanja cha ndege cha Kigoma, ni kiwanja ambacho kwa kweli kina *potential* kubwa sana, lakini kwa bahati mbaya hakijapanuliwa wala hakijatengenezwa kwa kiwango kinachotakiwa na siku hizi kinatumiwa na ndege kubwa za *monarchy,* zinakwenda kuhudumia nchi ya Kongo. Niwashukuru kwanza kwa jinsi walivyoanza kuweka uzio.

Lakini naiomba Wizara, kwa kweli iangalie uwezekano wa kupanua kiwanja hicho na kukijenga kwa *standard* ambayo inatakiwa. Kwa sababu ukijenga uwanja wa ndege wa Kigoma, kwa hakika utakuwa una-*tape* biashara ya Kongo, Rwanda na Burundi. Hutakuwa na sababu ya mtu kuzunguka na gari kuja kupita Kahama kuja Dar es Salaam kwa sababu usafiri wa ndege utakuwa unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika simu za mikononi *success history* kwa nchi nzima na ninawashukuru na kuipongeza Wizara kwa jinsi ambavyo wameweza kufikisha huduma hiyo mpaka Wilayani Kibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ningeomba kwa sababu mnara uko Wilayani, Wizara iangalie uwezekano wa kushauriana na wawekezaji kuongeza minara ili hasa Vijiji vya mpakani viweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo katika Vijiji vya mpakani, Vijiji vya Mayovu, Myama, Kitanga, Mabamba, Malenga, Muhange na Rumashi. Kunapotokea tatizo la kuvamiwa, hawana jinsi ya kufanya kwa sababu hawana mawasiliano ya aina yoyote. Inachukua siku mbili ndipo taarifa ya tukio inapofika Wilayani au Mkoani.

Kwa hiyo, ningeishauri Wizara na kuiomba kwamba wawashauri wawekezaji waangalie uwezekano wa kuongeza minara kutokea pale Kakoko kuelekea ukanda wa Nyaronga ili waweze kuhudumia Vijiji mipakani viweze kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba, Wizara hii kwa kweli ndiyo mkombozi kwa Mkoa wa Kigoma kwa sababu inahudumia Reli, inahudumia Bandari na inahudumia viwanja vya ndege. Kama tafsiri sahihi ya *Central Corridor* itakuwa imewekwa maanani na Bandari ya Kigoma ikaimarishwa na Reli ya Kati ikaimarishwa kupitia Tabora kwenda Kigoma ikaungana na miundombinu ya barabara ya kutoka Dodoma kwenda Kigoma kupitia Tabora na tukawa na uwanja wa ndege mkubwa unaokubalika pale Kigoma, kwa kweli tunaweza ku-*tape* utajiri wa biashara ulioko katika nchi za Maziwa Makuu ikiwemo Kongo. Kwa sababu hivi sasa Kongo wanataka kuchukua bidhaa kutoka Kigoma, lakini usafirishaji wake ni lazima wazunguke kupitia Kenya waende mpaka Uganda ndiyo waweze kusafirisha bidhaa hizo.

Sasa kama tutakuwa tumeimarisha reli, tukaimarisha na Bandari ya Kigoma na tukawa na uwanja wa ndege mzuri wa Kimataifa pale Kigoma, basi tunaweza kabisa ku-*tape potentiality* na biashara yote ya nchi hizi za Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Waziri hili anaweza kulifanya na tukaondokana na dhana ambayo haitufikishi mbali na kuiona kwamba Kigoma sasa badala ya Makao Makuu ya Maendeleo ya Kanda ya Kati, *Central Development Corridor* kuwa Kigali ikaletwa Kigoma ambapo ni rahisi kwa kweli kuweza kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumezuka mtindo na nilishauliza swali hapa Bungeni juu ya dhana ambayo imetokea ya kifuta machozi. Mimi naimpongeza Serikali kwamba inatoa kifuta machozi. Lakini mimi ninavyoiona, kifuta machozi inatokea tu mtu ndani ya Serikali anapofurahi kufanya hivyo. Hakuna sheria inayolenga kifuta machozi. Kwa hiyo, leo anaweza kufurahi akatoa Sh.100,000/=, kesho kwa ajali nyingine akatoa kifuta machozi Sh.200,000/=, hakuna sheria inayolenga kifuta machozi. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, unakuja kukuta kifuta machozi kinatolewa pale ambapo Serikali ina mkono au ina ubia katika hicho chombo cha usafiri. Wakati wa ajali ya treni watu walipata kifuta machozi, wakati wa ajali ya *MV Bukoba* watu walipata kifuta machozi na kwenye ajali ya daraja la Kilombero watu walipata kifuta machozi. Lakini kuna ajali ya Mwanza wakati Mheshimiwa Rais alikuwa kwenye kampeni, *bus* liliua watu 21 kwa mpigo, hakukutolewa kifuta machozi na mabasi yanapata ajali, kuna watu waliungua Mbeya kwa sababu ya mafuta hakukutolewa kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, sasa naiona dhana ya kifuta machozi hailengi katika kuleta utaratibu endelevu unaoeleweka kwa wananchi. Kama Serikali au mamlaka yoyote imeunda kuwa na chombo, ni vyema hicho kifuta machozi kikawa kinaeleweka vizuri kwa kukilazimisha hicho chombo kuwa na Bima inayotosheleza kulipa matatizo yote fidia. Kwa kweli iwe ni Bima ya kulipa fidia kwa hayo matatizo ambayo yatakuwa yanatokea na si kutegemea mtu ameamka vipi kwa siku hiyo. Kwa sababu hata hizo leso zenyewe za kuyafuta hayo machozi sijui zitakuwa kiasi gani! Kwa hiyo, ni vyema tukakubaliana kwamba kama ni meli kuwe na Bima ya kutosha kulipa fidia kwa hao ambao watakuwa wameathirika na si Serikali kwenda kutoa kifuta machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho la kuzungumzia ni suala la *TTCL*. Katika makubaliano ya awali, ilikuwa kwamba wafanyakazi hawatapunguzwa.

Lakini hivi karibuni tumeshuhudia kwenye Vyombo vya Habari, mzozo unaojitokeza kwamba hiyo Kampuni sasa inataka kupunguza wafanyakazi. Hivi hali hasa ikoje na kwa nini hivi sasa ndiyo waanze kukiuka makubaliano ya awali? Tungependa kujua msimamo wa Serikali ni nini?

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na kwamba simu za mikononi ni *success history,* tungependa wananchi wa kawaida waletewe simu ambazo ni rahisi kununua ambazo ni *simple* kwa *technology*. Hivi sasa simu za mkononi tunalipia *functions* ambazo hatuzitumii kabisa. Mwananchi wa kawaida hahitaji *calculator,* hahitaji *Internet* kwenye simu ya mkononi na hahitaji kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Wizara hii ingewasiliana na hao wanaoleta simu za mkononi kukawa na simu za watu *complicated* kama Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya na kukawa na simu za watu wa kati kama Beatus Magayane ambaye anataka tu kupiga simu na kupigiwa simu na sana sana kuandika *message* tu ili watu wengi waweze kuwa na simu za mkononi za namna hiyo. Hivi sasa tunalipia vitu ambavyo viko kwenye simu lakini wananchi wa kawaida hawavitumii kabisa nikiwemo hata mimi. *(Makofi)*

Mimi sihitaji simu kuniamsha asubuhi kwa sababu nina saa ya kawaida ukutani au pengine, sihitaji kuwa na *screen server*, lakini unavikuta vyote hivyo vimejazana kwenye simu unalipa shilingi 350,000/= na kuna kupiga picha, picha yenyewe hata ukipiga huwezi kuisafisha kirahisi.

Kwa hiyo, ningependekeza kwa kweli hao wawekezaji kwa kupitia Wizara yako, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwamba watuletee simu za mkononi ambazo ni nzuri na ngumu, lakini ambazo gharama yake iko chini kwa sababu *operations* zitakazokuwemo ziwe chache kumwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwa dhati kabisa nikitegemea kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ameyasikia hasa ya kiwanja cha ndege cha Kigoma, Bandari ya Kigoma na uwezekano wa ku-*improve* Reli ya Kati ili wananchi wa Mkoa wa Kigoma waweze kusafiri kwa urahisi na kwa wingi zaidi atakuwa ameyasikia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MCHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara kwa kuwasilisha hotuba yenye ufafanuzi na takwimu za kutosha.

Mheshimiwa Spika, bado upo utata juu a ubinafsishaji wa *ATC* pamoja na kwamba Serikali ina asilimia 51% ya hisa, lakini naishauri kuwa na mamlaka ya maamuzi. Hivyo namwomba Waziri aielezee asilimia 51% ya hisa za Serikali zina uzito gani?

Pili, Waziri ameelezea idadi kubwa ya wasafiri wanaokuja na kutoka Tanzania, ni vyema akatuelezea *ATCL* imefanikiwa kiasi gani katika kutoa huduma kabla ya ubinafsishaji na baada ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko ya kuwa uongozi wa *ATCL,* hutoa zabuni za kununua mahitaji yake kwa makampuni ya *South Africa* ambayo baadhi yake ni ya Wakurugenzi wa *ACTL,* jambo ambalo limesababisha Serikali kutumia vibaya mapato yake. Naomba maelezo juu ya tuhuma hizi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri pia atueleze ule mpango wa kusambaza simu za *land line* 300,000 zimefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ya hayo na naunga mkono hoja.

**MHE. ROBERT K. MASHALLA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa hotuba hii imezingatia sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye Wizara hii yapo mapungufu ambayo Wizara inatakiwa ifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, mfano hai wa mapungufu yaliyopo ni ukosefu wa Mawasiliano ya uhakika katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukombe, huduma za simu katika Wilaya hii ni duni sana asilimia 70% ya eneo la Wilaya ya Bukombe haina mawasiliano ya simu, maeneo muhimu ya uzalishaji yaani maduka, viwanda, sekondari na miji ya Masumbwe,

Lugunga, Gereza la Kanegere na maeneo ya Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Cargil, Mgodi wa Dhahabu wa Nyakafuru hayana huduma za simu. Aidha, huduma za simu zilizoko Bukombe zipo kwenye Mji wa Ushirombo tu ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kutoa huduma zaidi za simu kwenye maeneo tajwa hapo juu hasa katika Mji Mdogo wa Masumbwe ambao una zaidi ya wakazi 12,000 lakini hauna kabisa huduma ya simu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa vile Wizara hii imefanya kazi nzuri naitakia kila la kheri itekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii kwa mfano mzuri wa kuzisikiliza na kuzitatua shida mbalimbali katika majimbo yetu ya uchaguzi kama umeme wa jua.

Mheshimiwa Spika, wana Bukene wanamshukuru Mheshimiwa Waziri na uongozi wa Shirika la Reli kwa kukubali ombi letu la kutufungia umeme wa nguvu za jua pale pale *station* ya reli, Bukene.

Pamoja na shukrani zetu tungeomba ikiwezekana kama nguzo mbili zaidi zingesimikwa ili abiria wateremke kwenye nuru hasa wasafiri wa daraja la tatu maana kwa sasa bado wanateremkia gizani kwa sababu wote wanaotoka Mwanza na wale wanaotoka Tabora, huwasili Bukene usiku na mara nyingi huibiwa kwa hunyang'anywa mizigo yao na wanyang'anyi.

Mheshimiwa Spika, uwezekano ukiwepo ratiba ya magarimoshi ingerekebishwa ili kuwe na walau gari moja toka Tabora na moja kutoka Mwanza lipite Bukene mchana. Hii itaondoa adha waipatayo wasafiri ya kupoteza mali zao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu fika kuwa kampuni ya *Celtel* ilipeleka vifaa vya kujenga mnara pale Bukene. Kwa bahati mbaya vifaa hivyo vilihamishwa na kupelekwa Bugene. Sisi wa Bukene tumeachwa kama watoto yatima, hatujapewa matumaini ya kujengewa huo mnara maana watu wetu wengi wanazo simu za kiganja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anatuahidi nini Bukene?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mawasiliano na

Uchukuzi, kwa kazi nzuri wanayofanya, kwa hiyo, basi naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Katika ulimwengu huu wa *Information Technology,* Tanzania imepiga hatua kubwa kueneza simu za mkononi karibu nchi nzima hadi vijijini. Watu wengi wakiwemo wanawake hivi sasa wanatumia simu hizi kufanyia shughuli zao zikiwemo za kubiashara.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kulikuwa na hitilafu katika mawasiliano ya *Celtel.* Kulikuwa na usumbufu mkubwa, wateja walikuwa wanahangaika kutumia namba hizo, marekebisho yalichukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nashauri matatizo kama haya yakitokea basi wananchi waarifiwe mapema kuliko kuweka jamii inayotumia simu hizo *in surprise.*

Mheshimiwa Spika, *telecentres* ya Wizara ina mpango wa kuongeza *telecentres* hapa nchini?

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi sana, kwanza ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi nzuri sasa iliyoifanya katika eneo la Mawasiliano katika Wilaya yangu ya Kyela. Simu za mikononi za *Celtel, Vodacom* na *Mobitel* zinafanya kazi vizuri kabisa na kuifanya Wilaya ya Kyela kuwa sehemu ya ulimwengu wa kisasa.

Ombi langu ni kuikumbusha Wizara juu ya ahadi yake ya siku nyingi ya *TTCL* kupeleka simu Kasumulu na *Matema Beach. TTCL* inaonekana haina nia ya kutekeleza ahadi ya Serikali bila sababu yoyote ya maana. Matema hivi sasa ni kituo muhimu sana cha utalii. Simu za mkononi ni aghali sana kwa Watanzania walio wengi, kwa hiyo, simu za mezani ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri asisahau ni suala zima la uharibifu wa bandari ya Itungi. Bandari imejaa tope na mchanga, je, Serikali imeshindwa kabisa kuondoa tope lile? Hakuna njia yoyote ambayo Serikali inaweza kufanya kuondoa kero hii kwa wasafiri? Je, kuna mpango wowote wa kujenga gati pale *Itungi Port?*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana. Ninampongeza sana kwa kazi nzuri aliyoifanyia nchi yake. Ninawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichangie hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Aidha, naipongeza Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri inayofanyika kuboresha mawasiliano ya simu nchini. Shukrani za pekee ziende kwa Kampuni ya *TTCL, Vodacom* na *Celtel* kwa kufikisha huduma ya simu za kawaida na simu za mkononi Wilaya ya Kondoa, tunashukuru sana tunahimiza Kampuni nyingine zije Wilayani Kondoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi naomba sasa nitoe maombi yangu yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa mtandao wa simu za mkononi unapatikana Mjini Kondoa na hauwafikii wananchi wa vijijini. Kwa mfano, Tarafa za Kwamtoro, Farkwa, Goima na sehemu za Tarafa ya Mondo, naishauri Kampuni husika kujenga minara katika barabara ya Kondoa - Dodoma ili simu zipatikane njia nzima.

Aidha, minara iongezwe kati ya Kondoa na Babati, Kondoa na Kibaya na Kondoa - Kwamtoro ili kuwezesha mtandao wa simu za mkononi upatikane Wilaya nzima ya Kondoa.

Kwa kuwa simu za *TTCL* zinapatikana Mjini Kondoa peke yake hadi sasa, naomba *TTCL* wapeleke huduma hii hadi vijijini hususani katika Makao Makuu ya Tarafa zote za Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu mfupi natamka kuwa naunga mkono hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha kumshukuru Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mbunge na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa moyo wake wa upendo na mshikamano ambao aliuonyesha kwetu kwa kutembelea eneo letu la uchaguzi na kutoa mchango mkubwa katika nyanja ya mawasiliano na elimu.

Mheshimiwa Spika, kupitia *harambee* kubwa iliyoendeshwa na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, tuliweza kupata shilingi 12,800,000 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Kambarage na kwa sasa tayari imekwishasajiliwa na watoto wanasoma, tunamshukuru. Ziara hiyo aliifanya mwaka 2004 na bado tunaikumbuka hadi leo.

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, ambaye pia alitembelea Jimbo la Siha na kuweka msukumo mkubwa sana katika nyanja ya mawasiliano. Kufika kwa viongozi hawa wakuu wa Wizara kumetuwezesha Siha kuwa na huduma za *TTCL, Vodacom, Mobitel* na kiasi fulani *Celtel.* Nashukuru sana .

Hata hivyo wananchi wa Jimbo langu la Siha walimlilia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kuhusu kukosekana kwa huduma za simu za mkononi hasa katika eneo la *West Kilimanjaro* hususan maeneo ya Ngare-Nairobi, Londrosi, Lemosho, Namwai, Kambi ya Raha, Suzana, Bagamoyo, Engushai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ni maeneo muhimu sana kwa uchumi kwani ndipo yalipo katika mashamba makubwa ya *NAFCO, TBL, NARCO* na kadhalika.

Aidha, maeneo haya ni muhimu sana katika kilimo cha Shayiri, Ngano, Njegere, Mboga za Majani, Viazi, Mbao na bila kusahau eneo muhimu la Maliasili na Utalii. Maeneo haya yapo chini ya Mlima Kilimanjaro ambapo ndipo *Londrosi Gate* iendayo Mlima Kilimanjaro ilipo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya sababu za kiuchumi tumezungukwa na wenzetu wa Jimbo la Longido - Monduli, Rombo, Himo, Kenya na kadhalika ambapo pia watanufaika.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kuna *potential* kubwa kama makampuni ya simu za mikonomi yataamua kuwekeza katika maeneo haya kwani hata uwezo wa wananchi kifedha ni wa kuridhisha.

Katika kufuatilia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, tuliwasiliana na Kampuni ya *Celtel,* Dar es Salaam ambayo ilionyesha *interest* ya kuwekeza katika eneo hili mimi na Diwani wangu Mheshimiwa Daniel Sandewa, tulifuatilia suala hili Makao Makuu ya *Celtel* na wakakubaliana nasi na kweli wakatuma wawakilishi wao wakaja Siha, *West Kilimanjaro.* Waliahidi kulifanyia kazi ombi letu kazi, mpaka sasa hakuna lolote linaloendelea kwa maana ya utekelezaji wa ombi letu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa kuhudhurisha tena upya, ombi letu kwa *Celtel* ili watuwekee mtambo wa kunasa mawasiliano na wananchi waweze kunufaika na huduma muhimu ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine narudia kuishukuru Wizara kwa moyo wake wa upendo na ushirikiano kwetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kushukuru kwa kupata nafasi hii adimu. Nami kama wenzangu naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na mwakilishi wao Marehemu Abu Kiwanga.

Aidha, niwape pole kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sikonge wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa msiba walioupata kwa kufiwa Marehemu Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Rukwa, Mungu aziweke mahali pema peponi roho za Marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nianze kuishukuru Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi nzuri iliyoifanya, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wote wa ufuatiliaji wa kero za Jimbo langu, naomba sasa nichukue fursa hii kuendelea kuiomba Wizara iangalie kimsingi kero hizi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa simu za mkononi, pamoja na kuwepo matumaini ya Kampuni ya *Celtel* kuweka mitambo yake Sikonge hivi karibuni na kwa kuwa wananchi wamepata ahadi hii kwa muda mrefu naiomba Serikali itoe tamko kwa wananchi wa Sikonge ni lini kazi hii itaanza na wananchi wataanza kutumia huduma hii lini?

Pili kutokuwepo kwa Kituo cha Posta cha kisasa, Wilaya ya Sikonge inatumia kituo kidogo cha posta, kituo ambacho hakina hadhi ya Kiwilaya na zana zake ni za kizamani. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha imejenga kituo kikubwa cha kisasa kinachokwenda sambamba na hadhi ya Wilaya, posta walishapewa walichoomba.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na simu za *TTCL* za kisasa. Wilaya ya Sikonge ndio pekee inayotumia mtambo wa zamani wa kukoroga ukilinganisha na Wilaya zote za Mkoa wa Tabora ambazo zote zina mitambo ya kisasa. Naomba Wizara iangalie adha tunayoipata sisi wananchi wa Sikonge kwa kukosa mitambo ya kisasa za simu za *TTCL.* Baada ya maelezo haya nachukua nafasi hii kuishukuru tena Wizara na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuingia hadi hatua ya mwisho katika kinyang'anyiro cha Urais kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninazo hoja nne ambazo naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Bunge la mwezi Februari, 2005, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu simu za mikononi kusambazwa na kufikisha mawasiliano ya simu za mikononi hadi katika Jimbo la Kyerwa na yeye aliahidi kuwa Kampuni ya *Mobitel* ilikuwa tayari kuweka minara katika Jimbo la Kyerwa hata hivyo bado mpaka sasa hawajafanya hivyo, je, ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa za vyombo vya habari inasemekana kuwa *Celtel* ambayo ni Kampuni Tanzu ya *TTCL* ina mambo mawili yanayoisibu:-

Kwanza, kwamba *Celtel* imeuzwa kwa mwekezaji wa huko Kuwait.

Pili, kwamba *Celtel* inataka kujitenga na *TTCL* na kwamba inataka Serikali ya Tanzania iwe na hisa 30% na mwekezaji *MSI* awe na hisa 70%, je, madai haya yana ukweli wowote?

Je, mgawanyo wa hisa katika Kampuni ya *Celtel* ukoje kati ya Serikali na mwekezaji.

Tatu, napenda pia kujua mipango ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika kupanua njia ya reli ya kati toka Isaka hadi Murongo Wilayani Karagwe mpakani mwa

Uganda na Rwanda ili kuhudumia maeneo hayo ya Kusini mwa Uganda na Kaskazini mwa Rwanda.

Mheshimiwa Spika, nne katika hali isiyo ya kawaida, majengo yote ya shirika la Reli Tanzania yote ni machafu hayapakwi rangi, hayakarabatiwi, mfano *Dodoma Railway Station,* majengo ya Bandari ya Mwanza yote yana rangi iliyopakwa na mkoloni. Lakini kuna watalii na wageni kutoka nchi ya nje, je, ni picha gani wanayoipata kutokana na majengo hayo kuwa machafu?

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kujua kwa nini Makampuni kama *ATCL* yametoa picha halisi ya mapato yao, hasara au faida lakini Kampuni ya *Celtel* na *TTCL* hayakuonyesha picha halisi ya mapato yake.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu yaani hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kwanza huduma ya oosta, ni jambo la kujivunia kuona huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika hili zinaongezeka. Kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 4. Ni kweli kimtandao huduma zinaenea karibu maeneo yote ya nchi. Huduma kuenea ni jambo jema. Lakini wanaotoa huduma nao lazima waonekane kuipenda kazi hiyo kwa kuundiwa mazingira mema ya kutoa huduma. Maeneo yanayotoa huduma hizo mengi ni mabovu na hasa katika Wilaya ambazo zimeanzishwa baada ya 1975 hadi leo, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Spika, posta ya Bariadi pamoja na kuwa ni posta kamili, inatoa huduma katika jengo la kupanga, chumba kidogo ambapo wateja wanabanana na wakati mwingine hata vifurushi kutopata mahali pa usalama kuwekwa. Wafanyakazi na hasa *postmaster* na msaidizi wake nao wanaishi kwenye nyumba duni. Naelewa mtazamo wa sasa ni kutojenga nyumba za watumishi, lakini ni jambo jema mtumishi kuishi katika nyumba iliyo bora na salama kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningeomba watumishi hao waongezewe posho ya makazi ili wapange au kujenga nyumba zao zitakazowapa usalama wa kuishi, majengo ya posta kama Ofisi yajengwe, yafanane na huduma zenyewe na usalama wa fedha na mali nyingine zinazotunzwa na posta hizo. Ikumbukwe hadi leo hii hakuna huduma inayoaminika huko vijijini zaidi ya posta. Hivyo ni vyema jengo la posta likajengwa ili wanaopokea huduma wawe na imani kuwa mali zao nazo ziko salama.

Mheshimiwa Spika, *operation cost,* katika jedwali namba 3 shirika la posta linaonekana kuelekea kwenye kifo. Mapato ya shirika ukilinganisha na matumizi inaonekana kuwa sawa. Hivyo ikitokea dhahama ndogo tu shirika linapata hasara na si ajabu likashindwa kutoa huduma kabisa. Ni jambo la busara Serikali ilichunguze Shirika hili kuangalia namna gani linaweza kupunguza *operational cost* zake kwa lengo la kupunguza gharama za kuliendesha na hivyo liweza kupata faida na kuwekeza kwa maendeleo ya shirika.

Mheshimiwa Spika, leo kuna mabadiliko makubwa katika nyanja za mawasiliano na hata katika taratibu za kusafirisha vifurushi. Hivyo basi shirika ni lazima lijipange kulingana na mabadiliko hayo. Shirika kuanzisha *fleet* ya magani ya kusafirisha vifurushi na barua sidhani limesaidia kupunguza gharama za usafirishaji vifurushi hivyo. *Motor vehicle maintenance* yaweza kuwa ni ghali zaidi kuliko kusafirisha kwa kupitia reli, meli, mabasi *as surface mails.*

Mheshimiwa Spika, shirika hili tulitegemea kwa kuuzwa kwa *South Africa* lingeweza kutoa huduma bora zaidi na kupata faida kinyume chake Shirika la Ndege liko kwenye mwelekeo mbaya saa yoyote linaweza kufa. Kuna gharama kubwa sana na za hila kwa wanaoliendesha. Wakurugenzi wa *ATCL* wanajiri na masurufu makubwa kusababisha wafanyakazi kuona wanahujumiwa na wao wanaona siyo vibaya nao kushiriki kuhujumu. Hivi sasa shirika linaelekea kufa. Viongozi wake wanajikopesha ovyo tu. Mifano ipo na hai. Tungeomba Serikali ikae macho kuona kwamba *ATCL* haifi bali inabaki kama *Flag Carrier* ya nchi yetu. Hira za kuua *ATCL* zifanywe mapema kabla hatujalizika shirika letu. Ni afadhali tuwape wazawa kuliko kuwapa wageni ambao hawana uchungu na shirika hili pamoja na Wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, *speed boats.* Ni jambo la aibu kwamba wawekezaji wa nchi hizo za kwenda Mwanza *Lake Victoria,* walipitia njia zote, kabla ya kuzileta hapa kama wawekezaji walipitia *TIC* pia walizingatia sheria zilizopo zinazohusu usafirishaji na njia zilizopo za kuzifikisha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, leo inakuwaje linakuwa ni suala la malumbano. Natumaini kuonyesha ukomavu wa kuendesha mambo Kiserikali na kwa kufuata sheria, Baraza la Mawaziri wawe wanatoa msimamo wa pamoja na kutoa maamuzi yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, imekua ni aibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi anatoa kibali, meli hizo zipelekwe Mwanza. Wakaguzi wa meli wamepitisha zinafaa. Waziri wa Ujenzi anasema haliwezekani kupitisha meli hizo kwa barabara au reli. Jambo hili Mawaziri wangekaa na kutoa uamuzi unaofanana, kuliko sasa ambapo wanafanya kuwa malumbano ya kuonyeshana ubabe na kufanya umma uamini kuwa tunaumia kwa sababu Mawaziri hawakubaliani kila mmoja ajiona yuko zaidi ya mwenzake.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe neno la mwisho ni lini *speed boats* hizo zitafika Mwanza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara na watumishi wote kwa kazi nzuri zilizofanywa katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie maeneo mawili. Kwanza ni kuhusu Bandari ya Lindi. Wakati akijibu swali langu katika Mkutano wa Kumi na Nane wa

Bunge hili, Serikali iliahidi kufanya utafiti kujua sababu za kujaa kwa mchanga katika Bandari ya Lindi.

Napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuondoa mchanga katika Bandari ya Lindi kwa sababu hakuna mpango wowote unaoonekana katika hotuba ya Waziri. Napenda kujua tatizo ni nini au Serikali ndio imeshaamua kuiua Bandari ya Lindi? Kama sio kwa nini hakuna fedha zilizopangwa kwa ajili ya kuhudumia Bandari ya Lindi? Mamlaka ya Bandari imelipa fidia kubwa eneo kubwa katika Mji wa Lindi kwa matumizi ya Bandari. Lengo au mpango ya *THA* kwa eneo walilolipa fidia ni nini na utafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uwanja wa ndege Lindi. Lipo tatizo la ubora wa barabara za kurukia ndege kiasi cha kufanya mashirika ya ndege kushindwa kuleta ndege na kuwasababishia abiria wa Lindi kulazimika kupanda na kushuka *Mtwara Airport* hivyo kusababisha usumbufu mkubwa. Naomba kujua mpango wa Wizara wa kuboresha hali ya uwanja wa ndege wa Lindi. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri waliyotekeleza kwa kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, ingawa tumeletewa simu ya *TTCL* lakini inaendeshwa kwa mtambo mchakavu sana. Hivyo zipo *breakdowns* kila siku hasa kwa namba 025-2600959, 025-2600137, 025-2600312, 025-2600204, 025-2600038 na 025-2602556. Tuwekewe mtambo mpya. *DED* anahitaji *lines* mbili zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, tunahitaji simu katika kijiji cha Mkongo, Nakawale ili ihudumie wakazi wa Nakawale, Mkongo, Gulioni, Njalamatata na Mwangaza. Hapa ni rahisi kuweka *line* moja ya biashara ya kulipia kwa vile tayari ipo *special line* hapo jirani na Nakawale katika *seminary* ya Lighano namba 2602543 jirani tu. Naamini kutoka Lighano ni rahisi kuvuta simu hadi Nakawale.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunahitaji sana jengo la Posta mpya karibu na Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Namtumbo nje kidogo ya kijiji cha sasa cha Namtumbo. Kwa sasa jengo la posta ni la kukodisha ambapo lipo mbali sana Boma Mpya, Halmashauri na Ofisi mpya ya CCM Wilayani.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti nzuri hapa Bungeni leo hii tarehe 29 Juni, 2005. Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inathibitisha ufanisi wa hali ya juu uliofikiwa na Wizara hii katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeleta maendeleo makubwa katika sekta zote zinazosimamiwa na Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi. Hali nzuri ya mawasiliano

ya simu, usafiri wa anga, majini, reli na kadhalika inathibitisha kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimepiga hatua duniani katika masuala ya mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, mimi katika mchango wangu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, naiomba Wizara hii pamoja na Serikali yetu ya Muungano wa Tanzania kukiimarisha kiwanja cha ndege cha Pemba. Pia naomba gati yetu ya Mkoani Pemba ifanyiwe matengenezo kutokana na kuwa inaonyesha kuharibika sana kwani kuna sehemu inaonyesha kudidimia au ikiwezekana ni vizuri zaidi kama gati hii itajengwa kwa kiwango kilicho bora zaidi ya ilivyojengwa hivi sasa. Vile vile gati yetu ya Wesha Chake Chake, tunaomba ijengwe ili kuleta maendeleo makubwa katika kisiwa chetu cha Pemba na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naleta maombi haya kwa kuona kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna hata moja ambalo limeelezwa kuwa linaweza kuendelezwa katika bajeti hii hasa kwa maeneo haya ya uwanja wetu wa ndege wa Pemba na gati zetu hizi mbili ambazo Mheshimiwa Waziri alishawahi kuzitembelea pamoja na viongozi wengine mbalimbali wa Serikali ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kamati ya Miundombinu ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ilifanya ziara yao Pemba tarehe 3 Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kutoa ombi langu hili ni kutokana na kuwa dunia ya leo ili nchi au eneo lolote lile lionekane limeendelea ni kuwa na miundombinu iliyo mizuri, uhakika na ya kisasa. Kati ya miundombinu hiyo yenye kuleta maendeleo ni pamoja na mawasiliano ya simu, barabara, uwanja wa ndege, bandari, umeme wa uhakika na kuwepo kwa viwanda. Nayaomba haya ili kisiwa chetu cha Pemba kiweza kuwa katika ramani nzuri katika dunia ya leo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu hili linakwenda sambamba na taarifa ambayo nimeinukuu kutoka *Radio Tanzania,* kupitia taarifa ya habari ya tarehe 24 Juni, 2005 ya saa 7.00 mchana na saa 10.00 jioni. Taarifa hiyo ya habari ilisema kuwa Kamati Maalum iliyoundwa kushughulikia kero za Muungano imewasilisha ripoti yake. Miongoni mwa kero hizo ni suala la uchimbaji wa mafuta huko Pemba na uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, kama suala hili lipo kweli na kwa kuwa maeneo ambayo yanaweza kuhusika ni sehemu ya maji ya bahari ni vizuri tukaanza kujenga misingi mizuri ya maendeleo katika kisiwa hiki cha Pemba kwa faida na maendeleo ya Kisiwa hiki na wananchi wanaoishi Pemba na hatimaye kwa faida ya nchi yetu ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa umefika wakati muafaka kujenga misingi mikubwa ya maendeleo katika kisiwa hiki cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa katika hotuba yake ya kuadhimisha miaka 40 ya Muungano wetu wa Tanzania zilizofanyika uwanja wa Amani Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2005 alisema kuwa: "Mimi ni Rais atekelezaye sera ya Chama changu, sera ya Muungano wenye Serikali mbili. Niliapa kuilinda Katiba ya nchi, Katiba isemayo wazi kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Taifa moja huru lenye muundo wa Serikali mbili. Ninawajibika kwa dhati kuutetea na

kuulinda Muungano huo na zaidi ya yote, mimi mwenyewe ninaamini kwa dhati kuwa Muungano wetu na mfumo wake ndio sahihi.”

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama utanukuu vizuri maelezo haya ya Mheshimiwa Rais huwezi ukapinga kuwa Pemba sio sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati kwa Serikali zetu zote mbili kukaa kuamua kuondoa tofauti zetu zote kama zipo zimejitokeza ili kujenga na kuimarisha umoja na undugu wa Taifa letu na wananchi wake wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali zetu ziamue haraka masuala yanayohusu maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania kwa maslahi ya Tanzania na kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza Wizara hii kwa kutoa kibali kwa Kampuni ya *ZANTEL* kufanya shughuli zake Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia, ahsante.

**MHE. MIZENGO K.P. PINDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niliwasilisha maombi ya wananchi wa Tarafa za Inyonga na Mpimbwe ya kutaka wapatiwe mawasilliano ya simu za mkononi. Tarafa ya Mpimbwe ina wakazi zaidi ya 75,000 ambao ni wakulima wakubwa wa zao la mpunga, mahindi, alizeti na kadhalika. Aidha, ni wafugaji wakubwa wa ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika. Sehemu kubwa ya wakazi hawa ni Wasukuma wenye ari kubwa za ushindani. Maeneo yenye *potential* kubwa ni Kata za Mamba, Mbede, Usevya na Kibaoni. Kutokana na hali nzuri kiuchumi, Tarafa hii ina minada mingi na barabara zake zinazounganisha Mpanda na Sumbawanga zinapitika muda wote.

Mheshimiwa Spika, pili, Tarafa nyingine ni Inyonga. Tarafa hii iko katikati ya Mji wa Mpanda na Sikonge na ina idadi ya wakazi 20,000. Eneo hili linashughuli za kiuchumi kama vile tumbaku, asali, nta na mazao yatokanayo na misitu hususani mbao, karanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatu, tarafa zote mbili zinapakana na mbuga maarufu ya wanyama ya Katavi. Mbuga hii inavyo vituo vya utalii na viwanja vya ndege. Aidha, yapo maeneo katika misitu iliyohifadhiwa kama vile Ruhisa - Luhisati ambayo ina watalii wawindaji.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alinitumia nakala za barua alizoziandikia Makampuni ya Simu ya *Vodacom, Celtel* na *Mobitel* kuhusu maombi haya. Naomba kujua makampuni haya yanasema nini na lini tutarajie uchunguzi utafanyika na huduma hiyo kuanza kutolewa?

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na

watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri iliyofanywa kwa kipindi kilichopita 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba ya Waziri kwa mwaka huu, naomba kujielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, huduma ya simu. Katika Jimbo langu la Solwa huduma za simu za mkononi na za kawaida ni tatizo kubwa hasa katika maeneo ya miji midogo ya Iselamagazi, Solwa, Lyabukande na Salawe. Kupitia Wizara hii, naomba Kampuni ya *Vodacom, Celtel* na *Mobitel* kupeleka huduma hii katika maeneo haya. Aidha, *TTCL* waone uwezekano wa kupeleka huduma ya simu za *call box* katika *centre* hizi.

Pili ni kuhusu vivuko vya reli. Naomba Wizara kuweka vivuko vya reli katika maeneo ya Chembelo na Mascat vilivyoko katika Kata za Didia na Imesela kwenye Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, natumia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Wizara kupitia *TRC* kwa kuweka taa katika stesheni ya Didia - Luhumbo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya Posta, naomba Wizara kupitia Shirika lake la Posta kupeleka huduma ya posta katika Miji Midogo ya Lyabukande, Solwa na Salawe ili wananchi wa maeneo haya waweze kuwasiliana na wananchi wengine nchini ili kuchochea uchumi na ufanisi wa kijamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia tena kupongeza juhudi kubwa zenye ufanisi zilizofanywa na Wizara kupitia taasisi na mashirika yake anuwai.

Mheshimiwa Spika, nawatakia tena ufanisi kwa mwaka huu wa fedha 2005/2006 na kila la kheri kwa Mawaziri wachaguliwa wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosya, pamoja na Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Wziri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa shukrani nyingi kwa kuwezesha Mji Mdogo wa Ilula uliopo katika Wilaya ya Kilolo kupata huduma ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara hii iangalie uwezekano wa kutusaidia tena simu pale Makao Makuu ya Wilaya yaani Kilolo. Mheshimiwa Waziri kwa kweli Wizara hii imekuwa akitoa ahadi za kweli ningeomba sana hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa kuwa Wizara hii iliwahi kujenga majengo pale Ilula kwa ajili ya kufunga mtambo wa simu za kawaida na kwa kuwa majengo yale yamekaa bila kutumika kwa muda mrefu, naomba yale majengo nikodishwe mimi kama Mbunge kwa ajili ya kutoa huduma za simu/internet. Naomba sana nipewe jengo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri. Ajali nyingi zinazosababishwa na mabasi ya abiria, wananchi wengi wanajeruhiwa ama kupoteza maisha yao kwa sababu ya kukanyagana kwa kukosa sehemu ya kutokea na hii inasababishwa na mabasi kutokuwa na mlango wa dharura kwa ajili ya kutokea hivyo tafadhali sana liangalieni hili mkishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaomba wapiga kura wa Rungwe na Pemba wawarudishe Waheshimiwa hawa ili waendelee kukamilisha Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi 2005/2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika ili kuboresha mawasiliano na uchukuzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hatua zichukuliwe ili kuboresha mawasiliano ya *Radio Call* katika bandari za Manda, Liuli, *Mbambabay.* Aidha, Bandari ya Manda irudishiwe *generator* iliyoondolewa au mipango ifanyike kupata nishati ya *solar* kwa ajili ya bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza na kufufua biashara ya nchi jirani za Malawi na Tanzania kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, nashauri Serikali kukubaliana na Serikali ya Malawi kuweka huduma za meli kati ya bandari ya Manda na *Deep Bay* (Kilumba) au Kalonga Malawi kama ilivyokuwa zama hizo.

Mheshimiwa Spika, bado kuna hoja ya kushauri Kampuni za simu ya mkononi za *Celtel, Vodacom* na kadhalika kuwekeza katika Wilaya ya Ludewa hasa baada ya kamupuni za kuwekeza katika miradi ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma kufikia hatua nzuri.

Mwisho, naipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kuanza kuendeleza kwa kujenga gati la bandari ya Manda ambayo kwa sasa hali yake ilikuwa inatisha mno na kutishia usalama wa abiria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. KILONSTI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Nampongeza pia Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Nawapongeza sana na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kasulu Magharibi kuna mtandao mmoja tu, *Vodacom* ambao kwa bahati mbaya sana umewekwa kilometa tano toka Kasulu Mjini. Wananchi wengi wa Jimbo hilo walioko zaidi ya kilometa 20-25 au zaidi hawapati mawasiliano na wanayo hamu na shauku kubwa kupata mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba mtambo mwingine ufungwe Muharulo, mlima Uhiko katika Tarafa ya Manyovu karibu kilometa 30 toka Heru Juu. Ikiwezekana mitandao mingine kama *Celtel* na *Mobitel* nao ipeleke huduma zao Kasulu Magharibi wasiishie Kasulu Mjini tu.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini *rehabilitation* ya *Kigoma Port* itafanyika ili iweze ku-*handle more cargo and more people traveling to DRC*/Burundi/Rwanda na Zambia kwenda bandari ya Mpuhungu?

Mheshimiwa Spika, kiwanja che ndege cha Kigoma kikipanuliwa kitaweza kufanya biashara kubwa sana na nchi jirani. Ni lini kazi hii itafanyika maana kupanuliwa kwa kiwanja hiki kutasaidia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa kazi nzuri waliyofanya katika kubadilisha kabisa hali ya mawasiliano hasa ya simu nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, naomba niwakumbushe juu ya changamoto lukuki ambazo bado zinahitaji juhudi zao kwa upande wa sekta ya uchukuzi ambayo kwa wastani haijawa na mafanikio ya kuridhisha. Ni matarajio yangu kuwa bajeti hii itawasaidia katika malengo yao ya kuboresha mawasiliano na uchukuzi nchini. Ndiyo maana napenda kuinga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, wakati napongeza mafanikio katika sekta ya mawasiliano ambapo sasa kuna wateja wenye simu zaidi ya milioni mbili, likiwa ni ongezeko la zaidi ya mara kumi ndani ya kipindi kisichozidi mara kumi, napenda nihoji kutokushuka kwa ankara/gharama za kupiga simu.

Mheshimiwa Spika, mantiki ingekuwa ni kwamba bei/gharama zipungue wakati idadi ya wateja inapoongezeka. Hivi kwani *structure* ya bei hizo ikoje? Kwa ajili ya kujenga imani baina ya wateja na makampuni ya simu, ingekuwa vyema Mheshimiwa kama Waziri angetoa hizo *cost structures* za makampuni ya simu.

Mheshimiwa Spika, napenda nisisitize haja ya kuwa waangalifu zaidi katika hatua ya ubinafsishaji wa miundombinu ya reli. Niliwahi kulizungumzia suala hili katika vikao vya Kamati ya Miundombinu na Wizara hii, wakati wa kujadili bajeti yao. Sasa nasikia kulikuwa na waombaji wawili wa kutaka kukodisha hii reli na kubakia mmoja kutoka India.

Mheshimiwa Spika, wakati nikitatanishwa na utaratibu mzima wa kuwachuja hawa waombaji wa kukodisha reli, naomba Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo ya kutosha suala hili na mchakato mzima tangu ile duru ya kwanza ambapo mmoja wa hawa wakodishaji wawili aliondolewa kwa kutokuwa na sifa hadi hii duru ya pili ambapo sasa imekuwa ni zamu ya mkodishaji mwombaji yule mwingine sasa kaonekana kuwa na sifa.

Mheshimiwa Spika, suala hili linasababisha wasiwasi juu ya mchakato huu unavyoendeshwa na hivyo kuonekana kama kwamba litaliingiza Taifa hili katika gharama kubwa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, hapa kwa kweli naomba maelezo ya kina, kiasi cha kuthibitisha kuwa kwanza, mkodishaji atakuwa na uwezo, pili, huduma za reli hazitamalizwa kabisa na kuiondolea nchi yetu uwezo wake wa reli kama njia muhimu sana ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupewa maelezo fasaha kuhusu tabia ya Wizara kuchukua rasilimali zilizo chini ya *ATHCO* na kuzigawa kwa *ATCL* bure wakati *ATCL* ni Kampuni ya biashara na Serikali ina hisa zake. Kwa nini basi rasilimali hizo zisithaminishwe na kuongezwa katika hisa za Serikali ndani ya *ATCL?*

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imechukuwa nyumba za *ATHCO* bila kufuata utaratibu, bila uwazi wa kutosha. Ili kuondoa kiwingu hiki cha kuifilisi *ATHCO* kwa makusudi, ingekuwa ni vema kama zingetamkwa nyumba zilizotwaliwa na Serikali na zile zilizouzwa na wanunuzi wake najua tufahamu nyumba ambazo bado ama zina mgogoro wa kisheria Mahakamani, ama hatima yake imegubikwa na utata bado.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kutamka tena kuwa naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Je, ni lini gharama za simu za mkononi zitapunguzwa ili kupata wateja wengi?

Je, mpango wa kuwafikishia wananchi huduma za simu vijijini *TTCL,* simu za mkononi umefikia wapi?

Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha ajali za treni na hasa treni za mizigo reli ya kati? Je, ajali ngapi na hasara kiasi gani zimetokea 2004/2005? Je, reli ya kati itafanyiwa lini ukarabati mkubwa ili kupunguza ajali kwa kuwa mataruma mengi ni ya zamani?

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali, *Gulwe Railway Station* sasa ina huduma ya umeme, usalama na ulinzi mzuri.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya pamoja na wafanyakazi wote. Pia nampongeza Waziri kwa kufikia hatua ya mwisho ya kuchaguliwa kwenye kinyang'anyiro cha Urais. Lile sio suala dogo kufikia awamu ya mwisho yeye na Dr. Salim Ahmed Salim. Nawapongeza sana na wote waliogombea.

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru Wizara kwa kuhamasisha kampuni za simu hasa ile ya *Celtel* kwa kujenga minara pale Mkwajuni sasa angalau, simu za *Celtel* zinapatikana. Pamoja na hayo bado *Celtel* haisikiki sehemu nyingine za Jimbo.

Naomba Kampuni ya *Celtel* kwenda kufunga mnara ule, napenda huduma za *Celtel* ziimarishwe Songwe/Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulisema sana mimi na mwenzangu wa Jimbo la Lupa Juu ya ukosefu wa makampuni haya. Sasa hivi tunazo aina mbalimbali za simu pale Wilaya Chunya kama vile *Vodacom, Mobitel, Zantel* nao wanasema wanakuja pale Makao Makuu ya Wilaya. Tatizo ni kwamba pamoja na minara kuwepo Chunya bado simu hizi hazifiki Jimboni kwangu Songwe kabisa kama vile Mkwajuni/Kanga/Gahuka/Namkukwe. *Celtel* imejenga mnara haisikiki sehemu zote. Kwa kuwa upo mpango wa kupata umeme naomba minara iongezwe kwani ndiyo pekee inayotusaidia kimsingi. Wizara pia iwahamasishe viongozi wa makampuni ya *Mobitel* na *Vodacom* kwa kuwa wamefika Wilayani basi nao wafike Mkwajuni/Kanga/Namkukwe/Ngwara na kwinginepo Jimboni Songwe.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Wizara yake kuhusu kuendelea kujenga uwanja wa Songwe. Ombi liwe kumaliza haraka ujenzi wa kiwanja hiki ili kitoe huduma za Kimataifa kama kilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie uwezekano wa kuimarisha reli ya kati kwa kutoiuza ila kuikodisha na sasa mipango iwe kuanzisha huduma ya reli ya kasi kwenda Kigoma/Mwanza na huduma zilizopo ziboreshwe maradufu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ianzishe pia huduma ya usafiri wa treni pale Dar es Salaam baada ya kuona uwezekano wa kutoa huduma hiyo kimsingi huduma hii kwa sasa ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono. Naomba kabla ya Bunge kufungwa Waziri akafungue mnara pale Mkwajuni, Jimboni Songwe.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa utendaji kazi wake makini kwa kuiwezesha Tanzania kuwa na mfumo wa mawasiliano unaokua kwa haraka sana. Pia nampongeza kwa kupata medali ya shaba pale Chimwaga. Ni mafanikio makubwa na tunakuombea Mwenyezi Mungu akuzidishie siku zijazo ututumikie Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kupata nafasi ya kututembelea Kongwa na kwa misaada ya maendeleo aliyoitoa kwa sekondari ya Hogoro na shule ya msingi ya Songambele. Tunakushuru sana.

Maombi ya wana Kongwa ni mawili tu tena madogo, moja, hospitali ya Wilaya ya Kongwa, kwa muda mrefu sasa haina mawasiliano ya *TTCL,* huduma ya simu hakuna ila wanapelekewa bili tu kila mwezi. Hospitali hii ndiyo pekee ya rufaa Wiayani na iko Kongwa Mjini, kwa nini inashindikana kuweka simu?

Pili, tunaomba mnara mmoja tu *(Celtel/Vodacom)* kwenye kilima cha Hogoro/Songambele. Mnara huo utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Tarafa ya Zoissa. Naomba kilio hiki kisikilizwe na najua Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia jambo hili ni mchapakazi. Natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, kwa msiba wa ghafla uliowapata.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, naelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo, moja, mfumo wa kutuma fedha kwa njia ya posta. Hivi sasa mfumo huu umekuwa kero kubwa hasa katika maeneo ya Miji midogo yenye Ofisi za Posta. Wateja wanaotumiwa fedha wakipewa taarifa za kuwasili kwa fedha zao wanapofika Posta wanaambiwa Posta haina fedha za kuwalipa. Mara kadhaa Posta ya Muheza imekuwa inakabiliwa na matatizo hayo na wateja wengi kusubiri muda mrefu zaidi ya mwezi mmoja kusubiri makusanyo ya fedha shilingi 100,000/= ili mteja alipwe.

Wakati mwingine wateja wanalazimika kwenda Posta ya Tanga kwa gharama zao kuchukua fedha. Ni aibu kwa Shirika la Posta kufikia hatua hiyo na kushindwa na makamapuni ya usafirishaji kama Scandinavia na *Raha Leo Bus* la Tanga wanaosaidia wananchi huduma hii kwa haraka, ufasaha na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara inawaeleza nini wananchi juu ya kero hii?

Mheshimiwa Spika, mfumo wa simu za mkononi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunapongeza kampuni zote za simu za mkononi *Celtel, Mobitel, Vodacom, Zantel* na pia *TTCL* kwa huduma nzuri hadi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pongezi za ziada kwa kuwa sekta hii imeajiri Watanzania wengi ofisini, lakini pia nje ya ofisi zao katika sekta binafsi wananchi wengi hasa vijana wanatoa huduma za simu na kujipatia riziki.

Mheshimiwa Spika, simu zinasikika vizuri katika Vijiji vingi, lakini gharama zake bado ni kubwa na wananchi wanashindwa kuzimudu. Ili kuongeza mtandao na kuwezesha bei za simu kushuka ni vema mtandao wa simu za mkononi sasa uwe wazi kwa mawasiliano ya moja kwa moja ya Jumuiya yote ya Afrika Mashariki badala ya mfumo wa kupitia mkondo wa Kimataifa *(International Line)* au kulazimika kununua *line* mpya unapokuwa nje ya nchi moja ya Afrika Mashariki. Ni vyema sasa Bodi ya Mawasiliano ikapokea mapendekezo haya kama hoja muhimu na kuzitaka kampuni za simu za mkononi kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuboresha mawasiliano Wilaya ya Muheza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kufuatilia maombi niliyotoa kuhusu kuboresha mawasiliano ya simu za mkononi katika Mlima wa Amani ambapo kuna mashamba makubwa ya chai, Kituo cha Utafiti wa Malaria, Ofisi za Hifadhi ya Misitu, eneo kubwa la utalii, uvumbuzi wa dhahabu na kwamba Amani ni Tarafa yenye Kata tatu. Pamoja na mnara mpya kuanza kujengwa eneo la Kijiji cha Shebomeza, Amani bado ipo haja kuongeza uwezo ili eneo kubwa zaidi liweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na eneo la Amani pia niliomba eneo la Kata ya Misozwe liangaliwe upya hasa pendekezo nililotoa la kuweka mnara katika Mlima uliopo Misozwe mahali lilipojengwa Kanisa la Anglikana. Eneo hilo litaweza kuboresha mawasiliano eneo la Misozwe, Kwatango, Magula, Kicheba, Mashamba ya Mkonge ya Kibaranga na Mjesani, Mashamba ya Matunda, Mkwajuni na Segoma.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri muendelee kulitazama eneo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Wizara ifanye hima kuboresha njia ya reli ya kati na hasa kusogeza huduma hiyo karibu na nchi za Rwanda na Burundi hasa tukikumbuka kwamba sasa nchi jirani za Kenya na Uganda zinaelekeza kufungua mawasiliano ya reli na barabara na nchi za Sudan, Ethiopia na Somalia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa uongozi wake mzuri wa Wizara hii. Pia natoa pongezi kwa bajeti hii ambayo ni nzuri na imejitosheleza.

Mheshmniwa Spika, naunga mkono bajeti hii na napenda kuchangia haya yafuatayo:-

Moja, siku za karibuni hadi sasa, watumiaji wa simu za mkononi za aina ya *Celtel* wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa kuhusu matumizi ya simu hizo kwani hazipatikani kwa urahisi. Namba yoyote ukipiga majibu yamekuwa yakisema kuwa namba hiyo haipatikani au wakati mwingine inajibu huruhusiwi kupiga namba hiyo au angalia vizuri piga tena.

Pia kumekuwa na usumbufu wa kushindwa kuweka *voucher* kwenye simu ambapo watu wamekuwa wakipata hasara za kununua *voucher* na ambapo zinakataa kuingiza *units* kila ukiingiza *units* majibu yanakuwa, *voucher* hiyo haipo na ukizidi kurudia inajibu huduma imesitishwa kwa muda. Je, tatizo hili limetokana na nini na kwa nini wananchi hawakupewa maelezo na pia tatizo hili litakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, pili, uwanja wa ndege wa Bukoba ni mdogo sana na pia ni wa udongo siyo wa lami. Abiria wa Bukoba ni wengi, kuna msongamano mkubwa wa abiria na hii inasababisha rushwa na upendeleo wa nani aende.

Mheshimiwa Spika, pia majira ya mvua uwanja huu unakuwa tepetepe kiasi ambacho ndege inadidimia kwenye tope na kusababisha abiria na mizigo ipunguzwe ili ndege iweze kuwa nyepesi. Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi katika kutatua tatizo hilo ili ndege kubwa ziweze kutua huko? Kwa nini *Air Tanzania* haziendi huko?

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa hotuba yake nzuri. Pia natoa pongezi kwa Wizara kwa jinsi inavyotekeleza vizuri majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, moja, napendekeza kuwa *TRC* isiuzwe badala yake ikodishwe kwa kampuni itakayoweza kuiendesha vizuri.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ilitoa ahadi kuwa simu za mkononi toka *TTCL (Celtel)* itaanza kufanya kazi mwezi Desemba, 2004 ingawa minara imesimikwa kutoka Mjini Sumbawanga mpaka kukutana mpakani mwa Rukwa na Mbeya, lakini mpaka sasa eneo la Kwela bado kupatiwa mawasiliano ya simu. Napenda kujua lini simu za mkononi zitaanza kutumika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, tatu, bado simu za mkononi Tanzania ni ghali sana. Nashauri Tume inayohusika na mawasiliano ifanye uchunguzi ili gharama za simu ziweze kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, nne, tunataka uendeshwaji wa Bandari ya Kasanga utolewe kwa njia ya *tender* badala ya kutolewa kienyeji kama ilivyofanyika wakati ule alipopewa *GS Motors.*

Mheshimiwa Spika, narudia kutoa pongezi na pia naunga mkono hoja hii.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanaoifanya katika Wizara hii. Pili, bila kusahau naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii nina matatizo yanayonisumbua kama yafuatayo hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, tunajua wote reli ya Manyoni - Singida jinsi ilivyojengwa, mpaka sasa reli hiyo bado sio imara hasa tuta lake. Reli hii bado pia reli zake zinatofautiana unene na hivyo kufanya treni iende kwa kupwaya pwaya. Lakini pia kwa sababu tuta siyo imara treni inakwenda kwa mawimbi sana na kutimua vumbi kwa sababu hizo imefanya treni kuacha njia mara nyingi na kusababisha ajali hata kuua.

Mheshimiwa Spika, treni ya kwenda Singida ilikuwa ina mabehewa matatu ya abiria lakini sasa ina mabehewa mawili ambayo hayatoshi kulingana na abiria waliopo. Naomba behewa hilo lirudishwe ili wasafiri wasiendelee kupata tabu wanayoipata.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru Wizara hii pia kwa kuunga mkono juhudi za wananchi wa Singida walioamua kukarabati uwanja wao. Uwanja huu sasa unahitaji kiasi cha shilingi bilioni 2. Hivi kwa kutenga shilingi milioni 100 uwanja huu utaisha lini? Kwa matengenezo ya haraka uwanja huu unahitaji zaidi ya shilingi milioni 700. Tafadhali Waziri anieleze kama Wizara yake iko tayari kutoa angalau milioni mia saba kwa ajili ya angalau kukamilisha ili ndege zianze kutua tena. Pili, bado kuna wananchi ambao hawajalipwa fidia je, sasa watalipwa?

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kimsingi naunga mkono hoja hii muhimu sana. Pia nashukuru kupata mtandao wa simu za *Celtel* na *Vodacom.* Wananchi wa Kondoa wanatoa shukrani nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba maswali yafuatayo yajibiwe:-

Moja, mtandao wa *Mobitel,* walianza ujenzi wa mtambo wao na kwamba ujenzi wa mnara ulifikia kiasi cha asilimia arobaini, lakini wamesimama, ni kwa nini? Naomba maelezo ili wananchi wajue.

Pili, pamoja na usikivu kufika katika Miji ya Tarafa na Kata zifuatazo lakini usikivu sio mzuri. Simu hazikamati kabisa. Miji hiyo ni Pahi, Busi, Kwadelo, Hambi, Kalamba, Mnenia, Masange, Kisese, Kikore, Thani na Changaa. Miji hiyo ni ya kibiashara sana, kwa hiyo wananchi wana uwezo wa kununua simu.

Mheshimiwa Spika, nashauri busta ndogo ijengwe katika mlima wa Makongo ambayo itawezesha usikivu katika maeneo hayo yote. Kwa nini ushauri huo hauzingatiwi? Naomba majibu katika suala hili muhimu sana.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi nzuri wanazofanya. Hakika Mheshimiwa Waziri amewasilisha vizuri hotuba yake na naunga mkono hoja yake mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache wa mapungufu nachangia vipengele vifuatavyo, kwanza ni huduma za treni. Nimeshuhudia mimi mwenyewe mapungufu ya kiutendaji ndani ya treni. Kwanza vyoo vimebadilishwa kuwa stoo na kuwafanya abiria kutumia vyoo vilivyopo kwa foleni. Pili, bado baadhi ya abiria wanakaa kwenye *corridors* chini na maeneo ya vyumba vya kulala daraja la pili ni kero.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika yanayouza simu. Ni huduma nzuri lakini wameanza kukosa uaminifu wa kuuza simu/vipuri vyake vilivyotumika bila kuwa wazi kwa wanunuzi. Lakini naipongeza sana *TTCL* kwa utaratibu wa *prepaid.*

Mheshimiwa Spika, naomba mtindo wa magari madogo ya kuburuzia mizigo uwepo hapa Dodoma kama Dar es Salaam. Nashukuru kituo cha Dodoma kudhibiti wizi unaofanywa.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, pokea salaam za pongezi kwa kazi nzuri hasa ile iliyofanywa na makampuni ya simu, mfano, *Mobitel, Celtel* na *Vodacom* kuunganisha wananchi nchini kwa mtandao wa simu za mikononi. Naomba uwashukuru mno na kuwakumbusha waongeze usikivu hasa katika maeneo ya Jimbo la Nzega hususan Kata za Puge, Nkiniziwa, Utwigu na Mizibaziba.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara yako itazame kwa makini namna ya kusaidia kufanya kiwanja cha Mwanza kuwa *Hub* ya *Lake Zone* na pia njia jirani za Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya na hasa katika kutengeneza miundombinu kama *Apron* ni ndogo, *departure and arrival lounge* hazitoshi, maji, vyoo na *cargo terminal.*

Mheshimiwa Waziri, *Mwanza Airport* inarusha ndege za abiria na mizigo takribani 40 kwa siku. Napongeza *runway* ni nzuri mno. Kwa mwezi, upande wa *cargo Mwanza Airport* husafirisha hadi tani 1,500 za minofu, lakini hakuna *shed* na *apron* yake ni mbovu. Je, kwa uwanja wenye biashara kubwa kama hii, Serikali ina mpango gani? Itawezekana kufanya hatua za makusudi *Mwanza Airport* iwe *Hub* baada ya *DIA?*

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za kubinafsisha au kuuza Shirika la Reli *(TRC)* kwa mwekezaji. Kwa kuwa kumekuwa na matatizo katika maeneo mengine mfano, *TTCL, ATC* na *TES* iwe ya makini kuepusha migogoro lakini vyote vifanywe kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nakupongeza kwa ujasiri uliofanya kwa kuingia katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi ya kuwa Rais ingawa kura hazikutosha. Kumbuka mvumilivu hula mbivu na kila jambo lina kheri. Hongera sana.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Pamoja na kuunga mkono hoja yake, naomba anieleze kwa kuwa alipokuwa anajibu swali katika kikao cha Bunge lililopita alisema mtandao wa simu za *Celtel* utafikisha mnara wake katika Tarafa ya Kidete, Wilaya ya Kilosa. Kwa majibu yake hayo niliporudi Jimboni nilikwenda Kidete na kuhamasisha watu juu ya upatikanaji wa mnara wa *Celtel* pale Kidete.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi anieleze utekelezaji wa maelezo yake ya kupatiwa mnara wa *Celtel* Tarafa ya

Kidete umefikia hatua gani? Hoja ya kupatiwa mnara wa *Celtel* ni muhimu sana katika Tarafa iliyojengewa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na Tarafa hii ina uchumi mkubwa wa kilimo cha mboga mboga, nafaka na mazao ya biashara. Kiuchumi mnara wa *Celtel* utalipa yaani upo viable.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa hotuba hiyo, pengine nimshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada zao za kusimamia masuala ya mawasiliano na uchukuzi katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuikumbusha Serikali kuwa tunazo ahadi za kuboresha mambo yafuatayo katika Jimbo langu, kwanza, ujenzi wa posta ya kisasa Mpanda Mjini, pili, ujenzi wa nyumba ya kufikia wageni uwanja wa ndege Mpanda Mjini na tatu, kubadilisha reli toka ratili 56 kuwa ratili 80 Mpanda-Kaliua.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kama Serikali itakumbuka hayo na nina imani kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, atayatolea maelezo ya kina wakati atakapokuwa anatoa maelezo ya ziada baada ya hoja hizi wakati akijibu maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ninayo masikitiko makubwa ya kuyafikisha kwa Mheshimiwa Waziri. Treni yetu ya kutoka Tabora kwenda Mpanda ilipata ajali baada ya reli ya kati ya Tabora na Lolangulu kung'olewa na majambazi ikasababisha treni ya Mpanda kupata ajali. Cha kusikitisha ni kwamba ni kipindi kirefu sasa toka nilipowasiliana na Waziri kuhusu mabehewa ambayo yalikuwa yameharibika katika ajali hiyo ikiwa ni behewa daraja la kwanza, daraja la pili na *buffet car,* behewa ambazo zimesharejeshwa ni *buffet* na behewa la daraja la pili, lakini mpaka leo hii behewa daraja la kwanza bado. Sasa sijui nini tatizo wakati lipo behewa Tabora na Dar es Salaam la daraja la kwanza limeegeshwa tu. Wananchi wangu wanaendelea kupata taabu na kusafiri kwa adha kubwa, wakati uwezo wa kusafiri na daraja la kwanza wanao. Hivi Serikali inatoa maelekezo gani kwa suala hili, kwa wananchi na watumishi wa *TRC* wanaostahili kusafiria daraja la kwanza. Naomba nipewe maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia moja. Aidha, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi yao nzuri na ubunifu wa hali ya juu. Naipongeza Wizara kwa kuipatia Mamlaka ya Hali ya Hewa ofisi yenye hadhi ambayo imewapa wafanyakazi ari mpya na kasi mpya ya kufanya kazi katika mazingira mazuri. Vile vile, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, Dr. Mohamed Mhita, pamoja na wakurugenzi na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri wanayofanya kwa saa nyingi bila ya kujali muda wa saa za kazi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa juhudi zake mwenyewe za kuipatia Mamlaka mitambo na vifaa

vingine. Juhudi namna hii ni vyema zitambuliwe kinyume chake ni kuvunja ari ya watendaji wetu. Pamoja na jitihada za Mkurugenzi Mkuu, naomba Wizara iongeze bajeti ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kuongeza ari na kasi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mwisho, nawatakia kheri Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wengine wenye azma ya kugombea Ubunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kukutana leo hii kuichangia Bajeti hii yetu ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe kwanza pole zangu za dhati kwa ndugu na jamaa wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki, nao ni Waheshimiwa Marehemu Yete Mwalyego, Marehemu Kepteni Theodos Kasapira, Marehemu Hassan Diria, Marehemu Frank Mussati, Marehemu Abu Kiwanga na Marehemu Margareth Bwana. Ni vigumu kueleza michango yao ya mawazo waliyoitoa katika Wizara hii kwa muda wote tuliokuwa nao hapa. Lakini tunasema ni matakwa ya Mwenyezi Mungu, binadamu hawezi kuyapinga. Tunaziombe roho za marehemu hao zilale mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kugombea nafasi ya Urais. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume, kwa kupata nafasi tena kuendelea kugombea kiti chake na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kupata nafasi ya kugombea kama mgombea mwenza. Kwangu mimi nasema ninaahidi ushirikiano wa dhati na wa vitendo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa kabisa katika utekelezaji wa majukumu yetu hatukuweza mia kwa mia kukidhi mahitaji ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote. Lakini nikiri kuwa tumejitahidi kwa kadri tulivyoweza kutatua kero zinazowagusa wapiga kura wao kwani ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wa CCM kwamba wapiga kura wao ndiyo wapiga kura wangu na ndiyo hivyo shida zao zinazowagusa ndiyo shida zangu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Wizara hii kwa uchumi wa nchi hakuna asiyeujua ila namna gani na kwa kiasi gani Wizara hii inawezeshwa kufikia malengo ni changamoto tosha hasa katika hali yetu hii ngumu ya uchumi na kwa vile keki tuliyonayo ni ndogo na mahitaji ni mengi, hivyo haitowezekana tukapewe nusu au robo ya keki hiyo, itabidi tupate kidogo kama wanavyopata wengine.

Mheshimiwa Spika, kubwa niseme kwamba siku moja kama tukiamua kufumba macho na kuviboresha viwanja vya ndege vyote vinavyozalisha na kufungua maeneo ambayo yanazalisha bidhaa kwa kuwajengea wananchi bandari, kuwawekea reli ili

waweze kusafirisha bidhaa zao kwenda sokoni kwa urahisi zaidi, basi *impact* ya Wizara hii itaonekana katika Sekta ya Uchukuzi na tutaona uchumi wetu utakavyopaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani siku moja niione Tanzania yenye ubora wa reli, kuwa na *underground train* na njia mpya za reli ziendazo katika Miji mbalimbali, kama ningeweza kuunganisha Tanzania na nchi zote za jirani kurahisisha usafiri wa uchukuzi, basi roho yangu ingetulia, lakini haiwezekani kwa mara moja. Ningefurahi zaidi kama ningeona tunapata *International Airport* kwa kila Kanda na kuweza kufungua nchi yetu kwa njia hii na kuboresha uchumi wetu. Lakini naamini siku moja tutaweza kufanya hivyo kwani hata Roma haikuweza kujengwa kwa siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi ya maendeleo yalifanywa, yanafanywa na yanaendelea kufanywa katika Tanzania na Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi inajitahidi sana kutekeleza majukumu yake ya kuboresha Uchukuzi na Mawasiliano. Nakiri kwamba tumetoka mbali na tumejitahidi na naamini huko mbele uko mwanga mzuri wa mafanikio bora.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie hoja zilizopo mbele yangu. Maeneo nitakayochangia ni mengi na nina hakika sitokidhi mahitaji ya wote. Naomba nichangie kwenye viwanja vya ndege, usafiri wa majini na nchi kavu, *TAZARA, TRC* na Maziwa, Usafiri wa Anga na Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga, Bandari, Ndege ya Serikali na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya viwanja vya ndege yamejitokeza kadhaa. Moja, likiwa madaiano kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na JWTZ kwa ajili ya uharibifu uliotokea kule Tanga. Sisi tunasema hili linashughulikiwa Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi. Nia yetu ni kutengeneza pale ambapo pameharibika.

Mheshimiwa Spika, lilizungumzwa suala la *Mafia Airport* na Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Tunawahakikishia Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa Abdulkarim Shah kuwa nia yetu ni kuboresha kiwanja kile cha Mafia ili huduma za utalii ziweze kuendelea vizuri na utalii uweze kuchangia katika uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha ndege cha Kilwa kweli ni kizuri isipokuwa usafiri haupo, tunamwambia Mheshimiwa Mbunge tutajitahidi kushirikisha sekta binafsi waone umuhimu wa kwenda pale na yale marekebisho madogo madogo aliyozungumza Mheshimiwa Mbunge nadhani tutayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, lingine lilizungumziwa udhalilishaji unaofanywa na Ukaguzi wa Viwanja vya Kimataifa katika nchi za nje. Nafikiri tulikuwa wote hili suala limekuja baada ya kutokea masuala haya ya Septemba 11 na tumesema katika nchi zote hatuwezi ku-*compromise* masuala ya usalama. Kwa hiyo, inategemea nchi na nchi wanavyoweka taratibu zao. Ukitazama hata karatasi zile za *Immigration* za Canada nadhani hupendi hata siku moja uende Canada utakwenda kama huna budi kwenda.

Lakini tunakwenda kutokana na hali halisi ya mambo yalivyojitokeza kusingekuwa na mambo haya nadhani masuala yote haya yasingejitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla usafiri wa anga umeboreka, nakubaliana na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Waheshimiwa Wabunge wengine na pongezi tumezipata. Kweli tulipata taabu kidogo kwa kujenga uwanja wa ndege wa Songwe, lakini tukifungua huko Songwe hali ya mawasiliano itakuwa nzuri zaidi. Nina hakika tutaweza kuhudumia nchi za *SADC* vizuri zaidi na uchumi wa Tanzania utaboreka.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali alizungumzia *Karume Airport* isaidiwe, mimi nasema ombi lake tutalipeleka kwa wenzetu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, sisi tuko tayari kuwapa mawazo ni kwa namna gani, tunapita wapi, tunaomba wapi, tunakopa wapi, wakiwa tayari na sisi tuko tayari kabisa kusaidiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la *Dodoma Airport,* usafiri wa ndege vipi, kuna nini, kiwanja hakiboreshwi. Jana hapa Bungeni mimi nilijibu swali hilo. Jamani hapo nyuma usafiri wa ndege ulikuwepo hapa Dodoma. Tulipoboresha barabara, zikaboreka na mabasi yakawa mengi watu wakawa na *choice,* sasa watu wameona ni vizuri wenyewe wanapenda kusafiri kwa barabara. Lakini sisi bado tunaendelea kuwasisitiza wenye ndege waweze kuleta huduma hiyo. Lakini haya mambo ya siku hizi wanapima. Wanaowekeza wanapima, je, mimi nikipeleka ndege Dodoma italipa? Sasa wengi hawaji kwa sababu hawapati abiria wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo ni-*respond* kwa hoja za mtani wangu Mheshimiwa Bakari Shamis Faki. Napenda nimjibu yeye *specific* kwa sababu yeye ndiye anayesimamia sekta hii kwa upande wa wenzetu wa upinzani. Alizungumzia ndege ya Serikali, mimi nasema ndege ya Serikali tuliizungumza muda mrefu mbona haya tunayozungumza ni *history.* Sasa sijui kama Mheshimiwa Ibrahim Lipumba, akipata Urais sidhani kama ataupata, atakwenda kwa miguu, atatumia ndege hii hii iliyopo. Lakini hatutegemei kama atafika huko Ikulu. Tunamwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba ndege ni nzima, matatizo madogo madogo yanaweza kutokea kwa chombo chochote kile iwe ndege au iwe gari kama ilivyo kwa binadamu kupata mafua na homa ni kitu cha kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, meli zote zinazosafiri katika Maziwa zinafanyiwa ukaguzi, ni nzima na nyingine zimetengenezwa kule kule Mwanza na ukaguzi unafanywa kwa wakati kwa mujibu wa taratibu tulizoziweka. Chombo cha *SUMATRA* sasa hivi kinafuatilia kwa karibu sana masuala haya ya usalama. Kulikuwa na suala alilolizungumzia usafiri wa anga ni ghali na viwanja ni vichache havitengenezwi.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi napenda nimwambie Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, namkubusha kwamba Tanzania ina viwanja vya ndege 63 mbali na *airstrips.* Sisi tuko mbele kuliko nchi nyingine yoyote ya *East Africa.* Kwa hiyo, kusema kwamba ni viwanja kidogo tulivyonavyo, hivyo tulivyonavyo vinatosha, vinahitaji kuboreshwa ndiyo kitu kikubwa na cha msingi. Matengenezo tunafanya jinsi

fedha zinavyopatikana na hivi sasa tuko njiani kufikiria namna bora ya kushirikisha sekta binafsi kuingia katika msukumo huo wa kuendesha viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, alizungumzia juu ya reli kwamba ni chakavu nakubaliana naye, hii reli imejengwa kabla yeye na mimi hatujazaliwa. Lakini reli hii inaboreshwa kila leo kwa kufanyiwa *relaying,* kubadilishwa mataruma na kuwekwa reli mpya.Tukubaliane kwamba ilivyokuwa hapo nyuma na hivi sasa kama maboresho makubwa sana.

Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, pia alizungumzia matumizi ya reli ya Tanga, ni kama tulivyosema matumizi ya reli ya Tanga yameshuka kidogo kutokana na kwamba barabara ya kutoka Tanga kuja Dar es Salaam imeboreke na unaweza kwenda Tanga kwa saa mbili na nusu au saa tatu. Wengine wana *opt* kupeleka mizigo yao kwa kutumia barabara. Kuunganisha Arusha hadi Musoma suala lipo na lipo katika *East Africa Community* linajadiliwa namna ya kupata fedha za kufanya *feasibility study.* Naomba niunganishe hapo kwamba reli hiyo haitopita katikati ya Mbunga za wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu *TAZARA* alizungumzia migogoro ya mara kwa mara, lakini mimi nasema hilo halipo. Lililopo kwanza ni ukwasi kidogo na kupungua kwa shehena. Kwa sababu shehena kubwa ya usafirishaji inakwenda Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, lakini nasema hivi karibuni mimi nilipata nafasi kwenda Zambia kwa shughuli zangu, lakini na hili nalo nilipata nafasi ya kulizungumza na wale wenzetu ambao wanashughulikia mambo ya usafiri, ipo neema huko mbele ya kusafirisha *copper concentrate* kutoka machimboni kupitia katika reli hii kuja Dar es Salaam na tumeshawapa moyo wenzetu wenye nia ya kufanya hili kwamba nafasi iko wazi waendelee kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya kiwanja cha ndege cha Sumbawanga kwamba kiboreshwe sambamba na Songwe Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tunakubaliana naye kwamba katika mwaka fedha huu mamlaka imetenga shilingi milioni 200 kuboresha njia ya kuruka na kutua ndege na kazi hiyo inategemea kuanzia Oktoba, 2005 tunajua wakati huo huo yeye atakuwa yuko *busy,* lakini sisi tutakuwa tunaendelea na kazi zetu. Matengenezo hayo yatawezesha kiwanja kutumika katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, nafikiri wameridhika na majibu yetu kwamba fedha tutazitafuta ili tutengeneze kiwanja cha ndege cha Mafia kwa sababu ni kiwanja ambacho kinatoa huduma kwa watalii na kinasaidia sana kusukuma uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, barabara ya ndege ya Lindi Mjini ni mbovu, ina ubovu unaosababisha Mashirika ya ndege kutokwenda Lindi. Barabara ya ndege ya kiwanja cha Lindi inahitajika matengenezo ya kawaida kuendelea kutoa huduma na kuhudumia matumizi na baada ya matengenezo makubwa ya majengo yaliyofanyika hivi karibuni matengenezo mengine Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, yataendelea.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, alitoa mawazo kwamba kiasi cha shilingi milioni 100 zinazotengwa kila mwaka kwa kiwanja cha ndege cha Singida hazitoshi, nakubaliana naye. Nishukuru kwamba hivi karibuni mlipokuwa na kikao na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Waheshimiwa Wabunge wa Singida mlinipa nafasi na mimi kukaa nanyi kubadilishana mawazo juu ya namna ya kuboresha kiwanja cha ndege cha Singida.

Mheshimiwa Spika, msimamo wangu uko pale pale na Wizara tutaendelea kujitahidi kuona ni namna gani tunaweza kuwasaidia wananchi wa Singida. Mheshimiwa Diana Chilolo na Waheshimiwa Wabunge wa Singida, nawaomba tu mvute subira. Mheshimiwa Hamisi Nguli, ni hayo hayo uliyoyazungumzia tunakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Leonard Derefa, alizungumzia kiwanja chake cha Ibadakuli alitaka kiongezwe urefu kifikie mita 1,000 na kiwekwe lami. Tunasema kiwanja cha ndege cha Ibadakuli kina urefu wa mita 2,000 na mita 30 za upana. Sisi tunafikiria kinakidhi matumizi ya ndege ya abiria 50. Nia ya mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni kuona kwamba kiwanja hicho kinawekwa lami katika kipindi cha miaka mitano ijayo. *Solution* pale kama ilivyo katika sehemu nyingine kama Bukoba na kama ilivyo Singida, *solution* ya viwanja hivyo ni kuviwekea lami.

Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, tunakubaliana naye kwamba kiwanja cha ndege cha Kigoma kikipanuliwa kitaweza kufanya biashara kubwa sana katika nchi za jirani na kukuza uchumi na alitaka kujua ni lini. Sisi tunasema hoja yake ni nzuri Mheshimiwa Mbunge hivi sasa ninavyokwambia tunajitahidi kuzungumza na *UNDP* kuona ni namna gani wataweza wao kutusaidia kuboresha kiwanja cha ndege cha Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, mawazo yao ni mazuri ya Bukoba. Jana tulipata nafasi ya kujadiliana juu ya kiwanja kipya cha ndege cha Bukoba. Lakini hatuwezi kusema kiwanja kipya cha ndege ndiyo *substitute* ya kukiacha kiwanja cha ndege cha Bukoba, hapana.

Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, nia yetu ni kuona kwamba Bukoba itakuwa ni miongoni mwa vile viwanja ambavyo vitawekwa tabaka la lami katika miaka mitano ijayo. Wizara mpango huo inao na *TAA* itashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu ilikuwa na mawazo na mawazo yote tunayachukua.

Mheshimiwa Lephy Gembe alitoa mawazo kwamba tuna ahadi za ujenzi wa nyumba ya kufikia wageni na uwanja wa ndege wa Mpanda Mjini. Wazo tunalipokea na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege italifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye Mamlaka ya Hali ya Hewa. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuipongeza *TMA* na anaiomba Serikali iongeze Bajeti ya *TMA*. Pamoja naye namshukuru Mheshimiwa Diana Chilolo na yeye kwa kutupa ushauri huo. Niseme Mheshimiwa Zabein Mhita, tunakushukuru sana kwa sababu tunasema panapotokea *a success man there is a woman behind.* Kwa hivyo, tunakushukuru kwa kumwezesha *Director General* wa Mamlaka ya Hali ya Hewa kufanya kazi yake kwa utulivu zaidi na kutuwezesha kuboresha Mamlaka ya Hali ya Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Philip Magani, tunakushukuru kwa kuipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa huduma zake na nampongeza Mkurugenzi Mkuu kwa juhudi zake, kwa kweli sisi tunashukuru sana. Tumetoka mbali na hali imeboreka sana kwenye utabiri wa hali ya hewa. Nafikiri sasa kila siku tunapata utabiri wa hali ya hewa wa uhakika kwa sababu kumeboreshwa na vifaa vingi tu wamepata.

Mheshimiwa Charles Kagonji, tunakushukuru kwa pongezi zako na tunasema sisi pongezi hizo zinatutia moyo na nina hakika atakayechukua nafasi hii atakuwa anapo pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye masuala ya *Tanzania Port Authority*. Kulikuwa na hoja kwamba Serikali je, ina mpango gani wa kuondoa mchanga katika Bandari ya Lindi. Hili ni suala la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz la muda mrefu na Bandari inalifanyia kazi. Tunapenda tumwambie kwamba sasa Mhandisi Mshauri ameshateuliwa kuchunguza matatizo haya katika Bandari ya Dar es Salaam na Lindi na tunategemea mapema mwakani Februari, 2006 tutapata taarifa kamili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo la Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ina mpango gani wa matumizi ya eneo ambalo ardhi yake wamefidia. Tunasema kuendelezwa kwa Bandari yoyote ile hutegemea mahitaji ya shehena yanayopaswa kuhudumiwa. Lakini sisi tunaona ni vyema kuweka maeneo ambayo yanaweza kusaidia sana hapo baadaye, tusije tukafika tunataka kupanua Bandari, tunataka kufanya *free port,* tunataka kufanya *export processing zone* ikawa hamna maeneo mengine. Lengo letu kuu, ni kuboresha miundombinu ya bandari ikidhi mahitaji ya leo na baadae.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, alikuwa na maombi ya gati la Mkoani Pemba. Mimi nasema hata na mimi nimeliona linanigusa. Nitawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar tuone tunaweza kufanya nini tunashirikiana vipi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya alikuwa na mawazo kwamba uendeshaji wa Bandari ya Kasanga utolewe kwa njia ya *tender* badala ya kutolewa kienyeji kama ilivyofanywa hapo nyuma. Tunakubaliana naye tunasema Serikali imeingia mkataba na *GS Motor* kuendeleza Bandari hii katika masuala ya ujenzi ya vifaa na umeme. Lakini katika sheria mpya ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeipitisha ya *TPA* hivi karibuni, Bandari zote za Maziwa Makuu ikiwa ni pamoja na

Kasanga zimewekwa chini ya usimamizi wa *Tanzania Port Authority.* Mkataba uliopo ambao ni halali umerejewa na utapitiwa vizuri na *TPA* na Serikali ili kukidhi mahitaji ya sheria ya biashara na jamii. Endapo itabidi kuingia mkataba mpya ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, utazingatiwa.

Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ulikuwa na wazo je, ni lini matengenezo ya Bandari ya Kigoma yatafanyika ili iweze ku-*handle more cargo* na *more people* ambao wanatoka Kongo, Burundi, Rwanda na Zambia kwenda Bandari ya Mpulungu. Bandari ya Kigoma tunasema kwa hivi sasa ina uwezo wa kuhudumia mizigo yote inayokwenda nchi za jirani za Kongo, Burundi na Zambia. *MV Liemba* huwa inatoa huduma za abiria na mizigo kwenda Mpulungu Zambia na *MV Mwongozo* huwa inakwenda Bujumbura, Burundi kwa upande wa mizigo ya meli, nchi ya jirani ya Burundi zimeendelea kutoa huduma katika Ziwa Tanganyika. Hata hivyo chini ya *TPA* ukarabati utafanyika pale ambapo itahitajika.

Mheshimiwa Stanley Kolimba, hatua zichukuliwe kuboresha mawasiliano na *Radio Call* katika Bandari za Manda, Liuli na *Mbambabay* na kufufua biashara kati ya Bandari ya Manda na *Deep Bay,* Kirumba na Kalonga. Tunasema vituo vyote katika Ziwa Nyasa vina vifaa vya mawasiliano ya *Radio Call* Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo huwa mara chache vyombo hivyo huwa vinaharibika na mafundi huvihudumia na hufanya kazi tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jenereta iliyoondolewa kutoka Bandari ya Manda, jenereta hiyo iliondolewa baada ya vituo hivyo kuwekewa vifaa vya kuzalisha umeme kwa mionzi ya jua. Nafikiri hilo ndilo tulilolifanya.

Mheshimiwa Spika, biashara kati ya nchi ya Malawi na Tanzania inafanyika kupitia vituo vya *Mbambabay,* Tanzania na *Nkatta bay,* Malawi ndiyo maana mnapata sukari kwa urahisi zaidi kule. Aidha, huduma hizo hutolewa pale ambapo kunakuwa na mizigo kati ya *Mbambabay* na *Nkatta bay.* Biashara ya abiria imekuwa ni ya chini sana sio watu wengi wanaopenda kusafiri kutoka *Mbambabay* kwenda Malawi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Magufuli alikuwa amefurahia kwamba sasa safari za meli za Serengeti na Butiama ziongezwe kwenda Chato zifike mbili badala ya tatu. Tunakushukuru Mheshimiwa John Magufuli kwa sababu hapo mwanzo zilikuwa hazipo lakini sasa zipo. Tunasema safari za meli za Kampuni ya Huduma ya Meli zitaongezwa mara baada ya kukamilika matengenezo ya *MV Clarious* ambayo inategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema mawazo mengi yaliyotoka *TRC* tumeyapokea. Mawazo na ushauri kuhusu Mabasi tunayapokea. Mawazo ni mengi nisingeweza kumaliza kiu ya Waheshimiwa Wabunge wote lakini naomba nichukue nafasi hii niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao hakuna hata mmoja aliyesema kwa vibaya. Wote wamesifia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa juhudi tulizozifanya. Tunasema juhudi hizi zinatokana na moyo na mwongozo mliotupa Waheshimiwa Wabunge na ushirikiano wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nashukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge nakumbuka neno moja zito alilozungumza Mzee wetu Mzee Ali Hassan Mwinyi wakati fulani alisema nimehemewa, na mimi leo nimehemewa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ya kina. Nawashukuru sana kwa pongezi kwangu binafsi, kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na kwa wafanyakazi. Lakini sisi ni kioo tu cha Wizara. Kwa hiyo, pongezi kubwa kwa kweli ni za wafanyakazi. Wametuwezesha na wametupa nafasi sisi kuweza kuendeleza sekta hii kwa kipindi cha miaka mitano, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa kuwatambua waliochangia kwa mazungumzo katika ukumbi huu na waliochangia kwa maandishi.

Katika ukumbi huu waliochangia ni wafuatao, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Beatus Magayane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua michango mingi na ya kina vile vile kwa waliochangia kwa maandishi. Naomba niwatambue wafuatao, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Leonard Derefa *(Brother),* Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Isaac Cheyo na Mheshimiwa Esha Stima.

Wengine ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa

Edward Ndeka, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Lydia Boma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao ni Waheshimiwa Wabunge 50 waliochangia kwa maandishi, nawashukuru sana. Kwa maana hiyo haitakuwa rahisi kwa muda tulionao kuweza kujibu kila hoja ya kila Mheshimiwa Mbunge. Naomba mchukue kama ni ahadi kwamba kabla hatujamaliza kipindi hiki cha Bunge tutakuwa tumejibu kwa maandishi. Najua haitatusaidia sana majimboni lakini itatusaidia Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amepitia maeneo kadhaa kwa maana ya ufafanuzi. Mimi nitazungumzia maeneo yanayohusu sera kwa ujumla. Pale inapobidi nitapitia maeneo ya mawasiliano kwa maana ya Posta na Simu. Nianze na hili suala la maendeleo ya Kanda. Nini maana ya Kanda ya Kati, limeulizwa. Hili limezungumziwa na Mheshimiwa Dr. James Msekela, alipokuwa akichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ally Karavina alipokuwa akichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Leo hii Mheshimiwa John Singo, amelizungumzia na vile vile Mheshimiwa Beatus Magayane na Waheshimiwa Wabunge wengi, Waheshimiwa wenzangu.

Namshukuru sana Mheshimiwa John Magufuli. Alipata nafasi ya kutoa ufafanuzi mzuri sana kuhusu nini maana ya Kanda ya Kati. Sitarudia tena kulielezea hili. Niseme alikubaliana na mawazo mengi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili. Wote tunakubaliana yafuatayo kuhusu nafasi nzuri ya nchi yetu Tanzania kwa maana ya kijiografia na kila wakati tunasema ni zawadi iliyoje aliyotupa Mwenyezi Mungu. Hakuna kubwa zaidi ya jiografia ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zawadi hiyo inabidi tuitumie na kuitumia ni kuinua uchumi. Hilo tunakubaliana. Tumekubaliana kwamba mhimili wa Ukanda wa Kati ni njia fupi itakayounganisha Bandari zetu za Mwambao na nchi za Maziwa Makuu. Hili tunakubaliana halina utata. Kwa maana hiyo kuna umuhimu wa kuimarisha reli ya kati, kuirekebisha na penginepo ikiwezekana hapo baadaye kuwa na njia mbili au tatu. Hakutakuwa na treni za mwendo wa kasi.

Kwa hiyo, hili lazima tuliweke katika mipango yetu ya muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nadhani tunakubaliana vile vile kwamba kuna umuhimu wa kuwa na viungo, huwezi kuwa tu na mhimili bila viungo. Kwa hiyo, viungo muhimu ni kwa mfano Mpanda, viungo muhimu ni reli kwenda Mwanza, viungo muhimu reli kwenda Singida. Yote haya inafanya tuwe na Ukanda wa Kati au *Central Corridor.* Lakini vile vile kutokana na mchango wa Mheshimiwa Beatus Magayane, leo anatukumbusha kwamba huwezi ukawa na reli tu, ukawa na barabara ukasema ndio mhimili, lazima uangalie uchukuzi na usafiri kwa uwiano na kwa ujumla. Kwa hiyo, Viwanja vya Ndege kwa mfano cha Kigoma, Tabora na Mwanza ni mihimili katika Ukanda wa Kati. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Mwanza na Bandari ya Kigoma nazo ni muhimu kwa Kanda hii. Hili tunakubaliana. Lakini nakubaliana vile vile na Waheshimiwa Wabunge kwamba Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni muhimu, labda ina umuhimu mkubwa sana kwetu sisi. Ina ukanda mkubwa sana kuanzia Kusini Magharibi mwa Tanzania mpaka Kaskazini Magharibi. Kwa hiyo basi, kuna umuhimu wa kuunganisha kwa mfano Tunduma, Sumbawanga mpaka Kasanga. Hili halikwepeki hata kidogo. Huwezi ukaendeleza Tanzania kwa maana ya kuendeleza biashara na Kongo bila ya kuangalia sehemu hiyo. Vile vile kama nilivyosema kuangalia Tabora mpaka Kigoma kuiunganisha na Dodoma mpaka Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunakubaliana na mambo mengi.

Sasa naomba nifafanue kwa kifupi tu umuhimu wa reli ya Isaka na Kigali. Imezungumziwa na Mheshimiwa Dr. James Msekela na vile vile imezungumzia na ndugu yangu Mheshimiwa Ally Karavina. Niseme tu kwamba sisi tunaangalia suala la Kaskazini Mashariki ya Kongo kwa maana ya lile lile mlilotutuma, tuangalie uchumi wa jiografia yetu. Kwa hiyo, hatuwezi kuacha sehemu moja tukachukua nyingine. Kwa hiyo, tutakuwa na mhimili wa kati lakini kiungo kingine. Kiungo kimoja ni hiki cha Kasanga na kiungo kingine cha reli ya kutoka Isaka kwenda Kigali.

Lakini niseme vile vile labda hatujafafanua hii tuna sababu moja ya kuendeleza reli ya Isaka kwenda Kigali. Eneo la Ngara na eneo lote kuanzia Ngara mpaka Karagwe Mwenyezi Mungu ametupa zawadi nyingine. Tuna madini ya *nickel* ambayo kama tunataka tuweze tukaendeleza basi lazima tuwe na uchukuzi na uchukuzi wenyewe muhimu ni uchukuzi wa reli.

Kwa hiyo, hii ni sababu moja kubwa sana ingawa sasa hatuwezi tukawa tunaiendeleza, hiyo itakuwa kama tunazungumzia Tanzania tu. Kwa hiyo, lazima tuangalie hilo, tuangalie Rwanda, Burundi halafu tuangalie vile vile na Kongo Mashariki Kaskazini. Kwa mfano, Kabanga tu huko Ngara inakisiwa kuwa na tani milioni 26 za *nickel* ambayo tunakalia kama Tanzania. Hatujaziendeleza. Tatizo kubwa ni nini walikuwa wanasema bei sasa bei imepanda. Tatizo ni uchukuzi. Kwa hiyo, lazima tuendeleze hiyo reli na nadhani mtakubaliana na mimi kwamba tuna sababu kubwa ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Nizungumzie suala lingine zito la *ATCL.* Wizara yangu sasa tumekuwa sugu kidogo lakini sio kwa maana ya kupuuza mambo isipokuwa kwa maana ya kutostuka. Wiki mbili kabla ya Bajeti yangu miaka mitano kwa mfululizo lazima kunazuka jambo na hilo linawalenga Waheshimiwa Wabunge kuhusu Wizara yangu. Hili suala la *ATCL* limelenga huko. Lakini ni muhimu limejitokeza hivi karibuni. Lakini ni suala muhimu na Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia. *PSRC* walifanya kazi nzuri kwa kweli. Walijitahidi sana kuuza hisa zetu katika iliyokuwa Shirika la Ndege ambao sasa ni *ATCL.* Kulikuwa na ushindani mkali kati ya *Kenya Airways* na *South African Airways.* Wakati wa ushindani huo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisema na kweli kabisa wakasema jamani muangalie na mkumbuke yaliyotupata *East African Airways.* Tukasema sawa.

Kuhusu *South African Airways* wakasema hao jamani wanakuja tena ni wale wale Makaburu. Sasa tukawa katikati ya jiwe na mahali pagumu tufanye nini? Ikajitokeza kwamba *Kenya Airways* hawakutokea, *South African Airways* wakabaki peke yao. Kwa hiyo, kwa maana ya ushindani na maana ya zabuni tusingeweza kufanya lolote ilibidi tuwachukue na wakatoa bei nzuri dola milioni 20 mahali ambapo tulifikia kabisa kwenye sakafu karibu ingepita wiki mbili kabla ya *South African Airways* kuja *Air Tanzania* ingekuwa imefungwa kabisa.

Kwa hiyo, tukakubaliana wachukue hizo hisa lakini sisi tuendelee kuwepo. Lakini yamejitokeza masuala ambayo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana na ni masuala muhimu ambayo mmeyazungumzia kwa miaka mitatu mfululizo hasa kuhusu suala la tiketi. Mkataba wetu tulioingia ulikuwa ni hivyo kwamba tunaweza kutumia *system* zao za *Accounting* ili tuweze kufaidika na *Advanced systems.* Lakini hili linazungumzika kwa sababu faida zake si wazi sana. Si wazi basi tunaendelea kulizungumza na wenzetu. Wenzetu hawatuelewi lakini sisi tunasema bwana hili tatizo lisije likawa lile lile la *Alliance Air.* Kwa hiyo, nadhani tutalishughulikia na tutalimaliza kwa maana ya *code* yetu irudi tena.

Vile vile tumesaidiwa na kitu kingine kwamba *IATA* katika mkutano wake mkuu mwaka jana imetoa maagizo kwa wanachama ikiwa pamoja na sisi kwamba kila nchi na kila Kampuni katika *IATA* iwe na kodi yake. Kwa hiyo, lazima hatuna njia tuwe na *code* yetu. Tusipofanya hivyo hatutaingia katika mfumo mpya wa *automatic air ticketing.* Kwa hiyo, lazima itabidi turudi huko. Kwa hiyo, naomba muwe na subira tunapolimalizia hili suala. Hatuna njia lazima turudie na *code* yetu ya *ATC* namba 197. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya wafanyakazi wa *ATCL* yamezungumziwa. Tumemwagiza mambo mengi, lawama nyingi kukiuka taratibu na mambo mengine. Sisi tulichofanya tumemwagiza Msajili wa Hazina ambaye ndiyo mwenye hisa katika *ATCL* aiagize Bodi ishughulikie tena kwa haraka masuala yote haya ambayo yamezungumziwa na wafanyakazi kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine tunawaomba wafanyakazi, mimi ni mtu ambaye kwa kweli kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge ni mtu *very simple.* Unaweza kuingia ofisini wakati wowote. Wafanyakazi njooni, sio lazima mpeleke malalamiko kwenye magazeti. Hata mkipeleka basi njooni, mnione kwa sababu mna uhuru wa kufanya hivyo. Kwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kusikia kwa mara ya kwanza kuna tatizo la wafanyakazi, kwenda kulikuta kwenye magazeti. Sawa, magazeti yanauza lakini haisaidii kutatua tatizo.

Kwa hiyo, njooni mimi niko wazi kabisa na sina matatizo kabisa kuonekana. Mengi ya matatizo ya wafanyakazi ni mawasiliano tu. Kwa hiyo, naomba sana kama sio mimi anayefuata naomba naye mumpe ushirikiano huo ndugu zangu wafanyakazi. Kwa hiyo, yote yaliyozungumzwa, matatizo ya *ATCL,* yanayohusu ubadhirifu na nini yote yanazungumkia na Bodi na tumeomba watupatie ripoti jinsi wanavyoyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, tuna *Board Members* wa Tanzania pale bahati nzuri nadhani kati ya nane, wako sita Watanzania, kwa hiyo, hawa wana jukumu ili Kampuni hii isiwafie mikononi mwao. Tena ni watu muhimu tu kuna ndugu yangu Mufuruki, Mwenyekiti, Ndugu Muombwe toka Zanzibar, Ndugu Tecla Shangali, yuko Kleist Sykes, yuko ndugu Mtengeti toka *BOT,* yuko hata Balozi Mpungwe. Sasa hawa kweli wanataka *ATC* iwafie mikononi mwao? Nitaomba sana isife wakati mimi ni Waziri na vile vile isife hata baada ya mimi kumaliza Uwaziri. Kwa hiyo, ndugu zangu tutalishughulikia hili suala na Serikali inalichukuliwa kwa umakini. Kwa maana hiyo, tumewaandikia *South African Airways.* Shirika au Kampuni na sisi kuna masuala mbalimbali ambayo tunaona wameyafanya nje ya mkataba, tumewapa notisi, tumefuata taratibu za mkataba kama tulivyoshauriwa na wanasheria, tunangojea majibu yao. Tutawaeleza yatakayokuwa yanatokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukodishaji wa *TRC.* Umechukua muda mrefu. Lakini tumejifunza mengi toka Cameroon, Zambia, Colombia, Mozambique na Malawi, waliotutangulia. *PSRC* bila shaka watazingatia sana hayo mafunzo tuliyopata toka kwa wenzetu waliotutangulia. Lakini niseme tu baada ya zabuni kutangaza ni wazabuni wawili tu waliofaulu mchujo yaani hao ni *Rites Consortium* wa India na *Great Lakes Rail Consortium* ambao wamejiandikisha Afrika ya Kusini. Zabuni ilifunguliwa lakini ina awamu mbili.

Awamu ya kwanza ni kiufundi na awamu ya pili ni kifedha. Sasa ukishindwa awamu ya kwanza, ukishindwa huende awamu ya pili, ndiyo taratibu za *PSRC.* Kwa hiyo, *Rites* tu ndio walifuzu awamu ya kwanza wakaruhusiwa kwenda kufungua zabuni ya awamu ya pili zabuni ya kifedha lakini *Great Lakes Rail Consortium* wamekwenda Mahakamani kuishtaki *PSRC* kwa kutowaruhusu kuendelea kushiriki. Sasa hili linaweza likapunguza kasi ya zoezi hili lakini naamini vyombo vyetu vya sheria vitalichukulia hili suala kwa umuhimu na uharaka wake katika mazingira ya sasa ili Shirika lisiendelee kudidimia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Posta, Posta itarekebishwa. Tunategemea kwamba itakuwa ni Kampuni ambayo itamilikiwa na Serikali chini ya Sheria ya Makampuni badala ya Shirika kama ilivyokuwa sasa ili iweze ikajitegemea zaidi kimaamuzi. Vile vile maeneo yasiyokuwa ya kibiashara yatafidiwa na Serikali moja kwa moja kwa sababu ni wajibu wetu kutoa huduma za Posta kwa wananchi kwa gharama nafuu. Tunaweza kufidia moja kwa moja toka Hazina lakini vile vile kutakuwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ambao utakuwa unasaidia huduma za simu na vile vile huduma za Posta. Posta mpya zitajengwa kwa maombi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini zitajengwa kwa awamu na majengo yaliyopo tutaendelea kuyakarabati kama nilivyoeleza katika ripoti yangu asubuhi ya leo.

Kuhusu Benki ya Posta. Niseme mara nyingi tunaletewa maombi ya Benki ya Posta lakini hii ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha sio chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Sisi Posta ni mawakala tu. Huo uwakala tunaupata baada ya Benki Kuu inayosimamia taasisi za fedha kusema hapa panafaa kuwa Wakala hapa hapafai.

Kwa hiyo, tungependa kwenda vijijini na hizo huduma lakini sio zetu. Vile vile ninaambiwa kwamba Benki Kuu kufuatana na taratibu zake za kusimamia fedha imeruhusu Wakala mmoja tu wa vijijini na Wakala huo ni wa Peramiho, basi. Kwa hiyo, kwa wengine naambiwa huko Chato nako wanafanya upembuzi sasa kuangalia kama hizo huduma za Benki ya Posta zinaweza zikaenda. Kwa hiyo, hili ndilo nilitaka kutoa kama ufafanuzi. Lakini hata mkitujia sisi bado tutayafikisha maombi pale yanapohitaji kufika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo ya Same ambayo ni ucheleweshaji wa malipo, *Poster Master General* ameniahidi kwamba atafuatilia hili suala na kulipatia ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la boti, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare amelizungumzia jana, leo na nadhani atalizungumzia tena kesho. Sasa mimi sitaki kuingia mtego wa Upinzani. Wanachotaka kufanya ni kutugonganisha mimi na rafiki yangu Mheshimiwa John Magufuli, hilo hutaweza. Niseme tu tuna majukumu yanayoshabihiana, barabara ni muhimu, boti vile vile ni muhimu. Waheshimiwa Wabunge mmeshauri, vile vile Kamati ya Miundombinu imeshauri, tumesikia, Mheshimiwa John Magufuli amesikia. Tutakaa, tutaomba wataalamu wetu wakae kwa pamoja na mwekezaji, tumewapa wigo huo wa kuangalia, boti muhimu, barabara muhimu, naamini watatupa ushauri utakaotusaidia kupata ufumbuzi ili tupunguze adha kubwa ya usafiri Ziwani na vile vile tusiharibu barabara. Hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya mawasiliano, Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri, wametoa maombi yote tunayo. Kama mnavyojua kila mkizungumza kitu sisi tunakitilia maanani. Mpaka leo hii ninapokuja hapa nilikuwa nasaini maombi ya Waheshimiwa Wabunge kwenda *Celtel, Vodacom, Mobitel* na *Zantel.* Ndiyo kazi yangu hiyo. Kwa hiyo, nafurahi mimi kila kunapokuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwamba siku hizi lazima wapiga kura wapande kwenye miti ili waweze wakapata mawasiliano. Mheshimiwa John Singo, aliwahi kunieleza hilo nilipokuwa pale Same. Nikawaambia ndugu zangu wananchi pale nikasema aah, mmenipa kigezo kingine cha umuhimu wa miti nchini. Siku zote nilikuwa nafikiri ni kivuli, kinaongeza rutuba, ni dawa, ni chakula sasa kumbe una faida nyingine, mawasiliano. Lakini tumechukua yote waliyosema Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Omar Chubi kuhusu kupanda mlima halafu tena unapanda mlima halafu tena ukapande mti. Tutazingatia hayo kwa sababu tunapokwenda kasi hii si mbaya. Tumefika asilimia kama 60 tunakwenda 75, asilimia 100 tutafika tu. Mwisho wa mwaka huu tutakuwa na wateja milioni tatu wa simu za mkononi katika miezi sita ijayo tutakuwa na ongezeko la 500,000 kwa hiyo, tunakwenda vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue muda mfupi nizungumzie suala la *TTCL* na *Celtel.* Lakini kabla sijafanya hivyo niseme Mheshimiwa Said Nkumba, amezungumza kwa kila anapopata nafasi adha kubwa sana wanayopata wananchi wa Sikonge ni kama Wilaya iliyosahaulika. Namhakikishia ya kwamba *TTCL* wanasema watabadilisha mitambo ya kukoroga, wataleta mitambo ya kisasa. Hawajaniambia lini lakini ndugu yangu na mzee

wangu Mbowe yuko hapa ananisikia. *Celtel* wananiambia wameongezea muda, ilikuwa mwezi Juni sasa wanasema Desemba loo! Nikasema sasa sijui nimwambie nini Mheshimiwa Said Nkumba na wananchi wa Sikonge, lakini mtuamini kwamba tutafuatilia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Said Nkumba kwa kusimamia hili suala na kufuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, *TTCL* na *Celtel.* Nilianza na *TTCL* na namalizia na *TTCL.* Kuna siri moja, watoto wanaozaliwa *Police Line* wanaitwa watoto wa *line.* Labda Waheshimiwa Wabunge hawajui kwa nini hili la *TTCL* limeniandama mimi mpaka mwisho. Marehemu baba yangu alikuwa mfanyakazi wa Posta na Simu kwa miaka 40. Kwa hiyo, na mimi ni mzaliwa wa *TTCL. (Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, siwezi kulikwepa hili suala, limo ndani ya damu. Sasa *Celtel* na *TTCL* umiliki wa *Celtel Tanzania Limited,* niseme na kwa uhakika kabisa kwamba *Celtel Tanzania Limited* ni Kampuni tanzu inayomilikiwa asilimia 100 na *TTCL.* Hili halina utata hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa maana ya umiliki wa *TTCL,* asilimia 65 Serikali na asilimia 35 *Celtel International* basi unaweza kusema kama kioo kilivyo, kwamba kupitia *TTCL* Serikali inamiliki asilimia 65 ya *Celtel Tanzania* na *Celtel International* inamiliki asilimia 35 ya *Celtel Tanzania.* Ndiyo hivyo ilivyo, hakuna zaidi ya hapo, hakuna ujanja, hakuna nini. Sasa suala la kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika utendaji wa *TTCL* na katika mahusiano na nini, hili tunaendelea kulitatua mpaka hivi leo na nitatoa ripoti tulipofikia kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tumesikia sana, kwa makini sana mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwa miaka mingi, miaka mitatu, minne, kuhusu umiliki wa *TTCL.* Baada ya kwisha ukiritimba tumelitafakari sana hili suala. Tumekubaliana na mwenye hisa mwenzetu wa asilimia 35 katika *TTCL* kwamba Serikali kuanzia sasa itachukua usimamizi wa Bodi na Menejimenti ya *TTCL (Makofi).*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi ndiyo tunamiliki asilimia 65 na mmetushauri na tumelifanyia kazi na tumefikia hapo, tunawashukuru sana kwa mawazo yenu. Kwa hiyo hili tumelimaliza. Sasa vile vile kuna suala la ushauri wa mdhibiti, naomba mnisikilize kwa makini. Mdhibiti ni *Tanzania Communications Regulatory Authority* anasema kwamba na tunakubaliana naye, kwamba *TTCL* inahudumia kampuni zote, kwa sababu kampuni zote hizi huwa zinapitia *TTCL* kutoa huduma. Sasa imeibeba kampuni moja inaitwa *Celtel,* hivyo basi kwa maana ya kuleta usawa ni vema zikatenganishwa ili uwanja uwe sawa kwa kampuni zote. Sasa hili jamani nalo lina utata? Ni lakawaida sana katika soko la siku hizi. Vinginevyo makampuni haya mengine yataishitaki *TTCL* au yatamshitaki mdhibiti, lazima wakiona *TTCL* inaendelea kuibeba *Celtel.*

Mheshimiwa Spika, inaibeba kwa namna gani? Minara mingi ya *Celtel* ni ile ya *TTCL,* imepata *line* nyingi kuliko wengine hawa *Vodacom,* kupitia *TTCL,* lakini vile vile inakopa humo humo ndani, sasa wengine hawapati nafasi ya kukopeshwa toka *TTCL* na

wote inabidi washindane, kwa hiyo hili suala la ushindani limefanya kuwe na umuhimu wa kutenganisha *Celtel* na *TTCL.* Liko wazi wala sio shinikizo la mtu mwingine toka nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya hayo ili kuweza kuendeleza sekta. Uamuzi maana ya usawa na kwa kasi zaidi ni vema tukatenganisha *TTCL* na *Celtel* na uamuzi huo tayari umechukuliwa, wala halijatoka nje kama inavyokisiwa na watu wengine. Hapana, ulikuwa ni uamuzi wa Serikali baada ya kutafakari mambo yote haya ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano.

Sasa Serikali ikaamua kuzungumza na mbia maswala yote mawali, la kuturudishia umiliki wa usimamizi wa *TTCL* na vile vile suala la kutenganisha *TTCL* na *Celtel.* Sasa tumekubaliana na linafanyika. Lakini bado hatujaanza kulitekeleza lakini maamuzi yamechukuliwa. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba kwa upande wa *Celtel Tanzania* sisi pamoja na *Celtel International* tutamiliki *Celtel Tanzania* moja kwa moja bila kupitia *TTCL,* ndiyo maana yake hiyo haina maana kwamba tunaacha umiliki katika *Celtel Tanzania.*

Kwa hiyo, *Celtel Tanzania* itakuwa inatumia na itaendelea kutumia taratibu za wenye hisa kama zilivyo kataka sheria ya kampuni, hili ndilo ambalo limefanyika hivi karibuni na tumeendelea kulizungumza kwa maana ya kukamilisha utekelezaji wake. Matakwa ya wenye hisa ni kwamba *Celtel Tanzania* iendeshwe kibiashara nje ya *TTCL* kama kampuni nyingine zilivyo na italeta ushindani mzuri na kwa kweli maamuzi ya *Celtel* yatakuwa yanachukuliwa haraka bila kupitia *TTCL* na bila kupitia kwa mbia huko Ulaya na *Celtel* itakuwa na uhuru huo kwa hiyo itakwenda kwa kasi zaidi. Kwa hiyo, tumekubaliana hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa *Celtel International* jukumu lake itakuwa ni kutafuta fedha. Itakuwa *strategic partner* kutafuta fedha ili kuirekebisha hiyo *Celtel Tanzania* kwa sababu sisi kama Serikali kazi yetu si kufanyabiashara. Ili hili lifanyike tulichokubalina ni kwamba usimamizi wa Bodi kama nilivyosema pamoja na Menejimenti ya *TTCL* unarudishwa kwa mwenye hisa nyingi yaani Serikali ya Tanzania na usimamizi wa Bodi na Menejimenti ya *Celtel Tanzania* uendelee kibiashara uwe chini ya *Celtel International.* Kwa maana hiyo, *Celtel Tanzania Limited* umiliki wake utabadilika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, asilimia 60 itakuwa ni *Celtel International* na asilimia 40 itakuwa ya Serikali, mabadiliko haya hayafanyiki hivi hivi, yatafanyika ifuatavyo, malipo ya deni la *Celtel Tanzania* kwa *TTCL* yatalipwa katika kipindi cha miezi mitatu, halafu malipo ya marekebisho ya umiliki wa hisa za kampuni ya *Celtel Tanzania Limited* iliyorekebishwa yatalipwa kwa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, tunakamilisha mazungumzo ya malipo hayo, mpaka sasa tunaendelea kizungumza. Jioni ya leo nafikiri tutaendelea kuzungumza na itakapokamilika tutayaweka wazi na bayana kwa wenye hisa ambao ni wananchi wa Tanzania. Marekebisho haya yatazifanya *TTCL* na *Celtel* ziwe kampuni ambazo zinakua na zinaendelea kuleta mawasiliano ya kasi zaidi nchini. Niliona nifafanue hili kwa sababu nilizungumza kwa kasi tu na kwa kupitia asubuhi ya leo kwa maana ya maamuzi ya Serikali kuboresha mawasiliano kutumia hizi kampuni mbili.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa shukrani, kama nilivyoanza kukushukuru wewe kwa kutuongoza kwa miaka mitano kwa kutufanya tuwe na nidhamu ya hali ya juu. Umefanya Bunge pawe ni mahali ambapo hatuchoki kuja. Tumefurahia kusikia yote unayoyazungumza, vikaratasi vyako nimetusisimua pale ambapo tulikuwa tunalala, cha leo uliniletea ukasema, nukuu ya leo ni shaba si haba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hatuna maneno ya kukushukuru, ni mengi mno tunakutakia kila la kheri na maisha marefu na afya njema wewe na mama Anna Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, amenisaidia sana, sana, sana, amekuwa ni dada yangu. Nikisema mama yangu atasema namzeesha, lakini amenilea kama mama katika Wizara. Vile vile amenisaidia sana, namshukuru sana, sana. Nimefika mpaka Wete nyumbani kwake huko, kwa ruksa ya mzee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Ndugu Salim Himid Msoma ni mtu makini sana amenisaidia sana kama Katibu Mkuu, yeye ana sehemu mbili, moja, yeye ni mwanasiasa vile vile hawa ndiyo pamoja na *group* la Mheshimiwa Yoweri Museveni ndiyo walikuwa *USARF* hawa. Kwa hiyo, ametoka huko hata hivi leo ukimwambia kuhusu mabadiliko ukimwambia kuhusu kubinafsisha, anakurudisha kwenye *theories* za kama ndugu yangu Mwanri, Karl Marx, na nini. Lakini hivyo hivyo tumeenda pamoja ametusaidia sana kutuweka sawa na kutekeleza. Basi tumefaidika sana na usimamizi wa ndugu yangu Msoma akiwa kama Katibu Mkuu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Sasa hebu angalia sura ya Wizara hii kwa maana ya uongozi wa juu. Huipati popote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sura ya mtu mmoja anatoka Bara, anatoka Mbeya ni Waziri, mama mmoja anatoka Pemba, Naibu Waziri, bwana mmoja anatoka Unguja, Katibu Mkuu. Hebu sema kama unaweza kupata sura ya Muungano zaidi ya hiyo. Hapo ramani ya Tanzania imekamilika Bara na Visiwani, kwa hiyo, tunamshukuru sana aliyetupa nafasi ya kufanya kazi pamoja, namshukuru sana Mheshimiwa Benjamin Mkapa *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasimama hapa, tunasimama huko, tunazungumza, tunamshukuru kila mtu, mara chache sana tunazishukuru familia zetu zinazotufanya tuwepo hapa, shukrani kwa Wabunge wenzetu shukrani kwa Mheshimiwa Benjamin Mkapa, shukrani kwa Mheshimiwa Spika, kwa wapiga kura na kwa kila mtu, lakini shukrani kwa mama na watoto hatutoi. Sasa kweli mimi naweza kuwa na ubavu wa kuja hapa na kusimama kwa ujasiri kabisa kama mambo nyumbani yameharibika? Haiwezekani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uko hapa kila siku nadhani unafahamu kwanini? Kwa sababu katika *front row* hapa unapata faraja sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nachukua nafasi hii kwa kweli ikiwa mara yangu ya mwisho kwa maana ya kipindi hiki kumalizia kutoa hotuba yangu kwa kweli kuishukuru sana familia yangu, watoto wangu watatu, Max, Sekela na Emmanuel na vile vile mhimili

wetu mkubwa ambaye ni mama Lucy Mwandosya, ambaye leo hii yuko pale, naamini hamwezi mkanitolea shilingi kwa sababu hatapata hela ya kwenda sokoni. *(Kicheko)*

*(Hapa Mama Lucy Mwandosya alisimama na kuonekana kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 62 - Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi**

Kifungu 1001- *Administration and General* ... ... ... ... ... Sh. 1,389,173,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja majina yaandikwe ili kila mtu apate nafasi. Sasa ni programu ya 10 kifungu namba 1001 na mshahara wa mwenye medali ya shaba umo humu humu, sasa kifungu hicho kinajadiliwa sasa bado hakijaafikiwa, tunaanza na Mheshimiwa Stephen Kahumbi.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana programu ya *10 sub-vote 1001* kifungu kidogo cha 2501000 mshahara.

Nina swali dogo tu kwamba nimekuwa nikiwasiliana na Waziri na Naibu Waziri kuhusu mawasiliano ya simu ya *Celtel,* kampuni ya simu ya *Celtel* ilileta minara yake Bukene kwa nia ya kujenga mnara pale. Sisi wote tukafurahi hata Waziri alifurahi aliniandikia na ki-*note* kwa bahati mbaya si yeye nadhani lakini watu wengine wakaja wakahamisha mnara huo na kuupeleka Bugene. Lawama hiyo inaniandama mimi kwamba mimi ndiyo niliouhamisha, sina uwezo, na ndugu yangu hajanijibu labda anijibu ili nisitoke mlango wa Bunge hili nikienda na lawama za Wizara yake. Mheshimiwa Mwenyekiti naishia hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri *make a note* usianze kujibu moja, moja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa muda mrefu sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma tumekuwa tukiililia sana Wizara itusaidie kutuletea mawasiliano ya simu katika kipande kinachotoka eneo la Njombe mpaka kufika Songea Mjini. Kumekuwa kukitokea ajali nyingi, kumekuwa kukitokea matukio mengi ya ujambazi katika maeneo hayo na hivyo mara nyingi sana nimekuwa nikisimama kumwomba Mheshimiwa Waziri kama atatusaidia kuweka mnara katika eneo la Madaba basi ingetusaidia sana kuwa na mawasiliano kutoka Njombe, Madaba na Songea Mjini na hivyo kupunguza hizo hatari na ajali zote zinazoweza zikatokea katika kipande hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kuona tunawezaje kuboresha mawasiliano hayo ili kuweza kupunguza matokeo hayo makubwa yanayoweza yakatokea katika wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mnara wa Madaba umeandikwa, tunachukua maswali manne halafu Mheshimiwa Waziri utajibu halafu tutaendelea na mengine. Mheshimiwa George Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu, sina matatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ibara ya 17 amezungumzia kwamba shirika la reli limekarabati injini 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa na swali dogo tu, inaonekana hizi injini 63 mmezikarabati, lakini inawezekana kwamba ni mbovu na katika mchango wangu wa maandishi nimechangia kwamba hesabu zipi ambazo zinafanya kwamba mara nyingi kunakuwa na ajali mara kwa mara katika hii Reli ya Kati, sasa mpango wa kununua injini mpya hatukusikia kwa hiyo, nilikuwa naomba maelezo tu kwamba hizi injini 63 kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba kukarabati mara kwa mara inawezekana ni mbovu na zinaweza zikasababisha ajali mara kwa mara. Je, mpango wa kununua injini mpya wanasemaje? Ahsante Mwenyekiti.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu namba 10, *Sub-vote 1001,* kifungu 250100. Mheshimiwa Waziri ni shahidi, alikuja Mkoa wa Rukwa mwaka 2003, tulimpeleka akaona Bandari ya Kasanga inavyochezewa na kuharibiwa na huyo mtu ambaye alikuwa amepewa mkataba wa kienyeji *GS Motors* na mwenyewe Waziri kutokana na uwezo wake alipoelewa aliandika barua ya kuagiza mkataba ule utazamwe upya, kwa sababu *GS Motors* alishajenga *godown* juu ya gati lenyewe na lilitakiwa livunjwe.

Pili, kwenye Mkataba huo alipewa milioni 180 atengeneze ile bandari, hakutumia hata shilingi moja kutengeneza bandari na hii bandari imeendelea kuharibika na Waziri yeye mwenyewe aliona. Sasa leo wakati wa majibu nimestaajabu kusikia kwamba bado anaendelea na makataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika kikao chetu cha chama Tume iliundwa ikihusisha karibu Wizara tano pamoja na Mawasiliano na taarifa iliyoandikwa ilionekana kabisa kwamba kile kitu ni *scandal.* Sasa mimi nataka maelezo lini *tender* itatangazwa ili ile bandari sasa iweze kuwa *managed* na watu wenye uwezo na ameidangaya Serikali hela alipewa halafu hakutengeneza bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mwaka jana nilipouliza swali kuhusu simu za mkono Laela, walijibu kwamba zitaanza kutumika mwezi Desemba mwaka jana, sasa

nataka kujua tarehe gani kama Desemba haikuwezekana sasa watuambie ni lini itakuwa na hii ya bandari nataka niambiwe lini *tender* itatangazwa ?

**MWENYEKITI:** Nampa nafasi sasa Mheshimiwa Waziri ajibu hayo yaliyoulizwa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa masuala mbalimbali nikianzia na lile la Mheshimiwa Stephen Kahumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa masikitiko makubwa kwamba *Celtel* walipeleka vifaa vya ujenzi wa Mnara Bukene halafu baadaye wakavitoa. Baada ya mazungumzo na *Celtel Tanzania Limited,* wamenihakikishia kwamba Bukene imo katika mpango wao isipokuwa hawakutaka kuniambia ni lini lakini nina uhakika kabisa, kwa sababu ya kasi ambayo wanakwenda sasa, kwamba mwezi Januari walikuwa na wateja 400,000 sasa wana wateja 800,000. Basi kazi kubwa ni kusambaza minara nchini na nina hakika kwamba hata bila ya kuwa na ahadi ni mwezi gani, lazima watafika Bukene na mimi nachukua kama jukumu langu kabla sijamaliza muhula wangu kulisukuma hili suala kwa sababu tuna wajibu kwa ndugu zetu wa Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, amezungumzia kuhusu kuwa na mawasiliano katika barabara ya Njombe kwenda Songea. Naamini kwamba kuna sababu kubwa zaidi ya sababu za wahalifu. Kwa kuwa nina uhakika kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani itadhibiti uhalifu lakini jukumu letu sisi ni kuleta mawasiliano hata kama uhalifu upo au haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelichukua hili la kuwa na mnara katika eneo kama la Madaba pale kwenye milima ili liweze likasaidia mawasiliano kama kiungo kati ya maeneo yaliyo na simu za mkononi, eneo la Njombe na kuelekea Songea Mjini. Mimi mwenyewe nimepita eneo hili wakati nikienda kutafuta wadhamini.*(Kicheko)*

Kama nilivyokuwa nasema mimi mwenyewe hili eneo nalifahamu na bahati nzuri nilipita wakati wa usiku ambapo nilikuwa nahitaji usalama na kuwa na mawasiliano ilishindikana. Kwa hiyo, nalielewa hili suala, ni kama nilivyomjibu Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ambaye ni jirani wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba nitalifuatilia hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje amezungumzia kuhusu ukarabati wa injini. Ni kweli tunazozikarabati ni injini za zamani, ni mbovu, ni za zamani, nyingine zina miaka 25. Lakini tumekarabati hivi karibuni injini 13, tuliwapa *TRC* shilingi bilioni 2.3. Nia ni kununua injini mpya lakini uwezo kwa sasa hatuna. Lakini moja ya masharti ya mwendeshaji atakaye kuja ni kuleta pamoja na mambo mengine, injini mpya na kukarabati kufikia kiwango cha juu injini za zamani kwa sababu uendeshaji itakuwa ni jukumu lake. Kwa hiyo, niseme kuhusu ununuzi wa injini mpya hata kama tungekuwa na fedha leo tungengoja mwekezaji ndiye azinunue kwa fedha zake badala ya sisi kumnunulia ili atumie kupata faida, kwa sababu tunakaribia sana kulirekebisaha hili Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za ajali, mimi nizungumzie sababu moja. Sababu yenyewe ambayo nataka kuizungumzia ni ya udhaifu wa kibinadamu. Hivi karibuni pale nje kidogo ya Tabora, nadhani kama kilometa 11 hivi, wananchi fulani waling'oa reli, waling'oa kabisa kabisa yakabakia mataruma. Kwa hiyo, treni ya kwenda Mpanda ikaenda ikaanguka lakini bahati nzuri ilikuwa inakwenda kwa mwendo siyo wa kasi sana basi hatukupata madhara kama vile vifo.

Sasa hii ilikuwa ni hujuma tu, mambo mengi sana tunayakuta ya namna hiyo, *bolts* zinaondolewa kwenye madaraja ya reli. Amelizungumzia sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, katika moja ya hotuba zake na sisi tutaendelea kulizungumzia. Lakini reli ni ya wananchi pale walipo. Wajibu wa usalama kama ilivyo usalama wa binadamu, usalama wa vyombo vyetu ni wajibu wa wananchi. Hili ndilo nilitaka kusema kama moja ya sababu ya ajali za treni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kwamba nilipofanya ziara mkoa wa Rukwa mwaka 2003 tulienda pamoja Bandari ya Kasanga na yote anayosema nakubaliana naye mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio sababu Kasanga tumeiweka kama Bandari *special* hata katika maamuzi ya Serikali. Maamuzi ya Serikali yanasema kama maagizo kwa Mamlaka ya Usimamizi ya Bandari kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *TPA* Mpya, itasimamia Bandari zote za Mwambao na Bandari zote za Maziwa Makuu ikiwa ni pamoja na Kasanga, hakuna Bandari iliyotajwa, ni Kasanga kwa sababu ya umuhimu wake. Kwa maana hiyo, tumewaagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari waichukulie Kasanga kwa umuhimu huo. Hata mchana huu katika matayarisho yetu nilikuwa nimezingatia hilo katika kutoa maelekezo kwa Ndugu Luhigo ambaye ananisikiliza kwamba Kasanga ni Bandari muhimu sana Kusini mwa Ziwa Tanganyika. Ina mshindani Mpulungu, ina eneo kubwa ambalo inaweza kuhudumia Kusini Mashariki mwa Kongo.

Kwa hiyo, hatuwezi kuipuuza Kasanga hata siku moja. Kwa hiyo, maelekezo niliyotoa na yatazingatiwa ni kwamba kazi ya kwanza kuhusu Kasanga mbali na kwamba tumewatengea fedha hawa *TPA* waendelee kuiimarisha na watumie fedha zao kwa mwaka 2005/2006, inabidi wauangalie upya huo mkataba na kama wataona mapungufu ambayo mimi nimeyaona na wengi wameyaona, basi hatua itakayochukuliwa sitaki kuwasemea hapa kisheria, nadhani wamenielewa. Nadhani Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, naye amenielewa. Siwezi kusema zaidi ya hapo ili naye huyu asije akasema kwamba Waziri alisema mkataba ufutwe Bungeni, lakini maana yake ni hiyo hiyo tunakokwenda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anajumuisha hapa, nadhani kwa sababu nilikuwa nimefanya mchango wangu kwa maandishi inawezekana kwa sababu pia

tulikuwa wengi tulikuwa tumechangia kwa maandishi haukupata nafasi ya kuona hasa nilichokuwa nimezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme miongoni mwa vitu nilivyokuwa nimezungumza ilikuwa ni mali za *Air Tanzania Holding* ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali bila kutoa malipo yanayolingana na hizo mali na zinapelekwa sehemu nyingine. Kwa mfano kumekuwa na vipuri vyenye thamani nafikiri ya karibu kama milioni 300 hivi vilichukuliwa tu na nafikiri wakapewa hawa *Air Tanzania* hawa wapya na inasemekana kuna hata nyumba ambazo zimechukuliwa.

Sasa napenda Mheshimiwa Waziri anisaidie hapa nielewe. Ninapenda kufahamu ukweli wa kwamba nyumba za *Air Tanzania Holding* zimechukuliwa na Serikali na zingine zimechukuliwa na baadhi ya watumishi ambao kama walivyosema wengine hapa wamepata nyumba kutoka Serikalini pia. Kuna ukweli gani katika jambo hilo? Ahsante.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize jambo moja la mawasiliano ya simu za *Celtel, Vote 62,* programu 10 kifungu kidogo 250100. Wakati nachangia inawezekana Mheshimiwa Waziri hakuwa amenielewa. Nilisema kwamba katika barabara Kuu ya lami kutoka Same mpaka Mkomazi, miji yote iliyoko hapo inapata huduma ya simu za *Celtel.* Katika barabara ile ya changarawe ya kutoka Same mpaka Mkomazi, miji yote inapata huduma ya simu za *Celtel* isipokuwa kile kijiji cha Kisiwani tulichofanya mkutano na Kata za Mbagamsindo na Mbagamshewa. Sasa wale wananchi wanajisikia sehemu zote wanapata mawasiliano ya *Celtel* lakini pale hapana. *Celtel* imekuwa na nia ya kujenga mnara pale Kisiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, atawaambia wale wananchi ule mnara utajengwa lini na wao watapata mawasiliano ya *Celtel* lini kwa sababu jambo hili limeanzia tokea mwaka jana mwezi kama huu wakati Mheshimiwa Waziri alipotembelea pale. Sasa wananchi wale wanajisikia kwamba Serikali yao haiwatendei vizuri. Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 62* programu Na. 10, kifungu 2501100, *Basic Salary* na *Pensionable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi wa mambo matatu, la kwanza, ni vipi Serikali inakuwa na hisa 51 halafu inakuwa ndiyo inayoendeshwa na siyo inayoendesha. Kwa mfano, katika Shirika la *ATCL,* Serikali ina hisa 51 lakini *Management* yote na maamuzi yote yanafanywa na wale wenye hisa 49. Labda tungeelezwa ni utaratibu gani wa sheria za Kampuni zinazofuatwa?

La pili, ningependa vile vile kupata ufafanuzi, Serikali hivi sasa kwenye *Celtel* ina hisa 65 na huyu mbia ana hisa 35 lakini yeye ndiye anayemiliki maamuzi yote na sasa hivi Serikali inakusudia kuuza hisa hizo na kuwapa asailimia 60 na kubaki na asilimia 40. Hatima ya Watanzania itakuwaje katika utaratibu ikiwa wale wa kwanza ambapo mbia ana hisa 35, Serikali inaburuzwa. Je, hapo tutakapokuwa na hisa 40 itakuwa katika hali gani?

La tatu, wakati tunabinafsisha Shirika la Simu, tuliambiwa kwamba tutakuwa na *line* 300,000 za simu. Ile programu ilifikia wapi? Ahsante.

**MHE. BENEDICTO M. MTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuhoji. Nitahoji katika *Vote 62* programu 10, *Administration Sub-vote 101.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yangu na watu wa *TTCL* na Mheshimiwa Waziri unayafahamu na kila tunapochangia inaonekana mimi ni mkorofi. Lakini mengine nimeyaleta kwenye meza yako wakati fulani, nikaambiwa kesi iko Mahakamani Umoja wa Mataifa sijui wapi. Lakini, nashukuru kwamba walishindwa kama nilivyowatabiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine juzi hapa nilitaka kukamata *PSRC,* tuwakamate vizuri. Baadaye nikasema kwa sababu watu wanagombea urais wasije wakadhani nimehongwa ili niwachafulie, tukawaacha hivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ili nisikucheleweshe, nataka hapa tukubaliane kitu kimoja, naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. *TTCL* ilipouzwa kwa Mwekezaji alisema angejenga line 800,000 na kila kijiji chenye watu 3,000 kingepata simu. Anavyozungumza, mimi nina shule za Sekondari kwenye Jimbo langu hakuna simu.

Kwa hiyo, hakutakuwa na Kompyuta, hayo ndiyo madhara. Sasa huyu mwekezaji alinunua asilimia 35 kwa bilioni 120, akalipa 60. Baadaye ile bilioni 55 na kama nakosea nalidanganya Bunge lako mimi nitajiuzulu. Bilioni 55 zikapelekwa kuanzisha Kampuni Tanzu ya *Celtel.* Kwa hiyo, zile hela zilikuwa ni mali ya Tanzania zile *share* ambazo tuliuza 35. Kwa hiyo, *Celtel* tungeamini kwa watu wenye hekima na busara na akili zinazofanya mahesabu kwamba ile ni Kampuni yetu sisi Serikali ya Tanzania kwa niaba ya Watanzania kwa sababu zile alitulipa hakwenda kujenga zile line, nadhani tunaanzia hapo.

Sasa Mheshimiwa Waziri anaposema mwekezaji anamiliki asilimia 35 anazimiliki kutoka wapi? Swali la kwanza. Kwa sababu zile hela zilipaswa kwenda kule hazikwenda zikarudishwa huku, bilioni 55, nikikosea mimi nitajiuzulu. Sasa huyu anayemiliki asilimia 35 anamiliki kwa kuweka hela zipi? Naomba unilinde. Naomba aandike. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, anamiliki kwa pesa ipi aliyoweka, kwa sababu ile iliwekwa kule ikakopwa ikarudishwa huku?

Mheshimiwa Spika, sasa kama hizi zilipelekwa huku na kule kwenye *Celtel* hakukubaki hata thumni bado kwenye *TTCL* anamiliki asilimia 35, anazimiliki kwa hela gani alizoweka kule? Hilo swali la pili.

Swali la tatu, je, kama *Celtel International* walilipa bilioni 60, watazitoa kwenye mfuko upi hizo wanazotaka kulipa kwa sababu wameeleza hapa kwamba sasa wanataka

walipe? Sijui sasa kwenye *Celtel* sasa kuna mtaji wa bilioni 500, mimi sielewi. Atalipa kutoka huko nje?

Swali la nne, ni kwamba kama atalipa kutoka kule nje, sasa Waziri anaweza kutuambia ukubwa wa *Celtel* na faida iliyomo yamebaki mabilioni mangapi ili tuweze kuchekelea kwamba hizi tutapeleka kwenye MMES?

Swali la mwisho, ni kwa nini Serikali haitaki sasa kutangaza kwamba *share* zake zilizoko kwenye *Celtel* hizi asilimia 65 zishindaniwe kama zingekuwa zinashindaniwa kwenye Makampuni mengine, badala yake huyu *Celtel International* anataka kuzing'ang'aniza kwamba yeye ndiye aamue ajipe yeye, Serikali ya Tanzania ibaki na 40 kana kwamba ikibaki na 65 inakufa au inachapwa viboko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la mwisho, kama atajibu hayo nitapenda mwisho basi atuambie ni utaratibu gani ambao wanautumia kama upo wa kutangaza *tender* kwamba watu washindanie *share* za *Celtel* zilizomo zile 65 za Serikali ya Tanzania na wale ambao sasa wanavuruga utaratibu, lakini sisi ni Wabunge tumewekwa hapa kulinda mali za Watanzania. Hatukuwekwa hapa kuleta mzaha hapa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Zamu yako sasa Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa masuala mbalimbali muhimu ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge katika Kamati.

Mheshimiwa Dr. James Msekela, naomba kufafanua kwamba, vipuri ambavyo vimehamishiwa kutoka *Air Tanzania Holding Limited* kwenda *Air Tanzania* ni vipuri vya *Boeing 737* ambavyo vilikuwa havitumiki. Ni vipuri ambavyo havijapelekwa bure isipokuwa mwenye hisa ambaye ni Hazina amevipeleka huko kama mkopo, kwa hiyo itabidi vilipiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba, ni kweli kulikuwa na tatizo la nyumba kama nne hivi ambazo zaidi ya miaka 40, niseme tangu Uhuru zimekuwa zikikaliwa na wafanyakazi wa Serikali na hapa mwisho baadhi ya wafanyakazi hao walikuwa ni pamoja na Majaji. Sasa kulitokea utata wa hizi nyumba nne za Oysterbay ambazo wakati tunazihamishia *ATHCO* Wizara ya Ujenzi ikatuambia hizo ni nyumba za Serikali mtazihamishaje kwenda *ATHCO* ili mziuze? Basi ikaundwa timu ambayo pamoja na wengine ilihusisha wanaoshughulikia umiliki wa ardhi kwenda kuangalia *record* kila mahali pamoja na *record* za zamani. Ikathibitika kwamba hizo ni mali za Serikali. Kwa hiyo, ndiyo maana zimerudishwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna nyumba za baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa *Air Tanzania* ambazo kwa ujanja ujanja tu zilitaka kupotea, lakini tumegundua na tumesimamisha huo mchakato wa kuweza kuzichukua kwa njia ambayo ilikuwa ya kusikitisha kidogo kwa sababu kuna wengine ni hewa tu. Lakini watu hewa ambao hatuwezi kusema ni fulani na fulani wamepeleka malalamiko mahakamani

kwamba zile ni nyumba zao na wanataka walipwe fidia na *ATHCO.* Tuligundua kwamba makaratasi yote haya ni ya kughushi, watu wenyewe hawawezi kutambuliwa, hawaonekani, wakati huo Mahakama imeshatoa *ruling.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumepeleka kwa Polisi na sasa imekuwa ni *Police Case* kwa maana ya Mkurugenzi wa Upelelezi anaweza kuwakamata hao watu na kuwapeleka mahakamani. Walikwenda kuidanganya mahakama, sasa watakwenda kwa maana ya kushtakiwa. Kwa hiyo, hizi ni mbinu ambazo zimekuwa zikichukuliwa. Sina uhakika kama kuna wafanyakazi wa *ATC* ambao vile vile wamepata nyumba za Serikali na walinunua nyumba za *ATC,* lakini kama Mheshimiwa Dr. James Msekela au mtu mwingine yeyote ana taarifa za namna hiyo tutazifanyia kazi haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba ambazo zilikuwa za *ATC* zilizopo kwenye Balozi mbalimbali, tuna nyumba tano katika Balozi hizo, tatu ziko Nairobi, moja Johannesburg na moja iko Lusaka. Sasa kwa kweli tumezikabidhi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *ATHCO* ni Shirika la Serikali na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ilikuwa inazihitaji hizo nyumba ili wafanyakazi wetu walio nchi za nje wasitumie fedha nyingi za Taifa kukodi.

Sasa ni kama unachukua fedha kutoka mfuko mmoja unapeleka mfuko mwingine. Hata kama tungetaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa izinunue nyumba hizo izipeleke *ATHCO,* hizo zote ni fedha za Hazina kwa maana hili tatizo la nyumba za wafanyakazi walio nje ya nchi sisi hatukuona kama ni tatizo kubwa sana. Ni Serikali ile ile na imesaidia sana na vile vile Waziri wa Mambo ya Nje ni mgombea wa CCM. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kisiwani namshukuru sana Mheshimiwa John Singo. Nilipotembelea Same tulifika Kisiwani, tulikuwa na mkutano mkubwa wa hadhara, tulitoa ahadi ya kushirikiana na Wanasame na Wanakisiwani kuboresha mawasiliano na Kisiwani. Kweli kimawasiliano pale ni kisiwa.

Pia, Mheshimiwa John Singo, ananiuliza mnara utajengwa lini. Nataka kumhakikishia kwamba mawasiliano yatafika Kisiwani, lazima, lazima. Tuna mawasiliano ya karibu sana na *Celtel* kuhusu hili suala na kama nilivyowajibu Mheshimiwa Stephen Kahumbi na Mheshimiwa Jenista Mhagama, nitalivalia njuga suala la mawasiliano Kisiwani kwa kufuatilia kwa karibu sana hizi Kampuni za simu za mkononi. Binafsi napenda sana hii kazi, hasa ya kufuatilia. Watu wakiwasiliana ni furaha kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusafiri kunasaidia sana. Nilipofika Kisiwani, ile nafika tu pale, zahanati ya Kisiwani mtoto anazaliwa. Basi wakanipeleka kule na wakasema: "Mama amesema yule mtoto ataitwa jina lako." Kwa hiyo, napakumbuka sana Kisiwani na nachukua kama jukumu la kufuatilia hilo suala. Siyo mtoto wangu lakini, akikua nitapenda sana nimsomeshe kama hawezi kusomeshwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, unapochagua mbia unakuwa na sababu nyingi. Sababu yetu katika *ATCL* ilikuwa kuwa na kile tunachokiita *Strategic Partner.* Sasa kwa *Strategic Partner* wewe huwezi ukaendelea na *management* yeye akaendelea kuwa *Strategic Partner* akaleta fedha, akaleta *technology,* akaleta uzoefu halafu wewe ukaendelea kuwa meneja wake. Usimamizi wa *management* tumeiachia *South African Airways,* isipokuwa Bodi kama nilivyosema wakati nafanya majumuisho, kati ya Wakurugenzi wa Bodi nane , sita ni Watanzania. Kwa hiyo, kwa maana ya usimamizi wa kijumla kwa kweli Watanzania ndio wanaosimamia. Kama nilivyosema, mambo yakiharibika tutawabana wale Wakurugenzi. Hatuwabani *management* kwa sababu bodi ni wasimamizi kwa kile kinaitwa *fiduciary responsibility.* Kwa hiyo, kwa maana ya *Air Tanzania* bado Watanzania ndio watakaobanwa katika usimamizi wa suala hili. Maamuzi mengi ni ya Bodi, wala siyo *management.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina hisa asilimia 65 na 35 katika *Celtel.* Labda sikueleweka vizuri, nitarudia. Nilisema *Celtel Tanzania* inamilikiwa asilimia 100 na *TTCL.* Nilisema, kama unataka kuangalia kuna nini huko ndani unauliza ni watu gani wako huko, inabidi uwafuate sasa. Hutawapata katika vitabu vyao, hutampata kama ni *shareholder,* Serikali wala *Celtel International,* ila utakuta *TTCL* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakwenda kumwuliza Msajili wa Makampuni *TTCL* ni nani. Unakuta *TTCL* asilimia 65 ni Serikali na asilimia 35 ni *Celtel International.* Kwa hiyo, sasa ndio unarudi unasema: "Aah, basi kumbe hata yule mtoto babu yake ndiyo huyu. Mama yake ni *TTCL* na wazazi wa *TTCL* ni Serikali na *Celtel International."* Ndio maana yake hiyo. Sasa ukizitenganisha basi unakuwa na umiliki wa moja kwa moja. Ndiyo nilikuwa nalielezea hili na sababu nilizitoa. Kwa hiyo, naomba hili lieleweke hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Singo ameuliza swali ambalo limeulizwa vile vile na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. Naweza kujibu hapa kwamba, kulikuwa na programu ya kuongeza *line* za simu ingawa anasema ni 300,000 kwa simu za kawaida, lakini ilikuwa ni 450,000 na siyo 300,000. Halafu kutumia teknolojia nyingine pamoja na simu za mkononi ilikuwa ni 350,000, jumla 800,000. Sasa naulizwa masuala muhimu sana kwamba programu imefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya mawasiliano ya simu imebadilika sana kiasi cha kwamba duniani kote katika miaka mitatu iliyopita simu za kawaida ni pungufu kwa maana ya takwimu kuliko simu za mkononi. Kwa hiyo, hata *TTCL* hivi sasa ukitaka line unapata kwa maana ya pale Shirika lilipo kwa sababu kuna line za wazi 150,000 ambayo ni kama dead capital. 150,000 tu ndiyo zinatumiwa. Watu siku hizi wanataka simu zinazoitwa za mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zingekuwa 800,000 kila mtu angetushangaa hapa duniani kwamba tuna simu 800,000 lakini bado tunatumia 150,000! Teknolojia imebadilika. Sasa tuanze kuulizana mkataba ulikuwaje, basi waliotia saini mkataba huo hawakuangalia kwamba teknolojia itabadilika. Lakini siyo kwa nia mbaya, teknolojia imebadilika kwa nia njema tu. Sasa hivi watu karibu 3,000,000 watakuwa na simu za

mkononi                         mwezi Desemba mwaka huu.  Haya ni maendeleo makubwa sana katika mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi anauliza ilikuwa watu 3,000 wapate vibanda vya simu.  Ni kweli ilikuwa mpango wa *TTCL,* lakini kwa sababu hizi hizi ninazosema, *TTCL* ikifanya hivyo ni lazima uipatie fedha kutoka Serikalini kama unataka ifanye kazi kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa Uganda, programu hii ya kuweka vibanda katika watu 3,000 inafanywa, lakini ni jukumu la Serikali kupitia Mfuko wa Simu Vijijini.  Wanachofanya ni kwamba, wanatoa *tender* kwa Makampuni ya Simu, Makampuni ya Simu nayo yanashindana ili yatoe hizo huduma, lakini zinalipiwa na Mfuko wa Simu.   Sisi tulifikiri kwamba biashara unaweza ukaandika tu watu wakatoa, imeshindikana sababu nani atalipia!

Kwa hiyo, siku moja tutakuja hapa na kuleta ombi kwamba tuanzishe Mfuko wa Mawasiliano Vijijini.  Nadhani tutakwenda kwa kasi zaidi kwa sababu kwa *speed* waliyokwenda nayo wenzetu wa Uganda kwa muda mfupi wa miaka miwili kwenye huo mfuko, nimekwenda nimeona maajabu kabisa.  Kwa hiyo, nasi tumejifunza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba dola 55,000,000 zilipelekwa *Celtel,* labda nifafanue kuhusu fedha zilizoanzisha *Celtel Tanzania.*  Kama nilivyoanza kusema, *Celtel Tanzania* ilianzishwa na *TTCL,* haikuanzishwa na huyo mbia, ilianzishwa na *TTCL* yenyewe.  *TTCL* imeanzisha *Celtel* kwa mtaji ambao ndiyo mtaji mpaka sasa wa dola 5,000,000 na deni dola 82,000,000.

Sasa kampuni itaendeleaje namna hiyo?  Tunawashangaa hata hivyo wamefanya kazi kubwa kweli, ndiyo maana ni lazima tuirekebishe.   Hiyo ni pamoja na hilo deni la kununua vifaa ili kuanzisha hiyo kampuni.  *TTCL* ili-*extend* hilo deni kwa *Celtel Tanzania.*  Tunachosema sasa ni kwamba kama unataka kuzitenga ni lazima huo mkopo urudi, tena urudi na interest siyo bure.  Kwa hiyo hapa hakuna kusema nani alianzisha, aliyeanzisha ni *TTCL* na hiyo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba atalipaje, ukishazitenganisha na ukimpa jukumu la kwamba yeye ndiyo ana hisa nyingi ni jukumu lake kuendesha *Celtel* ilipe madeni.  Sisi kama Serikali ya Tanzania tunasema hatuwezi tukalipa.  *As a strategic partner* jukumu lake ni kuendesha *Celtel* kwa ufanisi ili iweze ikalipa deni. Sasa anaweza akakopa, lakini sisi ametuambia anaweza akakopa ili aweze kulipa hilo deni, sasa sisi hatukatai,  tunakubali kwa sababu  tunahitaji hizo fedha ziimarishe *TTCL,* zirudi Hazina. Kwa hiyo, mambo yetu yanakwenda vizuri tu, hakuna lililoharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba kwa nini hisa zisishindaniwe, mimi si mwanasheria, lakini ukisoma hii Sheria ya Makampuni mara nyingi hizi zinaitwa *memarts* nazo ni *standard.* Nyingi sana zinasema kwamba: "Mkiwa wabia wawili na kama mbia mmoja unataka kupunguza hisa zako katika kampuni, anayepata nafasi ya kwanza kisheria ya kumiliki zile hisa ambazo wewe unaziacha ni yule mbia mwenzako." Hata hizi hisa tunazoziuza ni mapatano kati ya wabia kwanza halafu ndiyo tunatoka nje

tunasema tutaziuza katika soko la Hisa la Dar es Salaam. Mwenye *priority* ya kwanza ni mbia, ndiyo sheria inavyosema na sheria hiyo ilipitishwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi, naamini katika mshahara wangu shilingi moja haitachukuliwa. Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Aaah! Hapa hakuna mwongozo, mwongozo ni kwa Spika, Mwenyekiti hana mwongozo. *(Kicheko)*

*Group* la mwisho ni Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate ufafanuzi kidogo *Vote 92,* kifungu 10, programu 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya bajeti mbili zilizopita 2003/2004 na 2004/2005 tulikuwa tumefanya mazungumzo ya muda mrefu kidogo na Mheshimiwa Waziri kuhusu umuhimu wa kuwa na gati angalau moja katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika ambao kuna vituo vya meli saba.

Katika majadiliano hayo Mheshimiwa Waziri alimshirikisha hata Meneja wa Kampuni za Meli, Meneja Mkuu, Kiondo, tukaafikiana kwamba ingefaa kituo cha Kalya kipewe kipaumbele kama kituo cha kwanza katika vituo vyote saba kujengewa gati na tuliangalia vigezo vya msingi vya kufanya kituo hicho kipewe kipaumbele. Kwanza kiko karibu na ...

**MWENYEKITI:** Naomba ufupishe kwa sababu muda unakaribia kuisha.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mwenyekiti, nashukuru.

Kwamba kiko karibu na ....

**MWENYEKITI:** Aah, unaomba kituo, unakumbushia juu ya kituo.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbushia kwamba haikuonekana kabisa katika hotuba yake. Je, gati litapatikana katika kituo hicho kwa sababu ambazo tulikuwa tumeziangalia pamoja? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, mwaka huo wa 2003 *Celtel* walifika Uvinza na wakawa wameonyesha utayari wa kujenga minara miwili kwa ajili ya kuweka mtandao pale, mpaka sasa hawajaonekana. Ningependa kujua hatma ya eneo hilo kama litapatiwa huo mtandao wa *Celtel.*Ahsante.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe hoja yangu kidogo, Fungu 62, programu ya 10, kifungu 1001, kifungu kidogo 250100. Ninachohitaji ni ufafanuzi tu, sina tatizo na bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Katika kitabu chake cha bajeti ukurasa wa 105, kifungu 156 ilipozungumziwa mtandao wa simu za *Vodacom,* halafu ukurasa wa 108, kifungu 157 mtandao wa *Celtel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba Waziri atoe ufafanuzi kwa sababu yaliyoandikwa hapa yanaweza kukatisha tamaa makampuni mengine ambayo yanataka kupeleka simu katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano, pale katikati unapoelezea Mkoa wa Tanga, unapotaja Lushoto inaweza kuwa na maana kwamba ni Lushoto nzima ina mtandao wa *Vodacom.* Pia kule kwa *Celtel,* unapotaja Lushoto kunaweza kuwa na maana kwamba ni Lushoto nzima ina mtandao wa *Celtel* kumbe sivyo, ni Mji mdogo wa Lushoto kipenyo cha kilometa 10.

Kwa hiyo, nadhani hii ingetolewa ufafanuzi ili makampuni mengine yanayotaka kwenda kuwekeza huko wapate nafasi ya kufanya hivyo. Sidhani kama ni Wilaya nzima iliyofanyiwa hivyo. Ahsante sana.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi naomba kuuliza swali katika *Vote 62,* programu namba 10, *Sub-vote 1001.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina matatizo na Mheshimiwa Waziri, isipokuwa nataka ufafanuzi tu katika mambo matatu. Kwanza ninataka nijue hatma ya wale wafanyakazi wa mamlaka ambao sasa hivi wako chini ya *SUMATRA* walioko Makao Makuu kwamba wao sasa watakuwa wapi.

La pili, nataka nipate ufafanuzi kuhusu *accident* nyingi sana hasa za mabasi zinazoongezeka. Suala la *speed governor* liko chini yenu na mnashughulikiaje? Tatu, nipate pia ufafanuzi kwa nini mabasi ya abiria yanakuwa na mlango mmoja na hayana *emergency door?* Kwa uzoefu ni kwamba, abiria wengi wanaofariki kwa *accident,* wanafariki kwa kukanyagwa na abiria wengine.

La mwisho ...

**MBUNGE FULANI:** La nne.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** La nne, nikumbushie tu kwamba sijaona mpango wa zile Wilaya mpya kwenye Makao Makuu ziko vipi kuhusu mambo ya mtandao. Nashukuru.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie na hoja za Mheshimiwa Edward Ndeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Tanganyika tumetoa kipaumbele kwa gati ya Karema na gati ya Kasanga. Tutaiongeza gati ya Kalya, tutaangalia mwaka kesho itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Celtel* Uvinza, kama nilivyojibu kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, nitalichukua kama kazi yangu na kufuatilia ili huduma hiyo ifike Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa William Shellukindo, kwa mapokezi na ziara nzuri tuliyofanya pamoja Bumbuli na vile vile nimhakikishie kwamba hapo ni Lushoto ule Mji Mdogo. Maeneo mbalimbali katika Wilaya hiyo yamepata huduma za simu, lakini tatizo bado lipo kwa sababu ya milima mingi na maeneo bado, tutaendelea kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu aliyozungumzia Mheshimiwa Venance Mwamoto, wafanyakazi waliokuwa Makao Makuu ya Wizara ambao wanahamishiwa *SUMATRA* wanahamishiwa kwa mujibu wa sheria ambayo ilipitishwa hapa ambayo kwa kweli ni kama inaendeleza ajira yao na kama hawahitajiki basi taratibu ambazo zimeainishwa katika sheria zitatumika na mafao yao yatalipwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *speed governor,* hili suala nafikiri ni la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini tutalipeleka, litazungumziwa na *SUMATRA* ambaye amechukua jukumu la usimamizi wa kijumla wa masuala ya usalama katika uchukuzi ikiwa ni pamoja na hilo suala la *emergency doors* kwenye mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Wilaya ni kitu muhimu sana na ni soko kubwa la huduma zote za kijamii na kila tunapopata Wilaya mpya tunaongezea katika mipango yetu. Kwa hiyo, Wilaya zote ambazo zimetangazwa hivi karibuni kuwa Wilaya kamili makao yake makuu tunayaingiza katika program zetu za mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu - 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... ... ... ... .. Sh. 884,651,400/=

Kifungu - 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.1,143,726,100/=

Kifungu - 2001-*Transport and Communication* ... ... ... Sh.37,373,389,700/=

Kifungu - 2002 - *Central Transport and Licensing*... ... ... Sh.127,719,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 62 - Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi**

Kifungu - 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... Sh.300,000,000/=
Kifungu - 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.150,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu - 2001 - *Transport and Communication* ... ... ...Sh.38,697,110,700/=

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho kifungu kidogo cha 6236, ujenzi wa *airport* za Arusha na Mafia. Wakati nikichangia niliomba nipate majibu ya zile fedha za *TAA* ambazo ilikuwa zitolewe kutengenezea uwanja wa ndege wa Mafia, zimepotelea wapi? Lakini pia katika hizo shilingi 50,000,000/= walizotenga ni kwamba hatutaziba viraka, tutasubiri mpaka hizo fedha nyingine zipatikane ili tuweze kutengeneza kiwanja kizima au vipi?

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu kwa Mheshimiwa mtoa hoja. Nimekuwa nikifanya mawasiliano kwa muda mrefu na yeye na Wizara kuhusu mnara wa *Celtel* katika Jimbo la Nyang'wale na *survey* imeshafanyika na wataalam walikuwa wameahidi kwamba mnara ungejengwa mwezi wa saba. Lakini tarehe 20 Juni, 2005 wakati najibiwa swali langu, Naibu Waziri alisema kwamba: "Mnara umeishajengwa kwenye Kijiji cha Kukuluma." Hicho ni kijiji ambacho hakipo jimboni kwangu! Mnara wa *Celtel* bado haujajengwa kule na *Celtel* waliahidi na wananchi nilishawaahidi hivyo na Waziri alikuwa kule suala hilo alilisikia. Ninaomba maelezo kuhusu mnara huo kwamba utajengwa lini katika mwezi wa saba. Ni kama ilivyopangwa au vinginevyo? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa suala alilozungumzia Mheshimiwa Halima Kimbau, kama ifuatavyo, Fedha zilizotengwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege zipo, ila zilikuwa hazitoshi. Mwaka 2005/2006 mamlaka itatumia shilingi 700,000,000/= kuboresha kiwanja hicho. Hizo shilingi 700,000,000 zinajumuisha fedha zilizotengwa mwaka jana na fedha za mwaka huu shilingi 50,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa James Musalika amezungumzia kuhusu mnara wa *Celtel.* Tunaendelea kufuatilia suala la mnara huo na yeye anajua jinsi tulivyo karibu sana na Mwenyekiti wa *Celtel Tanzania* ambaye vile vile nadhani anatoka katika Jimbo hilo hilo la Nyang'wale na nitazungumza naye jioni hii, nitasukuma hilo suala ili mnara huo upatikane. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi limepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo tumefikia mwisho wa kikao cha leo. Kwa hiyo, sasa Bunge linaahirishwa hadi kesho asubuhi saa 3.00.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 30 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*